**ILANI**
**SIO YA KUUZWA**

NAKALA HIZI ZINATOLEWA BILA MALIPO KWA MANUFAA YA WANANCHI.
NI HATIA KUUZA NAKALA HII YA KATIBA


Ikiwa umeuziwa nakala hii ya Katiba, tujulishe kwa njia ya simu : 020 213 55 61 au kwa njia ya barua pepe : info@uraia.or.ke

Uraia
Kenya's National Civic Education Programme


Uraia Trust,
P.O. Box 28151-00100, Nairobi, Kenya
Tel: 020 213 5561/ 0728 608 737
info@uraia.or.ke


**Demokrasia thabiti ina kuzwa na wananchi walio na ufahamu wa haki na majukumu yao**

KATIBA YA KENYA



**SIO YA KUUZWA**

# KATIBA YA KENYA

Uraia
Kenya's National Civic Education Programme

Nakala Rasimu ya Katiba

## DIBAJI

URAIA inanuia kusambaza Katiba ya Kenya ifikie watu wote nchini.

Tafsiri hii ya Katiba ya Kenya inatumia chapisho la Halmashauri ya Kitaifa ya Kuripoti Maswala ya Sheria ya tarehe 27 Agosti mwaka wa 2010.

Tumeamua kuchapisha na kusambaza chapisho hili kwa kuwa Kiswahili, kwa mujibu wa Katiba, ni lugha ya taifa ya Kenya na pia ni lugha rasmi pamoja na Kiingereza.

Tunatumai tafsiri hii itawawezesha Wakenya wengi zaidi kuisoma, kuifahamu, na kuitumia Katiba yao.

Pia kunatarajia uchapishaji, na matumizi yake yatachangia kuboreshwa kwa tafsiri hii. Kwa hivyo tunawakaribisha watumiaji wa tafsiri hii kuchangia katika kuiboresha kwa kutoa maoni yao kuhusu istilahi za kisheria zilivyotumika, matumizi ya msamiati na kadhalika. Wanaweza kutaja mapungufu watakayoyaona na/au kupendekeza mabadiliko yanayofaa.

Mapendekezo ya kuiboresha tafsiri hii yanaweza kutumwa kwa barua pepe kupitia –

info@uraia.or.ke

Tunatumai tukishirikiana hivi kuiboresha tafsiri hii, tutachangia kukamilisha mchakato wa kuwa na tafsiri rasmi inayotambulika kisheria.

Katika kutumia tafsiri hii ni muhimu kukumbuka matumizi yake yanasimamiwa na Katiba. Ibara ya 259(2) ya Katiba inaeleza kuwa ikiwa kutakuwa na utata au ubishi wowote kuhusu tafsiri yoyote, nakala rasmi itakayotumika ni ya Kiingereza.

Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa wale wote waliochangia kupatikana kwa chapisho hili tulilolitumia.

Uraia

Kenya's National Civic Education Programme


ILANI

SIO YA KUUZWA;

NAKALA HIZI ZINATOLEWA BILA MALIPO KWA MANUFAA YA WANANCHI.

Ikiwa umeuziwa nakala hii ya Katiba , tujulishe kwa njia ya simu : 020 213 55 61 au kwa njia ya barua pepe : info@uraia.or.ke


Agosti 27, 2010



## UTANGULIZI WA MPANGILIO WA VIFUNGU

**SURA YA KWANZA—MAMLAKA YA WANANCHI NA UKUU WA KATIBA HII**

1—Mamlaka ya wananchi.

2—Ukuu wa Katiba Hii.

3—Kutetea Katiba Hii.

**SURA YA PILI —JAMHURI**

4—Kutangazwa kwa Jamhuri.

5—Teritori ya Kenya.

6—Ugatuzi na upataji huduma.

7—Lugha ya taifa, lugha rasmi na lugha zingine.

8—Nchi na dini.

9—Nembo za kitaifa na siku za kitaifa.

10—Maadili ya kitaifa na kanuni za utawala.

11—Utamaduni.

**SURA YA TATU—URAIA**

12—Haki za raia.

13—Kupata na kudumisha uraia.

14—Uraia kwa kuzaliwa.

15—Uraia kwa kujiandikisha.

16—Uraia wa nchi mbili.

17—Kuondolewa kwa uraia.

18—Sheria kuhusu uraia.



*SIO YA KUUZWA*

## SURA YA NNE—SHERIA ZA HAKI


### Sehemu ya 1—Vifungu vya Kijumla Vinavyohusiana na Sheria za Haki

19—Haki na uhuru wa kimsingi.

20—Matumizi ya Sheria za Haki.

21—Utekelezaji wa haki na uhuru wa kimsingi.

22—Utekelezaji wa Sheria za Haki.

23—Mamlaka ya mahakama katika kudumisha na kutekeleza Sheria za Haki.

24—Udhibiti wa haki au uhuru wa kimsingi.

25—Haki na uhuru wa Kimsingi ambao hauwezi kudhibitiwa.

### Sehemu ya 2—Haki na Uhuru wa Kimsingi

26—Haki ya kuishi.

27—Usawa na uhuru kutokana na ubaguzi.

28—Heshima kwa binadamu.

29—Uhuru na usalama wa mtu.

30—Uhuru kutokana na utumwa, kukandamizwa, na kazi za lazima.

31—Faragha.

32—Uhuru wa dhamira, dini, imani na maoni.

33—Uhuru wa kujieleza.

34—Uhuru wa vyombo vya habari.

35—Uhuru kupata habari.

36—Uhuru wa kutangamana.

37—Uhuru wa kukutana, kuandamana, kugoma na kulalamika.

38—Haki za kisiasa.

39—Uhuru wa kwenda popote na kuishi popote.

40—Ulinzi wa haki ya kumiliki mali.

41—Mahusiano ya kikazi.

42—Mazingira.

43—Haki za kiuchumi na za kijamii.

44—Lugha na Utamaduni.

45—Familia.

46—Haki za watumiaji bidhaa na huduma.

47—Hatua za haki za kiutawala.

48—Upataji haki.

49—Haki za watu waliotiwa mbaroni.

50—Haki katika kusikizwa kwa kesi.

51—Haki za watu walio kizuizini, waliokamatwa au waliofungwa gerezani.

**Sehemu ya 3 — Utekelezaji Maalum wa Haki**

52—Ufafanuzi wa Sehemu Hii.

53—Watoto.

54—Watu wenye ulemavu.

55—Vijana.

56—Jamii za watu wachache na za watu waliotengwa.

57—Wazee katika jamii.

**Sehemu ya 4—Hali ya Hatari**

58—Hali ya hatari.

**Sehemu ya 5—Tume ya Kitaifa ya Kenya ya Haki za Binadamu na Usawa**

59—Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu na Usawa.

**SURA YA TANO—ARDHI NA MAZINGIRA**

**Sehemu ya 1—Ardhi**

60—Kanuni za sera ya ardhi. 61—Mangilio wa ardhi.

62—Ardhi ya umma.

63—Ardhi ya jamii.

64—Ardhi ya mtu binafsi.



*SIO YA KUUZWA*

65—Umiliki ardhi wa watu wasiokuwa Wakenya.

66—Usimamizi wa matumizi ya ardhi na mali.

67—Tume ya Kitaifa ya Ardhi.

68—Sheria zinazohusu ardhi.

**Sehemu ya 2—Mazingira na Mali-Asili**

69—Majukumu yanayohusiana na mazingira

70—Utekelezwaji wa haki za mazingira

71—Makubaliano yanayohusiana na mali-asili.

72—Sheria zinazohusu mazingira.

**SURA YA SITA—UONGOZI NA UADILIFU**

73—Wajibu wa uongozi.

74—Kiapo cha uaminifu cha Maafisa wa Serikali.

75—Mienendo ya maafisa wa Serikali.

76—Uadilifu wa kifedha wa maafisa wa Serikali.

77—Udhibiti katika shughuli za maafisa wa Serikali.

78—Uraia na uongozi.

79—Sheria ya kuundwa kwa tume ya maadili na kukabiliana na ufisadi.

80—Sheria zinazohusu uongozi.

**SURA YA SABA—UWAKILISHAJI WA WATU**

**Sehemu ya 1 — Mfumo na Mchakato wa Uchaguzi**

81—Kanuni za kijumla za mfumo wa uchaguzi.

82—Sheria ya uchaguzi

83—Kusajiliwa kama mpiga kura

84—Wagombea viti katika uchaguzi na vyama vya kisiasa kuzingatia kanuni za maadili

85—Ustahiki wa kusimama kama mgombea wa kibinafsi

86—Upigaji kura.

87—Mizozo ya uchaguzi

**Sehemu ya 2—Tume Huru ya Uchaguzi na Kuwekea Mipaka Maeneo ya Upigaji Kura**

88— Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka.

89—Uwekaji mipaka katika maeneo ya uchaguzi.

90—Ugawaji orodha ya viti vya chama.

**Sehemu ya 3—Vyama vya Kisiasa**

91—Mahitaji ya kimsingi kwa vyama vya kisiasa.

92—Sheria kuhusu vyama vya kisiasa.

**SURA YA NANE—MABUNGE**

**Sehemu ya 1—Kuundwa kwa Mabunge na Jukumu la Mabunge**

93—Muhula wa Mabunge.

94—Jukumu la Mabunge.

95—Jukumu la Bunge la Kitaifa.

96—Jukumu la Seneti.

**Sehemu ya 2—Muundo na Uanachama wa Bunge la Kitaifa**

97—Uanachama wa Bunge la Kitaifa.

98—Uanachama wa Seneti.

99—Ustahiki au kutostahiki katika kuchaguliwa kama mbunge.

100—Kukuza uwakilishi wa jamii zilizotengwa

101—Uchaguzi wa wabunge.

102—Muhula wa Bunge.

103—Mbunge kuondoka ofisini.



*SIO YA KUUZWA*

104—Haki ya kumwondoa mbunge mamlakani.

105—Uamuzi katika maswali yanayohusiana na uanachama.

**Sehemu ya 3—Afisi za Bunge**

106—Maspika na Manaibu Spika wa Bunge.

107—Kuongoza Vikao Bungeni.

108—Viongozi wa vyama.

**Sehemu ya 4—Taratibu za Kutunga Sheria Bungeni**

109—Matumizi ya mamlaka ya kutunga sheria.

110—Miswada kuhusu serikali za kaunti.

111—Miswada maalum inayohusu serikali za kaunti. 112—Miswada ya kawaida inayohusu serikali za kaunti.

113—Kamati za upatanishi.

114—Miswada ya Fedha.

115—Idhini na rufaa ya rais.

116—Sheria kuanza kutumika.

**Sehemu ya 5—Taratibu za Kijumla na Sheria za Bunge**

117—Mamlaka, haki maalum na kinga dhidi ya mashtaka.

118—Ufikiaji na kushiriki kwa umma

119—Haki ya kuwasilisha ombi kwa Bunge.

120—Lugha rasmi za Bunge.

121—Idadi ya wabunge inayohitajika katika kila kikao.

122—Kupiga Kura Bungeni.

123—Maamuzi ya Seneti.

124—Kamati na Sheria Zinazosimamia Vikao vya Bunge.

125—Mamlaka ya kuitisha ushahidi.

**Sehemu ya 6—Vipengee vya Ziada**



*SIO YA KUUZWA*

126—Eneo la vikao vya Bunge.

127—Tume ya Huduma za Bunge.

128—Makarani na wafanyakazi wa Bunge.

**SURA YA TISA—KITENGO CHA SERIKALI CHA UTENDAJI**

**Sehemu 1—Kanuni na Muundo wa Kitengo cha Utendaji cha Serikali ya Kitaifa.**

129—Kanuni za mamlaka kuu ya utendaji.

130—Mamlaka Kuu ya Kitaifa Inayosimamia Utendaji.

**Sehemu ya 2—Rais na Naibu wa Rais**

131—Uchaguzi wa Rais.

132—Majukumu ya Rais.

133—Mamlaka ya Kuwasamehe Waliohukumiwa.

134—Matumizi ya mamlaka ya rais wakati wa urais wa muda mfupi

135—Maamuzi ya Rais.

136—Uchaguzi wa Rais.

137—Ustahiki na kutostahiki katika kuchaguliwa kama Rais.

138—Mchakato wa uchaguzi wa rais.

139—Kifo kabla ya kuchukua hatamu.

140—Maswali kuhusu uhalali wa uchaguzi wa rais.

141—Kuchukua hatamu za Urais.

142—Muda wa kuhudumu katika ofisi ya Rais.

143—Ulinzi dhidi ya mashtaka.

144—Kuondolewa kwa Rais kwa misingi ya kukosa uwezo.

145—Kuondolewa kwa Rais kupitia kura ya kutokuwa na imani.

146—Nafasi Katika Ofisi ya Rais.

147—Majukumu ya Naibu wa Rais.

148—Kuchaguliwa na Kuapishwa kwa Naibu wa Rais.

149—Nafasi Katika ofisi ya Naibu wa Rais.

150—Kuondolewa kwa Naibu wa Rais.

151—Malipo na manufaa ya Rais na Naibu wa Rais.

**Sehemu ya 3—Baraza la Mawaziri**

152—Baraza la Mawaziri.

153—Maamuzi, majukumu na kuwajibika kwa Baraza la Mawaziri.

154—Katibu wa Baraza la Mawaziri.

155—Makatibu Wakuu.

**Sehemu ya 4—Ofisi Nyinginezo**

156—Mwanasheria Mkuu.

157—Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma.

158—Kuondolewa na kujiuzulu kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma.

**SURA YA KUMI—KITENGO CHA SERIKALI KINACHOSIMAMIA MAHAKAMA**

**Sehemu ya 1 – Mamlaka ya Mahakama na Mfumo wa Kisheria**

159—Mamlaka ya mahakama.

160—Uhuru wa Mahakama.

161—Ofisi na maafisa wa mahakama.

162—Mfumo wa mahakama.

**Sehemu ya 2— Mahakama za Kiwango cha Juu**

163—Mahakama ya Juu Zaidi

164—Mahakama ya Rufaa. 165—Mahakama Kuu.

166—Uteuzi wa Jaji Mkuu, Naibu wa Jaji Mkuu na majaji wengine.

167—Kipindi cha kuhudumu ofisini cha Jaji Mkuu na majaji wengine.

168—Kuondolewa ofisini.

**Sehemu ya 3—Mahakama za Kiwango cha Chini**

169—Mahakama ndogo.

170—Mahakama za Kadhi.

**Sehemu ya 4—Tume ya Huduma za Mahakama**

171—Kuundwa kwa Tume ya Huduma za Mahakama.

172—Kazi ya Tume ya Huduma za Mahakama.

173—Hazina ya Mahakama.

**SURA YA KUMI NA MOJA—SERIKALI YA UGATUZI**

**Sehemu ya 1—Malengo na Kanuni za Serikali ya Ugatuzi**

174—Malengo ya ugatuzi.

175—Kanuni za serikali ya ugatuzi.

**Sehemu ya 2—Serikali za Kaunti**

176—Serikali za kaunti.

177—Uanachama katika bunge la kaunti.

178—Spika wa bunge la kaunti.

179—Kamati za mamlaka ya utendaji katika kaunti.

180—Uchaguzi wa gavana wa kaunti na naibu gavana wa kaunti.

181—Kuondolewa kwa serikali ya kaunti.

182—Nafasi katika ofisi ya gavana wa kaunti.

183—Majukumu ya kamati za mamlaka ya utendaji katika kaunti.

184—Maeneo yenye miji na majiji.

185—Mamlaka ya utungaji sheria ya mabunge ya kaunti.

**Sehemu ya 3—Majukumu na Mamlaka ya Serikali za Kaunti**

186—Kazi na mamlaka ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti.

187—Uhamisho wa kazi na mamlaka kati ya ngazi za serikali.

**Sehemu ya 4—Mipaka ya Kaunti**

188—Mipaka ya kaunti.

**Sehemu ya 5—Mahusiano Kati ya Serikali**

189—Ushirikiano kati ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti.

190—Usaidizi kwa serikali za kaunti. 191—Mgongano wa sheria.

**Sehemu ya 6—Kusimamishwa kwa Serikali za Kaunti**

192—Kusimamishwa kwa serikali ya kaunti

**Sehemu ya 7—Vifungu vya Kijumla**

193—Ustahiki katika kuchaguliwa kama mwakilishi wadi katika bunge la kaunti.

194—Kuondolewa ofisini kwa mwakilishi wadi katika bunge la kaunti.

195—Mamlaka ya bunge la kaunti ya kuwaita mashahidi.

196—Kushiriki kwa umma na mamlaka, haki maalum na kinga dhidi ya mashtaka kwa bunge la kaunti.

197—Usawa wa kijinsia na utofauti katika bunge la kaunti.

198—Serikali ya kaunti katika kipindi cha mpito.

199—Kuchapishwa kwa sheria za kaunti.

200— Sheria Kuhusu Sura Hii.

**SURA YA KUMI NA MBILI—FEDHA ZA UMMA**

**Sehemu ya I—Kanuni na Mfumo wa Fedha za Umma**

201—Kanuni za fedha za umma.

202—Ugavi wenye usawa wa mapato ya kitaifa.

203—Ugavi wenye usawa na sheria zingine za kifedha.

204—Hazina ya Usawazishaji.



SIO YA KUUZWA

205—Mashauriano kuhusu sheria za kifedha zinazoathiri kaunti.

**Sehemu ya 2—Fedha Zingine za Umma**

206—Hazina ya jumla na hazina zingine za umma.

207—Hazina za Mapato za serikali za kaunti.

208—Hazina ya Dharura.

**Sehemu ya 3—Deni la Umma na Mamlaka ya Kuongeza Mapato**

209—Mamlaka ya kutoza ushuru na malipo mengine. 210—Kutoza ushuru.

211—Ukopaji wa serikali ya kitaifa.

212—Ukopaji wa kaunti.

213—Udhamini wa mikopo ya serikali ya kitaifa.

214—Deni la umma.

**Sehemu ya 4—Ugavi wa Mapato**

Tume ya Ugavi wa Mapato

216—Kazi ya Tume ya Ugavi wa Mapato

217—Ugavi wa mapato

218—Miswada ya Ugavi wa Mapato ya Kila Mwaka

219—Uhamishaji wa ugavi wenye usawa

**Sehemu ya 5—Bajeti na Matumizi**

220—Muundo, yaliyomo na wakati wa bajeti.

221—Mswada wa makadirio ya bajeti na Matumizi ya Mwaka.

222—Matumizi kabla ya kuidhinishwa kwa bajeti ya kila mwaka.

223—Matumizi ya ziada.

224—Miswada ya matumizi ya fedha za Kaunti.

**Sehemu ya 6—Udhibiti wa Fedha za Umma**

225—Udhibiti wa fedha.

226—Akaunti na ukaguzi wa mashirika ya umma.

227—Ununuaji wa bidhaa na huduma za umma.

**Sehemu ya 7— Maafisa wa Kifedha na Taasisi za Kifedha**

228—Msimamizi wa Bajeti.

229—Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

230—Tume ya Mishahara na Malipo.

231—Benki Kuu ya Kenya.

**SURA YA KUMI NA TATU—HUDUMA KWA UMMA**

**Sehemu ya 1—Maadili na Kanuni Katika Huduma kwa Umma**

232—Maadili na kanuni katika huduma kwa umma.

**Sehemu ya 2 —Tume ya Huduma za Umma**

234—Mamlaka na Kazi ya Tume ya Huduma kwa Umma.

235—Uajiri wa wafanyakazi wa serikali za kaunti.

236—Ulinzi wa wafanyakazi wa umma.

**Sehemu ya 3—Tume ya Huduma kwa Walimu**

237—Tume ya Huduma kwa Walimu.

**SURA YA KUMI NA NNE—USALAMA WA KITAIFA**

**Sehemu ya 1—Vitengo vya Usalama wa Kitaifa**

239—Taasisi za usalama wa kitaifa.

240—Kuundwa kwa Baraza la Usalama wa Kitaifa.

**Sehemu ya 2—Majeshi ya Ulinzi wa Kenya**

241—Kuundwa kwa Baraza la Ulinzi na Vikosi vya Ulinzi

**Sehemu ya 3—Huduma ya Upelelezi ya Kitaifa**

242— Kubuniwa kwa Huduma ya Upelelezi ya Kitaifa.

**Sehemu ya 4—Huduma ya Kitaifa ya Polisi**



*SIO YA KUUZWA*

243—Uongozi wa Huduma ya Kitaifa ya Polisi.

244—Malengo na kazi ya Huduma ya Kitaifa ya Polisi

245—Uongozi wa Huduma ya Kitaifa ya Polisi

246—Huduma ya Polisi ya Kitaifa.

247—Huduma zingine za polisi.

**SURA YA KUMI NA TANO—TUME NA OFISI HURU**

248—Kutumika kwa Sura.

249—Malengo, mamlaka na ufadhili wa tume na ofisi huru.

250—Muundo, uteuzi na muda wa kuwa ofisini.

251—Kuondolewa ofisini.

252—Kazi na mamlaka ya kijumla.

253—Tume na ofisi huru kuwa kama kampuni au shirika.

254—Kuripoti kwa tume na ofisi huru.

**SURA YA KUMI NA SITA—MAREKEBISHO YA KATIBA HII**

255—Marekebisho ya Katiba Hii.

256—Marekebisho kwa njia ya mapendekezo ya bunge.

257—Marekebisho kwa njia ya mapendekezo ya wananchi wengi.

**SURA YA KUMI NA SABA—VIFUNGU VYA KIJUMLA**

258—Utekelezaji wa Katiba Hii.

259—Kufasiri Katiba Hii.

260—Ufasiri.



*SIO YA KUUZWA*

**SURA YA KUMI NA NANE—VIFUNGU KUHUSU MUDA WA MPITO NA YATAKAYOFUATA**

261—Sheria zitakazofuata.

262—Vifungu kuhusu muda wa mpito na yatakayofuata.

263—Tarehe ya Kutekelezwa.

264—Kufutiliwa mbali kwa katiba ya hapo awali.

**VIAMBATISHO**

Kiambatisho cha Kwanza: Kaunti

Kiambatisho cha Pili: Nembo za Kitaifa

Kiambatisho cha Tatu: Viapo vya Kitaifa na Uthibitisho Kiambatisho cha Nne: Mgao wa Majukumu kati ya Serikali ya Kitaifa na serikali za kaunti

Kiambatisho cha Tano: Sheria zitakazotungwa na Bunge

Kiambatisho cha Sita: Vifungu kuhusu muda wa mpito na yatakayofuata




SIO YA KUUZWA

# UTANGULIZI

**Sisi, watu wa Kenya,**

*TUNATAMBUA* ukuu wa Mwenyezi Mungu muumba wa vyote:

*TUNAWAHESHIMU* mashujaa waliojitoa mhanga kuleta uhuru na haki nchini mwetu:

*TUNAJIVUNIA* tofauti zetu za kikabila, kitamaduni na kidini na tukiazimia kuishi kwa amani na umoja tukiwa taifa moja huru:

*TUNATHAMINI* mazingira, ambayo ndiyo urithi wetu na tukiazimia kuyadumisha kwa manufaa ya vizazi vijavyo:

*TUNAJITOLEA* kukuza na kuhifadhi maslahi ya mtu binafsi, familia, jamii na taifa: *TUNATAMBUA* matarajio ya Wakenya wote ya serikali iliyo na misingi bora ya maadili ya haki za binadamu, usawa, uhuru, demokrasia, haki za kijamii na utawala wa kisheria:

*TUNATUMIA* uhuru wetu na haki yetu ya kuamua aina ya uongozi katika nchi yetu na tukiwa tumeshiriki kikamilifu katika kuiunda Katiba hii: ***TUNAIKUBALI, TUNAIPITISHA,*** na kujipatia sisi wenyewe na vizazi vijavyo, Katiba hii.

*MUNGU IBARIKI KENYA*



SIO YA KUUZWA

# SHERIA ZA KENYA

Katiba ya Kenya, 2010



SIO YA KUUZWA

## SURA YA KWANZA — MAMLAKA YA WANANCHI NA UKUU WA KATIBA HII

**1.**

*Mamlaka ya wananchi.*

(1) Mamlaka yote makuu ni ya wananchi wa Kenya na yanaweza kutekelezwa tu kulingana na Katiba hii.

(2) Wananchi wanaweza kutekeleza mamlaka yao kwa njia ya moja kwa moja au kupitia wawakilishi wao waliochaguliwa kidemokrasia.

(3) Mamlaka ya wananchi katika Katiba hii yamepeanwa kwa idara za Serikali, ambazo zitafanya kazi zao kulingana na Katiba hii –

a) Bunge la Kitaifa na mabunge katika serikali za kaunti;

b) serikali ya kitaifa na mifumo ya serikali katika kaunti; na

c) Idara ya Mahakama na mahakama huru ya ngazi ya chini.

(4) Mamlaka makuu ya wananchi yanatekelezwa katika––

a) Ngazi ya kitaifa; na

b) Ngazi yakaunti.

**2.**

*Ukuu wa Katiba Hii.*

(1) Katiba hii ndio sheria kuu ya Jamhuri na inapaswa kufuatwa na watu wote na idara zote za Serikali katika ngazi zote mbili za serikali.

(2) Hakuna mtu anayeweza kudai kuwa na mamlaka au kutumia mamlaka ya Serikali ila tu kwa njia iliyoidhinishwa chini ya Katiba hii.

(3) Uhalali au uthabiti wa Katiba hii hauwezi kupingwa na au mbele ya mahakama yoyote au idara yoyote ya Serikali.



SIO YA KUUZWA

(4) Sheria yoyote, ikijumuisha sheria ya mila na tamaduni, ambayo haiambatani na Katiba hii ni batili kwa kiwango cha ukinzani huo, na tendo lolote au kutotenda kunakokiuka Katiba hii ni batili.

(5) Sheria za kijumla za kimataifa zitakuwa sehemu ya sheria za Kenya.

(6) Mkataba au maagano yoyote ambayo yataidhinishwa na Kenya yatakuwa sehemu ya sheria za Kenya chini ya Katiba hii.

**3.**

*Kuitetea Katiba Hii.*

(1) Kila mtu ana jukumu la kuiheshimu, kuitetea na kuilinda Katiba hii.

(2) Jaribio lolote la kubuni Serikali bila kufuata Katiba hii ni kinyume cha sheria.

## SURA YA PILI — JAMHURI

**4.**

*Kutangazwa kwa Jamhuri.*

(1) Kenya ni Jamhuri inayojitawala.

(2) Jamhuri ya Kenya itakuwa Taifa la kidemokrasia na lenye vyama vingi likiwa kwenye misingi ya maadili ya kitaifa na kanuni za utawala kama ilivyotajwa katika Kifungu cha 10.

*Eneo la Kenya.*

**5.** Eneo la Jamhuri ya Kenya linajumuisha nchi kavu na maji ya Taifa la Kenya katika tarehe ya kuanza kutekelezwa, na nchi yoyote kavu na yenye maji kama inavyofafanuliwa naSheria ya Bunge.

**6.**

*Ugatuzi na upataji huduma.*

(1) Eneo la Kenya limegawanywa katika kaunti zilizotajwa katika Ambatisho la Kwanza.

(2) Serikali katika ngazi za kitaifa na kaunti ni tofauti na zinategemeana na zitahusiana kwenye msingi wa mashauriano na ushirikiano.



SIO YA KUUZWA

(3) Idara ya Serikali ya kitaifa itahakikisha upatikanaji bora wa huduma zake katika sehemu zote za Jamhuri, kwa njia inayofaa na kulingana na hali ya huduma.

**7.**

*Lugha ya taifa, lugha rasmi na lugha zingine.*

(1) Lugha ya kitaifa ya Jamhuri ni Kiswahili.

(2) Lugha rasmi za Jamhuri ya Kenya ni Kiswahili na Kiingereza.

(3) Serikali––

a) itakuza na kulinda utofauti wa lugha za wananchi wa Kenya; na

b) itakuza ustawi na matumizi ya lugha za kiasili, Lugha ya Ishara ya Kenya, Breli na njia zingine za mawasiliano na teknolojia zinazoweza kufikiwa na watu wenye ulemavu.

**8.** Hakutakuwa na dini ya Taifa.

**9.**

*Nchi na dini. Nembo za kitaifa na Siku za kitaifa*

(1) Nembo za kitaifa za Jamhuri ni––

a) bendera ya taifa;

b) wimbo wa taifa;

c) nembo ya kitaifa inayoashiria mamlaka ya uhuru wa kujitawala; na

d) muhuri wa serikali.

(2) Nembo za kitaifa ni kama zilivyotajwa katika Ambatisho la Pili.

(3) Siku za kitaifa ni––

a) Siku ya Madaraka, itakayoadhimishwa tarehe 1 Juni;

b) Siku ya Mashujaa, itakayoadhimishwa tarehe 20 Oktoba; na

c) Siku ya Jamhuri, itakayoadhimishwa tarehe 12 Desemba.



*SIO YA KUUZWA*

(4) Siku ya kitaifa itakuwa siku ya mapumziko kote nchini.

(5) Bunge linaweza kupitisha sheria itakayoweka siku zingine zitakazokuwa siku za kitaifa na kuelekeza jinsi siku hizo zitakavyoadhimishwa.

**10.**

*Maadili ya kitaifa na kanuni za utawala.*

(1) Maadili ya kitaifa na kanuni za utawala katika Kifungu hiki ni lazima yafuatwe na idara zote za Serikali, maafisa wote wa Serikali, maafisa wa umma na watu wote kila wakati––

a) wanapotekeleza au kufasiri Katiba hii;

b) wanapopitisha, tekeleza au kufasiri sheria yoyote; au

c) wanapotunga, au kutekeleza maamuzi kuhusu sera za umma.

(2) Maadili ya kitaifa na kanuni za utawala zinajumuisha––

a) uzalendo, umoja wa kitaifa, kushirikiana na ugatuzi wa mamlaka, utawala wa sheria, demokrasia na kushiriki kwa watu;

b) heshima kwa binadamu, usawa, haki za jamii, kushirikishwa, haki za binadamu, kutobaguliwa na kulindwa kwa jamii za watu waliotengwa;

c) utawala mwema, uadilifu, uwazi na uwajibikaji; na

d) maendeleo endelevu.

**11.**

*Utamaduni.*

(1) Katiba hii inatambua utamaduni kuwa msingi wa taifa na ustaarabu wa kijumla wa taifa na watu wa Kenya.

(2) Serikali—



SIO YA KUUZWA

a) itakuza aina zote za kujieleza kitaifa na kitamaduni kupitia fasihi, sanaa, sherehe za kitamaduni, sayansi,

b) mawasiliano, habari, vyombo vya habari, uchapishaji, maktaba na urithi mwingine wa kitamaduni;

c) itatambua jukumu la sayansi na teknolojia za kiasili katika maendeleo ya nchi; na

d) itatambua haki za kiubunifu za watu wa Kenya.

(3) Bunge litatunga sheria ili—

a) kuhakikisha kwamba jamii zinapokea fidia au mrabaha kwa kutumiwa kwa tamaduni zao na urithi wao wa kitamaduni; na

b) kutambua na kulinda umiliki wa mbegu na mimea mbalimbali ya kiasili, hali zao tofauti za kimaumbile na matumizi yake miongoni mwa jamii za Kenya.

## SURA YA TATU—URAIA

**12.**

*Haki za raia.*

(1) Kila raia anastahiki––

a) kupata haki, fadhila na manufaa ya uraia kulingana na udhibiti uliowekwa au kama inavyoruhusiwa na Katiba hii; na

b) kupata pasipoti ya Kenya na hati yoyote ya usajili au utambulisho unaotolewa na Taifa kwa raia.

(2) Pasipoti au hati nyingine inayorejelewa katika ibara ya (1) (b) inaweza kutopeanwa kwa mtu, matumizi yake kusimamishwa au kupokonywa tu kulingana na Sheria ya Bunge ambayo inatosheleza vigezo vilivyotajwa katika Kifungu cha 24.

**13.**

*Kupata na kudumisha uraia.*

(1) Kila mtu ambaye alikuwa raia kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba hii atadumisha hali ya uraia wake kufikia tarehe hiyo.

(2) Uraia unaweza kupatikana kwa kuzaliwa au kwa kusajiliwa.

(3) Uraia haupotezwi kupitia kwa ndoa au kuvunjika kwa ndoa.

**14.**

*Uraia kwa kuzaliwa.*

(1) Mtu ni raia kwa kuzaliwa ikiwa katika siku yake ya kuzaliwa, bila kujalisha ikiwa mtu huyo amezaliwa nchini Kenya, baba au mama wa mtu huyo ni raia.

(2) Ibara ya (1) pia inatumika kwa mtu ambaye amezaliwa kabla ya tarehe ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii, bila kujalisha iwapo mtu huyo alizaliwa nchini Kenya, ikiwa mama au baba ya mtu huyo ni raia, au alikuwa raia.

(3) Bunge linaweza kutunga sheria ili kudhibiti athari za sehemu ya (1) na (2) kwa vizazi vya raia wa Kenya ambao wamezaliwa nje ya Kenya.

(4) Mtoto anayepatikana nchini Kenya ambaye anaonekana kuwa mwenye umri wa chini ya miaka nane, na ambaye uraia wake na wazazi wake hawajulikani, atachukuliwa kuwa raia wa Kenya kwa kuzaliwa.

(5) Mtu ambaye ni raia wa Kenya kwa kuzaliwa na ambaye katika tarehe ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii, amekoma kuwa raia wa Kenya kwa sababu mtu huyo alipata uraia wa nchi nyingine ana haki ya kurejeshewa uraia wa Kenya, kwakutuma ombi.

**15.**

*Uraia kwa kujiandikisha.*

(1) Mtu ambaye ameolewa na raia wa Kenya au ameoa raia wa Kenya kwa muda wa angalau miaka saba ana haki ya kusajiliwa kama raia kwa kutuma ombi.

(2) Mtu ambaye amekuwa mkazi nchini Kenya kihalali kwa muda wa miaka saba mfululizo, na ambaye anatimiza masharti yote yaliyotolewa na Sheria ya Bunge, anaweza kutuma ombi ili kusajiliwa kama raia.

(3) Mtoto ambaye si raia wa Kenya, lakini anapewa malezi na raia, ana haki ya kusajiliwa kama raia atumapo ombi.

(4) Bunge litatunga sheria itakayotoa masharti ambayo yatazingatiwa ili kuwapa uraia watu binafsi ambao ni raia wa nchi zingine.

(5) Kifungu hiki kinatumika kwa mtu kuanzia tarehe ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii, lakini mahitaji yoyote ambayo ni lazima yatimizwe kabla ya mtu huyo kustahiki ili kusajiliwa kama raia, yatachukuliwa kuwa yametimizwa pasi na kuzingatia ikiwa mtu huyu aliyatimiza kabla au baada ya tarehe ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii, au kwa kiwango fulani kabla, na kwa kiwango fulani baada ya tarehe ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii.

*Uraia wa nchi mbili.*

**16.** Mtu ambaye ni raia kwa kuzaliwa hapotezi uraia wake kwa sababu ya kupata uraia wa nchi nyingine.

*Kuondolewa kwa uraia.*

**17.**

(1) Iwapo mtu amepata uraia kwa kusajiliwa, uraia huo unaweza kufutiliwa mbali ikiwa mtu huyo––

a) alipata uraia huo kwa njia ya ulaghai, udanganyifu au kuficha ukweli wa maelezo yoyote husika;

b) alifanya biashara isiyo halali au kuwasiliana na adui wakati wa vita ambavyo Kenya ilihusika, amejihusisha au kushiriki katika biashara ambayo ilifanywa kwa njia ya kumsaidia adui katika vita hivyo;

c) katika kipindi cha miaka mitano baada ya



SIO YA KUUZWA

kusajiliwa, amepatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo cha miaka mitatu au zaidi; au

d) kwa wakati wowote ule baada ya kusajiliwa, amepatikana na hatia ya uhaini au hatia ambayo––

i. hukumu ya angalau miaka saba gerezani inaweza kutolewa; au

ii. hukumu kali zaidi inaweza kutolewa.

(2) Uraia wa mtu ambaye alichukuliwa kuwa raia kwa kuzaliwa, kama inavyobainiwa katika Kifungu cha 14 (4), unaweza kufutiliwa mbali ikiwa–

a) uraia huo ulipatikana kwa njia ya ulaghai, udanganyifu au kwa kuficha ukweli wa maelezo yoyote husika;

b) uraia au kuzaliwa kwa mtu huyo kunajulikana na kunafichua kwamba mtu huyo alikuwa raia wa nchi nyingine; au

c) umri wa mtu huyo unajulikana na unafichua kwamba alikuwa na umri wa zaidi ya miaka nane alipopatikana nchini Kenya.

*Sheria kuhusu uraia.*

**18.** Bunge litatunga sheria—

a) itakayoeleza taratibu ambazo kupitia kwazo mtu anaweza kuwa raia;

b) itakayosimamia uingiaji na makazi nchini Kenya;

c) itakayoeleza kuhusu hali ya wakazi wa kudumu;

d) itakayoeleza kuhusu kuwacha uraia kwa hiari;

e) itakayoeleza mchakato wa kufutiliwa mbali kwa kwa uraia;

f) itakayoeleza majukumu na haki za raia; na

g) kijumla, kuwezesha utekelezaji wa vifungu vya Sura hii.



SIO YA KUUZWA

# SURA YA NNE—SHERIA ZA HAKI

## Sehemu ya 1—Vifungu vya Kijumla Vinavyohusiana na Sheria za Haki

**19.**

*Haki na uhuru wa kimsingi.*

(1) Sheria za Haki ni kiungo muhimu katika utawala wa kidemokrasia nchini Kenya na ndio msingi wa sera za kijamii kiuchumi na kitamaduni.

(2) Lengo la kutambua na kulinda haki za binadamu na uhuru wa kimsingi ni ili kulinda hadhi ya watu binafsi na jamii tofauti na kukuza haki za kijamii na kufanikisha uwezo wa binadamu wote.

(3) Haki na uhuru wa kimsingi katika Sheria za Haki—

a) ni za kila mtu na wala hazitolewi na Serikali;

b) hazitengi haki zingine na uhuru wa kimsingi ambazo haziko katika Sheria za Haki, lakini zinazotambuliwa au kutolewa na sheria, isipokuwa kwa kiwango ambacho haki hizo na uhuru haziambatani na Sura hii; na

c) zinadhibitiwa tu kulingana na udhibiti uliobainiwa katika Katiba hii.

**20.**

*Matumizi ya Sheria za Haki.*

(1) Sheria za Haki zinatumika katika sheria zote na ni lazima zifuatwe na idara zote za Serikali pamoja na watu wote.

(2) Kila mtu atafurahia haki na uhuru wa kimsingi zilizo katika Sheria za Haki kwa kiwango kikubwa iwezekanavyo, kulingana na hali ya haki hiyo au uhuru huo wa kimsingi.

(3) Katika kufasiri kifungu cha Sheria za Haki, mahakama—

a) itakuza sheria kwa kiwango ambacho kitawezesha utekelezaji wa haki au uhuru wa kimsingi; na

b) itachukua fasiri inayopendelea utekelezaji wa haki au uhuru wa kimsingi kwa kiwango kikubwa.

(4) Katika kufasiri Sheria za Haki, mahakama, taasisi iliyo na mamlaka ya mahakama au mamlaka nyingine itakuza––

a) maadili ya kimsingi katika jamii iliyo wazi na ya kidemokrasia, kwenye misingi ya hadhi ya binadamu, usawa na uhuru; na

b) kusudi, madhumuni na malengo ya Sheria za Haki.

(5) Katika utekelezaji wa haki yoyote chini ya Kifungu cha 43, ikiwa Serikali itadai kwamba haina rasilimali za kutekelezea haki hiyo, mahakama, taasisi iliyo na mamlaka ya mahakama au mamlaka nyingine itaongozwa na kanuni zifuatazo––

a) ni jukumu la Serikali kuonesha kwamba rasilimali hazipatikani;

b) katika kugawa rasilimali, Serikali itaweka kipaumbele jukumu la kuhakikisha kwamba kuna manufaa makubwa zaidi ya haki hiyo au uhuru huo wa kimsingi, kulingana na hali ilivyo, ikijumuisha unyonge wa vikundi fulani vya watu au watu binafsi; na

c) mahakama, taasisi iliyo na mamlaka ya mahakama au mamlaka nyingine haiwezi kuingilia uamuzi wa idara ya Serikali kuhusu ugavi wa rasilimali zinazopatikana, hasa kwenye misingi kwamba ingefikia uamuzi tofauti.

**21.**

*Utekelezaji wa haki na uhuru wa kimsingi.*

(1) Ni wajibu wa kimsingi wa Serikali na kila idara ya Serikali kuzingatia, kuheshimu, kulinda, kukuza na kutimiza haki na uhuru wa kimsingi katika Sheria za Haki.



SIO YA KUUZWA

(2) Serikali itachukua hatua za kisheria, kisera na nyinginezo ikijumuisha uwekaji wa viwango ili kufanikisha upatikanaji endelevu wa haki hizo kama ilivyohakikishwa chini ya Kifungu cha 43.

(3) Ni wajibu wa idara zote za Serikali na maafisa wote wa umma kushughulikia mahitaji ya makundi ya watu walio hatarini katika jamii, ikijumuisha wanawake, wazee katika jamii, watu wenye ulemavu, watoto, vijana na jamii za walio wachache au zilizotengwa, pamoja na jamii fulani za kikabila, kidini au kitamaduni.

(4) Serikali itatunga na kutekeleza sheria ili kutimiza wajibu wake wa kimataifa kuhusu haki za binadamu na uhuru wa kimsingi.

**22.**

*Utekelezaji wa Sheria za Haki.*

(1) Kila mtu ana haki ya kuwasilisha kesi mahakamani akidai kwamba amenyimwa haki au uhuru wa kimsingi katika Sheria za Haki, kwamba haki au uhuru huo umekiukwa au kutishiwa.

(2) Zaidi ya mtu kuwasilisha kesi kwa niaba yake mwenyewe, kesi chini ya sehemu ya (1) inaweza kuwasilishwa na––

a) mtu anayewasilisha kesi kwa niaba ya mtu mwingine ambaye hawezi kuwasilisha kesi kwa jina lake mwenyewe;

b) mtu anayewasilisha kesi kwa niaba ya, au kama mwanachama wa kikundi au tabaka la watu;

c) mtu anayewasilisha kesi kwa manufaa ya umma; au

d) shirika linalowasilisha kesi kwa manufaa ya mwanachama mmoja au zaidi.

(3) Jaji Mkuu atatunga kanuni zitakazotoa mwongozo

katika kesi zilizorejelewa katika Kifungu hiki, ambazo zitatimiza vigezo kwamba––

a) haki za kuwasilisha kesi zilizotolewa katika sehemu ya (2) zinatekelezwa kikamilifu;

b) hali rasmi zinazohusiana na kesi hizo, ikijumuisha kuanzishwa kwa kesi, unawekwa kwa kiwango cha chini, na hasa kwamba iwapo ni muhimu, mahakama itakubali kuendeshwa kwa kesi kwenye msingi wa hati na rekodi zisizo rasmi;

c) hakuna ada itakayotozwa kwa kuanzisha kesi;

d) kwa kuzingatia kanuni za haki ya kimsingi, mahakama haitazuiwa na mahitaji madogo madogo ya utaratibu; na

e) shirika au mtu binafsi mwenye ujuzi maalum anaweza, kwa idhini ya mahakama, kujitokeza kama msaidizi wa mahakama katika kutatua maswala ya kisheria.

(4) Kukosekana kwa kanuni zinazoangaziwa katika sehemu ya (3) hakutadhibiti haki ya mtu yeyote ya kuwasilisha kesi mahakamani chini ya Kifungu hiki, na mahakama kuisikiza na kuiamua kesi hiyo.

**23.**

*Mamlaka ya mahakama katika kudumisha na kutekeleza Sheria za Haki.*

(1) Kwa mujibu wa Kifungu cha 165, Mahakama Kuu ina mamlaka ya kusikiliza na kuamua kesi zinazoomba haki dhidi ya kunyimwa, kukiukwa, kuvunjwa au kutishiwa kwa haki au uhuru wa kimsingi katika Sheria za Haki.

(2) Bunge litatunga sheria ili kutoa uwezo wa kiasili kwa mahakama za ngazi ya chini katika usikilizaji na kuamuliwa kwa kesi zinazoomba haki dhidi ya kunyimwa, kuvunjwa, kukiukwa au kutishiwa kwa haki au uhuru wa kimsingi katika Sheria za Haki.



SIO YA KUUZWA

(3) Katika kesi yoyote iliyowasilishwa chini ya Kifungu cha 22, mahakama inaweza kutoa uamuzi unaofaa, ikijumuisha––

a) kutangaza haki;

b) kutoa amri ya kusitisha kitendo kinachokiuka haki za mtu aliyewasilisha kesi;

c) kutoa amri ya kudumisha hali jinsi ilivyo;

d) kutoa tangazo au tamko kuhusu ubatili wa sheria yoyote ambayo inanyima, inakiuka au kutishia haki au uhuru wa kimsingi katika Sheria za Haki na ambayo haijathibitishwa kulingana na Kifungu cha 24;

e) amri ya fidia; na

f) amri ya mahakama ya kukagua hatua za kitawala zilizochukuliwa na shirika la umma.

**24.**

*Udhibiti wa haki au uhuru wa kimsingi.*

(1) Haki au uhuru wa kimsingi katika Sheria za Haki hazitadhibitiwa isipokuwa kulingana na sheria, na kwa kiwango ambacho kinafaa katika jamii iliyo wazi na ya kidemokrasia, na iliyo kwenye misingi ya hadhi ya binadamu, usawa na uhuru, na kwa kuzingatia maswala yote husika ikijumuisha––

a) hali ya haki hiyo au uhuru huo wa kimsingi;

b) umuhimu wa lengo la udhibiti huo;

c) hali na kiwango cha udhibiti huo;

d) umuhimu wa kuhakikisha kwamba kutekelezwa kwa haki hizo na uhuru huo wa kibinafsi wa mtu yeyote hautatizi haki na uhuru wa kimsingi wa watu wengine; na

e) uhusiano kati ya udhibiti huo na lengo lake, na ikiwa kuna njia zingine ambazo hazidhibiti sana na ambazo zinaweza kufikia lengo hilo.



SIO YA KUUZWA

(2) Licha ya sehemu ya (1), kifungu katika sheria kinachodhibiti haki au uhuru wa kimsingi—

a) ikiwa ni kifungu kilichotungwa au kurekebishwa katika, au baada ya siku ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, kifungu hicho sio halali, isipokuwa sheria hiyo idhihirishe kusudi la kudhibiti haki hiyo au uhuru huo wa kimsingi na kiwango cha udhibiti huo;

b) hakitachukuliwa kuwa kinadhibiti haki hiyo au uhuru huo isipokuwa kieleze wazi na kwa njia maalum kuhusu haki au uhuru wa kimsingi unaodhibitiwa na hali au kiwango cha udhibiti huo; na

c) hakitadhibiti haki au uhuru wa kimsingi kwa njia itakayotofautiana na maudhui muhimu ya haki au uhuru huo wa kimsingi.

(3) Serikali au mtu anayetaka kuhalalisha udhibiti fulani atathibitishia mahakama, taasisi iliyo na mamlaka ya mahakama au mamlaka nyingine kwamba mahitaji ya Kifungu hiki yameridhishwa.

(4) Vifungu katika Sura hii kuhusu usawa vitadhibitiwa katika utekelezaji wa Sheria ya Kiislamu katika mahakama za Kadhi kwa waumini wa dini ya Kiislamu, katika maswala yanayohusiana na hadhi zao za kibinafsi, hali ya ndoa, talaka na urithi.

(5) Licha ya sehemu za (1) na (2), kifungu katika sheria kinaweza kudhibiti utekelezaji wa haki na uhuru wa kimsingi katika vifungu vifuatavyo, kwa watu wanaohudumu katika Majeshi ya Ulinzi ya Kenya au Huduma ya Kitaifa ya Polisi–

a) 31—Faragha;

b) 36—Uhuru wa kutangamana;



SIO YA KUUZWA

c) 37—Mikutano, maandamano, migomo na maombi;

d) 41—Mahusiano ya kikazi;

e) 43—Haki za kiuchumi na za kijamii; na

f) 49—Haki za waliotiwa mbaroni.

*Haki na uhuru wa Kimsingi na uhuru wa Kimsingi ambao hauwezi kudhibitiwa.*

**25.** Licha ya kifungu kingine chochote katika Katiba hii, haki na uhuru wa kimsingi zifuatazo hazitadhibitiwa––

a) uhuru kutokana na mateso na unyanyasaji au adhabu zinazokiuka hadhi ya ubinadamu;

b) uhuru kutokana na utumwa;

c) haki ya usikilizaji wa kesi kwa usawa; na

d) haki ya kupewa amri ya kufikishwa mahakamani.

**Sehemu ya 2—Haki na Uhuru wa Kimsingi.**

**26.**

*Haki ya kuishi.*

(1) Kila mtu ana haki ya kuishi.

(2) Maisha ya mtu huanza wakati mimba inapotungwa.

(3) Mtu hatauawa kimakusudi, isipokuwa kwa njia inayoidhinishwa na Katiba hii au kwa sheria nyingine iliyoandikwa;

(4) Uavyaji mimba hauruhusiwi, isipokuwa kwa maoni ya mtaalamu wa masuala ya afya kuwa kuna haja ya matibabu ya dharura, au maisha au afya ya mama imo hatarini, au ukiwa umeidhinishwa na sheria nyingine iliyoandikwa;

**27.**

*Usawa na uhuru kutokana na ubaguzi.*

(1) Kila mtu ni sawa mbele ya sheria, na ana haki ya kulindwa na kupata manufaa sawa ya sheria.

(2) Usawa unajumuisha kufurahia haki zote na uhuru wote wa kimsingi kikamilifu na kwa usawa.



SIO YA KUUZWA

(3) Wanawake na wanaume wana haki ya kuchukuliwa kwa usawa ikijumuisha haki ya kupata nafasi sawa katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na kijamii.

(4) Serikali haitabagua mtu yeyote kwa njia ya moja kwa moja au vinginevyo kwenye misingi yoyote ikijumuisha asili, jinsia, ujauzito, hali ya mtu kindoa, hali ya kiafya, asili ya kikabila au kijamii, rangi, umri, ulemavu, dini, dhamira, imani, utamaduni, mavazi, lugha au kuzaliwa.

(5) Mtu hatambagua mtu mwingine kwa njia ya moja kwa moja au vinginevyo kwenye misingi iliyotajwa au kuelezewa katika ibara ya (4).

(6) Ili kuwezesha utekelezaji kamili wa haki zilizohakikishwa chini ya Kifungu hiki, Serikali itachukua hatua za kisheria na nyinginezo, ikijumuisha programu na sera za vitendo sawazishi ambazo zimebuniwa ili kusawazisha upungufu wowote uliowaathiri watu binafsi au vikundi vya watu kwa sababu ya ubaguzi wa hapo awali.

(7) Hatua yoyote inayochukuliwa chini ya ibara ya (6) itazingatia kikamilifu ili manufaa yoyote yawe kwenye msingi wa hitaji la kweli.

(8) Zaidi ya hatua zinazokusudiwa katika sehemu ya (6), Serikali itachukua hatua za kisheria na nyinginezo ili kutekeleza kanuni inayohitaji kwamba idadi ya watu waliochaguliwa au kuteuliwa katika mashirika yanayoteua au ambayo yanahitaji watu kuchaguliwa haitakuwa na idadi ya jinsia moja inayozidi thuluthi mbili.

*Heshima kwa binadamu.*

**28.** Kila mtu ana hadhi yake ya kiasili na haki ya hadhi hiyo kuheshimiwa na kulindwa.



SIO YA KUUZWA

*Uhuru na usalama wa mtu.*

**29.** Kila mtu ana haki ya uhuru na usalama wake ambao inajumuisha haki ya—

a) kutonyimwa uhuru kiholela au bila sababu;

b) kutozuiliwa bila kushtakiwa mahakamani, isipokuwa wakati wa hali ya dharura, ambapo kuzuiliwa huko lazima kulingane na matakwa ya Kifungu cha 58;

c) kuwa huru kutokana na aina yoyote ya ukatili kutoka kwa umma au watu binafsi;

d) kutoteswa kwa njia yoyote, iwe kimwili au kisaikolojia;

e) kutoadhibiwa kwa njia ya viboko; au

f) kutotendewa au kuadhibiwa kwa njia ya kikatili, inayodhalilisha hadhi ya ubinadamu.

**30.**

*Uhuru kutokana na Utumwa na kazi ya kulazimishwa.*

(1) Hakuna mtu atakayezuiliwa katika utumwa au ukandamizaji.

(2) Hakuna mtu atakayehitajiwa kufanya kazi ya kulazimishwa.

*Faragha.*

**31.** Kila mtu ana haki ya faragha, ambayo inajumuisha haki ya—

a) kutopekuliwa mwilini, na nyumbani au mali yake kutopekuliwa;

b) kutozuiliwa kwa mali yake;

c) maelezo yanayohusiana na familia yake, au masuala yake ya kibinafsi kutohitajiwa au kutofichuliwa ila tu iwapo kuna sababu muhimu; au

d) faragha ya mawasiliano yake kutovunjwa.

**32.**

*Uhuru wa dhamira, dini, imani na maoni.*

(1) Kila mtu ana haki ya uhuru wa kuwa na dhamira, dini, mawazo, imani na maoni..



SIO YA KUUZWA

(2) Kila mtu ana haki ya kufuata dini au imani yoyote kwa njia ya ibada, matendo, mafundisho au maadhimisho, ikijumuisha siku ya ibada, kibinafsi au pamoja na wengine, katika umma au kibinafsi.

(3) Mtu hatanyimwa ufikiaji wa taasisi yoyote, ajira au kituo chochote, au kupokea manufaa ya haki yoyote kwa sababu ya imani au dini yake.

(4) Mtu hatalazimishwa kutenda au kujihusisha na kitendo chochote ambacho ni kinyume na imani au dini yake.

**33.**

*Uhuru wa kujieleza.*

(1) Kila mtu ana haki ya uhuru wa kujieleza ambao unajumuisha—

a) uhuru wa kutafuta, kupokea au kutoa maelezo au maoni;

b) uhuru wa ubunifu wa kisanii; na

c) uhuru wa kiakademia na utafiti wa kisayansi.

(2) Haki ya uhuru wa kujieleza haijumuishi—

a) propaganda za vita;

b) uchochezi unaozua ghasia;

c) matamshi ya chuki; au

d) utetezi kwenye misingi ya chuki ambao—

i. unajumuisha uchochezi wa kikabila, kuwatusi wengine au uchochezi wa kusababisha madhara; au

ii. unaotokana na misingi yoyote ya ubaguzi iliyotajwa au kubainiwa katika Kifungu cha 27 (4).

(3) Katika kutekeleza uhuru wa kujieleza, kila mtu ataheshimu haki na hadhi ya watu wengine.



SIO YA KUUZWA

**34.**

*Uhuru wa vyombo vya habari.*

(1) Uhuru wa vyombo vya habari, ikijumuisha vyombo vya kuchapisha, vya kielektroniki na vinginevyo unahakikishwa, lakini haijumuishi njia yoyote ya kujieleza iliyotajwa katika Kifungu cha 33 (2).

(2) Serikali—

a) haitadhibiti au kuzuia mtu yeyote anayehusika katika utangazaji, uchapishaji au usambazaji wa chapisho lolote au usambazaji wa habari kwa kutumia njia yoyote; au

b) haitamwadhibu mtu yeyote kwa kutoa maoni au mtazamo wake, au kwa sababu ya masuala yaliyomo kwenye matangazo, chapisho au usambazaji.

(3) Utangazaji na vyombo vingine vya habari vya kielektroniki vina uhuru wa kuanzishwa chini ya taratibu za upataji leseni ambazo—

a) ni muhimu ili kudhibiti masafa ya utangazaji wa moja kwa moja na aina zingine za usambazaji wa masafa; na

b) hazidhibitiwi na serikali, au kwa madhumuni ya kisiasa au ya kibiashara.

(4) Vyombo vyote vya habari vinavyomilikiwa na Serikali—

a) vitakuwa huru kuamua kuhusu yaliyomo kwenye habari na matangazo yao au mawasiliano mengine;

b) havitaegemea upande wowote; na

c) vitatoa nafasi sawa ya kuwasilisha mitazamo tofauti na maoni yanayopinga maswala fulani.

(5) Bunge litatunga sheria itakayosimamia kuundwa kwa shirika ambalo—

a) halitadhibitiwa na serikali, madhumuni ya kisiasa au ya kibiashara;

b) litaangazia maslahi ya sehemu zote za jamii; na

c) litaweka viwango vya vyombo vya habari na kudhibiti na kufuatilia ufuataji wa viwango hivyo.

**35.**

*Uhuru wa upataji habari.*

(1) Kila mwananchi ana haki ya kupata—

a) habari au maelezo yaliyo na Serikali ; na

b) habari au maelezo ambayo mtu mwingine anayo na ambayo yanahitajika ili kutekeleza au kulinda haki yoyote au uhuru wowote wa kimsingi.

(2) Kila mtu ana haki ya kudai marekebisho au kufutuliwa mbali kwa habari zozote za uongo au zinazopotosha na ambazo zinamwathiri mtu huyo.

(3) Serikali itachapisha na kutangaza taarifa yoyote muhimu inayoathiri taifa.

**36.**

*Uhuru wa kutangamana.*

(1) Kila mtu ana haki ya uhuru wa kutangamana ambao unajumuisha haki ya kuanzisha, kujiunga na, au kushiriki katika shughuli za muungano wa aina yoyote.

(2) Mtu hatalazimishwa kujiunga na shirika la aina yoyote.

(3) Sheria yoyote inayohitaji usajili wa shirika la aina yoyote itaeleza kwamba—

a) usajili huo hauwezi kuzuiwa au kuondolewa bila sababu maalum; na

b) kutakuwepo haki ya kusikizwa kwa usawa kabla ya usajili huo kufutiliwa mbali.

*Uhuru wa Kukutana, kuandamana, kugoma na kulalamika.*

**37.** Kila mtu ana haki ya kukutana, kuandamana na kuwasilisha maombi au malalamishi yake kwa

mamlaka ya umma iwapo tu atafanya hivyo kwa amani na bila kuwa na silaha.

**38.**

*Haki za kisiasa.*

(1) Kila mwananchi ana uhuru wa kumchagua mtu amtakaye kisiasa, ikijumuisha haki ya—

a) kuunda, au kushiriki katika uundaji wa chama cha kisiasa;

b) kushiriki katika shughuli za chama cha kisiasa, au kusajili wanachama kwa niaba ya chama cha kisiasa; au

c) kupigia kampeni chama cha kisiasa au madhumuni ya kisiasa.

(2) Kila raia ana haki ya kushiriki katika uchaguzi huru, wa haki na unaofanyika mara kwa mara kwenye msingi wa haki ya kupiga kura kwa wote, na uhuru wa wapiga kura kueleza matakwa yao katika—

a) shirika au ofisi yoyote ya umma ambayo wanachama wake huchaguliwa na iliyoundwa chini ya Katiba; au

b) ofisi yoyote au chama chochote cha kisiasa ambacho raia huyo ni mwanachama.

(3) Bila kudhibitiwa kiholela, kila raia mwenye umri wa miaka kumi na nane au zaidi ana haki ya—

a) kusajiliwa kama mpiga kura;

b) kupiga kura ya siri katika uchaguzi wowote au katika kura ya maamuzi; na

c) kugombea wadhifa katika ofisi ya umma, au ofisi katika chama cha kisiasa ambacho raia huyo ni mwanachama na ikiwa atachaguliwa, kutekeleza majukumu ya ofisi hiyo.

**39.**

*Uhuru wa kwenda popote na kuishi popote*

(1) Kila mtu ana haki ya uhuru wa kutembea.

(2) Kila mtu ana haki ya kuondoka nchini Kenya.

(3) Kila raia ana haki ya kuingia, kubaki na kuishi kokote nchini Kenya.

**40.**

*Ulinzi wa haki ya kumiliki mali.*

(1) Kwa kuzingatia Kifungu cha 65, kila mtu ana haki, kibinafsi au kwa kuungana na wengine, kupata na kumiliki mali––

a) ya aina yoyote; na

b) katika sehemu yoyote ya Kenya.

(2) Bunge halitatunga sheria inayoruhusu Serikali au mtu yeyote—

a) kwa udhalimu kumpokonya mtu mali ya aina yoyote au kumnyima mtu haki yake katika mali ya aina yoyote;

b) kumzuia, au kwa njia yoyote kumzuia kufurahia haki yoyote chini ya Kifungu hiki kwenye misingi iliyobainishwa au kutajwa katika Kifungu cha (27) (4).

(3) Serikali haitamzuia mtu kumiliki mali ya aina yoyote, au kuwa na haki katika mali ya aina yoyote isipokuwa kuzuiwa huko—

a) kunatokana na upataji ardhi au manufaa fulani katika ardhi au ubadilishaji wa manufaa fulani ya ardhi au hatimiliki ya ardhi, kulingana na Sura ya Tano; au

b) ni kwa matumizi ya umma au ni kwa manufaa ya umma na kunatekelezwa kulingana na Katiba hii na Sheria yoyote ya Bunge ambayo—

i. inahakikisha malipo ya fidia na ya haki kikamilifu kwa mtu huyo; na

ii. inampa mtu yeyote aliye na manufaa au haki katika mali hiyo haki ya kufikia mahakama ya kisheria.

(4) Sheria hiyo inaweza kuruhusu wakazi wa ardhi iliyopatikana kulingana na sehemu ya (3), ambao huenda hawana hatimiliki ya ardhi hiyo, kufidiwa kwa nia njema.

(5) Serikali itatoa msaada, itakuza na kulinda hakimiliki ya uvumbuzi wa wananchi wa Kenya.

(6) Haki chini ya Kifungu hiki hazijumuishi mali yoyote ambayo ilipatikana kwa njia isiyo halali.

**41.**

*Mahusiano ya kikazi.*

(1) Kila mtu ana haki ya hatua na desturi za kikazi zilizo na usawa.

(2) Kila mfanyakazi ana haki ya—

a) kulipwa kwa haki;

b) mazingira ya kikazi yanayofaa;

c) kuunda, kujiunga au kushiriki katika shughuli na mipango ya chama cha wafanyakazi; na

d) kugoma.

(3) Kila mwajiri ana haki ya—

a) kuunda au kujiunga na shirika la waajiri; na

b) kushiriki katika shughuli na mipango ya shirika la waajiri.

(4) Kila chama cha wafanyakazi na chama cha waajiri kina haki ya—

a) kuamua usimamizi wake, mipango na shughuli zake;

b) kupanga; na

c) kuunda na kujiunga na chama cha wafanyakazi.



SIO YA KUUZWA

(5) Kila chama cha wafanyakazi, shirika la waajiri na mwajiri ana haki ya kushiriki katika maafikiano ya pamoja.

**42.**

*Mazingira.*

(1) Kila mtu ana haki ya mazingira safi na yenye afya, ambayo inajumuisha haki ya—

a) mazingira kutunzwa kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo kupitia kwa hatua za kisheria na nyinginezo, hasa zile ambazo zinakusudiwa katika Kifungu cha 69; na

b) majukumu yanayohusiana na mazingira kutimizwa chini ya Kifungu cha 70.

**43.**

*Haki za kiuchumi na za kijamii.*

(1) Kila mtu ana haki ya—

a) kupata kiwango cha juu zaidi kiwezekanacho cha afya, kinachojumuisha haki ya huduma za kiafya ikijumuisha huduma ya afya ya uzazi;

b) kupata makazi yanayofaa, na viwango vinavyo-stahili vya usafi;

c) kuwa huru kutokana na njaa, na kupata chakula cha kutosha na bora;

d) kupata maji safi na salama kwa viwango vinavyostahili;

e) usalama wa kijamii; na

f) elimu.

(2) Serikali itatoa ulinzi wa kijamii unaofaa kwa watu ambao hawawezi kujisimamia wao wenyewe pamoja na wanaowategemea.

**44.**

*Lugha na Utamaduni*

(1) Kila mtu ana haki ya kutumia lugha na kushiriki katika maisha ya kitamaduni ya chaguo lake.

(2) Mtu anayetoka katika utamaduni au ya lugha fulani, pamoja na wanajamii wenzake, ana haki ya—

a) kufurahia utamaduni wake na kutumia lugha yake; au

b) kuunda, kujiunga na kudumisha vyama vya kitamaduni na kilugha, na vitengo vingine vya wanaharakati wa kijamii.

(3) Hakuna mtu atakayemlazimisha mtu mwingine kutekeleza, kuadhimisha au kupitia katika mila zozote za kitamaduni.

**45.**

*Familia*

(1) Familia ndio kitengo cha asili na cha kimsingi cha jamii na ndio msingi muhimu katika utaratibu wa kijamii, na itafurahia kutambuliwa na kulindwa na Serikali.

(2) Kila mtu mzima ana haki ya kuoa mtu wa jinsia tofauti na yake na kulingana na idhini isiyolazimishwa ya watu hao wawili..

(3) Wanandoa wana haki sawa wakati wa kuoana, katika ndoa na wakati wa kuvunjwa kwa ndoa hiyo.

(4) Bunge litatunga sheria inayotambua—

a) ndoa zilizotekelezwa chini ya utamaduni wowote, au mfumo wowote wa kidini, sheria ya kibinafsi au kifamilia; na

b) mfumo wowote wa sheria ya kibinafsi au kifamilia chini ya utamaduni wowote, au unaofuatwa na waumini wa dini fulani kwa kiwango cha ndoa au mifumo hiyo ya kisheria kuambatana na Katiba hii.

**46.**

*Haki za watumiaji bidhaa na huduma.*

(1) Watumiaji wa bidhaa na huduma wana haki ya—

a) kupata bidhaa na huduma bora;

b) kupata maelezo ambayo ni muhimu kwao ili kupata manufaa kikamilifu kutokana na bidhaa na huduma hizo;

c) kulindwa kwa afya yao, usalama wao, na maslahi yao ya kiuchumi; na

d) kufidiwa kutokana na hasara au madhara yanayotokana na kasoro katika bidhaa au huduma hizo.

(2) Bunge litatunga sheria itakayohakikisha ulinzi wa watumiaji wa bidhaa na huduma, na wa matangazo yenye usawa, ya kweli na mazuri.

(3) Kifungu hiki kinatumika kwa bidhaa na huduma zitakazotolewa na mashirika ya umma au watu binafsi.

**47.**

*Hatua za kiutawala zenye haki.*

(1) Kila mtu ana haki ya hatua za kiutawala ambazo ni za haraka, zenye ufanisi, za kisheria, zifaazo na zenye utaratibu ulio na usawa.

(2) Ikiwa haki au uhuru wa kimsingi wa mtu umeathiriwa au unaweza kuathiriwa na hatua ya kiutawala, mtu huyo ana haki ya kupewa sababu za hatua hiyo

(3) Bunge litatunga sheria ili kuwezesha utekelezaji wa haki katika ibara ya (1) na sheria hiyo—

a) itatoa nafasi ya kukaguliwa kwa hatua hiyo ya kiutawala na mahakama au, ikiwezekana, mahakama maalum ya kiwango cha chini ambayo ni huru na isiyoegemea upande wowote; na

b) itakuza utawala wenye ufanisi.

**48.** Serikali itahakikisha upataji haki kwa watu wote na ikiwa ada yoyote itahitajika, itakuwa ada inayofaa na haitazuia upataji wa haki.

*Upataji wa haki.*

**49.**

*Haki za watu waliotiwa mbaroni.*

(1) Mtu aliyekamatwa ana haki ya—

a) kuarifiwa mara moja na kupitia kwa lugha anayoielewa, kuhusu—



SIO YA KUUZWA

i. sababu ya kukamatwa;

ii. haki ya kunyamaza kimya; na

iii. matokeo ya kutonyamaza kimya;

b) kunyamaza kimya;

c) kuwasiliana na wakili na watu wengine ambao msaada wao unahitajika;

d) kutolazimishwa kukiri au kukubali hatia, ambako kukubali huko kunaweza kutumiwa kama ushahidi dhidi ya mtu huyo;

e) kutenganishwa na watu wanaotumikia vifungo vyao;

f) kuletwa mahakamani haraka iwezekanavyo, lakini sio baada ya––

i. saa ishirini na nne baada ya kukamatwa; au

ii. ikiwa saa hizo ishirini na nne zimekamilika kwa wakati ambapo vikao vya mahakama haviendelei, au kwa siku isiyo ya mahakama, afikishwe mahakamani ifikapo mwisho wa siku ya mahakama inayofuata;

g) afikishwapo mahakamani kwa mara ya kwanza, kufunguliwa mashtaka au kuarifiwa kuhusu sababu ya kuendelea kuzuiliwa kwake, au kuachiliwa huru; na

h) kuachiliwa kwa dhamana, na kuwekewa masharti yanayoeleweka kabla ya kushtakiwa au kabla ya kesi kusikizwa, isipokuwa kukiwa na sababu zingine za kutomwachilia.

(2) Mtu hatazuiliwa katika rumande kwa kosa ikiwa kosa hilo linaweza kuadhibiwa kwa kutozwa faini pekee au kwa kufungwa gerezani kwa muda usiozidi miezi sita.



SIO YA KUUZWA

**50.**

(1) Kila mtu ana haki ya kutaka mzozo wowote unaoweza kusuluhishwa kisheria kuamuliwa katika kikao kilicho wazi na chenye usawa mahakamani au, ikiwezekana, kuamuliwa na taasisi iliyo na mamlaka ya mahakama, iliyo huru na isiyoegemea upande wowote.

(2) Kila mshtakiwa ana haki ya kesi yake kusikizwa kwa njia ya haki, ambayo inajumuisha haki ya—

*Usikilizaji kesi kwa haki.*

a) kuchukuliwa kama asiyekuwa na hatia hadi itakapothibitishwa kuwa ana hatia;

b) kuarifiwa kuhusu mashtaka na kupewa maelezo ya kutosha na yatakayomwezesha kujibu mashtaka hayo;

c) kuwa na wakati na vifaa vya kutosha ili kutayarisha jibu;

d) kesi kusikilizwa kwa njia ya uwazi mbele ya mahakama iliyobuniwa chini ya Katiba hii;

e) kesi kuanzishwa na kukamilishwa pasi na kuchelewa bila sababu;

f) kuwepo wakati wa kesi kusikizwa isipokuwa pale ambapo mienendo ya mshtakiwa inatatiza kuendelea kwa kesi hiyo;

g) kuchagua na kuwakilishwa na wakili, na kuelezwa kuhusu haki hii haraka iwezekanavyo;

h) kuwa na wakili aliyetolewa na Serikali na kwa gharama ya Serikali, ikiwa haki haitatendeka, na aarifiwe kuhusu haki hii haraka iwezekanavyo;

i) kunyamaza kimya na kutotoa ushahidi katika usikilizaji wa kesi;



SIO YA KUUZWA

j) kuelezwa mbeleni kuhusu ushahidi ambao kiongozi wa mashtaka ananuia kutumia, na kuweza kuufikia ushahidi huo;

k) kuleta na kupinga ushahidi;

l) kukataa kutoa ushahidi utakaopelekea yeye kupatikana na hatia;

m) kuwa na usaidizi wa mkalimani bila malipo ikiwa mshtakiwa hawezi kuelewa lugha inayotumiwa katika kesi yake;

n) kutohukumiwa kwa kitendo ambacho kwa wakati wa kutendeka kwake kitendo hicho hakikuwa—

i. kosa nchini Kenya; au

ii. kosa la jinai chini ya sheria ya kimataifa;

o) kutoshtakiwa kwa kosa ambalo mtu huyo amewahi kutenda, kuachiliwa au kuhukumiwa kwalo hapo awali;

p) kunufaika katika kupata adhabu iliyo na ukali wa chini zaidi kati ya adhabu zilizoruhusiwa katika kosa hilo ikiwa adhabu iliyoidhinishwa kwa kosa lake imebadilishwa kati ya muda wa kutendeka kwa kosa hilo na wakati wa kuhukumiwa; na

q) ikiwa atahukumiwa, kukata rufaa au kuwasilisha ombi la kukaguliwa kwa uamuzi huo katika mahakama iliyo katika kiwango cha juu kuliko mahakama iliyotoa uamuzi kama inavyobainishwa na sheria.

(3) Ikiwa Kifungu hiki kinahitaji maelezo au habari kutolewa kwa mtu, maelezo hayo yatatolewa katika lugha ambayo mtu huyo anaelewa.

(4) Ushahidi uliopatikana katika njia inayokiuka haki yoyote au uhuru wowote wa kimsingi katika Sheria



SIO YA KUUZWA

za Haki utatengwa ikiwa mahakama kuukubali ushahidi huo kutapelekea kesi hiyo kutozingatia haki, au kwa namna nyingine ushahidi huo utazuia kutendeka kwa haki.

(5) Mshtakiwa—

a) aliyeshtakiwa kwa kosa fulani, kando na kosa ambalo mahakama inaweza kukamilisha kwa haraka, atakuwa na haki ya kupata nakala ya kumbukumbu ya kesi aombapo nakala hiyo; na

b) ana haki ya kupata nakala ya kumbukumbu ya kesi ndani ya muda unaofaa baada ya kukamilishwa kwa kesi hiyo, na kwa malipo ya ada inayofaa kama ilivyoagizwa na sheria.

(6) Mtu aliyehukumiwa kwa kosa la jinai anaweza kuwasilisha ombi la kusikizwa upya kwa kesi katika mahakama kuu ikiwa––

a) rufaa ya mtu huyo imetupiliwa mbali na mahakama ya juu zaidi ambapo mtu huyo ana haki ya kukata rufaa, au ikiwa mtu huyo hakukata rufaa katika muda unaokubaliwa wa kukata rufaa; na

b) ushahidi mpya na wa kushawishi umepatikana.

(7) Ili haki itendeke, mahakama inaweza kumruhusu mtu tofauti kumsaidia mlalamishi au mshtakiwa ili awasiliane na mahakama.

(8) Kifungu hiki hakizuii kutengwa kwa vyombo vya habari au umma katika kesi yoyote mahakamani, ikiwa kutengwa huko ni muhimu, katika jamii huru na ya kidemokrasia, ili kulinda mashahidi au watu walio hatarini, kulinda maadili, utulivu wa umma, au usalama wa kitaifa.



SIO YA KUUZWA

(9) Bunge litatunga sheria itakayoelezea kuhusu ulinzi, haki na maslahi ya waathiriwa wa hatia.

**51.**

*Haki za walio kizuizini, waliokamatwa au waliofungwa gerezani.*

(1) Mtu yeyote aliyezuiliwa, kukamatwa au kufungwa gerezani kisheria, ana haki zote na uhuru wote wa kimsingi katika Haki za Sheria, isipokuwa iwe kwamba haki au uhuru wowote wa kimsingi hauambatani kamwe na hali kuzuiliwa, kukamatwa au kufungwa gerezani kwa mtu huyo.

(2) Mtu aliyezuiliwa au kukamatwa ana haki ya kuwasilisha ombi la kutolewa kwa amri ya yeye kufikishwa mahakamani.

(3) Bunge litatunga sheria ambayo––

a) inaagiza kuwa walio kizuizini, waliokamatwa au waliofungwa gerezani wapewe hadhi yao ya kibinadamu; na

b) inazingatia mikataba ya kimataifa inayohusiana na haki za binadamu.

**Sehemu ya 3 — Utekelezaji Maalum wa Haki**

**52.**

*Kutumika kwa Sehemu Hii.*

(1) Sehemu hii inafafanua kwa undani baadhi ya haki fulani ili kuhakikisha uhakika zaidi katika utekelezaji wa haki hizo na uhuru huo wa kimsingi katika vikundi fulani vya watu.

(2) Sehemu hii haitachukuliwa kana kwamba inadhibiti haki yoyote.

**53.**

*Watoto*

(1) Kila mtoto ana haki ya––

a) kupata jina na uraia wakati anapozaliwa;

b) kupata elimu ya kimsingi na ya lazima bila malipo;

c) kupata lishe bora ya kimsingi, makazi na huduma za afya;

d) kulindwa kutokana na dhuluma, kutelekezwa, tamaduni mbaya zinazoathiri, aina zote za ukatili, matendo na adhabu zisizo na ubinadamu, na kazi yoyote ya kunyanyasa au yenye kuhatarisha;

e) kutunzwa na kulindwa na wazazi, ambayo inajumuisha wajibu sawa wa mama na baba katika kukidhi mahitaji ya mtoto, bila kujalisha ikiwa wameoana au hawajaoana; na

f) kutozuiliwa, isipokuwa wakati ambapo hilo ndilo hatua pekee inayoweza kuchukuliwa, azuiliwe––

i. kwa muda mfupi zaidi unaostahili; na

ii. kwa kutenganishwa na watu wazima na katika hali inayozingatia umri na jinsia ya mtoto huyo.

(2) Maslahi mema zaidi ya mtoto ni muhimu sana katika kila suala linalomhusu mtoto.

**54.** *Watu wenye ulemavu*

(1) Mtu mwenye ulemavu wowote ana haki ya––

a) kupewa hadhi yake na heshima na kuzungumziwa na kutajwa kwa njia isiyomdunisha;

b) kufikia taasisi za elimu na vifaa vya watu wenye ulemavu vilivyowekwa katika jamii kwa kiwango kinachoambatana na maslahi ya mtu huyo;

c) kufikia ipasavyo maeneo yote, usafiri wa umma na habari au maelezo;

d) kutumia lugha ya ishara, Breli, au njia nyingine mwafaka ya mawasiliano; na

e) kupata nyenzo na vifaa vinavyoweza kumsaidia kukabiliana na matatizo ya ulemavu huo;



SIO YA KUUZWA

(2) Serikali itahakikisha utekelezaji unaoendelea wa kanuni kwamba, angalau asilimia tano ya watu walio katika mashirika ambayo wanachama huchaguliwa au kuteuliwa ni watu wenye ulemavu.

**55.**

*Vijana.*

(1) Serikali itachukua hatua, ikijumuisha programu za hatua sawazishi ili kuhakikisha kwamba vijana

a) wanapata elimu na mafunzo yanayofaa;

b) wana fursa ya kujumuika, kuwakilishwa na kushiriki katika nyanja za kisiasa, kijamii, kiuchumi na nyanja zingine za maisha;

c) wanapata ajira; na

d) wanalindwa kutokana na tamaduni zinazodhuru na kutokana na kunyanyaswa.

*Jamii za watu wachache na watu waliotengwa na kubaguliwa.*

**56.** Serikali itaweka programu za hatua sawazishi zilizokusudiwa kuhakikisha kwamba vikundi vya watu wachache waliotengwa na kubaguliwa—

a) vinashiriki na kuwakilishwa katika uongozi na katika nyanja zote za maisha;

b) vinapewa nafasi maalum katika nyanja za elimu na uchumi;

c) vinapewa nafasi maalum katika upataji wa ajira;

d) vinakuza tamaduni zao, lugha na desturi zao; na

e) vinapata maji, huduma za afya na miundombinu.

*Wazee katika jamii.*

**57.** Serikali itachukua hatua ili kuhakikisha haki za wazee––

a) kushiriki kikamilifu katika masuala ya jamii;

b) kufuatilia ustawi wao wa kibinafsi;

c) kuishi katika hadhi na heshima na kuwa huru kutokana na dhuluma; na

d) kupata malezi ya kufaa na msaada kutoka kwa familia zao na Serikali.



SIO YA KUUZWA

**Sehemu ya 4 — Hali ya Dharura**

**58.**

*Hali ya hatari.*

(1) Hali ya dharura inaweza kutangazwa tu chini ya Kifungu cha 132 (4) (d) na wakati ambapo––

a) Nchi inatishiwa na vita, uvamizi, upinzani kijumla,

b) vurugu, janga la kiasili au dharura nyingine ya umma; na

c) tangazo hilo ni muhimu ili kukabili hali ambayo imesababisha kutolewa kwa tangazo hilo la dharura.

(2) Tangazo la hali ya dharura, na sheria yoyote itakayotungwa au hatua nyingine itakayochukuliwa kutokana na tangazo hilo, litafaa tu—

a) ikiwa linalingana na matarajio; na

b) kwa muda usiozidi siku kumi na nne kuanzia siku ya kutangazwa kwa hali hiyo ya dharura, isipokuwa Bunge la Kitaifa liamue kuendeleza tangazo hilo.

(3) Bunge la Kitaifa linaweza kuendeleza tangazo la hali ya hatari —

a) kwa uamuzi uliokubaliwa—

i. kufuatia mjadala wa wazi katika Bunge la Kitaifa; na

ii. na idadi kubwa ya wabunge kama ilivyoelezewa katika sehemu ya (4); na

b) kwa muda usiozidi miezi miwili kwa wakati mmoja.

(4) Kuongezwa kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha hali ya dharura kunahitaji kura ya uungwaji mkono ya angalau thuluthi mbili ya wabunge wote katika



SIO YA KUUZWA

Bunge la Kitaifa, na kuongezwa kwa muda huo kwa mara nyingine kutahitaji kura ya uungwaji mkono ya angalau robo tatu ya wabunge wote katika Bunge la Kitaifa.

(5) Mahakama ya Juu Zaidi inaweza kuamua kuhusu uhalali wa—

a) tangazo la hali ya dharura;

b) kuongezwa kwokwote kwa muda wa tangazo la hali ya dharura;na

c) sheria yoyote itakayotungwa au hatua yoyote nyingine itakayochukuliwa kwa sababu ya tangazo la hali ya dharura.

(6) Sheria yoyote inayotungwa kwa sababu ya tangazo la hali ya dharura––

a) inaweza kudhibiti haki au uhuru wa kimsingi katika Sheria za Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu na Usawa ya Kenya. Haki kwa kiwango tu ambacho—

i. udhibiti huo unahitajika haswa katika dharura hiyo; na

ii. sheria hiyo inaambatana na majukumu ya Jamhuri chini ya sheria za kimataifa zinazotumika katika hali ya dharura; na

b) haitatekelezwa hadi itakapochapishwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali.

(7) Tangazo la hali ya dharura au sheria inayotungwa au hatua yoyote nyingine inayochukuliwa kwa sababu ya tangazo lolote haitaruhusu au kuidhinisha ulinzi dhidi ya mashtaka kwa Serikali au mtu yeyote, katika tendo lolote la ukiukaji wa sheria.



SIO YA KUUZWA

### Sehemu ya 5 — Tume ya Taifa la Kenya Kuhusu Haki za Binadamu na Usawa

**59.**

*Tume ya Taifa ya Kenya ya Haki za Binadamu na Usawa.*

(1) Tume ya Kitaifa ya Kenya ya Haki za Binadamu na Usawa ya Kenya Imebuniwa.

(2) Majukumu ya Tume hii ni—

a) kukuza heshima ya haki za binadamu na kuendeleza desturi ya kuheshimu haki za binadamu katika Jamhuri;

b) kukuza usawa wa kijinsia na usawa kijumla na kuratibu na kuhakikisha jinsia imezingatiwa katika maendeleo ya kitaifa;

c) kukuza ulinzi na kuzingatiwa kwa haki za binadamu katika taasisi za umma na za kibinafsi;

d) kufuatilia, kuchunguza na kuripoti jinsi haki za binadamu zinavyozingatiwa katika nyanja zote za kitaifa ikijumuisha jinsi idara za usalama wa kitaifa zinavyozingatia haki hizo;

e) kupokea na kuchunguza malalamishi kuhusu tuhuma za ukiukaji wa haki na kuchukua hatua za kupata suluhisho lifaalo pale ambapo haki za binadamu zimekiukwa;

f) kwa juhudi zake au kwenye msingi wa malalamishi, kuchunguza au kutafiti kuhusu suala la haki za binadamu, na kutoa mapendekezo ya kuimarisha utendakazi wa idara za Serikali;

g) kutenda kama idara kuu ya Serikali katika kuhakikisha kuwa majukumu chini ya mikataba na maagano yanayohusiana na haki za binadamu yamefikiwa;

h) kuchunguza mienendo yoyote katika masuala ya serikali, au matendo yoyote katika utawala

wa umma na katika nyanja zozote za serikali yanayotuhumiwa au kushukiwa kutokuwa ya haki au kutofaa, au kupelekea hali isiyofaa au kutotendeka kwa haki;

i) kuchunguza malalamishi yoyote kuhusu matumizi mabaya ya mamlaka, matendo yasiyo ya haki, kutotendeka kwa haki au mienendo rasmi isiyokuwa na usawa, inayonyanyasa au isiyoshughulika ipasavyo;

j) kuripoti malalamishi yaliyochunguzwa chini ya aya za (h) na (i) na kuchukua hatua zinazofaa; na

k) kutekeleza majukumu mengine yoyote yalioagizwa na sheria.

(3) Kila mtu ana haki ya kuilalamikia Tume akidai kwamba amenyimwa haki au uhuru wa kimsingi katika Sheria za Haki, kwamba haki au uhuru wa kimsingi umekiukwa, umevunjwa au kutishiwa.

(4) Bunge litatunga sheria ili kuwezesha kikamilifu utekelezaji wa Sehemu hii, na sheria nyingine yoyote kama hiyo inaweza kupanga upya Tume hiyo iwe tume mbili au zaidi tofauti.

(5) Ikiwa Bunge litatunga sheria ya kupanga upya Tume chini ya sehemu ya (4)––

a) sheria hiyo itagawa kila jukumu la Tume iliyotajwa katika Kifungu hiki kwa tume moja au nyingine zinazobuniwa;

b) kila mojawapo ya tume hizi zilizobuniwa itakuwa na mamlaka sawa na ile ya Tume iliyo chini ya Kifungu hiki; na

c) kila tume itakayobuniwa itakuwa tume katika ufafanuzi wa Sura ya Kumi na Tano, na itakuwa na hadhi na mamlaka ya tume chini ya Sura hiyo.

# SURA YA TANO — ARDHI NA MAZINGIRA

### Sehemu ya 1—Ardhi

**60.**

*Kanuni za sera ya ardhi.*

(1) Ardhi nchini Kenya itamilikiwa, kutumiwa na kusimamiwa kwa njia ambayo ni yenye usawa, ufanisi, uzalishaji na endelevu,na kwa kuzingatia kanuni zifuatazo—

a) uwezo sawa wa kupata ardhi;

b) usalama wa haki za ardhi;

c) usimamizi endelevu na wenye manufaa, wa rasilimali za ardhi;

d) usimamizi wa ardhi kwa uwazi na kwa gharama nafuu;

e) hifadhi na utunzaji bora wa maeneo muhimu ya kiekolojia;

f) kuondolewa kwa ubaguzi wa kijinsia katika sheria, mila na desturi zinazohusiana na ardhi na mali iliyomo katika ardhi; na

g) kuhimiza jamii kutatua mizozo kuhusu ardhi kupitia hatua za kijamii zinazotambuliwa na zinazoambatana na Katiba hii.

(2) Kanuni hizi zitatekelezwa kupitia kwa sera ya ardhi ya kitaifa itakayotengenezwa na kukaguliwa mara kwa mara na serikali ya kitaifa kupitia kwa sheria.

**61.**

*Mpangilio wa ardhi.*

(1) Ardhi yote nchini Kenya inamilikiwa na wakenya wote kijumla kama taifa, kama jamii na kama watu binafsi.

(2) Ardhi yote nchini Kenya imeainishwa kama ardhi ya umma, ya jamii au ya mtu binafsi.



SIO YA KUUZWA

**62.**

Ardhi ya umma.

(1) Ardhi ya umma ni—

a) ardhi ambayo ilikuwa inamilikiwa na serikali na ambayo haikuwa imegawanywa wakati wa kuanza kutumika kwa Katiba hii, kama ilivyo-elezewa na Sheria ya Bunge wakati iliyokuwa ikitumika wakati wa kuanza kutumika kwa Katiba hii;

b) ardhi inayomilikiwa, kutumiwa au ambapo idara yoyote ya Serikali inapofanyia kazi, isipokuwa ardhi ambayo idara ya Serikali imekodisha kama mkodishaji wa kibinafsi;

c) ardhi iliyokabidhiwa Serikali kwa njia ya kuuzwa, kurudishwa au kusalimishwa;

d) ardhi ambayo umiliki wake wa kijamii au kib-inafsi hauwezi kuthibitishwa kupitia mchakato wowote wa kisheria;

e) ardhi ambayo hakuna mrithi yeyote anayeweza kutambuliwa kupitia mchakato wowote wa kisheria;

f) ardhi yoyote iliyo na madini au mafuta ya madini kama ilivyoelezewa kisheria;

g) misitu ya serikali isipokuwa misitu inayota-jwa katika Kifungu cha hifadhi za wanyama, chemichemi za maji, mbuga za kitaifa, hifadhi za wanyama za serikali na maeneo maalum yaliyolindwa;

h) barabara zote kulingana na Sheria ya Bunge;

i) mito yote, maziwa yote na sehemu zingine za maji kama ilivyoelezewa na Sheria ya Bunge;

j) mipaka ya bahari, maeneo maalum ya kiuchumi

katika bahari na ardhi iliyo chini ya bahari;

k) Ardhi iliyo chini ya bahari lakini kwenye upande wa bahari usio kuwa wenye kina sana;

l) Ardhi yote iliyo kati ya nyanda za juu na za chini za maji;

m) ardhi yoyote ambayo haijaainishwa kama ya kibinafsi au ya jamii chini ya Katiba hii; na

n) ardhi yoyote iliyotangazwa kuwa ya umma kupitia kwa Sheria ya Bunge—

i. Iliyokuwa ikitumika katika tarehe ya kuanza kutumika kwa katiba hii; au

ii. iliyotungwa baada ya tarehe ya kuanza kutumika kwa katiba hii.

(2) Ardhi ya umma itamilikiwa na serikali ya kaunti kwa niaba ya wakazi katika kaunti hiyo, na itasimamiwa kwa niaba yao na Tume ya Kitaifa ya Ardhi ikiwa imeainishwa chini ya—

a) sehemu ya ibara ya (1) (a), (c), (d) au (e); na

b) sehemu ya (1) (b), isipokuwa ardhi ambayo inamilikiwa au inatumiwa na idara ya Serikali, au ambapo idara ya Serikali inafanyia kazi.

(3) Ardhi ya umma iliyoainishwa chini ya sehemu ya (1) (f) hadi (m) itamilikiwa na serikali ya kitaifa kwa niaba ya Wakenya na Tume ya Kitaifa ya Ardhi itasimamia ardhi hiyo kwa niaba yao.

(4) Ardhi ya umma haitatolewa au kutumiwa isipokuwa kwa kuzingatia Sheria ya Bunge inayofafanua hali na masharti ya kutolewa au matumizi hayo.

**63.**

*Ardhi ya jamii.*

(1) Ardhi ya jamii itamilikiwa na jamii zinazotambuliwa kwa misingi ya kikabila, kitamaduni au mahitaji sawa ya kijamii.



SIO YA KUUZWA

(2) Ardhi ya jamii inajumuisha—

a) ardhi iliyosajiliwa kisheria kwa jina la wawakilishi wa kikundi chini masharti ya sheria yoyote;

b) ardhi iliyokabidhiwa jamii fulani kisheria na kupitia kwa mchakato wowote wa kisheria;

c) ardhi nyingine yoyote itakayotangazwa na Sheria ya Bunge kuwa ardhi ya jamii ; na

d) ardhi ambayo—

i. inamilikiwa kwa uhalali, inasimamiwa au kutumiwa na jamii maalum kama misitu ya jamii, maeneo ya malisho ya mifugo au mahali patakatifu pa ibada;

ii. ni ya kiasili na ardhi ambayo kiasili inamilikiwa na jamii ya wawindaji; au

iii. inamilikiwa kisheria kama ardhi ya amana na serikali za kaunti, lakini isiyojumuisha ardhi yoyote ya umma inayomilikiwa na serikali ya kaunti kwa niaba ya wakazi wa kaunti hiyo chini ya Kifungu cha 62 (2).

(3) Ardhi yoyote ya jamii ambayo haijasajiliwa itamilikiwa na serikali za kaunit kwa niaba ya jamii hizo.

(4) Ardhi ya jamii haitatolewa au kutumiwa vinginevyo isipokuwa kulingana na sheria inayofafanua hali na viwango vya haki za kila mwanajamii kibinafsi au wanajamii wote kwa pamoja.

(5) Bunge litatunga sheria kuwezesha utekelezaji wa Kifungu hiki.

**64.**

*Ardhi ya mtu binafsi.*

(1) Ardhi ya kibinafsi inajumuisha —

a) ardhi yoyote iliyosajiliwa na inayomilikiwa na mtu yeyote chini ya umiliki unaodumu maishani mwa mtu huyo;

b) ardhi inayomilikiwa na mtu yeyote kwa kukodisha; na

c) ardhi yoyote nyingine iliyotangazwa kuwa ya kibinafsi chini ya Sheria ya Bunge.

**65.**

*Umiliki ardhi wa watu wasiokuwa Wakenya.*

(1) Mtu asiyekuwa raia wa Kenya anaweza kumiliki ardhi kwa njia ya kukodisha tu, na makubaliano yoyote ya kukodisha, bila kujalisha yalivyofikiwa, hayatazidi muda wa miaka tisini na tisa.

(2) Ikiwa kifungu katika makubaliano, mkataba au hati yoyote ya aina yoyote inampa mtu asiyekuwa raia wa Kenya uwezo wa kumiliki ardhi kwa zaidi ya miaka tisini na tisa, kifungu hicho kitachukuliwa kumpa mtu huyo umiliki wa miaka tisini na tisa na wala sio zaidi.

(3) Kwa madhumuni ya Kifungu hiki—

a) kampuni au shirika lolote litachukuliwa kama raia tu ikiwa shirika hilo linamilikiwa kikamilifu na raia mmoja au zaidi; na

b) Ardhi inayomilikiwa kwa niaba ya mtu au watu itachukuliwa kuwa inayomilikiwa na raia wa Kenya iwapo tu manufaa yote ya umiliki huo unawaendea watu ambao ni raia wa Kenya.

(4) Bunge linaweza kutunga sheria ili kutoa mwongozo zaidi katika utekelezaji wa Kifungu hiki.

**66.**

*Usimamizi wa matumizi ya ardhi na mali.*

(1) Serikali inaweza kudhibiti matumizi ya ardhi yoyote au haki yoyote katika ardhi kwa madhumuni ya ulinzi, usalama wa umma, utaratibu wa umma, maadili ya umma, afya ya umma, au mpangilio wa matumizi ya ardhi.



SIO YA KUUZWA

(2) Sheria ili kuhakikisha kwamba uwekezaji katika ardhi ni kwa manufaa ya jamii na uchumi wao.

**67.**

*Tume ya Kitaifa ya Ardhi.*

(1) Tume ya Huduma za Polisi za Kitaifa imebuniwa.

(2) Majukumu ya Tume ya Kitaifa ya Ardhi ni—

a) kusimamia ardhi ya umma kwa niaba ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti;

b) kupendekezea serikali ya kitaifa sera ya kitaifa kuhusu ardhi;

c) kushauri serikali ya kitaifa kuhusu programu ya kina itakayosimamia usajili wa umiliki wa ardhi kote nchini Kenya;

d) kufanya utafiti unaohusiana na ardhi na matumizi ya mali-asili, na kutoa mapendekezo kwa mamlaka yanayohusika;

e) kuanzisha uchunguzi kwa hiari yake au kutokana na malalamishi, kuhusu ukiukaji wa sasa wa haki za ardhi au ukiukaji wa kihistoria, na kupendekeza suluhisho linalofaa;

f) kuhimiza matumizi ya njia za kitamaduni zinazotumika kusuluhisha mizozo inayohusu ardhi;

g) kutathmini ushuru unaotozwa katika ardhi na malipo katika majengo yaliyo katika eneo lolote lililoteuliwa kisheria; na

h) kufuatilia na kuwa na jukumu la kusimamia mpangilio wa matumizi ya ardhi kote nchini.

(3) Tume ya Kitaifa ya Ardhi inaweza kutekeleza majukumu mengine yoyote yatakayotolewa na sheria ya kitaifa.

**68.** Bunge—

*Sheria zinazo husu ardhi.*

a) litarekebisha, kuunganisha na kusawazisha sheria zilizopo kuhusu ardhi;

b) litarekebisha sheria za kisekta kuhusu matumizi ya ardhi kulingana na kanuni zilizotajwa katika Kifungu cha 60 (1); na

c) litatunga sheria—

i. ili kutoa mwongozo kuhusu kiwango cha juu zaidi na cha chini zaidi cha ekari za ardhi zinazoweza kumilikiwa katika ardhi ya kibinafsi;

ii. ili kudhibiti njia ambazo ardhi yoyote inaweza kubadilishwa kutoka kwenye mfumo mmoja hadi mwingine;

iii. ili kudhibiti utambuzi na uhifadhi wa mali ya kindoa na hasa nyumba ya kindoa wakati wa ndoa na wakati wa kuvunjwa kwa ndoa hiyo;

iv. ili kulinda, kuhifadhi na kuwezesha ufikiaji wa ardhi yote ya umma;

v. ili kuwezesha kuchunguzwa kwa upataji wote au uhamishaji wote wa umiliki wa ardhi ya umma ili kuthibitisha uhalali wa upataji huo;

vi. ili kuwalinda wategemezi wa marehemu waliomiliki ardhi, ikijumuisha maslahi ya mke au mume wa marehemu ambaye anaishi kwenye ardhi hiyo; na

vii. Ili kutoa mwongozo katika suala lingine lolote muhimu linalohusu kuwezesha utekelezaji wa vifungu vya Sura hii.

**Sehemu ya 2—Mazingira na Mali-Asili**

**69.**

*Majukumu yanayohusiana na mazingira.*

(1) Serikali—

a) itahakikisha matumizi, usimamizi, na uhifadhi wa mazingira na mali-asili unaoendelea na kuhakikisha usawa katika ugavi wa manufaa



SIO YA KUUZWA

yanayopatikana;

b) itafanya juhudi ili kutimiza na kudumisha kupandwa kwa miti katika angalau asilimia kumi ya ardhi ya Kenya;

c) italinda na kukuza haki za uvumbuzi na elimu ya kiasili katika anuwai za viumbe na rasilimali za kiasili za jamii;

d) itahimiza kushiriki kwa umma katika usimamizi, utunzaji, na uhifadhi wa mazingira;

e) italinda rasilmali zote za kiasili na anuwai za viumbe;

f) itaanzisha mifumo ya kutathmini athari kwa mazingira, ukaguzi wa mazingira na usimamizi wa mazingira;

g) itaondoa michakato na shughuli ambazo zinaweza kuhatarisha mazingira; na

h) itatumia mazingira na mali-asili kwa manufaa ya Wakenya.

(2) Kila mtu ana jukumu la kushirikiana na idara za Serikali na watu wengine ili kulinda na kuhifadhi mazingira, na kuhakikisha kuwa kuna maendeleo endelevu ya kiekolojia na ya matumizi ya rasilimali.

**70.**

*Utekelezwaji wa haki za mazingira.*

(1) Ikiwa mtu atadai kuwa haki ya kupata mazingira safi na yenye afya njema inavyotambuliwa na kulindwa chini ya Kifungu cha 42 imekiukwa, inakiukwa au kuna uwezekano mkubwa wa mtu huyo kunyimwa haki hiyo au haki hiyo kukiukwa, kuvunjwa au kutishiwa, mtu huyo anaweza kuwasilisha kesi mahakamani ili kupata fidia pamoja na hatua zingine za kisheria zinazopatikana katika suala hilo.

(2) Ikiwa ombi litawasilishwa chini ya sehemu ya (1),



SIO YA KUUZWA

mahakama inaweza kutoa amri, au kutoa maelekezo yoyote ambayo yanafaa––

a) ili kuzuia, kukomesha au kusitisha tendo au kosa lolote ambalo ni hatari kwa mazingira;

b) ili kumshurutisha afisa yeyote wa umma kuchukua hatua zitakazozuia au kusitisha tendo au kosa lolote ambalo ni hatari kwa mazingira; au

c) kutoa fidia kwa mwathiriwa yeyote aliyeathirika kutokana na ukiukaji wa haki ya kupata mazingira safi na yenye afya njema.

(3) Kwa madhumuni ya Kifungu hiki, sio lazima kwa anayewasilisha ombi kuonyesha kwamba mtu yeyote amepata hasara au kujeruhiwa.

**71.**

*Makubaliano yanayohusiana na mali-asili.*

(1) Lazima makubaliano yapitishwe na Bunge ikiwa––

a) yanajumuisha utoaji wa haki au makubaliano na mtu yeyote, au kwa niaba ya mtu yeyote, ikijumuisha serikali ya kitaifa, kwa mtu mwingine, ili atumie mali-asili yoyote iliyo nchini Kenya; na

b) Yamefikiwa katika au baada ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii.

(2) Bunge litatunga sheria itakayotoa aina za makubaliano ambazo zitakuwa chini ya upitishaji wa Bunge kulingana na sehemu ya (1).

*Sheria zinazohusu mazingira .*

**72.** Bunge litatunga sheria ili kuwezesha utekelezaji wa vifungu katika Sehemu hii.



SIO YA KUUZWA

## SURA YA SITA — UONGOZI NA UADILIFU

**73.**

*Wajibu wa uongozi.*

(1) Mamlaka yaliyotolewa kwa afisa wa Serikali—

a) ni amana ya umma inayopaswa kutekelezwa kwa njia ambayo—

i. inaambatana na madhumuni na malengo ya Katiba hii;

ii. inaonyesha heshima kwa watu;

iii. inaleta sifa njema kwa taifa na heshima kwa ofisi hiyo; na

iv. inakuza imani ya umma katika uadilifu wa ofisi hiyo; na

b) inampa afisa huyo wa Serikali jukumu la kuwahudumia watu, na wala sio mamlaka ya kuwatawala.

(2) Kanuni zinazotoa mwongozo katika uongozi na uadilifu zinajumuisha—

a) uteuzi kwenye misingi ya uadilifu, ustadi kazini na kufaa kwa mtu huyo, au kuchaguliwa katika uchaguzi huru na wa haki;

b) kutopendelea upande wowote katika kufanya maamuzi na katika kuhakikisha kwamba maamuzi hayo hayatokani na mapendeleo ya kindugu, upendeleo, nia zingine zozote mbaya au vitendo vya kifisadi;

c) huduma ya kujitolea kwenye misingi ya manufaa kwa umma, inayoonyeshwa kwa—

i. uaminifu katika utekelezaji wa majukumu ya umma; na

ii. kutangaza maslahi ya kibinafsi yanayoweza kugongana na wajibu wake kwa umma;

d) uwajibikaji kwa umma kuhusu maamuzi na hatua zinazochukuliwa; na

e) nidhamu na kujitolea katika kuwahudumia watu.

*Kiapo cha uaminifu cha Maafisa wa Serikali.*

**74.** Kabla ya kuchukua hatamu katika ofisi ya serikali, au kutekeleza majukumu yoyote katika ofisi ya Serikali, mtu aliyechaguliwa au kuteuliwa ataapa au kukiri kwa uthibitisho kuwa atawajibikia ofisi hiyo, kwa kuzingatia njia iliyopendekezwa na Ambatisho la Tatu, au chini ya Sheria ya Bunge.

*Mienendo ya maafisa wa Serikali.*

**75.**

(1) Afisa wa Serikali atakuwa na mienendo inayokubalika, katika maisha yake ya kirasmi, katika maisha ya kibinafsi, au anapotangamana na watu wengine, na kwa njia ambayo inaepuka—

a) mgongano wowote kati ya maslahi ya kibinafsi na majukumu rasmi au ya umma;

b) kupendelea maslahi ya kibinafsi badala ya maslahi ya umma; au

c) kudunisha hadhi ya ofisi ambayo afisa huyo anasimamia.

(2) Mtu anayekiuka sehemu ya (1), au Kifungu cha 76, 77 au 78 (2)—

a) atawekwa chini ya taratibu za kinidhamu zinazotumika katika ofisi inayohusika;

b) kulingana na taratibu za kinidhamu zinazorejelewa katika aya ya (a), anaweza kuachishwa kazi au kwa njia nyingine kuondolewa ofisini.

(3) Mtu ambaye ameachishwa kazi au vinginevyo kuondolewa ofisini kwa kukiuka masharti yaliyotajwa katika sehemu ya (2) atapigwa marufuku dhidi ya kushikilia ofisi yoyote nyingine ya Serikali.

**76.**

*Uadilifu wa kifedha wa maafisa wa Serikali.*

(1) Zawadi au mchango wowote kwa afisa wa Serikali katika shughuli rasmi au za umma, utakuwa mchango au zawadi kwa Jamhuri na itakabidhiwa Serikali isipokuwa kuwe na Sheria ya Bunge itakayobatilisha hayo.

(2) Afisa wa Serikali—

a) hatamiliki akaunti ya benki nje ya Kenya isipokuwa kulingana na Sheria ya Bunge; au

b) hataomba au kukubali mkopo au manufaa ya kibinafsi katika hali zinazotatiza uadilifu wake.

**77.**

*Udhibiti katika shughuli za maafisa wa Serikali.*

(1) Afisa wa Serikali anayehudumu wakati wote hatashiriki katika ajira nyingine yenye mapato.

(2) Afisa yeyote wa Serikali aliyeteuliwa hatahudumu katika ofisi ya chama cha kisiasa.

(3) Afisa wa Serikali aliyestaafu na anayepokea malipo ya uzeeni kutoka kwenye fedha za umma, hatahudumu katika zaidi ya nyadhifa mbili zilizo na mshahara kwa wakati mmoja kama mwenyekiti, mkurugenzi au mfanyakazi wa—

a) kampuni inayomilikiwa au kudhibitiwa na Serikali; au

b) idara ya Serikali.

(4) Afisa wa Serikali aliyestaafu hatapokea malipo kutoka kwa fedha za umma isipokuwa kama ilivyobainishwa katika sehemu ya (3).

**78.**

*Uraia na uongozi.*

(1) Hakuna mtu anayepaswa kuchaguliwa au kuteuliwa katika ofisi ya Serikali ikiwa si raia wa Kenya.

(2) Afisa wa Serikali au afisa aliye katika vikosi vya ulinzi hatakuwa na uraia wa nchi mbili.



SIO YA KUUZWA

(3) Sehemu za (1) na (2) hazitumiki kwa—

a) majaji na wanachama wa tume; au

b) mtu yeyote ambaye amekuwa raia wa nchi nyingine kupitia kwa utekelezaji wa sheria ya nchi hiyo, na ambaye hana uwezo wa kuondoa uraia huo.

*Sheria ya kuanzisha tume ya maadili na kukabiliana na ufisadi.*

**79.** Bunge litatunga sheria ya kubuniwa kwa tume huru ya maadili na kupambana na ufisadi, ambayo itakuwa na hadhi na mamlaka sawa na tume iliyo chini ya Sura ya Kumi na Tano, kwa madhumuni ya kuhakikisha utimizaji na utekelezaji wa masharti ya Sura hii.

*Sheria zinazohusu uongozi.*

**80.** Bunge litatunga sheria—

a) itakayotoa taratibu na mikakati ya utekelezaji wa Sura hii kwa njia ifaayo;

b) itakayopendekeza adhabu za ziada, kando na zile zinazorejelewa katika Kifungu cha 75, ambazo zinaweza kuamriwa kwa sababu ya ukiukaji wa Sura hii;

c) itakayotoa mwongozo wa utekelezaji wa Sura hii kwa maafisa wa umma, pamoja na marekebisho yanayohitajika; na

d) Itakayotoa mwongozo wowote mwingine unaohitajika ili kuhakikisha ukuzaji wa kanuni za uongozi na uadilifu zilizotajwa katika Sura hii, na utekelezaji wa Sura hii.

# SURA YA SABA — UWAKILISHAJI WA WATU

### Sehemu ya 1 — Mfumo na Mchakato wa Uchaguzi

*Kanuni za kijumla za mfumo wa uchaguzi.*

**81.** Mfumo wa uchaguzi utazingatia kanuni zifuatazo––

a) uhuru wa raia wa kutekeleza haki zao za kisiasa chini ya sehemu ya 38;

b) katika mashirika ya umma ambayo wanachama huchaguliwa,wanachama wa jinsia moja hawatazidi theluthi mbili;

c) uwakilishi wa watu wenye ulemavu kwa njia yenye usawa;

d) haki ya kupiga kura kwa wote kwenye msingi wa uwakilishaji wenye usawa na usawa wa kura; na

e) uchaguzi huru na wenye usawa, ambao ni—

i. wa kura ya siri;

ii. huru na usio na ghasia, vitisho, ushawishi usiofaa, au ufisadi;

iii. unaosimamiwa na tume huru;

iv. wenye uwazi; na

v. unaoendeshwa kwa njia isiyo na upendeleo, yenye ufanisi, sahihi na iliyo na uwajibikaji.

*Sheria ya uchaguzi*

**82.**

(1) Bunge litatunga sheria ya kutoa mwongozo katika—

a) ugawaji wa maeneo ya upigaji kura wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka kwa sababu ya uchaguzi wa wabunge katika Bunge la Kitaifa na wawakilishi wadi katika bunge za kaunti;

b) uteuzi wa wagombea viti;

c) usajili unaoendelea wa raia kama wapiga kura;

d) usimamizi wenye ufanisi na udhibiti katika uchaguzi na kura za maoni, ikijumuisha uteuzi wa wagombea katika uchaguzi; na

e) usajili unaoendelea wa raia wanaoishi nje ya Kenya kama wapiga kura, na utekelezaji unaoendelea wa haki zao za kupiga kura.

(2) Sheria inayotakiwakatika ibara ya (1) (d) itahakikisha kwamba upigaji kura katika kila uchaguzi ni—

a) rahisi;

b) wenye uwazi; na

c) unazingatia mahitaji maalumu ya—

i. watu wenye ulemavu; na

ii. watu wengine au jamii za watu walio na mahitaji maalum.

**83.**

*Kusajiliwa kama mpiga kura*

(1) Mtu anastahiki kusajiliwa kama mpiga kura katika uchaguzi au kura za maamuzi ikiwa mtu huyo—

a) ni raia ambaye ni mtu mzima;

b) hajatangazwa kuwa mtu mwenye akili punguani; na

c) hajapatikana na hatia ya uchaguzi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

(2) Raia anayestahiki kusajiliwa kama mpiga kura atasajiliwa katika kituo kimoja tu cha usajili wa kupigia kura.

(3) Mipango ya kiusimamizi katika usajili wa wapiga kura na uendeshaji wa uchaguzi, itapangwa ili kuwezesha, na haitamnyima raia yeyote anayestahiki haki ya kupiga kura au kugombea kiti.

*Wagombea viti katika uchaguzi na vyama vya kisiasa kuzingatia kanuni za maadili.*

**84.** katika kila uchaguzi, wagombea wote na vyama vyote vya kisiasa vitazingatia kanuni za upigaji kura zilizowekwa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka.

*Ustahiki wa kusimama kama mgombea wa kibinafsi*

**85.** Mtu yeyote anastahiki kusimama kama mgombea huru katika uchaguzi, ikiwa mtu huyo––

a) si mwanachama katika chama cha kisiasa kilichosajiliwa na hajakuwa mwanachama kwa angalau miezi mitatu kabla ya tarehe ya uchaguzi; na

b) anatimiza mahitaji ya––

i. Kifungu cha 99 (1) (c) (i) au (ii), ikiwa ni mgombea katika uchaguzi wa wabunge katika Bunge la Kitaifa au Seneti, mtawalia; au

ii. Kifungu cha 193 (1) (c) (ii), ikiwa ni mgombea katika uchaguzi wa wawakilishi wadi katika bunge la kaunti.

*Upigaji kura.*

**86.** Katika kila uchaguzi, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka itahakikisha kwamba—

(1) bila kujalisha njia ya upigaji kura itakayotumiwa, mfumo huo una urahisi, ni sahihi, unaoweza kuthibitishwa, ulio salama, unaowajibika na ulio na uwazi;

(2) kura zinazopigwa zinahesabiwa, zinaorodheshwa na matokeo yanatangazwa mara moja na afisa msimamizi katika kila kituo cha upigaji kura;

(3) matokeo kutoka vituo vya upigaji kura yanajumlishwa kwa uwazi na kwa usahihi na kisha kutangazwa mara moja na afisa msimamizi katika kituo cha upigaji kura; na

(4) miundo na taratibu mwafaka zimewekwa ili kuondoa ukiukaji wa kanuni na sheria za uchaguzi, ikijumuisha uhifadhi salama wa vifaa vya uchaguzi.

**87.**

*Mizozo ya uchaguzi.*

(1) Bunge litatunga sheria ili kuweka taratibu za kusuluhishwa kwa mizozo ya uchaguzi katika muda unaofaa.

(2) Malalamishi kuhusu uchaguzi, isipokuwa uchaguzi wa urais, yatawasilishwa ndani ya siku ishirini na nane baada ya Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka kutangaza matokeo ya uchaguzi.

(3) Ufikishaji wa malalamishi unaweza kuwa wa moja kwa moja au kwa njia ya kutangazwa katika gazeti la kitaifa.

**Sehemu ya 2—Tume Huru ya Uchaguzi na Kuwekea Mipaka Maeneo ya Upigaji Kura**

**88.**

*Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (Kifungu cha.*

(1) Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka Imeundwa.

(2) Mtu hastahiki kuteuliwa kama mwanachama wa Tume ikiwa mtu huyo—

a) ndani ya miaka mitano iliyopita, amehudumu au kugombea kiti kama—

i. mbunge katika Bunge la Kitaifa au mwakilishi wadi katika bunge la kaunti; au

ii. mwanachama katika idara ya uongozi wa chama cha kisiasa; au

b) anahudumu katika ofisi yoyote ya Serikali.

(3) Mwanachama wa Tume hatahudumu katika ofisi nyingine ya umma.

(4) Tume ina wajibu wa kuendesha na kusimamia kura za maamuzi na uchaguzi katika shirika lolote ambalo wanachama wake wanachaguliwa au katika ofisi chini ya Katiba hii, na uchaguzi mwingine wowote kama ilivyoagizwa katika Sheria ya Bunge, na katika—

a) usajili unaoendelea wa raia kama wapiga kura;

b) ukaguzi wa mara kwa mara wa sajili ya wapiga kura;

c) uwekaji mipaka katika maeneo bunge na wadi;

d) kudhibiti mchakato ambao vyama hutumia katika kuteua wagombea wa uchaguzi;

e) kusuluhisha mizozo ya uchaguzi, ikijumuisha mizozo inayohusiana au kutokana na uteuzi lakini isiyohusisha malalamishi kuhusu uchaguzi na mizozo inayotokana na kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi;

f) usajili wa wagombea wa uchaguzi;

g) elimu kwa wapiga kura;

h) kuwezesha uchunguzi, usimamizi na tathmini ya uchaguzi;

i) udhibiti wa kiwango cha fedha kinachoweza kutumiwa na mgombea au kwa niaba yake, au na chama katika uchaguzi wowote;

j) uundaji wa kanuni za uchaguzi kwa wagombea na vyama vinavyogombea katika uchaguzi; na

k) ufuatiliaji kuhusu ufuataji wa sheria inavyohitajika chini ya Kifungu cha 82 (1) (b) kuhusiana na uteuzi wa wagombea katika vyama.

(5) Tume itatumia mamlaka yake kutekeleza majukumu yake kulingana na Katiba hii na sheria ya kitaifa.

**89.**

*Uwekaji mipaka katika maeneo ya uchaguzi.*

(1) Kutakuwa na maeneo bunge mia mbili tisini kwa madhumuni ya uchaguzi wa wabunge katika Bunge la Kitaifa kama ilivyoagizwa katika Kifungu cha 97 (1) (a).

(2) Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka itakagua majina na mipaka ya maeneo bunge kila baada ya muda usiopungua miaka nane na usiozidi miaka kumi na miwili, lakini ukaguzi wowote utakamilishwa angalau miezi kumi na miwili kabla ya uchaguzi mkuu wa wabunge.



SIO YA KUUZWA

(3) Tume itakagua idadi, majina na mipaka ya wadi mara kwa mara.

(4) Ikiwa uchaguzi mkuu utafanyika ndani ya miezi kumi na miwili baada ya kukamilika kwa ukaguzi wa Tume, mipaka hiyo mipya haitazingatiwa kwa madhumuni ya uchaguzi huo.

(5) Mipaka ya kila eneobunge italinganishwa, kwa kiasi kiwezekanacho, na idadi ya wakazi katika eneo bunge hilo, lakini idadi ya wakazi katika eneobunge inaweza kuwa kubwa au ndogo kuliko idadi ya watu inayolingana na eneo hilo kwa namna ambayo imetajwa katika Ibara ya (6) ili kuzingatia—

a) hali ya kijiografia na maeneo ya miji;

b) jamii ya eneo lile, historia, uchumi na mahusiano ya kitamaduni; na

c) mbinu za mawasiliano.

(6) Idadi ya wakazi katika eneobunge au wadi inaweza kuwa kubwa au ndogo zaidi ya idadi ya watu inayolingana na eneo hilo kwa kiwango kisichozidi —

a) asilimia arobaini kwa majiji na maeneo yaliyo na idadi ya watu iliyotawanyika; na

b) asilimia thelathini kwa sehemu nyingine.

(7) Katika kukagua mipaka ya maeneobunge na wadi, Tume-––

a) itashauriana na wote wanaohusika; na

b) itandelea kufanya kazi ili kuhakikisha kwamba idadi ya watu katika kila eneobunge na wadi, kadiri iwezekanavyo, ni sawa na idadi ya watu inayolingana na eneo hilo.

(8) Ikiwa itahitajika, Tume hii itabadilisha majina na mipaka ya maeneobunge na wadi, na idadi, majina na mipaka ya wadi.

(9) Kwa kuzingatia ibara ya (1) (2),(3) na (4), majina na maelezo ya kina kuhusu mipaka ya maeneobunge na wadi yaliyoamuliwa na Tume yatachapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali, na majina na maelezo hayo yataanza kutumika baada ya kuvunjwa kwa Bunge kwa mara ya kwanza baada ya kuchapishwa kwa maelezo hayo.

(10) Mtu anaweza kuwasilisha ombi kwa Mahakama Kuu chini ya Kifungu hiki ili uamuzi uliofanywa na Tume ukaguliwe.

(11) Ombi la kukaguliwa kwa uamuzi uliofanywa chini ya Kifungu hiki litawasilishwa ndani ya siku thelathini baada ya uchapishaji wa uamuzi huo katika Gazeti Rasmi la Serikali na litasikizwa na uamuzi kutolewa ndani ya miezi mitatu kuanzia siku ya kuwasilishwa kwa ombi hilo.

(12) Kwa madhumuni ya Kifungu hiki, "idadi ya watu inayolingana na eneo" inamaanisha idadi inayopatikana baada ya kugawa ifaavyo, idadi ya watu wanaoishi nchini Kenya kwa idadi ya maeneobunge au wadi ambazo Kenya imegawanywa kwayo chini ya Kifungu hiki.

**90.**

*Ugawaji orodha ya viti vya chama.*

(1) Uchaguzi wa nafasi zilizopo bungeni chini ya Kifungu cha 97 (1) (c) na 98 (1) (b), (c) na (d), na wa wawakilishi wadi chini ya Kifungu cha 177 (1) (b) na (c), utakuwa kwenye misingi ya uwakilishaji wenye usawa kwa kutumia orodha za vyama.

(2) Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka itawajibika katika uendeshaji na usimamizi wa uchaguzi wa nafasi zilizotolewa chini ya Ibara ya (1) na itahakikisha kwamba-—



SIO YA KUUZWA

a) kila chama cha kisiasa kinachoshiriki katika uchaguzi mkuu kimeteua na kuwasilisha orodha ya majina ya watu wote ambao wangalichaguliwa iwapo chama hicho kingalipewa viti vyote chini ya Ibara ya (1), ndani ya muda ulioagizwa kupitia sheria ya kitaifa;

b) isipokuwa katika nafasi zilizotolewa chini ya Kifungu cha 98 (1) (b), kila orodha ya chama ina idadi kamilifu ya wagombea wanaostahiki pamoja na watakaochukua nafasi zao, wa kiume na kike, kulingana na jinsi walivyowaorodhesha; na

c) isipokuwa katika nafasi za bunge la kaunti, kila orodha ya chama inazingatia tofauti za kieneo na za kikabila za Wakenya.

(3) Nafasi zilizotajwa katika ibara ya (1) zitagawiwa vyama vya kisiasa kulingana na idadi ya jumla ya viti walivyoshinda wagombeaji katika chama cha kisiasa kwenye uchaguzi mkuu.

**Sehemu ya 3—Vyama vya Kisiasa**

**91.**

*Mahitaji ya kimsingi kwa vyama vya kisiasa.*

(1) Kila chama cha kisiasa—

a) kitakuwa na sura ya kitaifa kama inavyoagizwa na Sheria ya Bunge;

b) kitakuwa na idara ya uongozi iliyochaguliwa kwa njia ya kidemokrasia;

c) kitadumisha na kukuza umoja wa kitaifa;

d) kitazingatia kanuni za kidemokrasia za utawala bora, kitakuza na kuendeleza demokrasia kupitia kwa uchaguzi wa mara kwa mara, wenye haki na huru katika chama;



SIO YA KUUZWA

e) kitaheshimu haki za kila mtu kushiriki katika mchakato wa kisiasa, ikijumuisha vikundi vya watu walio wachache na wale waliotengwa;

f) kitaheshimu na kukuza haki za binadamu na uhuru wa kimsingi, na usawa wa kijinsia na usawazishaji;

g) kitakuza malengo na kanuni za Katiba hii na utawala wa sheria; na

h) kitazingatia kanuni za maadili kwa vyama vya kisiasa.

*Sheria kuhusu vyama vya kisiasa.*

(2) Chama cha kisiasa—

a) hakitabuniwa kwenye misingi ya kidini, lugha, taifa, kabila, jinsia au eneo au kujihusisha katika kampeni za kusambaza chuki kwenye misingi kama hiyo iliyotajwa;

b) hakitajihusisha katika au kuchochea ghasia kwa kuwatisha wanachama wake, wafuasi, wapinzani au mtu mwingine yeyote;

c) hakitaanzisha au kudumisha vikosi vya jeshi la wanamgambo, makundi haramu au mashirika mengine kama hayo;

d) hakitajihusisha katika utoaji hongo au aina zingine za ufisadi; au

e) isipokuwa ilivyoelezwa katika Sura hii au katika Sheria ya Bunge, hakitakubali au kutumia rasilimali za umma ili kuimarisha maslahi ya chama au wagombeaji wake katika uchaguzi.

**92.** Bunge litatunga sheria ili kutoa mwongozo kuhusu—

a) jukumu la vyombo vya habari vinavyomilikiwa na Serikali pamoja na aina zingine za vyombo vya utangazaji vilivyotajwa, kugawa sawa muda



SIO YA KUUZWA

hewani ambao vyama vya kisiasa vinapewa kijumla au katika kampeni za uchaguzi; na

b) udhibiti wa uhuru wa kutangaza ili kuhakikisha kampeni zenye haki na usawa wakati wa uchaguzi;

c) udhibiti wa vyama vya kisiasa;

d) majukumu ya vyama vya kisiasa;

e) usajili na usimamizi wa vyama vya kisiasa;

f) kuundwa na kusimamiwa kwa hazina ya vyama vya kisiasa;

g) akaunti na ukaguzi wa vyama vya kisiasa;

h) udhibiti katika matumizi ya rasilimali ya umma ili kuendeleza malengo ya vyama vya kisiasa; na

i) masuala mengine muhimu katika usimamizi wa vyama vya kisiasa.



SIO YA KUUZWA

## SURA YA NANE--MABUNGE

**Sehemu ya 1—Kuundwa kwa Mabunge na Jukumu la Maunge**

**93.**

*Kuundwa kwa Mabunge.*

(1) Mabunge ya Kenya yameundwa, na yatajumuisha Bunge la Kitaifa na Seneti.

(2) Bunge la Kitaifa na Seneti yatatekeleza majukumu yao kulingana na Katiba hii.

**94.**

*Jukumu la Mabunge*

(1) Mamlaka ya utungaji wa sheria ya Jamhuri yametolewa na wananchi, na katika kiwango cha kitaifa, yamekabidhiwa kwa Bunge, na yanatekelezwa na Bunge.

(2) Bunge linadhihirisha utofauti wa taifa, linawakilisha matakwa ya wananchi, na linatekeleza mamlaka yao makuu.

(3) Bunge linaweza kuangalia kikamilifu na kupitisha marekebisho katika Katiba hii, na kubadilisha mipaka ya kaunti kama inavyoelezewa katika Katiba hii;

(4) Bunge litalinda Katiba hii na kukuza utawala wa kidemokrasia katika Jamhuri hii.

(5) Hakuna mtu yeyote au shirika lolote, isipokuwa Bunge, ambalo lina mamlaka ya kutoa maagizo au masharti ambayo yana nguvu za kisheria nchini Kenya isipokuwa chini ya mamlaka yaliyotolewa na Katiba hii au kupitia kwa sheria.

(6) Sheria ya Bunge, au sheria ya kaunti, inayotoa mamlaka kwa idara yoyote ya Serikali, afisa wa Serikali, au mtu yeyote ili kutunga sheria ambayo ina nguvu za kisheria nchini Kenya, kama inavyokusudiwa katika Ibara ya (5), itaeleza bayana malengo na madhumuni ya kutolewa kwa mamlaka hayo, mipaka ya mamlaka hayo, hali na upeo wa sheria ambazo zinaweza kutungwa, na kanuni na viwango vya ubora

vinavyotumika katika sheria iliyotungwa chini ya mamlaka hayo.

**95.**

*Jukumu la Bunge la Kitaifa.*

(1) Bunge la Kitaifa linawakilisha watu walio katika maeneobunge na walio na maslahi maalum katika Bunge la Kitaifa.

(2) Bunge la Kitaifa hushauriana kuhusu maswala yenye umuhimu kwa wananchi na kuyasuluhisha.

(3) Bunge la Kitaifa hutunga sheria kwa kuzingatia Sehemu ya 4 ya Sura hii.

(4) Bunge la Kitaifa––

a) huamua jinsi ya kugawa mapato ya kitaifa kati ya ngazi za Serikali, kama inavyobainishwa katika Sehemu ya 4 ya Sura ya Kumi na Mbili;

b) hugawa fedha kwa matumizi ya serikali ya kitaifa na vitengo vingine vya Serikali vya kitaifa; na

c) (c) hufuatilia uwajibikaji katika mapato ya kitaifa pamoja na matumizi yake.

(5) Bunge la Kitaifa—

a) hukagua utendakazi katika ofisi ya Rais, ya Naibu Rais na maafisa wengine wa Serikali na huanzisha mchakato wa kuwaondoa ofisini; na

b) hufuatilia uwajibikaji wa vitengo vya Serikali.

(6) Bunge la Kitaifa huidhinisha matangazo ya vita na kuongezwa kwa muda katika hali za hatari.

**96.**

*Jukumu la Seneti.*

(1) Seneti inawakilisha kaunti na inahudumu ili kulinda maslahi ya kaunti na ya serikali za kaunti hizo.

(2) Seneti hushiriki katika jukumu la Bunge la kutunga sheria kwa kutathmini, kujadiliana, kuidhinisha Miswada inayohusu kaunti, kama ilivyobainishwa katika Vifungu vya 109 hadi 113.

(3) Seneti huamua jinsi ya kugawa mapato ya kitaifa miongoni mwa kaunti kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 217, na hufuatilia uwajibikaji katika mapato ya kitaifa yaliyogawa katika serikali za kaunti.

(4) Seneti hushiriki katika uwajibikaji wa maafisa wa Serikali kwa kuzingatia na kutoa maamuzi kuhusu hoja ya kumwondoa Rais au Naibu wa Rais kutoka ofisini kulingana na Kifungu cha 145.

**Sehemu ya 2—Muundo na Uanachama wa Bunge la Kitaifa**

**97.**

*Uanachama wa Bunge la Kitaifa.*

(1) Bunge la Kitaifa linajumuisha—

a) wabunge mia mbili tisini, kila mmoja wao akiwa amechaguliwa na wapigakura waliosajiliwa katika maeneobunge yanayotoa mbunge mmoja kwa kila eneobunge;

b) wanawake arobaini na saba, kila mmoja wao akiwa amechaguliwa na wapiga kura waliosajiliwa katika kaunti, kila kaunti ikiwa na eneobunge linalotoa mbunge mmoja;

c) wabunge kumi na wawili walioteuliwa na vyama vya kisiasa vya bunge kulingana na idadi ya wabunge wa vyama hivyo katika Bunge la Kitaifa kwa mujibu wa Kifungu cha 90, ili kuwakilisha maslahi ya watu maalum ikijumuisha vijana, watu wenye ulemavu na wafanyakazi; na

d) Spika, ambaye ni mwanachama aliyechaguliwa na wabunge.

(2) Hakuna chochote katika Kifungu hiki kinachoweza kufasiriwa kama cha kumzuia mtu yeyote katika kugombea uchaguzi chini ya ibara ya (1) (a).



SIO YA KUUZWA

**98.**

*Uanachama wa Seneti.*

(1) Seneti inajumuisha—

a) wanachama arobaini na saba, kila mmoja wao akiwa amechaguliwa na wapiga kura waliosajiliwa katika kaunti, na kila kaunti ikiwa na eneobunge linalowakilishwa na mbunge mmoja;

b) wanawake kumi na sita watakaoteuliwa na vyama vya kisiasa kulingana na idadi ya maseneta wao katika Seneti waliochaguliwa chini ya ibara ya (a) kulingana na Kifungu cha 90;

c) wanachama wawili, wakiwa mwanamume mmoja na mwanamke mmoja, wanaowawakilisha vijana;

d) wanachama wawili, wakiwa mwanamume mmoja na mwanamke mmoja, wanaowawakilisha watu wenye ulemavu; na

e) Spika, ambaye atakuwa mwanachama aliyechaguliwa na maseneta katika Seneti.

(2) Wanachama waliotajwa katika ibara ya (1) (c) na (d) watachaguliwa kulingana na Kifungu cha 90.

(3) Hakuna chochote katika Kifungu hiki kinachoweza kufasiriwa kama cha kumzuia mtu yeyote katika kugombea uchaguzi chini ya ibara ya (1) (a).

**99.**

*Ustahiki na kutostahiki katika kuchaguliwa Kama Mbunge.*

(1) Isipokuwa kwa sababu za kutostahiki chini ya ibara ya (2), mtu yeyote anastahiki kuchaguliwa kama mwanachama wa Bunge la Kitaifa au Seneti ikiwa mtu huyo—

a) amesajiliwa kama mpiga kura;

b) anatosheleza mahitaji yoyote ya kielimu, ya kimaadili na ya uadilifu ambayo yanahitajika katika Katiba hii au katika Sheria; na



SIO YA KUUZWA

c) ameteuliwa na chama cha kisiasa, au ni mgombeaji huru ambaye anaungwa mkono––

i. na angalau wapiga kura elfu moja waliosajiliwa katika eneobunge, katika uchaguzi wa Bunge la Kitaifa; na

ii. na angalau wapiga kura elfu mbili waliosajiliwa katika kaunti, katika uchaguzi wa Seneti.

(2) Mtu hastahiki kuchaguliwa kama mwanachama wa Bunge la Kitaifa au Seneti ikiwa mtu huyo—

a) ni afisa wa Serikali au afisa wa umma, isipokuwa awe mwanachama wa Bunge la Kitaifa au Seneti;

b) alihudumu kama afisa katika Tume Huru ya Uchaguzi na Mipakakatika kipindi cha miaka mitano iliyopita kabla ya tarehe ya uchaguzi;

c) hajakuwa raia wa Kenya kwa angalau miaka kumi iliyopita kabla ya tarehe ya uchaguzi;

d) ni mwakilishi wadi katika bunge la kaunti;

e) hana akili timamu;

f) amefilisika;

g) anakabiliwa na hukumu ya kifungo cha miezi sita gerezani katika tarehe ya kusajiliwa kama mgombeaji, au katika tarehe ya uchaguzi; au

h) amepatikana, kwa mujibu wa sheria yoyote, kutumia vibaya mamlaka ya ofisi ya Serikali au ya umma, au kwa njia yoyote kukiuka kanuni za Sura ya Sita.

(3) Mtu hazuiliwi kugombea chini ya ibara ya (2) isipokuwa tu pale ambapo uwezekano wote wa rufaa au kukaguliwa kwa kifungo au uamuzi husika umekwisha.

*Kukuza uwakilishi wa makundi ya watu yaliyotengwa*

**100.** Bunge litatunga sheria ili kukuza uwakilishaji Bungeni wa—

a) wanawake;

b) watu wenye ulemavu;

c) vijana;

d) vikundi vya watu wa kikabila na vya walio wachache; na

e) jamii zilizotengwa.

*Uchaguzi wa wabunge.*

**101.**

(1) Uchaguzi mkuu wa wabunge katika Bunge la Kitaifa na katika Seneti utafanyika katika Jumanne ya pili ya mwezi wa Agosti katika kila mwaka wa tano.

(2) Panapotokea nafasi katika ofisi ya mbunge katika Bunge la Kitaifa chini ya Kifungu cha 97 (1) (c), au katika Seneti chini ya Kifungu cha 98 (1) (b), (c) au (d), Spika anayehusika atatoa notisi ya nafasi hiyo kwa njia ya maandishi ndani ya siku ishirini na moja za kutokea kwa nafasi hiyo, na notisi hiyo itatolewa kwa maandishi kuhusu nafasi hiyo ya kazi kwa—

a) Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka; na

b) chama cha kisiasa ambacho kupitia kwa orodha ya chama hicho, mwanachama huyo alichaguliwa au kuteuliwa.

(3) Nafasi hiyo iliyotajwa katika ibara ya (2), kwa kuzingatia ibara ya (5), itajazwa kwa namna iliyoagizwa na Sheria ya Bunge ndani ya siku ishirini na moja baada ya Spika anayehusika kuarifu kuhusu nafasi hiyo.

(4) Panapotokea nafasi ya kazi katika ofisi ya mwanachama wa Bunge la Kitaifa aliyechaguliwa chini ya Kifungu cha 97 (1) (a) au (b), au wa Seneti aliyechaguliwa chini ya Kifungu cha 98 (1) (a)—

a) Spika anayehusika, katika muda wa siku ishirini

na moja baada ya kutokea kwa nafasi hiyo, atatoa notisi kwa njia ya maandishi kuhusu nafasi hiyo kwa kuiandikia Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka; na

b) uchaguzi mdogo utafanyika katika muda wa siku tisini baada ya kutokea kwa nafasi hiyo, lakini kwa kuzingatia ibara ya (5).

(5) Nafasi iliyotajwa katika ibara ya (4) haitajazwa katika kipindi cha miezi mitatu kabla ya uchaguzi mkuu.

**102.**

*Muhula wa Bunge.*

(1) Muhula wa kila Bunge la Kitaifa na Seneti unamalizika katika tarehe ya uchaguzi mkuu unaofuata..

(2) Kenya ikiwa vitani, kwa uamuzi unaoungwa mkono na angalau wabunge wasiopungua thuluthi mbili ya wabunge wote katika kila kitengo cha bunge, Bunge linaweza kuongeza kipindi cha Bunge kwa muda usiozidi miezi sita kwa wakati huo.

(3) Muhula wa bunge hautaongezwa kwa jumla ya zaidi ya miezi kumi na miwili chini ya ibara ya (2).

**103.**

*Mbunge kuondoka ofisini.*

(1) Kiti cha Mbunge kitakuwa wazi—

a) ikiwa mwakilishi wadi huyo atafariki dunia;

b) ikiwa, katika kipindi chochote cha vikao vya Bunge, mwanachama huyo hajahudhuria vikao vinane vya kitengo cha bunge husika bila ruhusa ya Spika wa kitengo chake cha bunge kwa njia ya maandishi, na ameshindwa kutoa sababu ya kuridhisha kwa kamati husika kuhusu kutohudhuria kwake;

c) ikiwa mwanachama huyo ameondolewa ofisini vinginevyo chini ya Katiba hii au chini ya sheria iliyotungwa chini ya Kifungu cha 80;



SIO YA KUUZWA

d) ikiwa mbunge huyo atajiuzulu kwa kumwandikia barua Spika;

e) ikiwa, baada ya kuchaguliwa katika Bunge––

i. kama mwanachama katika chama cha kisiasa, mwanachama huyo ajiuzulu kutoka kwa chama hicho au achukuliwe kuwa amejiuzulu kutoka kwa chama hicho kama inavyobainishwa kulingana na sheria inayozingatiwa katika ibara ya (2); au

ii. kama mgombea huru, mwanachama huyo atajiunga na chama cha kisiasa;

f) baada ya kukamilika kwa muhula wa Bunge husika; au

g) ikiwa mbunge huyo hatastahiki tena kuchaguliwa katika uchaguzi wa Bunge chini ya Kifungu cha 99 (2) (d) hadi (h).

(2) Bunge litatunga sheria litakalotoa hali ambazo mwanachama wa chama cha kisiasa atachukuliwa kuwa amejiuzulu kutoka chama hicho, kwa madhumuni ya ibara ya (1) (e).

**104.**

*Kuondolewa mamlakani kwa Mbunge.*

(1) Wapiga kura chini ya Vifungu vya 97 na 98, wana haki ya kumwondoa mamlakani mbunge anayewakilisha eneobunge lao kabla ya kukamilika kwa muhula wa kitengo husika cha Bunge.

(2) Bunge litatunga sheria itakayotoa sababu ambazo zinaweza kupelekea kuondolewa kwa mwanachama wa bunge na taratibu itakayofuatwa.

**105.**

*Uamuzi katika maswali yanayohusiana na uanachama*

(1) Mahakama Kuu itasikiliza na kutoa maamuzi katika swali lolote kuhusu—



SIO YA KUUZWA

a) ikiwa mtu amechaguliwa kama mbunge kwa njia halali; au

b) ikiwa kiti cha mbunge kimekuwa wazi.

(2) Ombi chini ya ibara ya (1) itasikilizwa na kuamuliwa katika muda wa miezi sita kutoka tarehe ya kuwasilishwa kwa ombi au malalamiko hayo.

(3) Bunge litatunga sheria ili kuwezesha utekelezaji wa Kifungu hiki kikamilifu.

**Sehemu ya 3—Ofisi za Bunge**

**106.**

*Maspika na Manaibu Spika wa Bunge.*

(1) Kutakuwepo—

a) Spika wa kila kitengo cha Bunge, atakayechaguliwa na Kitengo hicho kulingana na Kanuni za Vikao vya Bunge, kutoka miongoni mwa watu wanaostahiki kuchaguliwa kama wanachama wa Bunge lakini ambao sio wabunge; na

b) Naibu Spika katika kila Kitengo cha Bunge, atakayechaguliwa na Kitengo hicho kutoka miongoni mwa wabunge katika Kiengo hicho kulingana na Kanuni za Vikao vya Bunge.

(2) Kiti cha Spika au Naibu wa Spika kitakuwa wazi—

a) wakati Kitengo cha Bunge kipya kitakapokutana kwa mara ya kwanza baada ya uchaguzi;

b) ikiwa anayehudumu, kama mwanachama wa Kitengo husika, ataondoka ofisini chini ya Kifungu cha 103;

c) ikiwa Kitengo husika kitaamua, kwa uamuzi ulioungwa mkono na kura za angalau wabunge wasiopungua thuluthi mbili; au

d) ikiwa anayehudumu atajiuzulu kwa kukiandikia barua Kitengo husika.

**107.**

*Kuongoza Vikao Bungeni.*

(1) Katika kikao chochote cha Kitengo cha Bunge—

a) Spika ndiye anayeongoza;

b) ikiwa Spika hayupo, Naibu wa Spika ataongoza; na

c) Spika na Naibu Spika wasipokuwepo, mwanachama mwingine wa Kitengo hicho aliyechaguliwa na Kitengo hicho ataongoza;

(2) Katika kikao cha pamoja kati ya Vitengo vya Bunge, Spika wa Bunge la Kitaifa ataongoza, akisaidiwa na Spika wa Bunge la Seneti.

**108.**

*Viongozi wa vyama.*

(1) Kutakuwa na kiongozi wa chama cha walio wengi na kiongozi wa chama cha walio wachache.

(2) Kiongozi wa chama cha walio wengi au kiongozi wa walio wengi bungeni kutokana na muungano wa vyama, ndiye atakayekuwa kiongozi wa chama kikubwa zaidi au muungano mkubwa zaidi katika Bunge la Kitaifa

(3) Kiongozi wa walio wachache ndiye atakayekuwa kiongozi wa chama cha pili kwa ukubwa au muungano wa pili kwa ukubwa katika Bunge la Kitaifa.

(4) Utaratibu ufuatao utazingatiwa katika Bunge la Kitaifa––

a) Spika wa Bunge la Kitaifa;

b) kiongozi wa chama cha walio wengi; na

c) kiongozi wa chama cha walio wachache.

**Sehemu ya 4—Taratibu za Kutunga Sheria**

**109.**

*Matumizi ya mamlaka ya kutunga sheria.*

(1) Bunge litatekeleza mamlaka yake ya kutunga sheria kupitia kwa Miswada itakayopitishwa Bungeni na kuidhinishwa na Rais.

(2) Mswada wowote unaweza kutoka kwa Bunge la Kitaifa.

(3) Mswada usiohusu serikali za kaunti utazingatiwa tu katika Bunge la Kitaifa, na kupitishwa kulingana na Kifungu cha 122 na Kanuni za Vikao vya Bunge.

(4) Mswada unaohusu serikali za kaunti unaweza kutoka kwa Bunge la Kitaifa au Seneti, na utapitishwa kulingana na Vifungu vya 109 hadi 113, Vifungu vya 122 hadi 123 na Kanuni za Vikao vya Bunge.

(5) Mswada unaweza kuwasilishwa na mwanachama yeyote au kamati yoyote ya Kitengo husika cha Bunge, lakini Mswada unaohusu fedha unaweza kuwasilishwa tu katika Bunge la Kitaifa kwa mujibu wa Kifungu cha 114.

**110.**

*Miswada kuhusu serikali za kaunti.*

(1) Katika Katiba hii, "Mswada unaohusu serikali ya kaunti" inamaanisha––

a) Mswada ulio na vifungu vinavyohusu majukumu na mamlaka ya serikali za kaunti zilizotajwa katika Ambatisho la Nne;

b) Mswada unaohusu uchaguzi wa wawakilishi wadi au wanachama katika kitengo cha utendaji cha serikali ya kaunti; na

c) Mswada uliorejelewa katika Sura ya Kumi na Mbili unaohusu fedha za serikali za kaunti.

(2) Mswada unaohusu serikali za kaunti ni––

a) Mswada maalum ambao utazingatiwa chini ya

Kifungu cha 111, ikiwa –

i. unahusiana na uchaguzi wa wawakilishi wadi katika bunge la kaunti au wanachama wa kitengo cha utendaji cha serikali ya kaunti; au

ii. ni Mswada wa Mgao wa Mapato ya Kaunti wa kila mwaka uliotajwa katika Kifungu cha 218; au

b) mswada wa kawaida ambao utazingatiwa chini ya Kifungu cha 112 katika hali nyingine yoyote.

(3) Kabla ya mojawapo ya vitengo vya Bunge kutathmini Mswada, Maspika wa Bunge la Kitaifa na Seneti kwa pamoja watasuluhisha suala lolote kuhusu ikiwa Mswada huo unahusu kaunti na ikiwa unahusu kaunti, kama ni Mswada maalum au ni wa kawaida.

(4) Mswada wowote unaohusu serikali ya kaunti unapopitishwa na Kitengo kimoja cha Bunge, Spika wa Kitengo hicho atamtumia Spika wa Kitengo hicho kingine Mswada huo.

(5) Ikiwa Vitengo vyote viwili vitaupitisha Mswada huo kwa hali sawa, Spika wa Kitengo ambacho kilitoa Mswada huo, ataupeleka kwa Rais katika muda wa siku saba ili uidhinishwe.

**111.**

*Miswada maalum inayohusu serikali za kaunti.*

(1) Mswada maalum unaohusu serikali ya kaunti utashughulikiwa kwa namna sawa na Mswada wa kawaida unaohusu serikali za kaunti, lakini kwa kuzingatia ibara ya (2) na (3).

(2) Bunge la Kitaifa linaweza kurekebisha au kutupilia mbali Mswada maalum uliopitishwa na Seneti kwa uamuzi tu ulioungwa mkono na angalau thuluthi mbili ya wabunge katika Bunge la Kitaifa.

(3) Ikiwa uamuzi wa kurekebisha au kutupilia mbali



SIO YA KUUZWA

Mswada maalum utakosa kupitishwa katika Bunge la Kitaifa, Spika wa Bunge ataupeleka Mswada huo, kwa hali iliyopitishwa na Seneti, kwa Rais katika muda wa siku saba ili uidhinishwe.

**112.**

*Miswada ya kawaida inayohusu serikali za kaunti.*

(1) Ikiwa Kitengo kimoja kitapitisha Mswada wa kawaida kuhusu kaunti, na Kitengo cha pili––

a) kiukatae Mswada huo, basi utapelekwa katika kamati ya upatanishi chini ya Kifungu cha 113; au

b) kiupitishe Mswada huo baada ya kuurekebisha, utarejeshwa kwa Kitengo kilichoutoa Mswada huo mwanzoni, ili kutathminiwa tena.

(2) Ikiwa, baada ya Kitengo kilichotoa Mswada huo kuutathmini tena chini ya ibara ya (1) (b), Kitengo hicho––

a) kitaupitisha Mswada kama ulivyorekebishwa, Spika wa Kitengo hicho ataupeleka kwa Rais katika muda wa siku saba ili uidhinishwe; au

b) kitaukataa Mswada huo kama ulivyorekebishwa, Mswada huo utatumwa kwa kamati ya upatanishi chini ya Kifungu cha 113.

**113.**

*Kamati za upatanishi.*

(1) Ikiwa Mswada utatumwa kwa kamati ya upatanishi chini ya Kifungu cha 112, Maspika wa Vitengo vyote viwili watateua kamati ya upatanishi itakayohusisha idadi sawa ya wanachama wa Vitengo vyote viwili ili kujaribu kutengeneza toleo jingine la Mswada litakalopitishwa na Vitengo vyote viwili.

(2) Ikiwa kamati ya upatanishi itakubali toleo la Mswada huo, kila Kitengo kitapiga kura ili kupitisha au kukataa toleo hilo la Mswada.

(3) Ikiwa Vitengo vyote viwili vitaidhinisha toleo hilo la

Mswada lililopendekezwa na kamati ya upatanishi, Spika wa Bunge la Kitaifa atautuma Mswada huo kwa Rais katika siku saba ili uidhinishwe.

(4) Ikiwa kamati ya upatanishi itakosa kuafikiana kuhusu toleo hilo la Mswada katika kipindi cha muda wa siku thelathini, au iwapo toleo hilo lililopendekezwa na kamati litakataliwa na mojawapo ya Vitengo vya Bunge, basi Mswada huo utakuwa umeshindwa.

**114.**

(1) Mswada wa fedha hauwezi kushughulikia suala lingine lolote isipokuwa tu yale ambayo yameorodheshwa katika ufafanuzi wa "Mswada wa fedha" katika ibara ya (3).

(2) ikiwa, kwa maoni ya Spika wa Bunge la Kitaifa, hoja linatoa mwongozo kwa suala lililotajwa katika ufafanuzi wa "Mswada wa fedha", Bunge linaweza kuendelea tu kwa mujibu wa mapendekezo ya kamati husika ya Bunge baada ya kuzingatia maoni ya Waziri wa fedha.

(3) Katika Katiba hii, 'Mswada wa fedha' unamaanisha, kando na Mswada uliotajwa katika Kifungu cha 218, Mswada ambao unahusu-—

a) ushuru;

b) Kutozwa kwa malipo katika hazina ya umma au ubadilishaji au kuondolewa kwa mojawapo ya malipo hayo;

c) kugawa, kupokea, kutunza, kuwekeza au kutoa pesa za umma;

d) kutafuta au kudhamini mkopo wowote au ulipaji wake; au

e) maswala yanayohusiana na maswala yaliyotajwa hapo juu.



SIO YA KUUZWA

(4) katika ibara ya (3), "ushuru", "fedha za umma", na "mkopo", hazijumuishi ushuru wowote, fedha za umma au mkopo uliochukuliwa na kaunti.

**115.**

*Idhini na rufaa ya rais.*

(1) Katika siku kumi na nne baada ya kupokea Mswada, Rais—

a) atauidhinisha Mswada huo; au

b) ataurejesha Mswada Bungeni ili kujadiliwa upya na Bunge huku likizingatia sababu zozote alizonazo Rais kuhusu mswada huo.

(2) Ikiwa Rais ataurejesha Mswada bungeni ili ujadiliwe tena, Bunge, kwa kuzingatia taratibu zinazofaa chini ya Sehemu hii, linaweza—

a) kuurekebisha Mswada huo kwa kuzingatia sababu alizotoa Rais; au

b) kuupitisha Mswada huo kwa mara ya pili bila kufanya marekebisho.

(3) Ikiwa Bunge litarekebisha Mswada huo na kuzingatia mapendekezo ya Rais kikamilifu, Spika anayehusika atauwasilisha tena Mswada huo kwa Rais ili auidhinishe.

(4) baada ya kuzingatia sababu za Rais, linaweza kuupitisha Mswada huo kwa mara ya pili bila marekebisho au na marekebisho ambayo hayazingatii kikamilifu hoja zilizotolewa na Rais, kwa kura ambayo itaungwa mkono na—

a) thuluthi mbili ya wabunge katika Bunge la Kitaifa; na

b) thuluthi mbili ya wawakilishi katika Seneti, ikiwa ni Mswada unaohitaji idhini ya Seneti.

(5) Ikiwa Bunge litapitisha Mswada chini ya ibara ya (4)—



SIO YA KUUZWA

a) Spika wa Bunge husika atawasilisha tena Mswada huo kwa Rais katika siku saba; na

b) Rais atauidhinisha Mswada huo ndani ya siku saba.

(6) Ikiwa Rais hatauidhinisha Mswada huo au kuurejesha kwa wakati unaopendekezwa katika Ibara ya (1), au kuuidhinisha chini ya ibara ya (5) (b), Mswada huo utachukuliwa kuwa umeidhinishwa ifikiapo mwisho wa kipindi hicho.

**116.**

*Sheria kuanza kutumika*

(1) Mswada uliopitishwa na Bunge na kuidhinishwa na Rais, utachapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali kama Sheria ya Bunge katika muda wa siku saba baada ya kuidhinishwa.

(2) Kwa kuzingatia ibara ya (3), Sheria ya Bunge inaanza kutekelezwa baada ya siku ya kumi na nne ya kuchapishwa kwake katika Gazeti Rasmi la Serikali, isipokuwa Sheria inapotoa tarehe au wakati tofauti wa kuanza kutekelezwa kwake.

(3) Sheria ya Bunge ambayo moja kwa moja inahusiana na maslahi ya kifedha ya wabunge haitatekelezwa hadi baada ya uchaguzi mkuu ya wanachama wa Bunge utakaofuata.

(4) Ibara ya (3) haitumiki kwa maslahi waliyonayo wanachama wa Bunge wakiwa kama wananchi.

**Sehemu ya 5—Taratibu za Kijumla na Kanuni za Bunge**

**117.**

*Ufikiaji na kushiriki kwa umma*

(1) Kutakuwa na uhuru wa kujieleza na majadiliano katika Bunge.

(2) (2) Bunge linaweza, kwa madhumuni ya uendeshaji bora wa shughuli za bunge, kutoa mamlaka, haki

maalum na kinga dhidi ya mashtaka kwa Bunge, kamati zake, kiongozi wa chama cha walio wengi, kiongozi wa chama cha walio wachache, wenyeviti wa kamati na wanachama.

**118.**

*Haki ya kuwasilisha ombi kwa Bunge.*

(1) Bunge—

a) litaendesha shughuli zake kwa njia wazi, na vikao vyake na vya kamati zake vitakuwa wazi kwa umma; na

b) litawezesha kushiriki na kuhusishwa kwa umma katika shughuli za kutunga sheria na shughuli zingine za Bunge na kamati zake.

(2) Bunge halitazuia umma au vyombo vyovyote vya habari dhidi ya kuhudhuria kikao chochote isipokuwa katika hali za kipekee ambazo Spika anayehusika ataamua kwamba kuna sababu za kuridhisha kuzuia umma au vyombo vya habari.

**119.**

*Mamlaka, haki na kinga dhidi ya mashtaka.*

(1) Kila mtu ana haki ya kuwasilisha ombi au malalamishi kwa Bunge ili lishughulikie suala lolote lililo katika mamlaka yake ikijumuisha kurekebisha au kutupilia mbali sheria yoyote.

(2) Bunge litatoa mwongozo kuhusu taratibu za kutekeleza haki hii.

**120.**

*Lugha rasmi Bungeni*

(1) Lugha rasmi za mabunge zitakuwa Kiswahili, Kiingereza na Lugha ya Ishara ya Kenya, na shughuli za maunge zinaweza kuendeshwa kwa Kiingereza, Kiswahili na kwa Lugha ya Ishara ya Kenya.

(2) Iwapo tafsiri tofauti za lugha katika matoleo ya Sheria ya Bunge zitakinzana, toleo la tafsiri lililotiwa saini na Rais ndilo litakalotumika.



SIO YA KUUZWA

**121.**

*Idadi ya watu inayohitajika ili kufanya kikao.*

(1) Idadi inayohitajika ili Bunge lifanye kikao itakuwa––

a) wabunge hamsini katika Bunge la Kitaifa; au

b) wanachama kumi na watano katika Seneti.

**122.**

*Kupiga Kura Bungeni.*

(1) Suala lolote litakalopendekezwa ili kuamuliwa katika mojawapo ya Vitengo vya Bunge, litaamuliwa na walio wengi katika Kitengo hicho, ambao wamehudhuria na kupiga kura, isipokuwa Katiba inapoagiza vinginevyo.

(2) Katika swali linalopendekezwa ili kuamuliwa katika mojawapo ya Vitengo vya Bunge—

a) Spika hatapiga kura; na

b) iwapo kura zitakuwa sawa katika pande zote, swali hilo litakuwa limeshindwa.

(3) Mwanachama hatapigia kura suala lolote ambalo ana maslahi ya kifedha kwalo.

(4) Katika kubaini idadi ya wanachama katika Kitengo cha Bunge kwa madhumuni yoyote ya upigaji kura katika Kitengo hicho, Spika wa Kitengo hicho hatahesabiwa kama mwanachama.

**123.**

*Maamuzi ya Seneti.*

(1) Katika uchaguzi, wanachama wote wa Seneti ambao walikuwa wamesajiliwa kama wapiga kura katika kaunti fulani kwa pamoja watachukuliwa kama mjumbe mmoja kwa madhumuni ya ibara ya (4) na mwanachama aliyechaguliwa chini ya Kifungu cha (98) (1)(a) atakuwa kiongozi wa wajumbe hao.

(2) Seneti itakapopiga kura kuhusu suala lolote isipokuwa Mswada, Spika ataamua iwapo suala hilo linaathiri au haliathiri kaunti.



SIO YA KUUZWA

(3) Seneti inapopiga kura kuhusu suala ambalo haliathiri kaunti, kila seneta atakuwa na kura moja.

(4) Isipokuwa mwongozo utolewe vinginevyo katika Katiba hii, kwa suala lolote katika Seneti linalohusu kaunti—

a) kila wajumbe wa kaunti watakuwa na kura moja itakayopigwa na kiongozi wa wajumbe hao kwa niaba ya, na endapo kiongozi wa wajumbe hao hayuko, kura itapigwa na mjumbe mwingine mmoja kati ya wajumbe hao ambaye ameteuliwa na kiongozi wa wajumbe hao;

b) mtu ambaye atapiga kura kwa niaba ya wajumbe hao ataamua ikiwa atapiga kura kwa kuunga mkono au kutounga mkono suala hilo, baada ya kushauriana na wajumbe; au

c) suala litakuwa limepitishwa ikiwa tu litaungwa mkono na wajumbe walio wengi.

**124.**

*Kamati na Sheria Zinazosimamia Vikao vya Bunge.*

(1) Kila Kitengo cha Bunge kinaweza kubuni kamati, na kitaweka Kanuni za Vikao vya Bunge ili kuendesha vikao kwa utaratibu, ikijumuisha vikao vya kamati za kitengo hicho.

(2) Bunge linaweza kubuni kamati za pamoja zinazo-jumuisha wanachama wa Vitengo vyote viwili vya Bunge na inaweza kudhibiti kwa pamoja utaratibu wa kamati hizo.

(3) Vikao vya Kitengo chochote cha Bunge havifanywi kuwa haramu kwa sababu tu ya—

a) nafasi katika uanachama wake; au

b) kuwepo au kushiriki kwa mtu yeyote asiyepaswa kuwepo au kushiriki katika vikao hivyo vya Kitengo hicho.



SIO YA KUUZWA

(4) Kitengo cha Bunge kinapozingatia uteuzi wowote ambao kuidhinishwa kwake kunahitajika chini ya Katiba hii au Sheria ya Bunge––

a) uteuzi huo utashughulikiwa na kamati husika ya Bunge;

b) mapendekezo ya kamati yatawasilishwa katika Kitengo hicho cha Bunge ili kuidhinishwa; na

c) vikao vya kamati na vya Bunge vitakuwa wazi kwa umma.

**125.**

*Mamlaka ya kuitisha ushahidi.*

(1) Kitengo chochote cha Bunge, na yoyote kati ya kamati zake, kina uwezo wa kumwita mtu yeyote kwa kusudi la kutoa ushahidi au maelezo mbele yake;

(2) Kwa madhumuni ya ibara ya (1), Kitengo cha Bunge na yoyote kati ya kamati zake kina mamlaka sawa na Mahakama Kuu—

a) ya kuhakikisha kuwa mashahidi wamehudhuria na kuwahoji chini ya kiapo, uthibitisho au vinginevyo;

b) kuhitaji utoaji wa hati kwa lazima; na

c) kutoa agizo au ombi la kuwahoji mashahidi walio nje ya taifa.

**Sehemu ya 6—Vipengee vya Ziada**

**126.**

*Eneo la vikao vya Bunge.*

(1) Vikao vya Kitengo chochote cha Bunge vinaweza kufanyiwa sehemu yoyote nchini Kenya, na kuanza kwa wakati wowote utakaoteuliwa na Bunge.

(2) Kila kutakapochaguliwa Bunge jipya, Rais, kwa kutoa notisi katika Gazeti Rasmi la Serikali, atateua mahali na tarehe ya kikao cha kwanza cha Bunge jipya, ambayo haitakuwa zaidi ya siku thelathini baada ya uchaguzi mkuu.



SIO YA KUUZWA

**127.**

*Tume ya Huduma za Bunge.*

(1) Tume ya Huduma za Bunge Imebuniwa.

(2) Tume hiyo inajumuisha—

a) Spika wa Bunge la Kitaifa, kama mwenyekiti;

b) naibu mwenyekiti aliyechaguliwa na Tume kutoka kwa wanachama walioteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha (c);

c) wanachama saba walioteuliwa na Bunge kutoka miongoni mwa wabunge na ambao—

i. wanne watateuliwa kwa usawa na chama au muungano wa vyama vinavyounda serikali ya kitaifa vilivyo katika Bunge na ambao angalau wawili kati yao watakuwa wanawake; na

ii. watatu watateuliwa na vyama visivyo kwenye serikali ya kitaifa, angalau mmoja akiteuliwa kutoka kila Kitengo cha Bunge, na angalau mmoja wao akiwa mwanamke; na

d) Mwanaume mmoja na mwanamke mmoja aliyeteuliwa na Bunge kutoka miongoni mwa watu ambao sio wabunge lakini wana uzoefu mkubwa katika masuala ya umma.

(3) Karani wa Seneti atakuwa Katibu wa Tume hiyo.

(4) Mwanachama wa Tume ataondoka ofisini—

a) ikiwa mtu huyo ni Mbunge—

i. baada ya kukamilika kwa muhula wa Kitengo cha Bunge ambacho mtu huyo alikuwa mbunge;

ii. ikiwa mtu huyo atawacha kuwa Mbunge; au

b) ikiwa mtu huyo ni mbunge mteule, baada ya kuondolewa kwa uteuzi wake na Bunge.

(5) Licha ya Ibara ya (4), muhula wa Kitengo cha Bunge

unapokwisha, mwanachama wa Tume aliyeteuliwa kwa mujibu wa ibara ya (2) (c) ataendelea kuhudumu ofisini hadi mwanachama mwingine atakapoteuliwa na Bunge litakalofuata ili kuchukua nafasi yake.

(6) Tume ina jukumu la—

a) kutoa huduma na msaada ili kufanikisha utendakazi bora na wenye ufanisi wa Bunge;

b) kubuni ofisi katika huduma ya Bunge, na kuteua na kuwasimamia wanaohudumu katika ofisi hizo;

c) kutayarisha makadirio ya matumizi ya fedha ya kila mwaka katika huduma za Bunge la Kitaifa na kuyawasilisha kwa Bunge la Kitaifa, na kudhibiti bajeti kuhusu huduma hizo;

d) Kuanzisha kibinafsi au kwa pamoja na mashirika husika, mipango ya kukuza maadili ya demokrasia ya bunge; na

e) kutekeleza majukumu mengine—

i. ambayonimuhimukwamanufaayawabungena wafanyakazi wa Bunge; au

ii. yatakayotolewa na sheria ya kitaifa.

**128.**

*Makarani na wafanyakazi wa Bunge.*

(1) Kutakuwa na Karani katika kila Kitengo cha Bunge, atakayeteuliwa na Tume ya Huduma za Bunge kupitia kwa idhini ya Kitengo cha Bunge kinachohusika.

(2) Ofisi za Makarani na ofisi za wafanyakazi wa Makarani zitakuwa ofisi katika Huduma ya Bunge.



SIO YA KUUZWA

# SURA YA TISA—KITENGO CHA SERIKALI CHA UTENDAJI

## Sehemu 1—Kanuni na Muundo wa Kitengo cha Utendaji cha Serikali ya Kitaifa.

**129.**

*Kanuni za mamlaka ya utendaji.*

(1) Mamlaka ya utendaji yametolewa na Wakenya na yatatekelezwa kulingana na Katiba hii.

(2) Mamlaka ya utendaji yatatekelezwa kwa namna ambayo inaambatana na kanuni ya huduma kwa Wakenya, na kwa ustawi na manufaa yao.

**130.**

*Mamlaka Kuu ya Kitaifa Inayosimamia Utendaji.*

(1) Kitengo cha Utendaji cha Serikali ya Kitaifa kina-jumuisha Rais, Naibu wa Rais na Baraza lote la Mawaziri.

(2) Muundo wa Kitengo cha Utendaji cha Serikali ya Kitaifa utaonyesha utofauti wa kieneo na kikabila wa Wakenya.

## Sehemu ya 2—Rais na Naibu wa Rais

**131.**

*Mamlaka ya Rais*

(1) Rais—

a) ndiye Kiongozi wa Taifa na Serikali;

b) ndiye anayetekeleza mamlaka ya utendaji ya Jamhuri, kwa usaidizi wa Naibu wa Rais na Mawaziri;

c) ndiye Amiri-Jeshi Mkuu wa Vikosi vya Ulinzi vya Kenya;

d) ndiye mwenyekiti wa Baraza la Kitaifa la Usalama; na

e) ni ishara ya umoja wa kitaifa.

(2) Rais—

a) ataiheshimu, kuitekeleza na kuilinda Katiba;



SIO YA KUUZWA

b) ataulinda uhuru wa Jamhuri ya Kenya;

c) atakuza na kuimarisha umoja wa taifa;

d) atakuza heshima ya utofauti wa watu najamii za Kenya; na

(3) atahakikisha ulinzi wa haki za kibinadamu na uhuru wa kimsingi, na utawala wa sheria.Rais hatahudumu katika ofisi yoyote nyingine ya Serikali au ya umma.

**132.**

*Majukumu ya Rais.*

(1) Rais—

a) atatoa hotuba katika kufunguliwa kwa kila Bunge jipya lililochaguliwa;

b) atahutubia kikao maalum cha Bunge mara moja kila mwaka na anaweza kuhutubia Bunge wakati mwingine wowote; na

c) mara moja kila mwaka—

i. anapohutubia taifa, atatoa ripoti kuhusu hatua zote ambazo zimechukuliwa na maendeleo ambayo yamepatikana katika ufikiaji wa maadili ya kitaifa yanayorejelewa katika Kifungu cha 10;

ii. atachapisha kwenye Gazeti Rasmi la Serikali maelezo kuhusu hatua zilizochukuliwa na maendeleo chini ya aya ndogo ya (i); na

iii. atawasilisha ripoti kwa Bunge la Kitaifa ili lijadiliwe kuhusu maendeleo ambayo yamepatikana katika utimizaji wa Jamhuri wa majukumu ya kimataifa. Katiba ya Kenya, 2010 77

(2) Rais atateua, na kwa idhini ya Bunge la Kitaifa, atateua kirasmi, na pia anaweza kuwaachisha kazi—

a) Mawaziri, kwa mujibu wa Kifungu cha 152;

b) Mwanasheria Mkuu, kwa mujibu wa Kifungu cha 156;

c) Katibu wa Baraza la Mawaziri, kwa mujibu wa Kifungu cha 154;

d) Makatibu Wakuu kwa mujibu wa Kifungu cha 155;

e) makamishna wakuu, mabalozi na wawakilishi wa kidiplomasia; na

f) kwa mujibu wa Katiba hii, afisa yeyote mwingine wa Serikali au wa umma ambaye kupitia kwa Katiba hii, Rais ana mamlaka ya kumteua au kumwachisha kazi.

(3) Rais—

a) ataongoza mikutano ya Baraza la Mawaziri;

b) ataelekeza na kuratibu majukumu ya wizara na idara za serikali; na

c) kwa uamuzi uliochapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali, atagawa majukumu ya utekelezaji wa Sheria ya Bunge kwa Waziri, kwa kiwango ambacho hakikinzani na Sheria yoyote ya Bunge.

(4) Rais anaweza—

a) kutekeleza jukumu lolote lingine la utendaji lililotolewa katika Katiba hii au katika sheria ya kitaifa na, isipokuwa Katiba hii inapoagiza vinginevyo, anaweza kubuni ofisi katika huduma ya umma kulingana na mapendekezo ya Tume ya Huduma kwa Umma;

b) kuwapokea mabalozi na wawakilishi wa kidiplomasia wa kigeni;

c) kutoa tuzo kwa jina la wananchi na la Jamhuri;



SIO YA KUUZWA

d) kulingana na Kifungu cha 58, kutangaza hali ya dharura; na

e) kwa idhini ya Bunge, anaweza kutangaza vita.

(5) Rais atahakikisha kwamba majukumu ya kimataifa ya Jamhuri yanatimizwa kupitia kwa utendaji wa Mawaziri husika.

**133.**

*Mamlaka ya Kuwasamehe Waliohukumiwa.*

(1) Kwa ombi la mtu yeyote, Rais anaweza kutekeleza mamlaka yake ya msamaha kwa mujibu wa ushauri wa Kamati ya Ushauri iliyoundwa chini ya ibara ya (2), kwa—

a) kumsamehe kabisa au kwa masharti mtu ambaye amepatikana na hatia;

b) kuahirisha utekelezaji wa adhabu iliyotolewa kwa muda uliowekwa au kwa muda usiojulikana;

c) kubadili adhabu kwa kiwango kisichokuwa na ukali sana; au

d) kuondoa adhabu yote au sehemu ya adhabu hiyo.

(2) kutakuwepo Kamati ya Ushauri kuhusu Mamlaka ya Msamaha wa Rais, itakayojumuisha—

a) Mwanasheria Mkuu;

b) Waziri anayehusika na huduma za urekebishaji; na

c) angalau watu wengine watano kama ilivyoagizwa na Sheria ya Bunge, lakini wasiwe maafisa wa Serikali au katika huduma ya umma.

(3) Bunge litatunga sheria ili kutoa mwongozo kuhusu—

a) muda wa kuhudumu kwa wanachama wa Kamati ya Ushauri;

b) taratibu za Kamati ya Ushauri; na

c) vigezo ambavyo vitatumiwa na Kamati ya Ushauri katika kufanya ushauri wake.



SIO YA KUUZWA

(4) Kamati ya Ushauri inaweza kuzingatia maoni ya waathiriwa wa hatia iliyotendwa wanapompendekezea Rais kuhusu msamaha wa hatia hiyo.

**134.**

*Matumizi ya mamlaka ya rais wakati wa urais wa muda mfupi*

(1) Mtu ambaye anahudumu kama Rais au yule ambaye ameidhinishwa kwa mujibu wa Katiba hii kutekeleza mamlaka ya Rais—

a) katika kipindi kinachoanzia mnamo tarehe ya kura ya kwanza kwenye uchaguzi wa rais, na kukamilika wakati Rais mpya aliyechaguliwa anapochukua hatamu za uongozi; au

b) kwa wakati ambao Rais hayupo au hawezi kutekeleza majukumu yake, au nyakati zingine zilizobainishwa katika kifungu cha 147 (3), hawezi kutekeleza mamlaka ya Rais yaliyotajwa katika ibara ya (2).

(2) Mamlaka yanayorejelewa katika ibara ya (1) ni—

a) uteuzi au uteuzi rasmi wa majaji wa mahakama ya ngazi juu;

b) uteuzi au uteuzi rasmi wa afisa yeyote mwingine wa umma ambaye Katiba hii au sheria hii inahitaji ateuliwe rasmi na Rais;

c) uteuzi au uteuzi rasmi au kuwachishwa kazi kwa Mawaziri na maafisa wengine wa umma au wa Serikali;

d) uteuzi au uteuzi rasmi au kuachishwa kazi kwa mabalozi au wawakilishi wa kibalozi na kidiplomasia;

e) mamlaka ya msamaha wa rais; na

f) mamlaka ya kutoa tuzo kwa jina la wananchi na la Jamhuri.



SIO YA KUUZWA

**135.** Uamuzi wa Rais katika utekelezaji wa jukumu lolote la Rais chini ya Katiba hii utakuwa kwa maandishi na utakuwa na muhuri na saini ya Rais. *Maamuzi ya Rais.*

**136.**

(1) Rais atachaguliwa na wapiga kura waliosajiliwa katika uchaguzi wa kitaifa utakaoendeshwa kwa mujibu wa Katiba hii na Sheria yoyote ya Bunge inayosimamia uchaguzi wa rais. *Uchaguzi wa Rais.*

(2) Uchaguzi wa Rais utafanyika––

a) katika siku sawa na ile ya uchaguzi mkuu wa Wabunge, ikiwa ni siku ya Jumanne ya pili ya mwezi Agosti, katika kila mwaka wa tano; au

b) katika hali ambazo zimebainishwa katika Kifungu cha 146.

**137.**

(1) Mtu anastahiki kuteuliwa kama mgombeaji wa urais ikiwa mtu huyo-— *Ustahiki na kutostahiki katika kuchaguliwa kama Rais.*

a) ni raia kwa kuzaliwa;

b) anastahiki kugombea uchaguzi kama mwana-chama wa Bunge;

c) ameteuliwa na chama cha kisiasa au ni mgombea huru; na

d) ameteuliwa na wapiga kura wasiopungua elfu mbili kutoka kila kaunti kwa idadi kubwa ya kaunti hizo.

(2) Mtu hastahiki kuteuliwa kama mgombea wa urais ikiwa mtu huyo-—

a) ameuweka uaminifu wake katika taifa la kigeni; au

b) ni afisa wa umma, au anahudumu katika ofisi yoyote ya Serikali au ya umma.



SIO YA KUUZWA

(3) Ibara ya (2) (b) haitatumika kwa—

a) Rais;

b) Naibu wa Rais; au

c) Mbunge.

**138.**

*Mchakati wa uchaguzi wa rais.*

(1) Ikiwa ni mgombea mmoja wa urais atakayeteuliwa, mgombeaji huyo atatangazwa kuwa amechaguliwa.

(2) Ikiwa ni wagombeaji wawili wa urais watakaoteuliwa, uchaguzi utafanyika katika kila eneobunge.

(3) Katika uchaguzi wa rais—

a) watu wote waliosajiliwa kama wapiga kura kwa madhumuni ya uchaguzi wa wabunge wana haki ya kupiga kura;

b) uchaguzi utakuwa kwa njia ya siri katika siku ambayo imeelezewa chini ya ibara ya 101 (1) na kwa wakati, mahali na kwa njia ambayo imeagizwa chini ya Sheria ya Bunge; na

c) baada ya kuhesabiwa kwa kura katika vituo vya kupigia kura, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka itahesabu na kuhakikisha hesabu ya kura na kutangaza matokeo.

(4) Mgombea wa urais atatangazwa kuchaguliwa kama Rais ikiwa mgombea huyo atapokea—

a) zaidi ya nusu ya kura zote zilizopigwa katika uchaguzi huo; na

b) angalau asilimia ishirini na tano ya kura zilizopigwa katika kila kaunti, katika zaidi ya idadi nusu ya kaunti zote.

(5) Ikiwa hakuna mgombea atakayechaguliwa, uchaguzi mwingine utafanyika upya katika kipindi cha siku thelathini baada ya uchaguzi uliopita, na katika



SIO YA KUUZWA

uchaguzi huo mpya, wagombeaji watakuwa tu—

a) mgombea au wagombea ambao walipokea kura nyingi zaidi; na

b) mgombeaji au wagombeaji ambao walipata idadi kubwa ya pili ya idadi ya kura.

(6) ikiwa wagombea zaidi ya mmoja atapokea idadi kubwa zaidi ya kura, ibara ya (5) (b) haitatumika na wagombeaji watakaokuwa katika uchaguzi mpya watakuwa wale ambao wamebainishwa katika ibara ya (5) (a).

(7) mgombeaji atakayepokea idadi kubwa zaidi ya kura katika uchaguzi mpya ndiye atakayetangazwa kuwa Rais.

(8) uchaguzi wa urais utafutiliwa mbali na uchaguzi mwingine mpya kufanyika ikiwa—

a) hakuna mtu ambaye ameteuliwa kama mgombea kabla ya kumalizika kwa kipindi kilichowekwa cha kuwasilisha walioteuliwa;

b) mgombeaji wa uchaguzi wa Rais au wa Naibu wa Rais atafariki katika au kabla ya tarehe ya kufanyika kwa uchaguzi; au

c) mgombea uchaguzi ambaye alistahili kutangazwa kuwa amechaguliwa kama Rais, atafariki kabla ya kutangazwa kuwa amechaguliwa kama Rais.

(9) Uchaguzi mpya wa urais chini ya ibara ya (8) utafanyika katika muda wa siku sitini baada ya tarehe iliyokuwa imewekwa ya uchaguzi uliopita.

(10) Katika muda wa siku saba baada uchaguzi wa urais, mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka—

a) atangaza matokeo ya uchaguzi; na

b) atawasilisha taarifa iliyoandikwa ya matokeo ya uchaguzi kwa Jaji Mkuu na Rais aliye mamlakani.

**139.**

*Kifo kabla ya kuchukua hatamu.*

(1) Ikiwa aliyetangazwa kuwa Rais-mteule atafariki dunia kabla ya kuchukua hatamu za uongozi––

a) Naibu wa Rais-mteule ataapishwa kama Rais wa muda mfupi mnamo tarehe ile ambayo Rais-mteule angeapishwa; na

b) uchaguzi mpya wa Rais utafanyika katika muda wa siku sitini baada ya kifo cha Rais-mteule.

(2) Ikiwa Naibu wa Rais-mteule atafariki kabla ya kuchukua hatamu za uongozi, kiti cha Naibu wa Rais kitatangazwa kuwa wazi baada ya Rais-mteule kuchukua hatamu za uongozi.

(3) Ikiwa watu wote wawili waliotangazwa kuchaguliwa kama Rais pamoja na Naibu wa Rais watafariki kabla ya kuchukua hatamu za uongozi––

a) Spika wa Bunge la Kitaifa atakuwa Rais wa muda mfupi kuanzia siku ambayo Rais mteule angeapishwa; na

b) uchaguzi mpya utafanyika katika muda wa siku sitini baada ya kifo cha pili.

**140.**

*Maswali kuhusu uhalali wa uchaguzi wa rais.*

(1) Mtu anaweza kuwasilisha ombi au malalamishi katika Mahakama ya Juu Zaidi ili kupinga uchaguzi wa Rais-mteule katika muda wa siku saba baada ya tarehe ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi wa urais.

(2) Katika muda wa siku kumi na nne baada ya kuwasilishwa kwa ombi au malalamishi, Mahakama ya Juu Zaidi itasikiza na kuamua kesi hiyo na uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

(3) Ikiwa Mahakama ya Juu Zaidi itaamua kuwa uchaguzi wa Rais mteule sio halali, uchaguzi mpya utafanyika katika muda wa siku sitini baada ya uamuzi huo.

**141.**

*Kuchukua hatamu za Urais.*

(1) Kuapishwa kwa Rais Mteule kutafanyika wazi na mbele ya Jaji Mkuu, au, ikiwa Jaji Mkuu hayupo, mbele ya Naibu Jaji Mkuu.

(2) Rais mteule ataapishwa Jumanne ya kwanza itakayofuata––

a) siku ya kumi na nne baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi wa urais, ikiwa hakuna kesi ya malalamishi iliyowasilishwa mahakamani chini ya Kifungu cha 140; au

b) siku ya saba kufuatia tarehe ambayo mahakama itatoa uamuzi na kutangaza kuwa uchaguzi ulikuwa halali, ikiwa kesi ya malalamishi iliwasilishwa chini ya Kifungu cha 140.

(3) Rais-mteule anachukua hatamu za uongozi kwa kula kiapo au kutoa uthibitisho wa uaminifu; na kiapo au uthibitisho wa kutekeleza majukumu ya ofisi kama ilivyoabainishwa katika Ambatisho la Tatu.

(4) Bunge, kupitia kwa sheria, litatoa taratibu za sherehe za kuapishwa kwa Rais-mteule.

**142.**

*Muda wa kuhudumu katika ofisi ya Rais.*

(1) Rais atahudumu kwa muhula utakaoanzia tarehe aliyoapishwa, na kukamilika wakati ambapo mtu atakayechaguliwa kuwa Rais mpya ataapishwa kwa mujibu wa Kifungu cha (136) (2) (a).

(2) Hakuna mtu atakayehudumu kama Rais kwa zaidi ya mihula miwili.



SIO YA KUUZWA

**143.**

*Ulinzi dhidi ya mashtaka.*

(1) Mashtaka yoyote ya jinai hayatafunguliwa au kusikizwa katika mahakama yoyote dhidi ya Rais au yeyote ambaye atakuwa anatekeleza majukumu ya ofisi hiyo wakati wa uongozi wake.

(2) Mashtaka katika kesi za madai hayatawasilishwa katika mahakama yoyote dhidi ya Rais au yeyote anayetekeleza majukumu ya ofisi hiyo kwa wakati wa uongozi wake, kutokana na chochote kilichofanywa au kutofanywa katika utekelezaji wa mamlaka yake chini ya Katiba hii.

(3) Iwapo mwongozo umetolewa katika sheria ili kudhibiti muda ambao mashtaka yanaweza kuwasilishwa dhidi ya mtu chini ya ibara ya (1) au (2), kipindi cha muda ambao mtu huyo anahudumu au kutekeleza majukumu ya ofisi ya Rais hazitazingatiwa katika kuhesabu kipindi cha wakati ambao umeagizwa na sheria hiyo.

(4) Kinga dhidi ya kushtakiwa kwa Rais katika Kifungu hiki, haitatumika kwa hatia ambayo Rais anaweza kushtakiwa chini ya mkataba wowote ambao Kenya imetia saini na ambao unatupilia mbali kinga hiyo.

**144.**

*Kuondolewa kwa Rais kwa misingi ya kukosa uwezo.*

(1) Mwanachama wa Bunge la Kitaifa anaweza kuwasilisha hoja Bungeni, ya kuchunguzwa kwa uwezo wa afya ya kiakili au ya kimwili ya Rais katika kutekeleza majukumu ya ofisi yake ikiwa ataungwa mkono na robo ya idadi ya wabunge wote.

(2) Ikiwa hoja chini ya ibara ya (1) itaungwa mkono na idadi kubwa ya wabunge katika Bunge la Kitaifa—

a) Spika wa Bunge atamjulisha Jaji Mkuu kuhusu uamuzi huo katika kipindi cha siku mbili; na

b) Rais ataendelea kutekeleza majukumu ya ofisi hiyo kabla ya matokeo ya taratibu zinazohitajika katika Kifungu hiki.

(3) Katika muda wa siku saba baada ya kupokea notisi ya uamuzi huo kutoka kwa Spika, Jaji Mkuu atateua kikundi cha watu watakaosikiza na kuamua swala hilo, ikijumuisha—

a) watu watatu ambao wanastahiki kuhudumu kama matabibu chini ya sheria za Kenya, na walioteuliwa na taasisi ambayo kwa kisheria inawajibika katika kudhibiti taaluma ya utabibu;

b) wakili mmoja wa Mahakama Kuu aliyeteuliwa na taasisi ambayo kisheria inawajibika katika kudhibiti utendakazi katika taaluma ya mawakili; na

c) mtu mmoja atakayeteuliwa na Rais.

(4) Ikiwa Jaji Mkuu atashindwa kuteua kikundi hiki chini ya ibara ya (3) , Naibu Jaji Mkuu atakiteua kikundi hicho.

(5) Ikiwa Rais atashindwa kumteua mtu anayehitajika kuteuliwa chini ya ibara ya (3) (c), mtu huyo atateuliwa na––

a) mwanafamilia katika familia ya Rais; au

b) ikiwa hakuna mwanafamilia yeyote ambaye yuko tayari au ana uwezo wa kufanya uteuzi huo, uteuzi huo utafanya na jamaa wa karibu wa Rais.

(6) Kikundi hicho kitachunguza suala hilo na kuripoti kwa Jaji Mkuu na Spika wa Bunge la Kitaifa katika muda wa siku kumi na nne baada ya kuteuliwa.

(7) Spika atawasilisha ripoti hiyo ya kikundi kilichoteuliwa mbele ya Bunge la Kitaifa katika kipindi cha muda wa siku saba baada ya kuipokea.



SIO YA KUUZWA

(8) Ripoti hiyo ya kikundi kilichoteuliwa itakuwa ya mwisho na isiyoweza kukatiwa rufaa na ikiwa kikundi hicho kitaripoti kwamba Rais ana uwezo wa kutekeleza majukumu ya ofisi hiyo, Spika wa Bunge la Kitaifa atatangaza ripoti hiyo katika Bunge la Kitaifa.

(9) Ikiwa kikundi hicho kitaripoti kwamba Rais hana uwezo wa kutekeleleza majukumu ya ofisi hiyo, Bunge la Kitaifa litapiga kura ya kuidhinisha au kutoidhinisha ripoti hiyo.

(10) Ikiwa idadi kubwa ya wabunge wote katika Bunge la Kitaifa watapiga kura ya kuunga mkono kuidhinishwa kwa ripoti hiyo, Rais atang'atuka mamlakani.

**145.**

*Kuondolewa kwa Rais kupitia kura ya kutokuwa na imani naye.*

(1) Mwanachama katika Bunge la Kitaifa, iwapo ataungwa mkono na thuluthi moja ya wabunge wote, anaweza kuwasilisha hoja ya kutokuwa na imani na Rais—

a) kwenye msingi wa ukiukaji mkubwa wa Kifungu cha Katiba hii au sheria nyingine yoyote;

b) ikiwa kuna sababu muhimu za kuamini kwamba Rais amehusika katika uhalifu chini ya sheria za kitaifa au kimataifa; au

c) kwenye msingi wa mwenendo mbaya zaidi ofisini.

(2) Ikiwa thuluthi mbili ya wabunge wote katika Bunge la Kitaifa wataunga mkono hoja chini ya ibara ya (1)—

a) Spika atamuarifu Spika wa Bunge la Seneti kuhusu uamuzi huo katika muda wa siku mbili; na

b) Rais ataendelea kutekeleza majukumu ya ofisi hiyo kabla ya matokeo ya taratibu zinazohitajika katika Kifungu hiki.

(3) Katika kipindi cha siku saba baada ya kupokea notisi ya uamuzi kutoka kwa Spika wa Bunge la Kitaifa—



SIO YA KUUZWA

a) Spika wa Seneti ataandaa mkutano wa Seneti ili kusikia mashtaka dhidi ya Rais; na

b) Bunge la Seneti, kwa uamuzi wake, linaweza kuteua kamati maalum itakayojumuisha maseneta kumi na moja ili kuchunguza suala hilo.

(4) Kamati maalum iliyoteuliwa chini ya ibara ya (3) (b)—

a) itachunguza suala hilo; na

b) kuripotikwaSenetikatikamudawasikukumiikiwa tuhuma dhidi ya Rais zimethibitishwa kwa maoni ya Kamati hiyo.

(5) Rais atakuwa na haki ya kufika na kuwakilishwa mbele ya Kamati hiyo maalum wakati wa uchunguzi.

(6) Ikiwa Kamati Maalum itaripoti kwamba maelezo yaliyotolewa katika tuhuma dhidi ya Rais—

a) hayajathibitishwa, hakuna usikilizaji zaidi utakaoendelea chini ya Kifungu hiki unaohusiana na tuhuma hizo.

b) yamethibitishwa, Bunge la Seneti litapiga kura katika mashtaka ya kutokuwa na imani baada ya kumpa Rais nafasi ya kusikizwa.

(7) Ikiwa angalau thuluthi mbili ya wanachama wote wa Seneti watapiga kura ya kukubaliana na mashtaka ya kutokuwa na imani, Rais ataondoka ofisini.

**146.**

*Nafasi Katika Ofisi ya Rais.*

(1) Ofisi ya Rais itakuwa wazi ikiwa anayehudumu katika ofisi hiyo—

a) Atafariki dunia;

b) atajiuzulu kwa kumwandikia barua Spika wa Bunge la Kitaifa; au



SIO YA KUUZWA

c) atakapoondoka ofisini vinginevyo chini ya Kifungu cha 144 au cha 145 au chini ya Kifungu kingine cha Katiba hii.

(2) Nafasi inapotokea katika ofisi ya Rais—

a) Naibu wa Rais atahudumu kama Rais kwa muda uliosalia wa muhula wa Rais; au

b) Ikiwa kuna nafasi katika ofisi ya Naibu wa Rais, au Naibu wa Rais hawezi kuhudumu kama Rais, Spika wa Bunge la Kitaifa atahudumu kama Rais na uchaguzi wa urais utafanyika katika muda wa siku sitini baada ya nafasi hiyo kutokea katika ofisi ya Rais.

(3) Mtu atakayehudumu kama Rais chini ya ibara ya (2) (a) au kufuatia uchaguzi unaohitajika chini ya ibara ya (2) (b), isipokuwa aondolewe mamlakani kwa mujibu wa Katiba hii, ataendelea kuhudumu kama Rais hadi wakati ambapo Rais aliyechaguliwa upya aapishwe baada ya uchaguzi unaofuatia kama ilivyoratibiwa chini ya Kifungu cha 136 (1).

(4) Ikiwa Naibu wa Rais atahudumu kama Rais chini ya ibara ya (2) (a) au mtu achaguliwe kuwa Rais chini ya Ibara ya (2) (b), Naibu wa Rais au mtu huyo aliyechaguliwa atachukuliwa kwa madhumuni ya Kifungu cha 142 (2) kuwa—

a) amehudumu kama Rais kwa muhula mzima ikiwa katika tarehe

b) ambayo mtu huyo alianza kuhudumu, kumesalia zaidi ya miaka miwili na nusu kabla ya tarehe ya uchaguzi ulioratibiwa kikawaida chini ya Kifungu cha 136 (2) (a); au

c) hajahudumu kama Rais kwa muhula mzima katika hali ingine yoyote.



SIO YA KUUZWA

**147.**

*Majukumu ya Naibu wa Rais.*

(1) Naibu wa Rais ndiye atakayekuwa msaidizi mkuu wa Rais na atakuwa kaimu wa Rais katika utekelezaji wa majukumu ya Rais.

(2) Naibu wa Rais atatekeleza majukumu yaliyotolewa na Katiba hii na majukumu mengine yoyote ya Rais ambayo Rais anaweza kutoa.

(3) Kwa mujibu wa Kifungu cha 134, wakati ambapo Rais hayupo au hawezi kutekeleza majukumu yake kwa muda mfupi, na katika kipindi kingine chochote ambacho Rais anaweza kuamua, Naibu wa Rais atahudumu kama Rais.

(4) Naibu Rais hatahudumu katika ofisi nyingine ya Serikali au ya umma.

**148.**

*Kuchaguliwa na Kuapishwa kwa Naibu wa Rais.*

(1) Kila mgombea katika uchaguzi wa urais atateua mtu ambaye anastahiki kuteuliwa kuwa mgombeaji wa urais, kama mgombeaji wa kiti cha Naibu wa Rais.

(2) Kwa madhumuni ya ibara ya (1), hakutakuwa na mchakato tofauti wa kumteua Naibu wa Rais na Kifungu cha 137 (1) (d) hakitatumika kwa mgombea wa kiti cha Naibu wa Rais.

(3) Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka itamtangaza mgombeaji aliyeteuliwa na mtu ambaye amechaguliwa kuwa Rais, kuwa amechaguliwa kama Naibu wa Rais.

(4) Kuapishwa kwa Naibu wa Rais mteule kutafanyika mbele ya Jaji Mkuu, au iwapo Jaji Mkuu hayupo, mbele ya Naibu wa Jaji Mkuu na kwa uwazi.

(5) Naibu wa Rais mteule atachukua hatamu za uongozi kwa—

a) kula kiapo au kutoa uthibitisho wa uaminifu; na

b) Kula kiapo au kutoa uthibitisho wa kutekeleza majukumu ya ofisi,kama ilivyoagizwa katika Ambatisho la Tatu.

(6) Muhula wa kuhudumu kama Naibu wa Rais utaanzia tarehe ya kuapishwa kwa Naibu wa Rais, na utakamilika—

a) wakati ambapo mtu atakayechaguliwa kuwa Rais anayefuata katika uchaguzi chini ya Kifungu cha (136) (2) (a) ataapishwa;

b) Naibu wa Rais anapohudumu kama Rais; au

c) kwa kijiuzulu, kufariki au kuondolewa mamlakani kwa Naibu wa Rais.

(7) Naibu wa Rais anaweza, kwa wakati wowote, kujiuzulu kwa kumwandikia barua Rais na kujiuzulu huko kutatekelezeka katika saa na tarehe iliyobainiwa katika barua hiyo, au ikiwa tarehe haijabainishwa, adhuhuri ya siku ifuatayo baada ya kupokelewa kwa barua hiyo.

(8) Hakuna mtu yoyote atakayehudumu kama Naibu wa Rais kwa zaidi ya mihula miwili.

**149.**

*Nafasi Katika ofisi ya Naibu wa Rais.*

(1) Katika muda wa siku kumi na nne baada ya nafasi kutokea katika ofisi ya Naibu wa Rais, Rais atamteua mtu mwingine kuijaza nafasi hiyo, na Bunge la Kitaifa litapiga kura kuhusu uteuzi huo katika muda wa siku sitini baada ya kuupokea.

(2) Ikiwa mtu atahudumu kama Naibu wa Rais chini ya ibara ya (1), basi, kwa madhumuni ya Kifungu cha 148 (8), mtu huyo atachukuliwa—

a) kuwa amehudumu katika muhula mzima kama Naibu wa Rais ikiwa, kwa wakati ambao mtu huyo alianza kuhudumu katika ofisi hiyo, zaidi

ya miaka miwili na nusu inasalia kabla ya uchaguzi unaofuatia ulioratibiwa chini ya Kifungu cha 136 (2); au

b) hajahudumu kama Rais kwa muhula mzima katika hali ingine yoyote.

**150.**

*Kuondolewa kwa Naibu wa Rais.*

(1) Naibu wa Rais anaweza kuondolewa ofisini—

a) kwenye msingi wa kutokuwa na uwezo wa kiakili au kimwili wa kutekeleza majukumu ya ofisi; au

b) kwa kura ya kutokuwa na imani—

i. kwenye msingi wa kukiuka Katiba hii au sheria yoyote nyingine;

ii. iwapo kuna sababu kuu za kuamini kwamba Naibu wa Rais amefanya uhalifu chini ya sheria ya kitaifa au ya kimataifa; au

iii. kwenye msingi wa mwenendo mbaya zaidi ofisini.

(2) Sheria katika Vifungu vya 144 na 145 vinavyohusiana na kuondolewa mamlakani kwa Rais, kwa kuzingatia mabadiliko yanayostahili, itatumika katika kumuondoa Naibu wa Rais.

**151.**

*Malipo na manufaa ya Rais na Naibu wa Rais.*

(1) Mshahara na manufaa ambayo Rais na Naibu wa Rais watapata utatolewa kwenye Hazina Jumuishi.

(2) Malipo, manufaa na haki maalum wanazopata Rais na Naibu wa Rais hayatabadilishwa kwa lengo la kutowanufaisha wakiwa ofisini.

(3) Malipo ya uzeeni anayopaswa kulipwa Rais mstaafu na Naibu wa Rais mstaafu pamoja na haki maalum na marupurupu mengine wanayopata hayatabadilishwa ili kutowanufaisha katika maisha yao yote.

**Sehemu ya 3 – Baraza la Mawaziri**

**152.**

*Baraza la Mawaziri.*

(1) Baraza la Mawaziri linajumuisha—

a) Rais;

b) Naibu wa Rais;

c) Mwanasheria Mkuu; na

d) Mawaziri wasiopungua kumi na wanne au wasiozidi ishirini na wawili.

(2) Rais atawapendekeza, na kwa idhini ya Bunge la Kitaifa kuwateua Mawaziri.

(3) Waziri hatakuwa Mbunge.

(4) Kila mtu atakayeteuliwa kama Waziri—

a) ataanza kuhudumu kwa kuapa au kutoa thibitisho la uaminifu kwa watu na Jamhuri ya Kenya na kuapa kuitii Katiba hii, mbele ya Rais na kwa mujibu wa Ambatisho la Nne; na

b) anaweza kujiuzulu kwa kumwasilishia Rais taarifa iliyoandikwa ya kujiuzulu kwake.

(5) Rais––

a) anaweza kubadilisha wizara ambayo Waziri atahudumu;

b) anaweza kumwachisha kazi Waziri; na

c) atamwachisha kazi Waziri iwapo atahitajika kufanya hivyo, kwa uamuzi uliokubaliwa chini ya ibara ya (6) hadi (10).

(6) Mwanachama wa Bunge la Kitaifa anayeungwa mkono na angalau robo moja ya wabunge wote katika Bunge la Kitaifa, anaweza kupendekeza hoja wa kumtaka Rais amwachishe kazi Waziri—

a) kwenye msingi wa ukiukaji mkubwa wa Kifungu cha Katiba hii au sheria nyingine yoyote;

b) Iwapo kuna sababu kuu za kuamini kwamba Waziri huyo amefanya uhalifu chini ya sheria ya kitaifa au ya kimataifa; au

c) kwa msingi wa mwenendo mbaya zaidi ofisini.

(7) Ikiwa hoja chini ya ibara ya (5) itaungwa mkono na angalau thuluthi moja ya wabunge wote katika Bunge la Kitaifa—

a) Bunge la Kitaifa litateua kamati maalum akayojumuisha wanachama kumi na mmoja kuchunguza suala hili; na

b) katika muda wa siku kumi, kamati hii maalum itaripoti kwa Bunge la Kitaifa ikiwa limepata madai dhidi ya Waziri kuthibitishwa.

(8) Waziri ana haki ya kufika au kuwakilishwa mbele ya kamati maalum wakati wa uchunguzi wake.

(9) Ikiwa kamati hiyo maalum itaripoti kwamba imepata madai hayo

a) othibitishwa, hakuna taratibu zingine zitakazofuatwa; au

b) kuthibitishwa, Bunge la Kitaifa––

i. litampa Waziri nafasi ya kusikizwa; na

ii. litapiga kura ili kuidhinisha uamuzi unaomtaka Waziri kuachishwa kazi.

(10) Ikiwa uamuzi ulio chini ya ibara ya (8) unaomtaka Rais kumwachisha kazi Waziri utaungwa mkono na idadi kubwa ya wabunge katika Bunge la Kitaifa––

a) Spika atamwasilishia Rais uamuzi huu kwa haraka; na

b) Rais atamwachisha kazi Waziri huyo.



SIO YA KUUZWA

**153.**

*Maamuzi, majukumu na kuwajibika kwa Baraza la Mawaziri.*

(1) Uamuzi wa Baraza la Mawaziri utakuwa kwa maandishi.

(2) Mawaziri wanawajibika kibinafsi na kwa pamoja kwa Rais katika utekelezaji wa mamlaka yao na utendakazi wa majukumu yao.

(3) Waziri atahudhuria kikao cha kamati ya Bunge la Kitaifa au Seneti, anapohitajiwa na kamati, na kujibu swali lolote kuhusu suala linalomhusu.

(4) Mawaziri––

a) watatekeleza majukumu yao kulingana na Katiba hii; na

b) watawasilisha kwa Bunge ripoti kamili na za mara kwa mara kuhusu masuala yaliyo chini ya udhibiti wao.

**154.**

*Katibu wa Baraza la Mawaziri;*

(1) Ofisi ya Katibu katika Baraza la Mawaziri imebuniwa, ambayo ni ofisi katika huduma ya umma.

(2) Katibu katika Baraza la Mawaziri—

a) atapendekezwa, na kwa idhini ya Bunge la Kitaifa kuteuliwa na Rais; na

b) anaweza kuachishwa kazi na Rais.

(3) Katibu katika Baraza la Mawaziri—

a) atasimamia ofisi ya Baraza la Mawaziri;

b) atakuwa na jukumu la kupanga shughuli na kuweka kumbukumbu za mikutano ya Baraza la Mawaziri, kulingana na maelekezo ya Baraza hilo;

c) atawasilisha uamuzi wa Baraza la Mawaziri kwa watu au mamlaka zinazofaa; na

d) atakuwa na majukumu mengine kama atakavyoelekezwa na Baraza la Mawaziri.

(4) Katibu katika Baraza la Mawaziri anaweza kujiuzulu kwa kutoa notisi kwa njia ya maandishi, kwa Rais.

**155.**

*Makatibu Wakuu.*

(1) Ofisi ya Katibu Mkuu limebuniwa, ambayo ni ofisi katika huduma ya umma.

(2) Kila idara ya Serikali itakuwa chini ya usimamizi wa Katibu Mkuu.

(3) Rais—

a) atapendekeza mtu ili ateuliwa kama Katibu Mkuu kutoka miongoni mwa wale watakaopendekezwa na Tume ya Huduma za Umma; na

b) atawateua Makatibu Wakuu kwa idhini ya Bunge la Kitaifa.

(4) Rais anaweza kubadilisha idara ambayo itasimamiwa na Katibu Mkuu.

(5) Katibu Mkuu anaweza kujiuzulu kwa kumwandikia Rais notisi.

**Sehemu ya 4—Ofisi Zinginezo**

**156.**

*Mwanasheria Mkuu.*

(1) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Imebuniwa.

(2) Mwanasheria Mkuu atapendekezwa na Rais, na kwa idhini ya Bunge la Kitaifa, kuteuliwa na Rais.

(3) Ustahiki katika kuteuliwa kama Mwanasheria Mkuu ni sawa na wa kuteuliwa katika ofisi ya Jaji Mkuu.

(4) Mwanasheria Mkuu—

a) ndiye mshauri mkuu wa kisheria katika Serikali.

b) atawakilisha Serikali ya kitaifa mahakamani au katika kesi zinginezo za kisheria ambazo serikali ya kitaifa inahusika, isipokuwa kesi za jinai; na

c) atatekeleza majukumu mengine yoyote yatakayotolewa na Sheria ya Bunge au Rais.



SIO YA KUUZWA

(5) Mwanasheria Mkuu atakuwa na mamlaka, kwa ruhusa ya mahakama, ya kuisaidia mahakama katika kutatua kesi za uraia ambazo Serikali sio mhusika.

(6) Mwanasheria Mkuu ataukuza, kuulinda na kuutetea utawala wa sheria na kutetea maslahi ya umma.

(7) Mamlaka ya Mwanasheria Mkuu yanaweza kutekelezwa kibinafsi au kupitia kwa maafisa wasaidizi watakaotekeleza majukumu hayo kulingana na maagizo maalum au ya kijumla.

**157.**

*Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma.*

(1) Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma imebuniwa.

(2) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma atapendekezwa na Rais, na kwa idhini ya Bunge la Kitaifa, atateuliwa na Rais.

(3) Ustahiki wa kuteuliwa kama Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma ni sawa na zile wa uteuzi wa Jaji wa Mahakama Kuu.

(4) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma atakuwa na mamlaka ya kumwagiza Inspekta Jenerali wa Huduma ya Polisi ya Kitaifa kuchunguza habari yoyote au madai ya vitendo vya jinai, na Inspekta Jenerali huyo atafuata maelekezo hayo.

(5) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma atahudumu kwa muhula wa miaka minane na hatastahiki kuteuliwa tena.

(6) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma atatekeleza mamlaka ya Serikali ya kufungua mashtaka na anaweza—

a) kufungua mashtaka katika kesi ya uhalifu dhidi ya mtu yeyote katika mahakama yoyote (isipokuwa mahakama ya kijeshi) kutokana na kosa lolote linalodaiwa kufanywa;



SIO YA KUUZWA

b) kuchukua na kuendeleza kesi zozote ya uhalifu zilizoanzishwa katika mahakama yoyote (isipokuwa katika mahakama ya kijeshi) na ambazo zilifunguliwa au kusimamiwa na mtu mwingine au mamlaka nyingine; na

c) kwa mujibu wa ibara ya (7) na (8), kusitisha, kwa wakati wowote kabla ya hukumu kutolewa, kuendelea kwa kesi zozote za jinai, zilizowasilishwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka ya Umma au kuendelezwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka ya umma chini ya aya ya (b)

(7) Ikiwa kusitishwa kwa kesi zozote chini ya ibara ya (6) (c) kutafanyika baada ya upande wa mashtaka kufunga kesi yao, mshtakiwa ataachiliwa huru.

(8) Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka ya Umma hawezi kusitisha kuendelea kwa kesi bila ruhusa ya mahakama.

(9) Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma yanaweza kutekelezwa naye kibinafsi au kupitia kwa maafisa wasaidizi watakaotekeleza mamlaka hayo kulingana na masharti maalum au ya kijumla.

(10) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma hatahitaji idhini ya mtu au mamlaka yoyote ili kuwasilisha kesi za kijinai, na katika kutekeleza mamlaka au majukumu yake hataelekezwa au kudhibitiwa na mtu au mamlaka yoyote.

(11) Katika kutekeleza mamlaka yaliyotolewa na Kifungu hiki, Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma atazingatia maslahi ya umma, utekelezaji wa haki na hitaji la kuzuia na kuepuka matumizi mabaya ya mchakato wa kisheria.



*SIO YA KUUZWA*

(12) Bunge linaweza kutunga sheria itakayotoa mamlaka ya kufungua mashtaka kwa taasisi zingine kando na Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma.

**158.**

*Kuondolewa na kujiuzulu kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma.*

(1) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma anaweza kuondolewa ofisini kwenye misingi ya—

a) kutoweza kutekeleza majukumu ya ofisi hiyo kutokana na kukosa uwezo wa kiakili au wa kimwili;

b) kutozingatia Sura ya Sita;

c) kufilisika;

d) kutokuwa na uzoefu unaohitajika; au

e) mwenendo mbaya zaidi ofisini au tabia mbaya.

(2) Mtu anayetaka kuondolewa mamlakani kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma anaweza kuwasilisha ombi au malalamishi kwa Tume ya Huduma za Umma ambayo yatakuwa kwa njia ya maandishi, yakiainisha madai yanayounda msingi wa kuondolewa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma.

(3) Tume ya Huduma za Umma itajadili malalamishi hayo na ikiridhika kwamba yanafichua kuwepo kwa msingi wa kuondolewa ofisini chini ya Ibara ya (1), itawasilisha ombi au malalamishi hayo kwa Rais.

(4) Baada ya kupokea na kuchunguza ombi au malalamishi hayo, Rais, katika muda wa siku kumi na nne, atamsimamisha kazi Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma kabla ya hatua kuchukuliwa na Rais kulingana na ibara ya (5) na kwa ushauri wa Tume ya Huduma za Umma, atateua kikundi cha watu watakaosikiza na kutoa uamuzi kuhusu ombi hilo, itakayojumuisha—

a) wanachama wanne kutoka miongoni mwa wale ambao wanahudumu au wamewahi kuhudumu

kama majaji katika mahakama ya ngazi ya juu, au wanaostahiki kuteuliwa kuwa majaji katika mahakama ya ngazi ya juu;

b) wakili mmoja ambaye amehudumu kwa angalau miaka kumi na mitano na atakayeteuliwa na taasisi ya kisheria inayowajibika katika udhibiti wa taaluma ya mawakili; na

c) watu wengine wawili walio na uzoefu katika masuala ya umma.

(5) Kikundi hicho kitachunguza swala hilo kwa haraka na kuripoti kuhusu ukweli uliopo na kutoa mapendekezo kwa Rais, ambaye atachukua hatua kulingana na mapendekezo ya kikundi hicho.

(6) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma, ambaye amesimamishwa kazini kulingana na ibara ya (4) atapokea nusu ya mshahara wake hadi atakapoondolewa au kurudishwa ofisini kwake.

(7) Kikundi kitakachoteuliwa chini ya ibara ya (4) kitamchagua mwenyekiti miongoni mwao wanachama wake.

(8) Kikundi kitakachoteuliwa chini ya ibara ya (4) kitakuwa na jukumu la kudhibiti taratibu zake.

(9) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma anaweza kujiuzulu kwa kumwandikia Rais notisi.



*SIO YA KUUZWA*

# SURA YA KUMI—KITENGO CHA SERIKALI KINACHOSIMAMIA MAHAKAMA

## Sehemu ya 1 – Mamlaka ya Mahakama na Mfumo wa Kisheria

**159.**

*Mamlaka ya mahakama.*

(1) Mamlaka ya Mahakama yametolewa na wananchi na yatatekelezwa na mahakama na taasisi zilizo na mamlaka ya mahakama zilizobuniwa chini ya Katiba hii.

(2) Katika kutekeleza mamlaka ya mahakama, mahakama na taasisi zilizo na mamlaka ya mahakama zitaongozwa na kanuni zifuatazo—

a) haki itatendewa wote, bila kuzingatia hadhi;

b) utekelezaji wa haki hautacheleweshwa;

c) njia mbadala za kusuluhisha kesi, ikijumuisha upatanishi, mashauriano, maridhiano na njia za kitamaduni za kusuluhisha mizozo zitakuzwa, lakini kulingana na ibara ya (3);

d) haki itatekelezwa bila kuzingatia kwa uzito changamoto za kiutaratibu; na

e) lengo na kanuni za Katiba hii zitalindwa na kukuzwa.

(3) Mbinu za kitamaduni za kusuluhisha mizozo hazitatumiwa kwa njia ambayo—

a) inakiuka Sheria za Haki;

b) Haikubaliki kimaadili na katika haki au inayosababisha matokeo ambayo sio ya haki au yasiyokubalika kimaadili;

c) haiambatani na Katiba hii au na sheria yoyote iliyoandikwa.

**160.**

*Uhuru wa Mahakama.*

(1) Katika utekelezaji wa mamlaka ya mahakama, Kitengo cha Serikali Kinachosimamia Mahakama, kama

kilivyobuniwa chini ya Kifungu cha 161, kitazingatia Katiba hii na sheria, na hakitadhibitiwa wala kuelekezwa na mtu au mamlaka yoyote.

(2) Afisi ya jaji wa mahakama iliyo katika ngazi ya juu haitafutiliwa mbali wakati ambao kuna afisa anayehudumu katika afisi hiyo.

(3) Mishahara na marupurupu ambayo majaji wanalipwa yatatoka katika Hazina Jumuishi.

(4) Kwa kuzingatia Kifungu cha 168 (6), mishahara na marupurupu ambayo jaji anapaswa kulipwa, hayatabadilishwa kwa njia itakayomwathiri, na manufaa ya kustaafu ya jaji aliyestaafu hayatabadilishwa ili kumuathiri jaji huyo mstaafu katika maisha yake yote.

(5) Mwanachama wa mahakama hatawajibika katika hatua au kesi inayohusiana na chochote kilichofanywa au ambacho hakikufanywa kwa nia njema katika utendakazi wa kisheria majukumu ya mahakama yanapotekelezwa.

**161.**

*Ofisi na maafisa wa mahakama.*

(1) Kitengo cha Mahakama kinajumuisha majaji wa mahakama za ngazi ya juu, mahakimu na maafisa na wafanyakazi wengine katika Kitengo cha Mahakama.

(2) Imebuniwa ofisi ya––

a) Jaji Mkuu, ambaye atayekuwa Kiongozi wa Kitengo cha Mahakama;

b) Naibu Jaji Mkuu, atakayekuwa Naibu Mkuu katika Kitengo cha Mahakama;

c) Msajili Mkuu katika Kitengo cha Mahakama, ambaye atakuwa msimamizi mkuu wa kiutawala na afisa wa uhasibu wa Kitengo cha Mahakama.

(3) Tume ya Huduma za Mahakama inaweza kubuni ofisi zingine za msajili itakavyohitajika.



SIO YA KUUZWA

**162.**

*Mfumo wa mahakama.*

(1) Mahakama za ngazi ya juu ni Mahakama ya Juu Zaidi, Mahakama ya Rufaa, Mahakama Kuu na mahakama zilizotajwa katika ibara ya (2).

(2) Bunge litabuni mahakama zenye hadhi ya Mahakama Kuu ili kusikiliza na kuamua mizozo inayohusu—

a) ajira na mahusiano ya kikazi; na

b) mazingira, matumizi, hatimiliki na umiliki wa ardhi.

(3) Bunge litaamua mamlaka na majukumu ya mahakama zinazobainishwa katika ibara ya (2).

(4) Mahakama za ngazi ya chini ndizo mahakama zilizobuniwa chini ya Kifungu cha 169, au zilizobuniwa na Bunge kulingana na Kifungu hicho.

**Sehemu ya 2—Mahakama za Ngazi ya Juu**

**163.**

*Mahakama ya Juu Zaidi.*

(1) Mahakama ya Juu Zaidi imebuniwa, na itajumuisha—

a) Jaji Mkuu, ambaye atakuwa rais wa mahakama hiyo;

b) Naibu Jaji Mkuu, ambaye—

i. atakuwa naibu wa Jaji Mkuu; na

ii. atakuwa naibu wa rais wa mahakama hiyo; na

c) majaji wengine watano.

(2) Katika usikilizaji wa kesi, mahakama itakuwa imepangwa vizuri ikiwa itakuwa na majaji watano.

(3) Mahakama ya Juu Zaidi—

a) itakuwa na mamlaka ya kipekee na ya kiasili ya kusikiliza na kuamua kesi zinazohusu uchaguzi wa urais chini ya Kifungu cha 140; na

b) Kwa kuzingatia ibara ya (4) na (5), itakuwa na mamlaka ya rufaa ya kusikiliza na kuamua rufaa kutoka—

i. Mahakama ya Rufaa; na

ii. mahakama nyingine yoyote au taasisi iliyo na mamlaka ya mahakama itakavyoagizwa kupitia kwa sheria ya kitaifa.

(4) Kukatwa Rufaa kutatoka Mahakama ya Rufaa hadi Mahakama ya Juu Zaidi—

a) kwa msingi wa haki katika kesi yoyote inayohusiana na ufasiri na utekelezaji wa Katiba hii; na

b) katika kesi nyingine yoyote ambayo Mahakama ya Juu Zaidi au Mahakama ya Rufaa itathibitisha kwamba suala lililohusishwa lina umuhimu wa kijumla kwa umma, lakini kwa kuzingatia ibara ya (5).

(5) Uthibitisho wa Mahakama ya Rufaa chini ya ibara ya (4) (b) unaweza kukaguliwa na Mahakama ya Juu Zaidi, na kisha kukubaliwa, kurekebishwa au kufutiliwa mbali.

(6) Mahakama ya Juu Zaidi inaweza kutoa maoni ya ushauri kwa serikali ya kitaifa, kitengo chochote cha Serikali, au kwa serikali yoyote ya kaunti katika suala lolote linalohusiana na serikali ya kaunti iwapo litaombwa kufanya hivyo.

(7) Mahakama zingine zote ila Mahakama ya Juu Zaidi zitafuata maamuzi ya Mahakama ya Juu Zaidi.

(8) Mahakama ya Juu Zaidi itatunga sheria zitakazoongoza utekelezaji wa mamlaka yake.

(9) Sheria ya Bunge inaweza kutoa mwongozo zaidi kuhusu utendakazi wa Mahakama ya Juu Zaidi.



*SIO YA KUUZWA*

**164.**

*Mahakama ya Rufaa.*

(1) Mahakama ya Rufaa imebuniwa, ambayo—

a) itakuwa na idadi ya majaji ambao hawatapungua kumi na wawili kulingana na Sheria ya Bunge; na

b) itapangwa na kusimamiwa kulingana na mwongozo utakaotolewa na Sheria ya Bunge.

(2) Kutakuwa na Rais wa Mahakama ya Rufaa ambaye atachaguliwa na majaji wa Mahakama ya Rufaa kutoka miongoni mwao.

(3) Mahakama ya Rufaa ina mamlaka ya kusikiliza kesi za rufaa kutoka—

a) Mahakama Kuu; na

b) Mahakama au taasisi yoyote nyingine iliyo na mamlaka ya mahakama kama itakavyoagizwa kupitia kwa Sheria ya Bunge.

**165.**

(1) Mahakama Kuu imebuniwa, ambayo—

a) itakuwa na idadi ya majaji kama itakavyobainishwa katika Sheria ya Bunge;

b) itapangwa na kusimamiwa kulingana na Sheria ya Bunge.

(2) Kutakuwa na Jaji Kinara wa Mahakama Kuu, ambaye atachaguliwa na majaji wa Mahakama Kuu kutoka miongoni mwao.

(3) Kwa kuzingatia ibara ya (5), Mahakama Kuu—

a) Itakuwa na mamlaka ya kiasili katika kesi za jinai na kesi za kiraia;

b) mamlaka ya kubaini iwapo haki au uhuru wa kimsingi katika Sheria za Haki imezuiwa, kukiukwa, kuvunjwa au kutishiwa; au

c) mamlaka ya kusikiliza kesi ya rufaa kutoka katika



*SIO YA KUUZWA*

uamuzi wa taasisi iliyo na mamlaka ya mahakama iliyoteuliwa chini ya Katiba hii kuchunguza kuondolewa kwa mtu ofisini, isipokuwa taasisi iliyoteuliwa chini ya Kifungu cha 144;

d) mamlaka ya kusikiliza suala lolote kuhusu kufasiriwa kwa Katiba hii ikijumuisha—

i. iwapo sheria yoyote haiambatani na, au inakiuka, Katiba hii;

ii. iwapo chochote kinachosemekana kutekelezwa chini ya mamlaka ya Katiba hii au sheria yoyote, hakiambatani, au kinakiuka, Katiba hii;

iii. suala lolote linalohusu mamlaka ya kikatiba ya vitengo vya serikali katika serikali za kaunti na suala lolote linalohusu uhusiano wa kikatiba kati ya ngazi za serikali; na

iv. swali linalohusu mkinzano wa sheria chini ya Kifungu cha 191; na

e) swala kuhusu mamlaka yake mengine yoyote, ya kiasili au ya rufaa, ambayo yametolewa na sheria.

(4) Suala lolote linalothibitishwa na mahakama kuwa linazua utata mkubwa kisheria chini ya ibara ya (3) (b) au (d) litasikilizwa na idadi isiyo shufwa ya majaji, na isiyopungua watatu, watakaoteuliwa na Jaji Mkuu.

(5) Mahakama Kuu haitakuwa na mamlaka kuhusiana na masuala—

a) yaliyotengewa mamlaka ya kipekee ya Mahakama ya Juu Zaidi chini ya Katiba hii; au

b) yaliyo chini ya mamlaka ya mahakama zilizotajwa katika Kifungu cha 162 (2).



SIO YA KUUZWA

(6) Mahakama Kuu ina mamlaka ya kusimamia mahakama za ngazi ya chini, mtu yeyote, taasisi au halmashauri inayotekeleza jukumu la kimahakama, lakini sio mahakama ya ngazi ya juu.

(7) Kwa malengo ya ibara ya (6), Mahakama Kuu inaweza kuitisha kumbukumbu za kesi yoyote inayoendelea katika mahakama ya ngazi ya chini, mtu, taasisi au halmashauri inayorejelewa katika ibara ya (6) na inaweza kutoa maagizo yoyote na kutoa maelekezo yanayofaa kwa maoni ya mahakama hiyo ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka.

**166.**

*Uteuzi wa Jaji Mkuu, Naibu wa Jaji Mkuu na majaji wengine.*

(1) Rais atateua—

a) Jaji Mkuu na Naibu Jaji Mkuu kulingana na mapendekezo ya Tume ya Huduma za Mahakama na kwa idhini ya Bunge; na

b) majaji wengine wote, kulingana na mapendekezo ya Tume ya Huduma za Mahakama.

(2) Kila jaji wa mahakama ya ngazi ya juu atateuliwa kutoka miongoni mwa watu ambao—

a) wana shahada ya sheria kutoka chuo kikuu kinachotambulika, au ni mawakili wa Mahakama Kuu, au wamehitimu kwa njia hii kutoka nchi nyingine inayotumia mfumo wa sheria unaokuzwa na majaji kupitia maamuzi yao;

b) wana uzoefu unaohitajika chini ya ibara ya (3) hadi (6), bila kujalisha kwamba uzoefu huo ulipatikana nchini Kenya au katika nchi nyingine inayotumia mfumo wa sheria katika Jumuiya ya Madola; na

c) wana mienendo na maadili mema, uadilifu na wasioegemea upande wowote.



SIO YA KUUZWA

(3) Jaji Mkuu na majaji wengine wa Mahakama ya Juu Zaidi watateuliwa kutoka miongoni mwa watu ambao—

a) wana uzoefu wa angalau miaka kumi na mitano kama jaji katika mahakama ya ngazi ya juu; au

b) wana uzoefu wa angalau miaka kumi na mitano kama wasomi wanaoheshimika, maafisa wa mahakama, wanasheria au uzoefu wa kiasi sawa katika nyanja nyingine ya kisheria inayohusika; au

c) amehitimu kwa viwango vilivyotajwa katika aya ya (a) na (b) kwa muda wa miaka kumi na mitano kijumla;

(4) Kila jaji wa Mahakama ya Rufaa atateuliwa kutoka miongoni mwa watu ambao—

a) wana uzoefu wa angalau miaka kumi kama jaji wa mahakama ya ngazi ya juu; au

b) wana uzoefu wa angalau miaka kumi kama wasomi wanaoheshimika au wanasheria au uzoefu sawa katika nyanja nyingine ya kisheria inayohusika; au

c) wamehitimu kulingana na aya ya (a) na (b) na kwa muda wa miaka kumi kijumla.

(5) Kila jaji wa Mahakama Kuu atateuliwa kutoka miongoni mwa watu ambao—

a) wana uzoefu wa angalau miaka kumi kama jaji wa mahakama ya ngazi ya juu; au

b) wana uzoefu wa angalau miaka kumi kama wasomi wanaoheshimika au wanasheria au uzoefu sawa katika nyanja nyingine ya kisheria inayohusika; au



SIO YA KUUZWA

c) wamehitimu kwa viwango vilivyotajwa katika aya ya (a) na (b) na kwa muda wa miaka kumi kijumla.

**167.**

*Kipindi cha kuhudumu ofisini cha Jaji Mkuu na majaji wengine.*

(1) Jaji atastaafu kutoka ofisini atakapofikisha umri wa miaka sabini, lakini anaweza kuamua kustaafu wakati wowote baada ya kufikisha miaka sitini na mitano.

(2) Jaji Mkuu atahudumu ofisini kwa jumla ya miaka kumi au hadi atakapostaafu chini ya ibara ya (1), kustaafu huko kukizingatia itakayotimia mwanzo.

(3) Ikiwa muhula wa Jaji Mkuu wa kuhudumu utakamilika kabla ya Jaji Mkuu kufikisha umri wa kustaafu chini ya ibara ya (1), Jaji Mkuu anaweza kuendelea kuhudumu kama jaji wa Mahakama ya Juu Zaidi.

(4) Ikiwa, wakati wa kukamilika kwa muhula wa kuhudumu kwa Jaji Mkuu, Jaji huyo ataamua kuendelea kuhudumu mahakamani chini ya ibara ya (3), mtu atakayeteuliwa kama Jaji Mkuu atateuliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 166 (1) ingawa uteuzi huo unaweza kusababisha idadi ya majaji kuzidi idadi inayokubalika ya majaji wa Mahakama ya Juu Zaidi.

(5) Jaji Mkuu na jaji mwingine yeyote anaweza kujiuzulu kutoka ofisini kwa kumwandikia Rais notisi.

**168.**

*Kuondolewa ofisini.*

(1) Jaji wa mahakama ya ngazi ya juu anaweza kuondolewa kutoka ofisini tu kwenye misingi ya—

a) kutoweza kutekeleza majukumu ya ofisi hiyo kutokana na kukosa uwezo wa kiakili au wa kimwili;

b) kukiuka kanuni za utendakazi zilizowekewa majaji wa mahakama za ngazi ya juu kupitia kwa Sheria ya Bunge;

c) kufilisika;

d) kutokuwa na uzoefu unaohitajika; au

e) mwenendo mbaya zaidi ofisini au tabia mbaya.

(2) Hatua ya kumuondoa jaji inaweza kuanzishwa na Tume ya Huduma za Mahakama kwa kuchukua hatua hiyo kivyake, au kwa ombi au malalamishi ya mtu yeyote, yatakayowasilishwa kwa Tume hii.

(3) Ombi au malalamishi ya mtu kwa Tume ya Huduma za Mahakama chini ya ibara ya (2) yatawasilishwa kwa maandishi, yakiainisha maswala yanayodaiwa kuwa msingi wa kumwondoa jaji.

(4) Tume ya Huduma za Mahakama itaangalia malalamishi hayo na iwapo itaridhika kwamba ombi au malalamishi hayo yanafichua sababu chini ya ibara ya (1), itatuma ombi au malalamishi hayo kwa Rais.

(5) Katika muda wa siku kumi na nne baada ya kupokea malalamishi hayo, Rais atamsimamisha kazi jaji huyo, na kwa kuzingatia ushauri wa Tume ya Huduma za Mahakama—

a) iwapo itakuwa ni Jaji Mkuu, itateua taasisi iliyo na mamlaka ya mahakama, itakayojumuisha—

i. Spika wa Bunge la Kitaifa, kama mwenyekiti;

ii. majaji watatu wa mahakama za ngazi ya juu kutoka nchi zinazotumia mfumo wa sheria wa Jumuiya ya Madola;

iii. wakili mmoja mwenye uzoefu wa miaka kumi na mitano; na

iv. watu wengine wawili wenye uzoefu katika masuala ya umma; au

b) iwapo ni jaji mwingine ambaye sio Jaji Mkuu, itateua taasisi iliyo na mamlaka ya mahakama, itakayojumuisha—



SIO YA KUUZWA

i. mwenyekiti na wanachama wengine watatu ambao wanahudumu au wamewahi kuhudumu kama jaji wa mahakama ya ngazi ya juu, au ambao wamehitimu kuteuliwa kama jaji wa mahakama ya ngazi ya juu, lakini ambao hawajakuwa wanachama wa Tume ya Huduma za Mahakama katika muda wa miaka mitatu iliyopita;

ii. wakili mmoja mwenye uzoefu wa miaka kumi na mitano; na

iii. watu wengine wawili walio na uzoefu katika masuala ya umma.

(6) Licha ya kifungu cha (160) (4), mshahara na marupurupu ya jaji ambaye amesimamishwa kazi chini ya ibara ya (5) yatapunguzwa kwa nusu hadi wakati ambapo jaji huyo ataondolewa au kurudishwa ofisini.

(7) Taasisi iliyoteuliwa chini ya ibara ya (5)—

a) itakuwa na jukumu la kudhibiti vikao vyake, kwa kuzingatia sheria yoyote inayobainishwa katika ibara ya (10); na

b) itachunguza suala hilo kwa haraka, kutoa ripoti kuhusu ukweli wa suala hilo, na kuwasilisha mapendekezo ambayo Rais atatekeleza.

(8) Jaji ambaye hajaridhika na uamuzi wa taasisi hiyo chini ya Kifungu hiki anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo kwa Mahakama ya Juu Zaidi ndani ya siku kumi baada ya taasisi hiyo kutoa mapendekezo yake.

(9) Rais atachukua hatua kulingana na mapendekezo yaliyotolewa na taasisi hiyo kufikia mwisho wa—

a) muda uliotolewa wa kukata rufaa chini ya ibara ya (8), iwapo rufaa kama hiyo haijakatwa; au



SIO YA KUUZWA

b) kukamilika kwa haki zote za ukataji rufaa katika kesi yoyote inayokubalia ukataji huo wa rufaa chini ya Ibara ya (8), iwapo rufaa kama hiyo imekatwa na uamuzi wa mwisho katika swala hilo unaafikiana na mapendekezo ya taasisi hiyo.

(10) Bunge litatunga sheria itakayotoa mwongozo wa taratibu za taasisi itakayoteuliwa chini ya Kifungu cha hiki.

**Sehemu ya 3—Mahakama za Ngazi ya Chini**

**169.**

*Mahakama za ngazi ya chini.*

(1) Mahakama za ngazi ya chini ni—

a) mahakama za Mahakimu;

b) mahakama za Kadhi;

c) Mahakama za Kijeshi; na

d) mahakama yoyote nyingine au taasisi itakayobuniwa kwa Sheria ya Bunge, isipokuwa mahakama zilizobuniwa inavyohitajika chini ya Kifungu cha 162 (2). (2) Bunge litatunga sheria itakayotoa mamlaka, na majukumu ya mahakama ambazo zimebuniwa chini ya ibara ya (1).

**170.**

*Mahakama za Kadhi.*

(1) Kutakuwa na Kadhi Mkuu na Kadhi wengine wasiopungua watatu kulingana na mwongozo wa Sheria ya Bunge.

(2) Hakuna mtu atakayestahiki kuteuliwa ili kuhudumu katika ofisi ya Kadhi isipokuwa mtu huyo—

a) ni muumini wa dini ya Kiislamu; na

b) ana ufahamu wa sheria ya Kiislamu inayotumika katika madhehebu ya Waislamu, ambao kwa maoni ya Tume ya Huduma za Mahakama, unamwezesha mtu huyo kuhudumu katika mahakama ya Kadhi.



SIO YA KUUZWA

(3) Bunge litabuni mahakama za kadhi, na kila mahakama ya Kadhi itakuwa na mamlaka yaliyotolewa kulingana sheria, lakini kwa kuzingatia ibara ya (5).

(4) Kadhi Mkuu na makadhi wengine, au Kadhi Mkuu na Kadhi wengine (wasiopungua watatu) kama inavyoweza kutolewa mwongozo na Sheria ya Bunge, watapewa mamlaka ya kuhudumu katika mahakama ya Kadhi iliyo na mamlaka nchini Kenya.

(5) Mamlaka ya mahakama ya Kadhi yatadhibitiwa ili kushughulikia maswala kuhusu sheria ya Uislamu yanayohusiana na hadhi ya kibinafsi, ndoa, talaka au urithi katika kesi ambazo pande zote husika zinakiri dini ya Kiislamu na zinatii mamlaka ya mahakama za Kadhi.

**171.**

*Kazi ya Tume ya Huduma za Mahakama.*

(1) Tume ya Huduma za Mahakama imebuniwa.

(2) Tume hiyo itajumuisha—

a) Jaji Mkuu, atakayekuwa mwenyekiti wa Tume;

b) Jaji mmoja wa Mahakama ya Juu Zaidi aliyeteuliwa na majaji wa Mahakama ya Juu Zaidi;

c) Jaji mmoja wa Mahakama ya Rufaa aliyeteuliwa na majaji wa Mahakama ya Rufaa;

d) Jaji mmoja wa Mahakama Kuu na hakimu mmoja, mwanamke mmoja na mwanaume mmoja, walioteuliwa na wanachama wa muungano wa majaji na mahakimu;

e) Mwanasheria Mkuu;

f) mawakili wawili, mwanamke mmoja na mwanaume mmoja, kila mmoja akiwa na uzoefu wa angalau miaka kumi na mitano, walioteuliwa na chama kinachowajibika kisheria kudhibiti taaluma ya mawakili;

g) mtu mmoja aliyeteuliwa na Tume ya Huduma za Umma; na

h) mwanamke mmoja na mwanaume mmoja watakaowakilisha umma, na wasiokuwa wanasheria, watakaoteuliwa na Rais kwa idhini ya Bunge la Kitaifa.

(3) Msajili Mkuu wa Kitengo cha Mahakama ndiye atakayekuwa Katibu wa Tume hiyo.

(4) Wanachama wa Tume hiyo, isipokuwa Jaji Mkuu na Mwanasheria Mkuu, watahudumu kwenye ofisi hiyo kwa kipindi cha miaka mitano na watastahiki kuteuliwa ili kuhudumu kwa muhula mwingine mmoja wa miaka mitano, mradi tu wawe wamehitimu,

**172.**

*Kazi ya Tume ya Huduma za Mahakama.*

(1) Tume ya Huduma za Mahakama itahakikisha na kuimarisha uhuru na uwajibikaji wa kitengo cha mahakama, na kuimarisha utekelezaji bora wa haki, ulio wazi na wenye ufanisi na—

a) itapendekezea Rais watu watakaoteuliwa kama majaji;

b) itakagua na kutoa mapendekezo kuhusu masharti ya kuhudumu kwa—

i. majaji na maafisa wengine wa mahakama, kando na mishahara yao; na

ii. wafanyakazi katika kitengo cha mahakama;

c) itateua, kupokea malalamishi, kuchunguza na kuwaondoa ofisini au vinginevyo kuwachukulia hatua za kinidhamu wasajili, mahakimu, maafisa wengine wa mahakama na wafanyakazi wengine katika kitengo cha mahakama, kwa namna ambayo imebainiwa na Sheria ya Bunge;



SIO YA KUUZWA

d) itandaa na kutekeleza programu za elimu na mafunzo yanayoendelea kwa majaji, mahakimu na maafisa wengine mahakama; na

e) itaishauri serikali ya kitaifa kuhusu uboreshaji wa utendakazi katika utekelezaji wa haki.

(2) Katika utekelezaji wa majukumu yake, Tume itaongozwa na yafuatayo—

a) ushindani na michakato yenye uwazi katika uteuzi wa maafisa wa mahakama na wafanyakazi wengine katika kitengo hicho cha mahakama; na

b) ukuzaji wa usawa wa kijinsia.

**173.**

*Hazina ya Mahakama.*

(1) Hazina itakayojulikana kama Hazina ya Kitengo cha Mahakama, ambayo itasimamiwa na Msajili Mkuu wa Kitengo cha Mahakama imebuniwa.

(2) Hazina hiyo itatumika kugharamia usimamizi wa Kitengo cha Mahakama na madhumuni mengine yatakayohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya Mahakama.

(3) Katika kila mwaka wa kifedha, Msajili Mkuu ataandaa makadirio ya matumizi ya mwaka utakaofuata, na kuyawasilisha kwa Bunge la Kitaifa ili kuidhinishwa.

(4) Bunge la Kitaifa litakapoidhinisha makadirio hayo, matumizi haya yatagharamiwa kutoka kwenye Hazina Jumuishi na fedha hizo zitalipwa moja kwa moja katika Hazina ya Mahakama.

(5) Bunge litatunga sheria ili kudhibiti matumizi ya Hazina hiyo.



SIO YA KUUZWA

# SURA YA KUMI NA MOJA — SERIKALI YA UGATUZI

**Sehemu ya 1—Malengo na Kanuni za Serikali ya Ugatuzi**

**174.**

(1) Malengo ya serikali ya ugatuzi ni—

*Malengo ya ugatuzi.*

a) kukuza utekelezaji wa mamlaka kwa njia ya kidemokrasia na kwa uwajibikaji;

b) kukuza umoja wa kitaifa kwa kutambua utofauti ulioko;

c) kuwapa wananchi mamlaka ya kujitawala na kuboresha ushiriki wa wananchi katika utekelezaji wa mamlaka ya Serikali na katika kufanya maamuzi yanayowaathiri;

d) kutambua haki za jamii katika kusimamia masuala ya jamii hizo na katika kuboresha maendeleo yao;

e) kulinda na kukuza maslahi na haki za watu walio wachache na jamii zilizotengwa;;

f) Kukuza maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi, na utoaji wa huduma zilizo karibu na zinazofikiwa kwa urahisi nchini Kenya;

g) kuhakikisha kuna ugavi wenye usawa wa rasilimali zote za kijamii na za kitaifa kote nchini;

h) kuwezesha ugatuzi wa vitengo vya Serikali, majukumu na huduma zao kutoka jiji kuu la Kenya; na kuboresha uwajibikaji na ugavi wa mamlaka.

**175.**

(1) Serikali za kaunti zilizobuniwa chini ya Katiba hii zitazingatia kanuni zifuatazo––

*Kanuni za serikali ya ugatuzi.*

a) serikali za kaunti zitazingatia kanuni za kidemokrasia na ugawaji wa mamlaka;

b) serikali za kaunti zitakuwa na njia zinazoweza kutegemewa katika uzalishaji wa mapato ili kuziwezesha kutawala na kutoa huduma kwa njia bora; na

c) katika uanachama wa idara wakilishi katika kila serikali ya kaunti, idadi ya wanachama wa jinsia moja haitazidi thuluthi mbili ya wanachama wote.

**Sehemu ya 2—Serikali za Kaunti**

**176.**

*Serikali za kaunti.*

(1) Kila kaunti itakuwa na serikali yake ya kaunti, itakayokuwa na bunge la kaunti na kitengo kinachosimamia utendaji katika kaunti.

(2) Kila serikali ya kaunti itagatua majukumu yake na utoaji wa huduma zake kwa kiwango kinachowezekana na ambacho kinaleta ufanisi.

**177.**

*Uanachama katika bunge la kaunti.*

(1) (1) Bunge la kaunti linajumuisha—

a) wanachama waliochaguliwa na wapiga kura waliosajiliwa katika wadi, uchaguzi huo ukifanyika siku ile ile ya uchaguzi mkuu wa wabunge, ambayo ni Jumanne ya pili ya mwezi Agosti baada ya kila miaka mitano na kila wadi ikijumuisha eneo la kuwakilishwa na mwanachama mmoja;

b) idadi ya wabunge maalum inayohitajika ili kuhakikisha kwamba hakuna zaidi ya wabunge thuluthi mbili wa jinsia moja katika bunge hilo;

c) idadi ya wanachama kutoka vikundi vya watu waliotengwa, wakiwemo watu wenye ulemavu na vijana, kama inavyoagizwa katika Sheria ya Bunge; na

d) Spika, ambaye ni mwanachama aliyechaguliwa na wabunge.

(2) Wanachama wanaobainishwa katika ibara ya (1) (b) na (c) watateuliwa na vyama vya kisiasa kulingana na idadi ya viti ambavyo kila chama cha kisiasa kilipata katika uchaguzi wa kaunti hiyo chini ya ibara ya (a) kulingana na Kifungu cha 90.

(3) Kujazwa kwa viti maalum chini ya ibara ya (1) (b) kutaamuliwa baada ya kutangazwa kwa wanachama waliochaguliwa katika kila wadi.

(4) Bunge la kaunti linachaguliwa kwa muhula wa miaka mitano.

**178.**

*Spika wa bunge la kaunti.*

(1) Kila bunge la kaunti litakuwa na spika aliyechaguliwa na bunge la kaunti kutoka miongoni mwa watu wasio wanachama wa bunge hilo.

(2) Kikao cha bunge la kaunti kitaongozwa na––

a) spika wa bunge hilo; au

b) iwapo spika hayuko, mwanachama mwingine wa bunge hilo aliyechaguliwa na bunge.

(3) Bunge litatunga sheria itakayotoa mwongozo katika kuchaguliwa na kuondolewa ofisini kwa maspika wa mabunge ya kaunti.

**179.**

*Kamati za mamlaka ya utendaji katika kaunti.*

(1) Mamlaka ya utendaji katika kaunti yamepewa, na yatatekelezwa, na kamati za utendaji katika kaunti.

(2) Kamati ya utendaji katika kaunti inajumuisha—

a) gavana wa kaunti na naibu gavana wa kaunti; na

b) wanachama walioteuliwa na gavana wa kaunti, kwa idhini ya bunge la kaunti, kutoka miongoni mwa watu ambao sio wanachama wa bunge hilo.



SIO YA KUUZWA

(3) Idadi ya wanachama walioteuliwa kwa mujibu wa ibara ya (2)(b) haitazidi—

a) thuluthi moja ya wanachama wa bunge la kaunti ikiwa bunge hilo lina chini ya wanachama thelathini; au

b) kumi, ikiwa bunge lina wanachama thelathini au zaidi.

(4) Gavana wa kaunti na naibu gavana wa kaunti ndio afisa mkuu na naibu wa afisa mkuu wa kaunti, mtawalia.

(5) Wakati ambapo gavana wa kaunti hayupo, naibu gavana wa kaunti ndiye atakayehudumu kama gavana wa kaunti.

(6) Wanachama wa kamati ya utendaji katika kaunti wanawajibikia gavana wa kaunti katika utekelezaji wa majukumu na mamlaka yao.

(7) Ikiwa nafasi katika ofisi ya gavana itatokea, wanachama wa kamati ya utendaji katika kaunti walioteuliwa chini ya ibara ya (2) (b) hawatahudumu tena.

**180.**

*Uchaguzi wa gavana wa kaunti na naibu gavana wa kaunti.*

(1) Gavana wa kaunti atachaguliwa moja kwa moja na wapiga kura waliosajiliwa katika kaunti hiyo, siku ile ile ya uchaguzi mkuu wa wabunge, itakayokuwa Jumanne ya pili ya mwezi Agosti, baada ya kila miaka mitano.

(2) Lazima mtu astahiki kuchaguliwa kama mwakilishi wadi ili astahiki kuchaguliwa kama gavana wa kaunti.

(3) Ikiwa mgombea mmoja tu wa kiti cha gavana ndiye atakayeteuliwa, mtu huyu atatangazwa kuwa amechaguliwa.

(4) Ikiwa wagombea wawili au zaidi watateuliwa, uchaguzi utafanywa katika kaunti hiyo na mgombeaji

atakayepata idadi kubwa zaidi ya kura ndiye atakayetangazwa kuwa amechaguliwa.

(5) Kila mgombea kiti cha gavana wa kaunti atamteua mtu mmoja ambaye anastahiki kuchaguliwa kama gavana wa kaunti kuwa mgombea kiti cha naibu gavana.

(6) Tume Huru ya Uchaguzi na Mipakahaitasimamia uchaguzi tofauti wa naibu wa gavana, lakini itamtangaza mgombea aliyeteuliwa na yule mtu anayechaguliwa kama gavana wa kaunti, kuwa amechaguliwa kama naibu wa gavana .

(7) Hakuna atakayehudumu––

a) kama gavana wa kaunti kwa zaidi ya mihula miwili; au

b) kama naibu gavana wa kaunti kwa zaidi ya mihula miwili.

(8) Kwa madhumuni ya ibara ya (7), mtu ambaye amechukua hatamu za uongozi kama gavana wa kaunti atachukuliwa kuwa amehudumu katika muhula mzima, lakini kwa kuzingatia Kifungu cha 182 (3) (b) tu.

**181.**

*Kuondolewa kwa gavana wa kaunti.*

(1) Gavana wa kaunti anaweza kuondolewa ofisini kwa msingi wowote kati ya yafuatayo––

a) ukiukaji mkubwa wa Katiba hii au sheria yoyote nyingine;

b) ikiwakunasababukuuzakuaminikuwagavanahuyo wa kaunti amefanya uhalifu chini ya sheria ya taifa au kimataifa;

c) matumizi mabaya ya mamlaka au mwenendo mbaya zaidi ofisini; au

d) kukosa uwezo wa kimwili au kiakili ili kutekeleza majukumu ya ofisi ya gavana wa kaunti.

(2) Bunge litatunga sheria itakayotoa taratibu za kumwondoa gavana wa kaunti ofisini, kwenye msingi wowote kati ya iliyotajwa katika ibara ya (1).

**182.**

*Nafasi ya kazi katika afisi ya gavana wa kaunti.*

(1) Afisi ya gavana wa kaunti itakuwa wazi ikiwa anayehudumu katika afisi hiyo—

a) Atafariki dunia;

b) atajiuzulu kwa kumwandikia spika wa bunge la kaunti;

c) atawacha kutimiza mahitaji ya kustahiki ili kuchaguliwa kama gavana wa kaunti chini ya Kifungu cha 180 (2);

d) atapatikana na hatia ambalo linaadhibiwa kwa kifungo gerezani kisichopungua miezi kumi na miwili;

e) ataondolewa ofisini kwa mujibu wa Katiba hii.

(2) Ikiwa nafasi itatokea katika ofisi ya gavana wa kaunti, naibu gavana wa kaunti atahudumu kama gavana wa kaunti kwa muda wa muhula uliosalia wa gavana wa kaunti.

(3) Ikiwa mtu atachukua hatamu za uongozi katika ofisi ya gavana wa kaunti chini ya ibara ya (2), kwa madhumuni ya Kifungu cha 180 (7), mtu huyo atachukuliwa kuwa—

a) amehudumu kwa muhula mzima kama gavana wa kaunti ikiwa, katika tarehe ambayo mtu huyo alianza kuhudumu, zaidi ya miaka miwili na nusu ilikuwa inasalia kabla ya tarehe ya uchaguzi utakaofuata ulioratibiwa kikawaida chini ya Kifungu cha 180 (1); au

b) hajahudumu kwa muhula mzima kama gavana wa kaunti katika hali nyingine yoyote.

(4) Ikiwa nafasi itatokea katika ofisi ya gavana wa kaunti na katika ofisi ya naibu gavana wa kaunti, au ikiwa naibu gavana wa kaunti hawezi kuhudumu kwa muda, spika wa bunge la kaunti ndiye atakayehudumu kwa muda kama gavana wa kaunti.

(5) Ikiwa nafasi itatokea katika hali zilizobainishwa chini ya ibara ya (4), uchaguzi wa gavana wa kaunti utafanywa ndani ya siku sitini baada ya tarehe ya spika kuanza kuhudumu kama gavana wa kaunti.

(6) Mtu atakayechukua hatamu za uongozi katika ofisi ya gavana wa kaunti chini ya Kifungu hiki, isipokuwa aondolewe ofisini vinginevyo chini ya Katiba hii, mtu huyo atahudumu hadi gavana wa kaunti aliyechaguliwa upya atakapoanza kuhudumu baada ya uchaguzi utakaofuata chini ya Kifungu cha 180 (1).

**183.**

*Majukumu ya kamati za mamlaka ya utendaji katika kaunti*

(1) Kamati ya utendaji katika kaunti—

a) itatekeleza sheria za bunge la kaunti;

b) itatekeleza, katika kaunti, sheria za kitaifa kwa kiwango kinachohitajiwa na sheria hiyo;

c) itasimamia na kuratibu majukumu ya utawala wa kaunti na idara zake; na

d) itatekeleza majukumu mengine yoyote yaliyotolewa na Katiba hii na sheria ya kitaifa.

(2) Kamati ya utendaji katika kaunti inaweza kuandaa sheria iliyopendekezwa ili itathminiwe na bunge la kaunti.

(3) Kamati ya utendaji katika kaunti itatoa ripoti kamili za mara kwa mara kwa bunge la kaunti kuhusu masuala yanayohusiana na kaunti.



SIO YA KUUZWA

**184.**

*Maeneo yenye miji na majiji.*

(1) Sheria ya Kitaifa itatoa mwongozo kuhusu utawala na usimamizi wa maeneo ya miji na majiji, na hasa—

a) itabuni vigezo vya kuainisha maeneo kama miji na majiji,

b) itabuni kanuni za utawala na usimamizi wa maeneo ya miji na majiji; na

c) itatoa mwongozo kuhusu ushiriki wa umma katika utawala wa maeneo ya miji na majiji.

(2) (2) Sheria ya kitaifa inayorejelewa katika ibara ya (1) inaweza kujumuisha njia za kutambua kategoria mbalimbali za maeneo ya miji na majiji, na utawala wao.

**185.**

*Mamlaka ya utungaji sheria ya mabunge ya kaunti.*

(1) Mamlaka ya kutunga sheria ya kaunti yamepewa bunge la kaunti, na yatatekelezwa na bunge la kaunti.

(2) Bunge la kaunti linaweza kutunga sheria zozote muhimu, au zinazohitajika katika ufanikishaji wa utekelezaji wa majukumu yake, na utekelezaji wa mamlaka ya serikali ya kaunti kwa mujibu wa Ambatisho la Nne.

(3) Bunge la kaunti, kwa kuzingatia kanuni ya ugawaji wa mamlaka, lina uwezo wa kusimamia kamati ya utendaji katika kaunti, pamoja na idara zinginezo katika kitengo cha utendaji cha serikali ya kaunti.

(4) Bunge la kaunti linaweza kupokea na kuidhinisha mipango na sera ya-—

a) usimamizi na utumiaji wa rasilimali za kaunti; na

b) maendeleo na usimamizi wa miundo-msingi na taasisi za kaunti hiyo.



SIO YA KUUZWA

**Sehemu ya 3—Majukumu na Mamlaka ya Serikali za Kaunti**

**186.**

*Kazi na mamlaka ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti.*

(1) Isipokuwa Katiba hii itoe mwongozo vinginevyo, majukumu na mamlaka ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti ni kama yalivyoelezwa katika Ambatisho la Nne.

(2) Jukumu au mamlaka yaliyotolewa kwa zaidi ya kiwango kimoja cha serikali ni jukumu au mamlaka ambayo yanaweza kutekelezwa na viwango vyote vya serikali.

(3) Jukumu au mamlaka ambayo hayajatolewa kwa kaunti na Katiba hii au sheria ya kitaifa, ni jukumu au mamlaka ya serikali ya kitaifa.

(4) Kwa uhakika zaidi, Bunge la kitaifa linaweza kuitungia Jamhuri sheria kuhusu jambo lolote.

**187.**

*Uhamisho wa kazi na mamlaka kati ya ngazi za serikali.*

(1) Jukumu au mamlaka ya serikali katika ngazi moja yanaweza kuhamishwa kwa serikali katika ngazi hiyo nyingine kwa makubaliano kati ya serikali hizo mbili ikiwa—

a) mamlaka au jukumu hilo litatekelezwa vyema zaidi na serikali hiyo inayopokea jukumu au mamlaka hayo; na

b) kuhamishwa kwa mamlaka au jukumu hakujapigwa marufuku chini ya sheria ambayo kuhamishwa huko kungetekelezwa.

(2) Ikiwa jukumu au mamlaka yatahamishwa kutoka ngazi moja ya serikali hadi nyingine—

a) mipango itafanywa ili kuhakikisha kwamba rasilimali zinazohitajika katika utekelezaji wa mamlaka au jukumu hilo zimehamishwa; na



SIO YA KUUZWA

b) uwajibikaji wa kikatiba katika utekelezaji wa jukumu au mamlaka utabakia na serikali iliyopewa jukumu au mamlaka hayo chini ya Ambatisho la Nne.

**Sehemu ya 4—Mipaka ya Kaunti**

**188.**

*Mipaka ya kaunti.*

(1) Mipaka ya kaunti inaweza kubadilishwa tu kwa uamuzi––

a) uliopendekezwa na tume huru iliyobuniwa na bunge kwa lengo hilo; na

b) uliopitishwa na––

i. Bunge la Kitaifa, ukiungwa mkono na wabunge wasiopungua thuluthi mbili ya wanachama wa Bunge hilo; na

ii. Seneti, ukiungwa mkono na angalau wajumbe wa kaunti wasiopungua thuluthi mbili ya wajumbe wa kaunti.

(2) Mipaka ya kaunti inaweza kubadilishwa ili kuzingatia—

a) wingi wa watu na uongezekaji wao;

b) miundombinu ya kiasili na ya kibinadamu;

c) historia na tamaduni za watu hao;

d) gharama ya usimamizi;

e) maoni ya jamii zilizoathirika;

f) malengo ya ugatuzi wa serikali; na

g) mandhari ya kijiografia.



SIO YA KUUZWA

**Sehemu ya 5—Uhusiano Kati ya Serikali**

**189.**

*Ushirikiano kati ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti.*

(1) Serikali katika ngazi yoyote—

a) iwapo ni serikali ya kaunti, serikali hiyo itatekeleza majukumu na mamlaka yake kwa namna inayoheshimu hadhi na uadilifu wa kitaasisi katika ngazi hiyo ya serikali, na kwa namna inayoheshimu hadhi ya kikatiba na taasisi za serikali katika ngazi hiyo nyingine ya serikali;

b) itasaidia, itashirikiana na kushauriana na serikali katika ngazi hiyo nyingine, na ifaavyo, itatekeleza sheria za serikali iliyo katika ngazi hiyo nyingine; na

c) itashauriana na serikali katika kiwango hicho kingine kwa madhumuni ya kubadilishana mawazo, kuratibia sera na utawala, na kuboresha uwezo wa kutekeleza majukumu.

(2) Serikali katika ngazi zote, na serikali tofauti katika ngazi ya kaunti, zitashirikiana katika kutekeleza majukumu na mamlaka yao, na kwa lengo hilo, zinaweza kubuni kamati na mamlaka ya pamoja.

(3) Katika mzozo wowote kati ya serikali, serikali hizo zitachukua hatua zote iwezekanavyo ili kutatua mzozo huo, ikijumuisha taratibu zilizotolewa chini ya sheria ya kitaifa.

(4) Sheria ya kitaifa itatoa taratibu za kutatua mizozo kati ya serikali kwa mbinu mbadala za kutatua mizozo zikiwemo kushauriana na upatanishi.

**190.**

*Usaidizi kwa serikali za kaunti.*

(1) Bunge litatunga sheria ili kuhakikisha kwamba serikali za kaunti zina usaidizi wa kutosha ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yao.



SIO YA KUUZWA

(2) Serikali za kaunti zitaendesha mifumo ya usimamizi wa fedha inayoafikiana na matakwa ya sheria ya kitaifa.

(3) Bunge litatunga sheria itakayoruhusu serikali ya kitaifa kuingilia kati ikiwa serikali ya kaunti—

a) imeshindwa kutekeleza majukumu yake; au

b) haiendeshi mfumo wa usimamizi wa fedha unaoambatana na matakwa ya sheria ya kitaifa.

(4) Sheria inayorejelewa katika ibara ya (3) inaweza, hasa, kuipa serikali ya kitaifa mamlaka ya-—

a) kuchukua hatua mwafaka ili kuhakikisha kwamba majukumu ya serikali ya kaunti yanatekelezwa na kwamba serikali hiyo inaendesha mfumo wa usimamizi wa fedha unaoafikia mahitaji yaliyotolewa; na

b) kuwajibika katika utekelezaji wa majukumu husika ikiwa itahitajika.

(5) Sheria inayorejelewa chini ya ibara ya (3)—

a) itahitaji notisi kutolewa kwa serikali ya kaunti kuhusu hatua zozote ambazo serikali ya kitaifa inanuia kuchukua;

b) itaruhusu serikali ya kitaifa kuchukua tu hatua ambazo ni muhimu;

c) itahitaji serikali ya kitaifa kuchukua hatua ambazo zitaisaidia serikali ya kaunti kurejelea kikamilifu utekelezaji wa majukumu yake serikali hiyo inapoingilia kati; na

d) itatoa mchakato ambao Seneti inaweza kutumia ili kukomesha uingiliaji kati wa serikali ya kitaifa.

**191.**

*Mgongano wa sheria.*

(1) Kifungu hiki kinahusu mgongano kati ya sheria za kitaifa na zile za kaunti, katika masuala ambayo



SIO YA KUUZWA

viwango vyote viwili vya serikali vina mamlaka au majukumu kuyahusu.

(2) Sheria ya kitaifa itatawala juu ya sheria ya kaunti ikiwa—

a) sheria za kitaifa inatumika kwa usawa kote nchini Kenya na masharti mengine yaliyowekwa katika ibara ya (3) yametoshelezwa; au

b) sheria ya kitaifa inalenga kudhibiti hatua zisizofaa katika kaunti, ikiwa hatua hizo—

i. zinaweza kuwa na athari mbaya kiuchumi, kiafya au katika usalama wa Kenya au kaunti nyingine; au

ii. zitazuia utekelezaji wa sera ya kiuchumi ya kitaifa.

(3) Masharti yanayorejelewa katika ibara ya (2) (a) ni kama yafuatayo (2) (a)––

a) sheria ya kitaifa inatoa mwongozo kuhusu suala ambalo haliwezi kudhibitiwa kwa ufanisi na sheria zitakazotungwa katika kila kaunti;

b) sheria ya kitaifa inatoa mwongozo kuhusu suala ambalo linahitaji usawa kote nchini ili kutekelezwa kwa ufanisi, na sheria hiyo ya kitaifa inatoa usawa huo kwa kubuni—

i. kanuni na viwango vya ubora; au

ii. sera za kitaifa; au

c) sheria hiyo ya kitaifa ni muhimu katika—

i. kudumisha usalama wa kitaifa;

ii. kudumisha umoja wa kiuchumi;;

iii. kulinda soko la shirikisho katika usafirishaji wa bidhaa, huduma, rasilimali na wafanyakazi;



SIO YA KUUZWA

iv. kukuza shughuli za kiuchumi katika mipaka ya kaunti;

v. kukuza nafasi sawa au usawa katika ufikiaji wa huduma za serikali; au

vi. kulinda mazingira.

(4) Sheria ya kaunti zitatawala juu ya sheria ya kitaifa ikiwa hali zote zinazobainiwa katika ibara ya (2) hazitumiki.

(5) Katika kutatua mgongano kati ya sheria za viwango tofauti vya serikali, mahakama itapendelea ufasiri wa sheria ambao utazuia mgongano badala ya ufasiri ambao utapelekea mgongano.

(6) Uamuzi wa mahakama kwamba kifungu cha sheria ya kiwango kimoja cha serikali kinatawala juu ya kifungu katika sheria ya kiwango kingine cha serikali hakubatilishi kifungu cha sheria cha kiwango kile kingine, ila tu kifungu hicho hakitatekelezwa kwa kiwango ambacho hakiambatani na kifungu kilichoamuliwa kutawala.

**Sehemu ya 6—Kusimamishwa kwa Muda kwa Serikali za Kaunti**

**192.**

*Kusimamishwa kwa serikali za kaunti*

(1) Rais anaweza kusimamisha serikali ya kaunti kwa muda—

a) katika hali ya dharura inayotokana na mzozo wa kindani au vita; au;

b) katika hali zingine maalum.

(2) Serikali ya kaunti haitasimamishwa kwa muda chini ya ibara ya (1) (b) isipokuwa tume huru imefanya uchunguzi wa madai dhidi ya serikali ya kaunti, Rais ameridhika kwamba madai hayo yamethibitishwa na Seneti imeidhinisha kusimamishwa huko.

(3) Kwa wakati ambao serikali ya kaunti imesimamishwa kwa muda chini ya Kifungu hiki, mikakati itawekwa ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya serikali ya kaunti kulingana na Sheria ya Bunge.

(4) Kwa wakati wowote, Seneti inaweza kutupilia mbali kusimamishwa huko.

(5) Kusimamishwa kwa muda chini ya Kifungu hiki hakutaendelea kwa zaidi ya kipindi cha siku tisini.

(6) Kipindi kilichotolewa chini ya ibara ya (5) kinapokamilika, uchaguzi wa serikali ya kaunti husika utafanyika.

**Sehemu ya 7—Vifungu vya Kijumla**

**193.**

*Ustahiki katika kuchaguliwa kama mwakilishi wadi katika bunge la kaunti;*

(1) Isipokuwa kutostahiki chini ya ibara ya (2),mtu anastahiki kuchaguliwa kama mwakilishi wadi katika bunge la kaunti ikiwa mtu huyo—

a) amesajiliwa kama mpiga kura;

b) anatosheleza mahitaji yoyote ya kielimu, ya kimaadili na ya uadilifu ambayo yanahitajika katika Katiba hii au katika Sheria ya Bunge; na

c) lazima awe—

i. ameteuliwa na chama cha kisiasa; au

ii. mgombea huru anayeungwa na angalau wapiga kura mia tano waliosajiliwa katika wadi husika.

(2) Mtu hastahiki kuchaguliwa kama mwakilishi wadi ikiwa mtu huyo—

a) ni afisa wa Serikali au wa umma, isipokuwa mwakilishi wadi katika bunge la kaunti;

b) amehudumu katika Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka katika miaka mitano iliyopita kabla ya tarehe ya uchaguzi.



SIO YA KUUZWA

c) hajakuwa raia wa Kenya kwa angalau miaka kumi iliyopita kabla ya tarehe ya uchaguzi;

d) hana akili timamu;

e) amefilisika;

f) anatumikia kifungo gerezani cha miezi sita au zaidi; au

g) amepatikana kuwa, kulingana na sheria yoyote, ametumia vibaya mamlaka ya ofisi ya umma au kuwa amekiuka Sura ya Sita.

(3) Mtu hazuiliwi kugombea chini ya ibara ya (2) isipokuwa tu pale ambapo uwezekano wote wa rufaa au kukaguliwa kwa kifungo au uamuzi husika umekwisha.

**194.**

*Kuondolewa ofisini kwa mwakilishi wadi katika bunge la kaunti.*

(1) Afisi ya mwakilishi wadi itakuwa wazi—

a) ikiwa mwakilishi wadi huyo atafariki dunia;

b) Ikiwa mwakilishi wadi huyo atakosa kuhudhuria vikao vinane vya bunge bila idhini iliyoandikwa ya spika wa bunge, na hawezi kutoa sababu za kutosheleza kuhusu kutohudhuria huko;

c) ikiwa mwanachama huyo ameondolewa ofisini vinginevyo chini ya Katiba hii au chini ya sheria iliyotungwa chini ya Kifungu cha 80;

d) Ikiwa mwakilishi wadi huyo atajiuzulu kwa kumwandikia spika wa bunge la kaunti;

e) ikiwa baada ya kuchaguliwa katika bunge la kaunti––

i. kama mwanachama wa chama cha kisiasa, mwakilishi wadi huyo atajiuzulu kutoka chama hicho, au ikiwa atachukuliwa kuwa amejiuzulu kulingana na sheria



SIO YA KUUZWA

ii. inavyobainishwa katika ibara ya (2); au

iii. kama mgombea huru, mwanachama huyo atajiunga na chama cha kisiasa;

f) mwishoni mwa muhula wa bunge hilo la kaunti; au

g) ikiwa mwakilishi wadi huyo hatastahiki kuchaguliwa kwenye misingi iliyobainiwa katika Kifungu cha 193 (2).

(2) Bunge litatunga sheria litakalotoa hali ambazo mwanachama wa chama cha kisiasa atachukuliwa kuwa amejiuzulu kutoka chama hicho, kwa madhumuni ya ibara ya (1) (e).

**195.**

*Mamlaka ya bunge la kaunti ya kuwaita mashahidi.*

(1) Bunge la kaunti au yoyote kati ya kamati zake, lina uwezo wa kumwita mtu yeyote mbele yake kwa madhumuni ya kutoa ushahidi au maelezo.

(2) Kwa madhumuni ya ibara ya (1), bunge la kaunti lina mamlaka sawa na Mahakama Kuu katika—

a) kuamrisha mashahidi kuhudhuria na kuwahoji baada ya wao kula kiapo, kutoa uthibitisho au vinginevyo;

b) kulazimisha utoaji wa hati; na

c) Kutoa ombi la kuwahoji mashahidi walio ng'ambo.

**196.**

*Kushiriki kwa umma na mamlaka ya bunge la kaunti, haki maalum na kinga dhidi ya mashtaka.*

(1) Bunge la kaunti—

a) litaendesha shughuli zake kwa uwazi, na kufanya vikao vyake na vya kamati zake hadharani; na

b) litawezesha ushiriki wa umma katika kutunga sheria na katika shughuli zingine za bunge hilo na za kamati zake.

(2) Bunge la kaunti halitazuia umma, au vyombo vya habari, kuhudhuria kikao chochote isipokuwa katika hali maalum ambayo spika wa bunge ameamua kwamba kuna sababu zinazotosheleza za kufanya hivyo.

(3) Bunge la kitaifa litatunga sheria itakayotoa mwongozo kuhusu mamlaka, haki maalum na kinga dhidi ya mashtaka kwa mabunge ya kaunti na wanachama wake.

*Usawa wa kijinsia na utofauti katika bunge la kaunti.*

**197.**

(1) Idadi ya jinsia moja ya wanachama wa bunge lolote la kaunti au wa kamati ya utendaji katika kaunti, halitazidi thuluthi mbili ya wanachama hao.

(2) Bunge litatunga sheria ili—

a) kuhakikisha kwamba utofauti wa kijamii na wa kitamaduni unazingatiwa katika bunge la kaunti na kamati za utendaji katika kaunti; na

b) kuweka mikakati ya kuwalinda walio wachache katika kaunti hizo.

*Serikali ya kaunti katika kipindi cha mpito.*

**198.** Uchaguzi utakapofanywa ili kuunda bunge la kaunti chini ya Sura hii, kamati ya utendaji katika kaunti, ilivyoundwa mara ya mwisho, itakuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu ya usimamizi hadi kamati mpya ya utendaji itakapoundwa baada ya uchaguzi.

*Kuchapishwa kwa sheria za kaunti.*

**199.**

(1) Sheria ya kaunti haianzi kutumika isipokuwa ichapishwe katika Gazeti Rasmi la Serikali.

(2) Sheria ya kitaifa na sheria za kaunti zinaweza kutoa masharti ya ziada kuhusu uchapishaji wa sheria za serikali ya kaunti.



SIO YA KUUZWA

**200.**

*Sheria Kuhusu Sura Hii.*

(1) Bunge litatunga sheria itakayotoa mwongozo katika masuala yote muhimu au yanayohitajika ili kuwezesha utekelezaji wa Sura hii.

(2) Hasa, sheria inaweza kubuniwa ili iangazie––

a) usimamizi wa mji mkuu, majiji mengine na maeneo ya miji;

b) kuhamishwa kwa majukumu na mamlaka kutoka ngazi moja cha serikali hadi nyingine, ikijumuisha kuhamisha uwezo wa kutunga sheria kutoka kwa serikali ya kitaifa hadi serikali za kaunti;

c) taratibu za uchaguzi au uteuzi wa watu, na kuondolewa kwao ofisini katika serikali za kaunti, ikijumuisha ustahiki wa wapiga kura na wagombeaji;

d) taratibu za mabunge ya kaunti na kamati za utendaji katika kaunti, ikijumuisha mwenyekiti wa mikutano na jinsi mikutano hiyo itafanywa, idadi ya watu wanaohitajika ili mkutano kufanyika na upigaji kura; na

e) kusimamishwa kwa muda kwa mabunge ya kaunti na kamati za utendaji.

# SURA YA KUMI NA MBILI — FEDHA ZA UMMA

## Sehemu ya I—Kanuni na Taratibu Kuhusu Fedha za Umma

*Kanuni za fedha za umma.*

**201.** Kanuni zifuatazo zitaongoza maswala yote yanayohusiana na fedha za umma katika Jamhuri-—

a) kutakuwa na uwazi na uwajibikaji, ikijumuisha kushiriki kwa umma katika maswala ya kifedha;

b) mfumo wa fedha za umma utakuza jamii yenye usawa, na hasa—

i. mzigo wa utozaji ushuru utashirikiwa kwa haki;

ii. mapato yanayopatikana katika ngazi ya kitaifa yatagawanywa kwa usawa kati ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti; na

iii. matumizi ya fedha yatakuza maendeleo yenye usawa nchini, ikijumuisha utoaji wa mgao maalum kwa vikundi vya watu waliotengwa au wanaotoka maeneo yaliyotengwa; na

c) mizigo na manufaa ya matumizi ya rasilimali na ukopaji wa umma yatashirikiwa kwa usawa kati ya vizazi vya sasa na vizazi vijavyo;

d) fedha za umma zitatumiwa kwa njia ya busara na yenye uwajibikaji; na

e) usimamizi wa fedha utakuwa wenye uwajibikaji, na kuripoti kuhusu hazina ya serikali na matumizi yake kutakuwa wazi.

**202.**

*Ugavi wenye usawa wa mapato ya kitaifa.*

(1) mapato yanayozalishwa katika kiwango cha kitaifa yatashirikiwa kwa usawa kati ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti;

(2) Serikali za kaunti zinaweza kupewa mgao wa ziada

kutoka kwenye sehemu ya mapato ya serikali ya kitaifa, kwa masharti au bila masharti.

**203.**

*Ugavi wenye usawa na sheria zingine za kifedha.*

(1) Vigezo vifuatavyo vitazingatiwa katika kutoa uamuzi kuhusu migao sawa iliyobainiwa chini ya Kifungu cha 202 na katika sheria zote za kitaifa zinazohusu serikali ya kaunti zinazotungwa kulingana na Sura hii—

a) maslahi ya kitaifa;

b) mgao wowote ambao lazima utolewe kwa mujibu wa deni la umma na majukumu mengine ya kitaifa;

c) mahitaji ya serikali ya kitaifa yatakayoamuliwa kwa kutumia vigezo visivyoegemea upande wowote;

d) hitaji la kuhakikisha kwamba serikali za kaunti zina uwezo wa kutekeleza majukumu yaliyotolewa kwa serikali hizo;

e) uwezo wa kifedha na ufanisi wa serikali za kaunti;

f) maendeleo na mahitaji mengine ya serikali za kaunti;

g) tofauti za kiuchumi miongoni mwa kaunti na kati ya kaunti na hitaji la kuzisawazisha;

h) hitaji la kuchukua hatua sawazishi kwa sababu ya maeneo na vikundi vya watu wanyonge;

i) hitaji la kuboresha uchumi katika kila kaunti na kutoa motisha ya kuboresha uwezo wa kuzalisha mapato katika kila kaunti;

j) matamanio kuhusu mgao wa mapato ulio thabiti na unaoweza kutabirika;

k) hitaji la wepesi katika kukabiliana na majanga na mahitaji mengine ya muda mfupi, kwenye



SIO YA KUUZWA

misingi sawa ya vigezo visivyoegemea upande wowote.

(2) Katika kila mwaka wa fedha, mgao unaolingana na mapato yaliyozalishwa kitaifa ambao utatengewa serikali za kaunti hautakuwa chini ya asilimia kumi na tano ya mapato yote ambayo yalikusanywa na serikali ya kitaifa.

(3) Kiasi cha fedha zilizotajwa katika ibara ya (2) zitahesabiwa kwenye msingi wa akaunti zilizokaguliwa hivi majuzi kuhusu mapato yaliyokusanywa, kama ilivyoidhinishwa na Bunge la Kitaifa.

**204.**

*Hazina ya Usawazishaji.*

(1) Imebuniwa Hazina ya Usawazishaji ambayo itachukua asilimia ya nusu moja ya mapato yote yatakayokusanywa na serikali ya kitaifa katika kila mwaka, mapato hayo yakihesabiwa kwenye msingi wa akaunti zilizokaguliwa hivi majuzi kuhusu mapato yaliyokusanywa, kama ilivyoidhinishwa na Bunge la Kitaifa.

(2) Serikali ya kitaifa itatumia Hazina ya Usawazishaji kutoa huduma za kimsingi tu ikijumuisha maji, barabara, matibabu na nguvu za umeme katika maeneo yaliyotengwa kwa kiwango kitakachoboresha huduma hizo katika maeneo hayo ili ziwe sawa na viwango vya huduma vinavyotolewa katika maeneo mengine nchini, kama iwezekanavyo.

(3) Serikali ya kitaifa inaweza kutumia Hazina ya Usawazishaji––

a) kwa kiasi tu ambacho matumizi ya fedha za hazina hiyo yameidhinishwa tu katika Mswada wa Matumizi ya Fedha uliopitishwa na Bunge; na



SIO YA KUUZWA

b) kwa njia ya moja kwa moja au vinginevyo kupitia kwa ruzuku zilizo na kwa kaunti ambazo zina jamii zilizotengwa.

(4) Ushauri wa Tume ya Ugavi wa Mapato utatafutwa na mapendekezo yake kuzingatiwa kabla ya Bunge kupitisha Mswada wowote unaoidhinisha matumizi ya fedha kutoka kwenye Hazina ya Usawazishaji.

(5) Fedha zozote katika Hazina ya Usawazishaji ambazo hazitakuwa zimetumiwa kufikia mwisho wa mwaka wa kifedha, zitasalia katika Hazina hiyo kwa matumizi kulingana na ibara ya (2) na (3) katika mwaka wa fedha utakaofuata.

(6) Kutekelezwa kwa Kifungu hiki kutamalizika miaka ishirini baada ya tarehe ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii, lakini kwa kuzingatia ibara ya (7).

(7) Bunge linaweza kupitisha sheria itakayositisha utekelezaji wa ibara ya (6) kwa kipindi cha ziada cha miaka iliyowekwa, lakini kwa kuzingatia ibara ya (8).

(8) Sheria chini ya ibara ya (7) itaungwa na zaidi ya nusu ya wabunge wote katika Bunge la Kitaifa, na zaidi ya nusu ya wajumbe wote wa kaunti katika Seneti.

(9) Fedha hazitaondolewa katika Hazina ya Usawazishaji isipokuwa Msimamizi wa Bajeti awe ameidhinisha kuondolewa huko.

**205.**

*Mashauriano kuhusu sheria za kifedha zinazoathiri kaunti.*

(1) Wakati ambao Mswada unaojumuisha miongozo kuhusu ugavi wa mapato, au suala lolote la kifedha linalohusu serikali za kaunti utakapochapishwa, Tume ya Ugavi wa Mapato itachunguza miongozo hiyo na kutoa mapendekezo kwa Bunge la Kitaifa na Seneti.



SIO YA KUUZWA

(2) Mapendekezo yoyote ya Tume hii yatawasilishwa Bungeni, na kila Kitengo cha Bunge kitazingatia mapendekezo hayo kabla ya kupigia Mswada huo kura.

**Sehemu ya 2—Hazina Zinginezo za Umma**

**206.**

*Hazina ya Kijumla na fedha zingine za umma.*

(1) Hazina Jumuishi imebuniwa, ambayo itahifadhi fedha zilizozalishwa au kupokewa na, au kwa niaba ya serikali ya kitaifa, isipokuwa fedha ambazo—

a) zimetengwa kutoka kwa Hazina hiyo kwa sababu maalum zilizotolewa na Sheria ya Bunge, na ambazo zitawekwa katika hazina nyingine ya umma iliyobuniwa kwa lengo maalum; au

b) zinaweza, chini ya Sheria ya Bunge, kuhifadhiwa na kitengo cha Serikali kilichozipokea kwa lengo la kugharamia mahitaji ya kitengo hicho.

(2) Fedha zinaweza kuondolewa kutoka kwenye Hazina Jumuishi tu—

a) kulingana na kuidhinishwa kwa matumizi yake kupitia kwa Sheria ya Bunge;

b) kulingana na Kifungu cha 222 au 223; au

c) kama malipo kutoka kwa Hazina hiyo kama ilivyoidhinishwa na Katiba hii au na Sheria ya Bunge.

(3) Fedha hazitaondolewa kwenye hazina nyingine yoyote ya fedha za umma kando na Hazina Jumuishi, isipokuwa kuondolewa kwa fedha hizo kumeidhinishwa na Sheria ya Bunge.

(4) Fedha hazitaondolewa kwenye Hazina Jumuishi isipokuwa Msimamizi wa Bajeti ameidhinisha kuondolewa huko.

**207.**

*Hazina za Mapato za serikali za kaunti.*

(1) Hazina ya Mapato ya kila serikali ya kaunti imeundwa. Hazina hii itapokea fedha zote zilizozalishwa au kupokelewa na, au kwa niaba ya serikali ya kaunti, isipokuwa fedha ambazo kwa sababu maalum zimetengwa na Sheria ya Bunge.

(2) Fedha zinaweza kutolewa kutoka kwenye Hazina ya Mapato ya serikali ya kaunti—

a) kama malipo yanayotolewa kwenye Hazina ya Mapato na ambayo yameidhinishwa na Sheria ya Bunge au sheria ya kaunti; au

b) kama ilivyoidhinishwa na sheria ya matumizi ya fedha katika kaunti hiyo.

(3) Fedha hazitatolewa kwenye Hazina ya Mapato isipokuwa Msimamizi wa Bajeti aidhinishe kutolewa huko.

(4) Sheria ya Bunge inaweza—

a) kutoa idhini ya ziada ya kutolewa kwa fedha kutoka kwenye Hazina ya Mapato ya serikali ya kaunti; na

b) kutoa mwongozo kuhusu kubuniwa kwa hazina zinginezo katika kaunti, na usimamizi wa hazina hizo.

**208.**

*Hazina ya Dharura.*

(1) Hazina ya Dharura imebuniwa na usimamizi wake utakuwa kulingana na Sheria ya Bunge.

(2) Sheria ya Bunge itatoa mwongozo kuhusu kutolewa kwa fedha kutoka kwenye Hazina ya Dharura ikiwa waziri anayehusikana na fedha ataridhika kwamba kuna hitaji la dharura na ambalo halikutarajiwa, ambalo halipo chini ya mamlaka yoyote.



SIO YA KUUZWA

**Sehemu ya 3—Deni la Umma na Mamlaka ya Kuongeza Mapato**

**209.**

*Mamlaka ya kutoza ushuru na malipo mengine.*

(1) Serikali ya kitaifa tu ndio inayoweza kutoza—

a) kodi ya mapato;

b) kodi katika uuzaji wa bidhaa na huduma;

c) ushuru wa forodha na kodi zingine zinazotozwa katika bidhaa zinazoingizwa nchini na kuuzwa nje ya nchi; na

d) ushuru wa bidhaa zilizotengenezwa.

(2) Sheria ya Bunge inaweza kuipa mamlaka serikali ya kitaifa kutoza ushuru au kodi nyingine yoyote, isipokuwa kodi iliyotajwa katika ibara ya (3) (a) au (b).

(3) Kaunti inaweza kutoza—

a) kodi katika umiliki wa ardhi;

b) makodi ya burudani; na

c) kodi nyingine yoyote ambayo imeruhusiwa na Sheria ya Bunge kutoza.

(4) Serikali ya kitaifa na serikali za kaunti zinaweza kutoza malipo kwa huduma zinazotolewa.

(5) Mamlaka ya utozaji ushuru na mengine ya kuzalisha mapato ya kaunti hayatatekelezwa kwa njia ambayo inaathirisha sera za kiuchumi za kitaifa, shughuli za kiuchumi katika mipaka ya kaunti au usafirishaji wa bidhaa, huduma, rasilimali au wafanyakazi kote nchini.

**210.**

*Kutoza ushuru.*

(1) Hakuna kodi yoyote au ada ya leseni itakayotozwa, kuondolewa au kubadilishwa isipokuwa kulingana na sheria.

(2) Ikiwa sheria itaruhusu kuondolewa kwa ushuru au ada ya leseni—

a) rekodi iliyowekwa wazi kwa umma kuhusu kuondolewa kwa kodi, pamoja na sababu za kuondolewa huko itadumishwa; na

b) kila kuondolewa kwa kodi, na sababu zake, kutaripotiwa kwa Mkaguzi Mkuu.

(3) Hakuna sheria yoyote ambayo itamtenga au kumwondoa afisa wa Serikali katika ulipaji wa ushuru kwa sababu za—

a) ofisi ambayo afisa huyo wa Serikali anahudumu; au

b) hali ya kazi ya afisa huyo wa Serikali.

**211.**

*Ukopaji wa serikali ya kitaifa.*

(1) Kupitia kwa sheria, Bunge linaweza—

a) kutoa masharti ambayo yanapaswa kutimizwa na serikali ya kitaifa inapokopa; na

b) kulazimisha mahitaji ya kuripoti.

(2) Katika muda wa siku saba baada ya Kitengo chochote cha Bunge kutoa ombi kwa uamuzi, Waziri anayehusikana na fedha atawasilisha maelezo kuhusu mkopo au udhamini wowote mbele ya kamati husika, ikijumuisha maelezo yote yanayohitajika ili kuonyesha—

a) kiwango cha deni lote kwa kuonyesha kiasi hasa kilichokopwa na kiasi jumla cha riba;

b) mkopo huo ulivyotumiwa au utakavyotumiwa;

c) mikakati iliyowekwa ili kuulipa mkopo huo; na

d) hatua zilizochukuliwa katika kulipa mkopo huo.



SIO YA KUUZWA

**212.**

*Ukopaji wa kaunti*

(1) Serikali ya kaunti inaweza kukopa tu—

a) ikiwa serikali ya kitaifa itadhamini mkopo huo; na

b) kwa idhini ya bunge la kaunti.

**213.**

*Udhamini wa mikopo ya serikali ya kitaifa.*

(1) Sheria ya Bunge itaweka kanuni na masharti ambayo kwayo serikali ya kitaifa inaweza kudhamini mikopo.

(2) Katika muda wa miezi miwili baada ya kukamilika kwa kila mwaka wa fedha, serikali ya kitaifa itachapisha ripoti itakayoonyesha udhamini wote uliotolewa katika mwaka huo.

**214.**

*Deni la umma.*

(1) Deni la umma ni deni linalolipwa kutoka kwenye Hazina Jumuishi, lakini Sheria ya Bunge inaweza kutoa mwongozo kuhusu kulipwa kwa sehemu ya deni hilo kupitia kwa hazina zingine za umma.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "deni la umma" linamaanisha madeni yote yanayohusisha mikopo iliyokopwa au kudhaminiwa na amana iliyotolewa au kudhaminiwa na serikali ya kitaifa.

**Sehemu ya 4—Ugavi wa Mapato**

**215.**

*Tume ya Ugavi wa Mapato.*

(1) Tume ya Ugavi wa Mapato imebuniwa.

(2) Tume hii itajumuisha watu wafuatao watakaoteuliwa na Rais—

a) mwenyekiti, atakayeteuliwa na Rais na kuidhinishwa na Bunge la Kitaifa;

b) watu wawili watakaoteuliwa na vyama vya kisiasa vinavyowakilishwa katika Bunge la Kitaifa kulingana na idadi ya wabunge katika vyama hivyo walio bungeni;

c) watu watano watakaoteuliwa na vyama vya kisiasa vinavyowakilishwa katika seneti kulingana na idadi ya maseneta wa vyama hivyo walio katika Seneti; na

d) Katibu Mkuu katika Wizara inayosimamia fedha.

(3) Watu watakaoteuliwa kwa mujibu wa ibara ya (2) hawatakuwa wanachama wa Bunge.

(4) Ili kuhitimu kuwa mwanachama wa Tume hii chini ya ibara ya (2) (a), (b) au (c), lazima mtu awe na uzoefu mpana wa kitaaluma katika masuala ya kifedha na uchumi.

**216.**

*Kazi ya Tume ya Ugavi wa Mapato*

(1) Jukumu kuu la Tume ya Ugavi wa Mapato ni kutoa mapendekezo kuhusu misingi ya ugavi wa mapato yanayozalishwa na serikali ya kitaifa kwa njia yenye usawa––

a) kati ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti; na

b) miongoni mwa serikali za kaunti.

(2) Tume hiyo pia itatoa mapendekezo katika masuala mengine yanayohusiana na ufadhili wa serikali za kaunti na usimamizi wa fedha katika serikali hizi, kulingana na Katiba hii na sheria za kitaifa.

(3) Katika uandalizi wa mapendekezo, Tume hiyo itazingatia––

a) kukuza na kuwezesha utekelezaji wa vigezo vilivyotajwa katika Kifungu cha 203 (1);

b) kwa wakati ufaao, kufafanua na kuboresha njia za uzalishaji wa mapato za serikali ya kitaifa na serikali za kaunti; na

c) kuhimiza uwajibikaji wa kifedha.

(4) Tume itaamua, itachapisha na kukagua mara kwa mara sera ambayo kwayo inatoa vigezo vya kutambua

maeneo yaliyotengwa kwa madhumuni ya Kifungu cha 204 (2).

(5) Tume itawasilisha mapendekezo yake kwa Seneti, Bunge la Kitaifa, kitengo cha utendaji cha serikali ya kitaifa, mabunge ya kaunti na vitengo vya utendaji katika serikali za kaunti.

**217.**

*Ugavi wa mapato*

(1) Mara moja baada ya kila miaka mitano, Seneti, kwa njia ya uamuzi, itaamua misingi itakayotumiwa kugawa mapato ya kitaifa ambayo hutolewa kwa serikali za kaunti kila mwaka.

(2) Katika kuamua msingi wa ugavi wa mapato chini ibara ya (1), Seneti—

a) itazingatia vigezo katika Kifungu cha 203 (1);

b) itaomba kupata mapendekezo ya Tume ya Ugavi wa Mapato na kuyazingatia;

c) itashauriana na magavana wa kaunti, Waziri anayesimamia fedha na usimamizi wowote wa serikali za kaunti; na

d) itawaalika watu, ikijumuisha mashirika ya kitaaluma ili yawasilishe maoni yao kuhusu suala hilo.

(3) Katika muda wa siku kumi baada ya Seneti kuidhinisha uamuzi chini ya ibara ya (1), Spika wa Seneti atawasilisha uamuzi huo kwa Spika wa Bunge la Kitaifa.

(4) Katika muda wa siku sitini baada ya uamuzi wa Seneti kuwasilishwa kama inavyorejelewa katika ibara ya (3), Bunge la Kitaifa linaweza kutathmini uamuzi huo, na kuupigia kura ili kuuidhinisha kwa marekebisho au bila marekebisho, au linaweza kuukataa.

(5) Ikiwa Bunge la Kitaifa––

a) halitapiga kura kuhusu uamuzi huo ndani ya siku sitini, uamuzi huo utachukuliwa kuwa umeidhinishwa na Bunge la Kitaifa bila marekebisho; au

b) litapiga kura kuhusu uamuzi huo, uamuzi huo utakuwa––

i. umerekebishwa ikiwa angalau thuluthi mbili ya wabunge itapiga kura ya uungaji mkono wa marekebisho hayo;

ii. umekataliwa ikiwa idadi isiyopungua thuluthi mbili ya wabunge watapiga kura kuukataa, bila kujalisha kwamba umerekebishwa kwanza na Bunge la Kitaifa; au

iii. umeidhinishwa, katika hali nyingine yoyote.

(6) Ikiwa Bunge la Kitaifa litaidhinisha uamuzi uliorekebishwa, au kuukataa uamuzi huo, Seneti, kwa uchaguzi wake, linaweza––

a) kupitisha uamuzi mpya chini ya ibara ya (1), na katika hali hii, miongozo katika ibara ya (4) na (5) itatumiwa upya; au

b) kuomba kwamba suala hilo liwasilishwe mbele ya kamati ya pamoja ya Vitengo vyote viwili vya Bunge kwa madhumuni ya upatanisho chini ya Kifungu cha 113, kitakachotumiwa kwa kuzingatia mabadiliko yatakayohitajika.

(7) Uamuzi chini ya Kifungu hiki utakaokuwa umeidhinishwa chini ya ibara ya (5) utatekelezwa hadi uamuzi ufuatao utakapoidhinishwa.

(8) Licha ya ibara ya (1), Seneti, kwa uamuzi ulioungwa mkono na wanachama wasiopungua thuluthi mbili, inaweza kurekebisha uamuzi kwa wakati wowote baada ya kuidhinishwa kwake.

(9) Ibara ya (2) hadi (8), kwa kuzingatia mabadiliko



SIO YA KUUZWA

yanayohitajika, zitatumika katika uamuzi uliotolewa chini ya ibara ya (8).

*Miswada ya Ugavi wa Mapato ya Kila Mwaka*

**218.**

(1) Katika muda wa angalau miezi miwili baada ya kukamilika kwa kila mwaka wa kifedha, yafuatayo yatawasilishwa bungeni––

a) Mswada Kuhusu Ugavi wa Mapato, ambao utagawa mapato yaliyozalishwa na serikali ya kitaifa kati ya viwango vya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti kwa mujibu wa Katiba hii; na

b) Mswada wa Kutenga Mapato kwa Serikali za Kaunti, ambao utagawa mapato yaliyotengwa kwa serikali za kaunti katika kila kaunti, kwenye misingi itakayoamuliwa kulingana na uamuzi unaotekelezwa chini ya Kifungu cha 217.

(2) Kila Mswada unaohitajika chini ya ibara ya (2) utaambatanishwa na hati itakayoweka wazi––

a) maelezo kuhusu mgao wa mapato kama ilivyopendekezwa na Mswada;

*Mswada wa makadirio ya bajeti na Matumizi ya Mwaka.*

b) tathmini ya Mswada kulingana na vigezo vilivyotajwa katika Kifungu cha 203 (1); na

c) muhtasari wa tofauti zozote muhimu dhidi ya mapendekezo ya Tume ya Ugavi wa Mapato, na maelezo kwa kila tofauti iliyopo.

*Uhamishaji wa ugavi wenye usawa.*

**219.** Mgao wa kaunti wa mapato yaliyozalishwa na serikali ya kitaifa utahamishiwa kaunti bila kucheleweshwa pasipo sababu na bila kupunguzwa, isipokuwa uhamishaji huo unapositishwa chini ya Kifungu cha 225.

### Sehemu ya 5—Bajeti na Matumizi

**220.**

*Muundo, yaliyomo na wakati wa bajeti.*

(1) Bajeti za serikali ya kitaifa na serikali za kaunti zitajumuisha—

a) makadirio ya mapato na matumizi, zikitofautisha matumizi ya kawaida na yale ya kimaendeleo;

b) mapendekezo kuhusu jinsi upungufu wowote wa kifedha unaotarajiwa katika kipindi ambacho bajeti hizo zitatumika utashughulikiwa; na

c) mapendekezo kuhusu kukopa na madeni yoyote ya umma ambayo yataongeza deni la umma katika mwaka utakaofuata

(2) Sheria za kitaifa zitatoa mwongozo kuhusu—

a) muundo wa mipango ya maendeleo na bajeti za kaunti;

b) wakati ambao mipango na bajeti za serikali za kaunti zitawasilishwa katika mabunge ya kaunti; na

c) njia na namna ya mashauriano kati ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti katika mchakato wa kuandaa mipango na bajeti.

**221.**

(1) Kwa kipindi kisichopungua miezi miwili kabla ya kukamilika kwa kila mwaka wa kifedha, Waziri anayehusika na fedha atawasilisha mbele ya Bunge la Kitaifa makadirio ya mapato na matumizi ya serikali ya kitaifa ya mwaka ufuatao wa kifedha.

(2) Makadirio yaliyotajwa katika ibara ya (1)––

a) yatajumuisha makadirio ya matumizi kutoka kwenye Hazina ya Usawazishaji; na

b) yatakuwa kwa muundo, na kwa mujibu wa utaratibu utakaotolewa na Sheria ya Bunge.



SIO YA KUUZWA

(3) Bunge la Kitaifa litazingatia makadirio yaliyowasilishwa chini ya ibara ya (1) pamoja na makadirio yaliyowasilishwa na Tume ya Huduma za Bunge na Msajili Mkuu wa Kitengo cha Mahakama chini ya Kifungu cha 127 na 173, mtawalia.

(4) Kabla ya Bunge la Kitaifa kuzingatia makadirio ya mapato na matumizi, kamati ya Bunge itajadili na kukagua makadirio hayo na kutoa mapendekezo yake kwa Bunge.

(5) Katika kujadili na kukagua makadirio hayo, kamati itazingatia maoni ya umma na mapendekezo hayo ya umma yatazingatiwa kamati hiyo itakapowasilisha mapendekezo yake kwa Bunge la Kitaifa.

(6) Makadirio ya matumizi ya serikali ya kitaifa na makadirio ya matumizi ya Kitengo cha Mahakama na ya Bunge yatakapoidhinishwa na Bunge la Kitaifa, makadirio hayo yatajumuishwa katika Mswada wa Matumizi ya Fedha, utakaowasilishwa mbele ya Bunge la Kitaifa ili kuidhinisha kutolewa kwa fedha za matumizi zinazohitajika kutoka kwenye Hazina Jumuishi, na kwa matumizi ya fedha hizo kwa madhumuni yaliyotajwa katika Mswada huo.

(7) Mswada wa Matumizi ya Fedha uliotajwa katika ibara ya (6) hautajumuisha matumizi yanayolipiwa kutoka kwenye Hazina Jumuishi kulingana na Katiba hii au Sheria ya Bunge.

**222.**

*Matumizi kabla ya kuidhinishwa kwa bajeti ya kila mwaka.*

(1) Ikiwa Sheria Kuhusu Matumizi ya Fedha katika mwaka wa kifedha haijaidhinishwa na Rais, au hakuna uwezekano mkubwa wa sheria hiyo kuidhinishwa na Rais mwanzoni mwa mwaka wa kifedha, Bunge la Kitaifa linaweza kuidhinisha kutolewa kwa fedha kutoka kwenye Hazina Jumuishi.



SIO YA KUUZWA

(2) (2) Fedha zitakazotolewa chini ya ibara ya (1)—

a) zitatumiwa kwa madhumuni ya kuendesha huduma za serikali ya kitaifa katika mwaka huo hadi wakati ambapo Sheria Kuhusu Matumizi ya Fedha itakapoidhinishwa na Rais;

b) kwa jumla, hazitazidi nusu ya fedha zilizopendekezwa katika makadirio ya matumizi ya mwaka huo yaliyowasilishwa katika Bunge la Kitaifa; na

c) zitajumuishwa kwenye Sheria Kuhusu Matumizi ya Fedha, katika vitengo tofauti vya matumizi, na katika huduma mbalimbali ambazo fedha hizo zilikusudiwa kutekeleza.

**223.**

*Matumizi ya ziada.*

(1) Kwa kuzingatia ibara ya (2) hadi (4), serikali ya kitaifa inaweza kutumia fedha ambazo hazijaidhinishwa ikiwa—

a) kiasi kilichotengwa kwa madhumuni yoyote chini ya Sheria Kuhusu Matumizi ya Fedha hakitoshi au hitaji limetokea la matumizi ambayo hayakuwa yamekadiriwa na kuidhinishwa na Sheria hiyo; au

b) fedha zimetolewa kutoka kwenye Hazina ya Dharura.

(2) Idhini ya Bunge kuhusu matumizi yoyote chini ya Kifungu hiki itafuatiliwa katika muda wa miezi miwili baada ya fedha kutolewa kwa mara ya kwanza, lakini kwa kuzingatia ibara ya (3).

(3) Ikiwa Bunge halitakuwa na vikao katika muda uliobainishwa katika ibara ya (2), au lina vikao lakini liende mapumzikoni kabla ya idhini kutolewa, idhini hiyo itafuatiliwa katika muda wa wiki mbili baada ya kikao chake kitakachofuata.



SIO YA KUUZWA

(4) Bunge la Kitaifa litakapokuwa limeidhinisha matumizi chini ya ibara ya (2), Mswada kuhusu matumizi ya fedha utawasilishwa ili kuidhinisha matumizi ya fedha.

(5) Katika mwaka wowote wa kifedha, serikali ya kitaifa haiwezi kutumia fedha chini ya Kifungu hiki, kwa kiasi kinachozidi asilimia kumi ya fedha zilizotengwa na Bunge kwa mwaka huo, isipokuwa Bunge liidhinishe asilimia ya juu kuliko asilimia kumi, katika hali maalum.

*Miswada kuhusu matumizi ya fedha katika kaunti.*

**224.** Kwenye msingi ya Mswada wa Ugavi wa Mapato uliopitishwa na Bunge chini ya Kifungu cha 218, kila serikali ya kaunti itaandaa na kupitisha bajeti yake ya mwaka na Mswada wa matumizi ya fedha kwa muundo, na kulingana na taratibu zilizotolewa na Sheria ya Bunge.

### Sehemu ya 6—Udhibiti wa Fedha za Umma

**225.**

*Udhibiti wa fedha.*

(1) Sheria ya Bunge itatoa mwongozo kuhusu kubuniwa kwa Hazina ya kitaifa, majukumu na uwajibikaji wa Hazina hiyo.

(2) Bunge litatunga sheria ili kuhakikisha kuwa kunausimamizi wa matumizi na uwajibikaji katika serikali zote na litaweka mikakati ili kuhakikisha kwamba usimamizi huo na uwajibikaji umetekelezwa.

(3) Sheria chini ya ibara ya (2) inaweza kumwidhinisha Waziri anayehusika na fedha kusitisha uhamishaji wa fedha kwa kitengo fulani cha Serikali au shirika lolote la umma—

a) iwapo tu kuna ukiukaji mkubwa au ukiukaji wa mara kwa mara wa hatua zilizowekwa chini ya sheria hiyo; na



SIO YA KUUZWA

b) kwa kuzingatia mahitaji ya ibara ya (4) hadi ya (7).

(4) Uamuzi wa kusitisha uhamishaji wa fedha chini ya ibara ya (3) hauwezi kusitisha uhamishaji wa zaidi ya asilimia hamsini ya fedha zinazopaswa kuhamishwa kwa serikali ya kaunti.

(5) Uamuzi wa kusitisha uhamishaji wa fedha, unavyobainishwa chini ya ibara ya (3)—

a) hautasitisha kuhamishwa kwa fedha kwa zaidi ya siku sitini; na

b) unaweza kutekelezwa mara moja, lakini unaweza kuwacha kutekelezwa kwa mtazamo wa muda uliopita isipokuwa katika muda wa siku thelathini baada ya tarehe ya uamuzi huo, Bunge liidhinishe kwa uamuzi utakaopitishwa katika ngazi zote mbili za Bunge.

(6) Bunge linaweza kuweka upya uamuzi wa kusitisha uhamishaji wa fedha, lakini kwa siku zisizozidi sitini kwa wakati mmoja.

(7) Bunge haliwezi kuidhinisha au kuweka upya uamuzi wa kusitisha uhamishaji wa fedha isipokuwa—

a) Msimamizi wa Bajeti amewasilisha ripoti kuhusu suala hilo Bungeni; na

b) shirika hilo la umma limepewa nafasi ya kujibu madai dhidi yake, na kujitetea mbele ya kamati husika ya bunge.

**226.**

*Akaunti na ukaguzi wa mashirika ya umma.*

(1) Sheria ya Bunge itatoa mwongozo kuhusu—

a) kuhifadhi rekodi za kifedha na ukaguzi wa hesabu za serikali zote na mashirika mengine ya umma, na itatoa mwongozo kuhusu hatua zinginezo za kuhakikisha usimamizi wazi wa fedha; na

b) cheo cha afisa wa uhasibu katika kila shirika la umma katika ngazi ya serikali ya kitaifa na ya kaunti.

(2) Afisa wa uhasibu wa shirika la umma la kitaifa anawajibikia Bunge la Kitaifa katika usimamizi wa fedha wa shirika hilo, na afisa wa uhasibu wa shirika la umma la kaunti anawajibikia bunge la kaunti katika usimamizi wa fedha wa shirika hilo.

(3) Kwa kuzingatia ibara ya (4), hesabu za vitengo vyote vya Serikali na viwango vyote vya serikali zitakaguliwa na Mkaguzi Mkuu.

(4) Hesabu za ofisi ya Mkaguzi Mkuu zitakagulia na mhasibu anayestahiki kitaaluma na atakayeteuliwa na Bunge la Kitaifa, na mhasibu huyo ataripoti kuhusu hesabu hizo.

(5) Ikiwa mhudumu katika ofisi ya umma, ikijumuisha ofisi ya kisiasa, ataelekeza au kuidhinisha matumizi ya fedha za umma kinyume na sheria au maagizo, mtu huyu atawajibikia hasara yoyote itakayotokana na matumizi hayo na atagharimia hasara hiyo, bila kujalisha ikiwa mtu huyo ataendelea kuhudumu katika ofisi hiyo.

**227.**

*Ununuaji wa bidhaa na huduma za umma.*

(1) Kitengo cha serikali au shirika lolote la umma linapotoa kandarasi za ununuzi wa bidhaa au huduma, shirika au kitengo hicho kitafanya hivyo kulingana na mfumo ambao ni wa haki, wenye usawa, uwazi, wenye ushindani na wenye bei nafuu.

(2) Sheria ya Bunge itatoa mwongozo kuhusu jinsi sera zinazohusiana na ununuzi na uuzaji wa mali zitavyotekelezwa na inaweza kutoa mwongozo kuhusu suala moja au masuala yote—

a) kategoria za kupewa kipaumbele wakati wa kutoa kandarasi;

b) ulinzi au maendeleo ya watu, kategoria za watu au vikundi vya watu ambao walinyanyaswa kwa ushindani usio wa haki au uliowabagua na kuwatenga hapo awali;

c) adhabu dhidi ya wanakandarasi ambao utendakazi wao hautimizi viwango vilivyokubaliwa kitaaluma, makubaliano ya kimkataba au sheria; na

d) adhabu dhidi ya watu ambao hawajalipa kodi au ushuru, au ambao wamehusika katika ufisadi au ambao wamekiuka vikubwa sheria kuhusu uajiri wa haki.

**Sehemu ya 6— Maafisa wa Kifedha na Taasisi za Kifedha**

**228.**

*Msimamizi wa Bajeti.*

(1) Kutakuwa na Msimamizi wa Bajeti atakayependekezwa na Rais, na kwa idhini ya Bunge la Kitaifa, kuteuliwa na Rais.

(2) Ili kustahiki kuwa Msimamizi, lazima mtu awe na ufahamu mkubwa katika masuala ya fedha za umma, au uzoefu wa muda usiopungua miaka kumi katika ukaguzi au usimamizi wa fedha za umma.

(3) Kwa kuzingatia Kifungu cha 251, Msimamizi atahudumu kwa muhula wa miaka minane na hatastahiki kuteuliwa tena.

(4) Msimamizi wa Bajeti atasimamia utekelezaji wa bajeti ya kitaifa na bajeti za serikali za kaunti kwa kuidhinisha kutolewa kwa fedha kutoka kwa hazina za umma chini ya Vifungu vya 204, 206 na 207.



SIO YA KUUZWA

(5) ***Msimamizi huyo hataidhinisha kutolewa kwa fedha kutoka kwa hazina ya umma isipokuwa aridhike kuwa kutolewa huko kumeidhinishwa kisheria.

(6) Kila baada ya miezi minne, Msimamizi huyo atawasilisha mbele ya kila Kitengo cha Bunge ripoti kuhusu utekelezaji wa bajeti ya kitaifa na bajeti za serikali za kaunti.

**229.**

*Mkaguzi Mkuu.*

(1) Kutakuwa na Mkaguzi Mkuu atakayependekezwa na Rais, na kwa idhini ya Bunge la Kitaifa, kuteuliwa na Rais.

(2) Ili kustahiki kuwa Mkaguzi Mkuu, lazima mtu awe na ufahamu mkubwa katika masuala ya fedha za umma, au uzoefu wa muda usiopungua miaka kumi katika ukaguzi au usimamizi wa fedha za umma.

(3) Kwa kuzingatia Kifungu cha 251, Mkaguzi Mkuu atahudumu kwa muhula wa miaka nane na hatastahiki kuteuliwa tena.

(4) Katika muda wa miezi sita baada ya kukamilika kwa kila mwaka wa kifedha, Mkaguzi Mkuu, kwa madhumuni ya mwaka huo wa kifedha, atakagua na kuripoti kuhusu masuala yafuatayo—

a) hesabu za serikali ya kitaifa na serikali za kaunti;

b) hesabu za hazina zote na mashirika ya serikali ya kitaifa na ya serikali za kaunti;

c) hesabu za mahakama zote;

d) hesabu za kila tume na ofisi huru zilizobuniwa chini ya Katiba hii;

e) hesabu za Bunge la Kitaifa, Seneti na mabunge ya kaunti;

f) hesabu za fedha za vyama vya kisiasa ambazo zinatoka katika hazina za umma.



SIO YA KUUZWA

g) deni la umma; na

h) hesabu za shirika lingine lolote ambalo linatakiwa kisheria kufanyiwa ukaguzi na Mkaguzi Mkuu.

(5) Mkaguzi Mkuu anaweza kukagua na kutoa ripoti kuhusu hesabu za shirika lolote linalopokea fedha kutoka kwenye hazina za umma.

(6) Ripoti ya ukaguzi itathibitisha iwapo fedha za umma zimetumiwa kwa mujibu wa sheria na kwa njia yenye ufanisi.

(7) Ripoti za ukaguzi zitawasilishwa katika Bunge au katika bunge la kaunti.

(8) Katika muda wa miezi mitatu baada ya kupokea ripoti ya ukaguzi, Bunge la Kitaifa au la kaunti litazingatia na kujadili ripoti hiyo na kuchukua hatua ifaayo.

**230.**

*Tume ya Mishahara na Malipo.*

(1) Tume ya Mishahara na Malipo imebuniwa.

(2) Tume ya Mishahara na Malipo inajumuisha watu wafuatao watakaoteuliwa na Rais—

a) mwenyekiti;

b) watu walioteuliwa na mashirika yafuatayo, miongoni mwa watu ambao sio wanachama au wafanyakazi katika mashirika hayo—

i. Tume ya Huduma za Bunge;

ii. Tume ya Huduma za Umma;

iii. Tume ya Huduma za Mahakama;

iv. Tume ya Huduma kwa Walimu;

v. Tume ya Kitaifa ya Huduma za Polisi;

vi. Baraza la Ulinzi; na

vii. Seneti, kwa niaba ya serikali za kaunti;

c) mtu mmoja aliyeteuliwa na—



SIO YA KUUZWA

i. shirika linalowakilisha vyama vya wafanyakazi;

ii. shirika linalowakilisha waajiri; na

iii. baraza la pamoja la mashirika ya kitaaluma kulingana na sheria;

d) mtu mmoja aliyeteuliwa na—

i. Waziri anayewajibikia masuala ya fedha; na

ii. Mwanasheria Mkuu; na

e) mtu aliye na uzoefu katika usimamizi wa wafanyakazi katika huduma za umma, aliyeteuliwa na Waziri anayesimamia huduma za umma.

(3) Makamishna waliotajwa katika ibara ya (1) (d) na (e) hawatakuwa na uwezo wa kupiga kura.

(4) Mamlaka na majukumu ya Tume ya Mishahara na Malipo yatakuwa—

a) kuweka viwango vya mishahara na marupurupu ya maafisa wote wa Serikali, na kukagua mishahara na marupurupu hayo; na

b) kushauri serikali ya kitaifa na serikali za kaunti kuhusu mishahara na marupurupu ya maafisa wote wengine wa serikali.

(5) Katika kutekeleza majukumu yake, Tume hiyo itazingatia kanuni zifuatazo—

a) hitaji la kuhakikisha kuwa bili ya kijumla ya malipo kwa umma ni endelevu kifedha;

b) hitaji la kuhakikisha kwamba huduma za umma zina uwezo wa kuwavutia na kudumisha wahudumu walio na ujuzi unaohitajika ili kutekeleza majukumu yao;

c) hitaji la kutambua uzalishaji na utendakazi; na

d) uwazi na usawa.



SIO YA KUUZWA

**231.**

*Benki Kuu ya Kenya.*

(1) Benki Kuu ya Kenya imebuniwa.

(2) Benki Kuu ya Kenya itakuwa na jukumu la kutengeneza sera ya kifedha, kukuza udhabiti wa bei,kutoa sarafu na kutekeleza majukumu mengine kama yalivyotolewa na Sheria ya Bunge.

(3) Benki Kuu ya Kenya haitakuwa chini ya uelekezi au udhibiti wa mtu au shirika lolote katika utekelezaji wa mamlaka yake na majukumu yake.

(4) Noti na sarafu zinazotolewa na Benki Kuu ya Kenya zinaweza kuwa na picha zinazoashiria Kenya au jambo lolote kuhusu Kenya, lakini hazitakuwa na picha ya mtu yeyote.

(5) Sheria ya Bunge itatoa mwongozo kuhusu watakaojumuishwa katika huduma, mamlaka, majukumu na utendakazi wa Benki Kuu ya Kenya.



SIO YA KUUZWA

# SURA YA KUMI NA TATU — HUDUMA KWA UMMA

**Sehemu ya 1—Maadili na Kanuni za Huduma kwa Umma**

**232.**

*Maadili na kanuni za huduma za umma.*

(1) Maadili na kanuni za huduma kwa umma zinajumuisha—

a) viwango vya juu vya maadili ya kitaaluma;

b) matumizi ya rasilimali kwa njia bora, ya kiuchumi na yenye ufanisi;

c) utoaji huduma kwa njia inayokabiliana na hitaji, kwa haraka, kwa njia yenye ufanisi na usiokuwa na mapendeleo;

d) kushirikishwa kwa wananchi katika mchakato wa kutengeneza sera;

e) uwajibikaji katika hatua za kiutawala;

f) uwazi na utoaji wa maelezo yaliyo sahihi na kwa wakati ufaao kwa umma;

g) kwa kuzingatia aya za (h) na (i), ushindani wenye usawa na ustahiki kuwa misingi ya kuteuliwa na kupandishwa cheo;

h) uwakilishi wa jamii tofauti za Kenya; na

i. (i) kutoa nafasi za kutosha na zenye usawa katika kuteua, kutoa mafunzo na kupandishwa vyeo katika ngazi zote za huduma kwa umma, kwa––

ii. wanaume na wanawake;

iii. watu wa jamii zote; na

iv. watu wenye ulemavu.

(2) Maadili na kanuni za huduma za umma zinatumika kwa huduma za umma katika—



SIO YA KUUZWA

a) vitengo vyote vya Serikali katika viwango vyote viwili vya serikali; na

b) mashirika yote ya Serikali.

(3) Bunge litatunga sheria ili kuwezesha utekelezaji wa Kifungu hiki kikamilifu.

**Sehemu ya 2 —Tume ya Huduma za Umma**

**233.**

*Tume ya Huduma za Umma;*

(1) Tume ya Huduma za Bunge Imebuniwa.

(2) Tume ya Huduma za Umma inajumuisha mwenyekiti, naibu mwenyekiti na wanachama wengine saba walioteuliwa na Rais na kuidhinishwa na Bunge la Kitaifa.

(3) Kwa kuzingatia ibara ya (4), mtu hastahiki kuteuliwa kama mwanachama wa Tume hiyo ikiwa mtu huyo––

a) ndani ya miaka mitano iliyopita, amehudumu au kugombea uchaguzi kama—

i. mbunge katika Bunge la Kitaifa au mwakilishi wadi katika bunge la kaunti; au

ii. mwanachama katika idara ya uongozi wa chama cha kisiasa; au

b) anahudumu katika ofisi yoyote ya Serikali;

c) anagombea, au kwa wakati wowote mwingine amewahi kugombea kuwa mwanachama katika Bunge la Kitaifa au katika bunge la kaunti; au

d) anahudumu, au kwa wakati wowote mwingine, amewahi kuhudumu katika shirika la kisiasa linalofadhili au kuunga mkono mgombeaji wa uanachama katika Bunge la Kitaifa au bunge la kaunti.



SIO YA KUUZWA

(4) Ibara ya (3) (c) na (d) hazitatumika iwapo uchaguzi mkuu umefanywa mara mbili tangu mtu huyo alipogombea kiti au alipohudumu ofisini.

(5) Kutakuwepo na katibu wa Tume hiyo.

(6) Katibu––

a) ndiye mtendaji mkuu katika Tume; na

b) atateuliwa na Tume kwa muhula wa miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena mara moja tu.

**234.**

*Mamlaka na Kazi ya Tume ya Huduma kwa Umma.*

(1) Majukumu na mamlaka ya Tume ni kama yalivyoelezwa katika Kifungu hiki.

(2) Tume—

a) kwa kuzingatia Katiba hii na sheria––

i. itabuni na kuondoa nafasi za kuhudumu katika huduma za umma; na

ii. itateua watu watakaohudumu katika ofisi hizo, na itathibitisha uteuzi;

b) itadumisha nidhamu na kuwaondoa kazini watu wanaohudumu katika ofisi hizo au walioteuliwa ili kuhudumu kwa muda mfupi;

c) itakuza maadili na kanuni zilizotajwa katika Vifungu vya 10 na 232 kote katika utoaji wa huduma za umma;

d) itachunguza, kufuatilia, na kutathmini mipangilio, usimamizi na mienendo ya wafanyakazi walio katika huduma za umma;

e) itahakikisha huduma za umma ni zenye ufanisi na bora;

f) itakuza uwezo wa wafanyakazi katika huduma za umma;

g) itachunguza na kutoa mapendekezo kwa serikali ya kitaifa kuhusu hali za utendakazi, kanuni



SIO YA KUUZWA

za maadili na ustahiki wa maafisa walio katika huduma za umma;

h) itatathmini na kuripoti kwa Rais na Bunge kuhusu kiwango ambacho maadili na kanuni zilizotajwa katika Vifungu vya 10 na 232 zinazingatiwa katika huduma za umma;

i) itasikiza na kuamua maombi kuhusu masuala yanayohusiana na huduma za umma katika serikali za kaunti;

j) itatekeleza majukumu na mamlaka mengine yoyote kama yatakavyotolewa na sheria ya kitaifa.

(3) Ibara za (1) na (2) hazitatumika katika ofisi zozote kati ya zifuatazo, zilizo katika huduma za umma––

a) ofisi za Serikali;

b) ofisi ya kamishna mkuu, balozi au mwakilishi yeyote wa kidiplomasia katika Jamhuri;

c) ofisi au wadhifa ulio chini ya––

i. Tume ya Huduma za Bunge;

ii. Tume ya Huduma za Mahakama;

iii. Tume ya Huduma kwa Walimu;

iv. Tume ya Huduma za Kitaifa za Polisi; au (b) ofisi inayohudumia serikali ya kaunti, isipokuwa ilivyobainiwa katika ibara ya (2) (i).

(4) Tume haitamteua mtu chini ya ibara ya (2) ili kuhudumu au kutoa huduma kwa muda mfupi katika ofisi yoyote iliyo kati ya wafanyakazi wa kibinafsi wa Rais au Rais mstaafu, isipokuwa kwa idhini ya Rais au Rais mstaafu huyo.

(5) Kupitia kwa njia ya maandishi, Tume inaweza, kwa masharti au bila ya masharti, kukabidhi majukumu

na mamlaka yake yoyote chini ya Kifungu hiki kwa mwanachama au wanachama wake, au kwa afisa yeyote, shirika au mamlaka katika huduma za umma.

**235.**

*Uajiri wa wafanyakazi katika serikali za kaunti.*

(1) Kwa kuzingatia taratibu sawa na kanuni zilizoidhinishwa na Sheria ya Bunge, serikali ya kaunti ina wajibu wa––

a) kubuni na kufutilia mbali nafasi za huduma katika huduma zake za umma;

b) kuteua watu ili kuhudumu au ili watoe huduma kwa muda mfupi katika ofisi hizo na kuidhinisha uteuzi; na

c) kudumisha nidhamu pamoja na kuwaondoa watu wanaohudumu katika ofisi hizo au wanaotoa huduma kwa muda mfupi.

(2) Ibara ya (1) haitatumika kwa ofisi au wadhifa wowote ulio chini ya Tume ya Huduma kwa Walimu.

*Ulinzi wa maafisa wa umma.*

**236.** Afisa wa umma—

a) hataonewa au kubaguliwa kwa kutekeleza majukumu ya kiofisi kulingana na Katiba hii au sheria nyingine yoyote; au

b) hatafutwa kazi, kuondolewa ofisini au kushushwa cheo au kuchukuliwa hatua za kinidhamu bila mchakato uliopo wa kisheria kufuatwa.

### Sehemu ya 3—Tume ya Huduma kwa Walimu

**237.**

*Tume ya Huduma kwa Walimu.*

(1) Tume ya Huduma kwa Walimu limebuniwa.

(2) Majukumu ya Tume hiyo ni—

a) kuwasajili walimu waliopata mafunzo;

b) kuajiri walimu waliosajiliwa;



SIO YA KUUZWA

c) kuwatuma walimu walioajiriwa na Tume hiyo ili wahudumu katika shule au taasisi yoyote ya umma;

d) kuwapandisha vyeo na kuwahamisha walimu;

e) kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya walimu; na

f) kuwafuta kazi walimu.

(3) Tume hiyo––

a) itakagua viwango vya elimu na mafunzo ya watu wanaojiunga na huduma ya ualimu;

b) itakagua hitaji la walimu na idadi ya walimu waliopo; na

c) itashauri serikali ya kitaifa kuhusu masuala yanayohusiana na taaluma ya ualimu.

# SURA YA KUMI NA NNE — USALAMA WA KITAIFA

**Sehemu ya 1—Vitengo vya Usalama wa Kitaifa**

**238.**

*Kanuni za usalama wa kitaifa.*

(1) Usalama wa kitaifa ni ulinzi kutokana na vitisho vya ndani na vya nje kwa mipaka ya Kenya na uhuru wa Kenya, watu wake, haki zao, uhuru, mali, amani, uthabiti na maendeleo, na maslahi mengine ya kitaifa.

(2) Usalama wa kitaifa wa Kenya utakuzwa na kuhakikishiwa kulingana na kanuni zifuatazo––

a) usalama wa kitaifa uko chini ya mamlaka ya Katiba hii na Bunge;

b) usalama wa kitaifa utatekelezwa kulingana na sheria, na kwa heshima kuu ya utawala wa sheria, demokrasia, haki za binadamu na uhuru wa kimsingi;

c) katika kutekeleza majukumu na mamlaka yao, vitengo vya usalama wa kitaifa vitaheshimu tamaduni tofauti za jamii zilizo nchini Kenya; na

d) uajiri katika vitengo vya usalama vya kitaifa utaonyesha utofauti wa wananchi wa Kenya katika viwango sawa.

**239.**

*Taasisi za usalama wa kitaifa.*

(1) Vitengo vya usalama wa kitaifa ni—

a) Vikosi vya Ulinzi wa Kenya;

b) Huduma za Upelelezi za Kitaifa; na

c) Huduma za Polisi za Kitaifa.

(2) Lengo la kimsingi la vitengo vya usalama wa kitaifa na mfumo wa usalama ni kukuza na kutoa hakikisho kuhusu usalama wa kitaifa kulingana na kanuni zilizotajwa katika Kifungu cha 238 (2).



SIO YA KUUZWA

(3) Katika kutekeleza majukumu na mamlaka yao, vitengo vya usalama wa kitaifa na kila mwanachama wa vitengo hivyo vya usalama wa kitaifa—

a) hatahudumu kwa njia inayopendelea;

b) hataendeleza maslahi au malengo ya chama chochote cha kisiasa; au

c) kuhujumu maslahi ya kisiasa au malengo ya kisiasa ambayo ni halali chini ya Katiba hii.

(4) Hakuna mtu atakayebuni kikosi cha kijeshi au kikosi chenye hadhi ya kijeshi au shirika linalodai kuendeleza na kutoa hakikisho kuhusu usalama wa kitaifa isipokuwa inavyoruhusiwa na Katiba hii au Sheria ya Bunge.

(5) Vitengo vya usalama wa kitaifa vitakuwa chini ya mamlaka ya kiraia.

(6) Bunge litatunga sheria itakayotoa mwongozo kuhusu majukumu, utaratibu na usimamizi wa vitengo vya usalama wa kitaifa.

**240.**

*Kuundwa kwa Baraza la Usalama wa Kitaifa.*

(1) Baraza la Usalama wa Kitaifa limebuniwa.

(2) Baraza hilo linajumuisha—

a) Rais;

b) Naibu wa Rais;

c) Waziri anayewajibika kuhusu ulinzi;

d) Waziri anayewajibika kuhusu masuala ya kigeni;

e) Waziri anayewajibika kuhusu usalama wa ndani;

f) Mwanasheria Mkuu;

g) Mkuu wa Vikosi vya Ulinzi wa Kenya;

h) Mkurugenzi Mkuu wa Huduma za Upelelezi za Kitaifa; na

i) Inspekta-Jenerali wa Huduma za Polisi za Kitaifa.



SIO YA KUUZWA

(3) Baraza hilo litakuwa na mamlaka ya kusimamia vitengo vya usalama wa kitaifa na kutekeleza majukumu mengine yoyote yatakayotolewa na sheria ya kitaifa.

(4) Rais ataongoza mikutano ya Baraza.

(5) Baraza litateua katibu wake.

(6) Baraza hilo—

a) litaunganisha sera za humu nchini, za kigeni na za kijeshi zinazohusiana na usalama wa kitaifa ili kuviwezesha vitengo vya usalama wa kitaifa kushirikiana na kufanya kazi kikamilifu; na

b) litatathmini na kukadiria malengo, kujitolea katika utendakazi, na hatari kwa Jamhuri kwa kuzingatia uwezo halisi na uwezo unaokuzwa, wa usalama wa kitaifa.

(7) Baraza hilo litatoa ripoti kwa Bunge kila mwaka kuhusu hali ya usalama nchini Kenya.

(8) Kwa idhini ya Bunge, Baraza linaweza—

a) kuvipeleka vikosi vya kitaifa nje ya Kenya kwa madhumuni ya—

i. kutoa msaada wa kudumisha amani katika eneo hili au kimataifa; au

ii. shughuli zingine za kutoa msaada; na

b) kuidhinisha kuletwa kwa vikosi vya kigeni nchini Kenya.

**Sehemu ya 2—Vikosi vya Ulinzi wa Kenya**

**241.**

*Kuundwa kwa Vikosi vya Ulinzi na Baraza la Ulinzi.*

(1) Vikosi vya Ulinzi wa Kenya vimebuniwa.

(2) Vikosi hivyo vya Ulinzi vinajumuisha—

a) Jeshi la Kenya la Nchi Kavu;

b) Jeshi la Kenya la Anga; na



SIO YA KUUZWA

c) Jeshi la Kenya la Wanamaji.

(3) Vikosi vya Ulinzi—

a) vina jukumu la ulinzi wa uhuru na mamlaka ya mipaka ya Jamhuri;

b) vitasaidia na kushirikiana na mashirika mengine katika hali za dharura au majanga, na kutoa ripoti kwa Bunge la Kitaifa wakati wowote yanapotekeleza shughuli kama hizo; na

c) vinaweza kupelekwa ili kurejesha amani katika sehemu yoyote nchini Kenya inayokumbwa na machafuko, lakini tu kwa idhini ya Bunge la Kitaifa.

(4) Uongozi katika Vikosi vya Ulinzi utaonyesha utofauti wa kimaeneo na kijamii wa watu wa Kenya.

(5) Baraza la Ulinzi limebuniwa.

(6) Baraza litajumuisha—

a) Waziri anayewajibika kuhusu ulinzi, ambaye ndiye mwenyekiti;

b) Mkuu wa Vikosi vya Ulinzi vya Kenya;

c) makamanda watatu wa vikosi vya ulinzi; na

d) Katibu Mkuu katika wizara inayowajibika kuhusu ulinzi.

(7) Baraza––

a) linawajibika katika sera ya kijumla, udhibiti na usimamizi wa Vikosi vya Ulinzi vya Kenya; na

b) hutekeleza majukumu mengine yoyote yaliyotolewa kwa mujibu wa sheria ya kitaifa.



SIO YA KUUZWA

**Sehemu ya 3—Huduma ya Upelelezi ya Kitaifa**

**242.**

*Kubuniwa kwa Huduma ya Upelelezi ya Kitaifa.*

(1) Huduma ya Upelelezi ya Kitaifa imebuniwa.

(2) Huduma ya Upelelezi ya Kitaifa––

a) Inawajibika katika upelelezi wa kiusalama na wa kuzuia tishio lolote kwa usalama ili kuboresha usalama wa kitaifa kulingana na Katiba hii; na

b) hutekeleza majukumu mengine yoyote yaliyotolewa kwa mujibu wa sheria ya kitaifa.

**Sehemu ya 4—Huduma za Polisi za Kitaifa**

**243.**

*Uongozi wa Huduma ya Polisi ya Kitaifa.*

(1) Huduma za Polisi za Kitaifa imebuniwa.

(2) Huduma za Polisi za Kitaifa zinajumuisha—

a) Huduma za Polisi wa Kenya; na

b) Huduma za Polisi wa Utawala.

(3) Huduma za Polisi za Kitaifa ni huduma za kitaifa ambazo zitatekelezwa kote nchini Kenya.

(4) Bunge litatunga sheria ili kuwezesha utekelezaji wa Kifungu hiki kikamilifu.

**244.**

*Malengo na kazi ya Huduma ya Polisi ya Kitaifa.*

(1) Huduma za Polisi za Kitaifa—

a) zitajitahidi kufikia viwango vya juu zaidi vya utaalamu na nidhamu miongoni mwa wanachama wa huduma hizo;

b) zitazuia ufisadi, na kukuza na kutekeleza uwazi na uwajibikaji;

c) zitazingatia viwango vya kikatiba vya haki za binadamu na uhuru wa kimsingi;

d) zitawapa wafanyakazi wake mafunzo kwa viwango vya juu zaidi iwezekanavyo katika ustadi na uadilifu na kuheshimu haki za binadamu, uhuru wa kimsingi na hadhi ya binadamu; na



SIO YA KUUZWA

e) zitajenga na kukuza mahusiano na jamii.

**245.**

*Uongozi wa Huduma ya Polisi ya Kitaifa.*

(1) Ofisi ya Inspekta-Jenerali wa Huduma za Polisi za Kitaifa imebuniwa.

(2) Inspekta-Jenerali––

a) anateuliwa na Rais kwa idhini ya Bunge; na

b) atatekeleza uongozi huru katika Huduma za Polisi za Kitaifa na kutekeleza majukumu mengine yoyote yatakayotolewa kwa mujibu wa sheria ya kitaifa.

(3) Huduma za Polisi nchini Kenya na Huduma za Polisi wa Utawala, zitaongozwa na Naibu Inspekta-Jenerali atakayeteuliwa na Rais kulingana na mapendekezo ya Tume ya Huduma za Polisi za Kitaifa.

(4) Waziri anayehusikana na huduma za polisi anaweza kutoa agizo kisheria kwa Inspekta-Jenerali kuhusu suala lolote la sera ya Huduma za Polisi za Kitaifa; lakini hakuna mtu yeyote atakayetoa maelekezo kwa Inspekta-Jenerali kuhusiana na—

a) uchunguzi wa hatia fulani;

b) utekelezaji wa sheria dhidi ya mtu au watu fulani; au

c) kuajiriwa, kutoa majukumu, kupandishwa cheo, kusimamishwa au kufutwa kazi kwa mwana-chama yeyote wa Huduma za Polisi za Kitaifa.

(5) Maelekezo yoyote yatakayotolewa na Waziri anayehusikana na huduma za polisi kwa Inspekta-Jenerali chini ya ibara ya (4), au Maelekezo yoyote yatakayotolewa na Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma kwa Inspekta-Jenerali chini ya Kifungu cha 157 (4), yatakuwa kwa njia ya maandishi.



SIO YA KUUZWA

(6) Inspekta-Jenerali atateuliwa ili kuhudumu kwa muhula mmoja wa miaka minne, na hatastahiki kuteuliwa tena.

(7) Inspekta-Jenerali anaweza kuondolewa ofisini na Rais kwenye misingi tu ya—

a) ukiukaji mkubwa wa Katiba hii au sheria nyingine yoyote, ikijumuisha ukiukaji wa Sura ya Sita;

b) mwenendo mbaya zaidi katika utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo au vinginevyo;

c) kutokuwa na uwezo wa kimwili au kiakili wa kutekeleza majukumu ya ofisi hiyo;

d) kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo;

e) kufilisika; au

f) sababu yoyote nyingine yenye haki.

(8) Bunge litatunga sheria ili kuwezesha utekelezaji wa Kifungu hiki kikamilifu.

**246.**

*Tume ya Huduma za Polisi za Kitaifa.*

(1) Tume ya Huduma za Polisi za Kitaifa imebuniwa.

(2) Tume hiyo inajumuisha—

a) watu wafuatao, kila mmoja wao akiwa ameteuliwa na Rais—

i. mtu anayestahiki kuteuliwa kama Jaji wa Mahakama Kuu;

ii. maafisa wawili wa polisi wa ngazi ya juu waliostaafu; na

iii. watu watatu waadilifu ambao wamewahi kuhudumia umma kwa umahiri mkubwa;

b) Inspekta-Jenerali wa Huduma za Polisi za Kitaifa; na

c) Manaibu wote wawili wa Inspekta-Jenerali wa Huduma za Polisi za Kitaifa.



SIO YA KUUZWA

(3) Tume—

a) itaajiri na kuteua watu ili kuhudumu au kutoa huduma kwa muda mfupi katika ofisi zilizo kwenye huduma hizo, itaidhinisha uteuzi na kuamua watakaopandishwa vyeo na kuhamishwa katika Huduma za Polisi za Kitaifa;

b) itazingatia mchakato uliowekwa, itachukua hatua za kinidhamu na kuwaondoa watu wanaohudumu katika ofisi za Huduma hizo; na

c) itatekeleza majukumu mengine yoyote yatakayotolewa kwa mujibu wa sheria ya kitaifa.

(4) Uajiri na uanachama katika Huduma za Polisi za Kitaifa utaonyesha utofauti wa kimaeneo na kikabila wa wananchi wa Kenya.

*Huduma zingine za polisi.*

**247.** Bunge linaweza kutunga sheria zitakazobuni huduma zingine za polisi chini ya usimamizi wa Huduma za Polisi za Kitaifa na uongozi wa Inspekta-Jenerali wa Huduma hizi.



SIO YA KUUZWA

# SURA YA KUMI NA TANO — TUME NA OFISI HURU

**248.**

*Kutumika kwa Sura.*

(1) Sura hii inatumika kwa tume zilizotajwa katika ibara ya (2) na ofisi huru zilizotajwa katika ibara ya (3), isipokuwa kwa kiwango ambacho Katiba hii inatoa mwongozo vinginevyo.

(2) Tume hizo ni—

a) Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu na Usawa;

b) Tume ya Kitaifa ya Ardhi;

c) Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka;

d) Tume ya Huduma za Bunge;

e) Tume ya Huduma za Mahakama;

f) Tume ya Ugavi wa Mapato;

g) Tume ya Huduma za Umma;

h) Tume ya Mishahara na Malipo;

i) Tume ya Huduma kwa Walimu; na

j) Tume ya Huduma za Polisi za Kitaifa.

(3) Ofisi huru ni—

a) Mkaguzi Mkuu; na

b) Msimamizi wa Bajeti.

**249.**

*Malengo, mamlaka na ufadhili wa tume na ofisi huru.*

(1) Malengo ya tume hizo na ofisi huru ni—

a) kulinda mamlaka makuu ya wananchi;

b) kuhakikisha kwamba vitengo vyote vya serikali vinazingatia kanuni na maadili ya kidemokrasia; na

c) kukuza mfumo wa kikatiba.

(2) Tume hizo na wanaohudumu katika ofisi hizo huru—

a) wako chini ya Katiba hii na sheria tu; na

b) wako huru na hawako chini ya maelekezo au udhibiti wa mtu au mamlaka yoyote.

(3) Bunge litatenga fedha za kutosha ili kuwezesha kila tume na ofisi huru kutekeleza majukumu yake na bajeti ya kila tume na ofisi huru itakuwa kando.

**250.**

*Muundo, uteuzi na muda wa kuwa ofisini.*

(1) Kila tume itakuwa na angalau wanachama watatu, lakini wasiozidi tisa.

(2) Mwenyekiti na kila mwanachama wa tume, pamoja na anayehudumu katika ofisi huru—

a) watatambuliwa na kupendekezwa ili wateuliwe kwa namna iliyoagizwa na sheria ya kitaifa;

b) wataidhinishwa na Bunge la Kitaifa; na

c) watateuliwa na Rais.

(3) Ili kuteuliwa, mtu atapaswa kuwa na ustahiki maalum unaohitajika na Katiba hii au sheria ya kitaifa.

(4) Uteuzi wa wanachama wa tume na wa maafisa wa ofisi huru utazingatia maadili ya kitaifa yanayorejelewa katika Kifungu cha 10, na kanuni kwamba uanachama wa tume na wanaohudumu katika ofisi huru, kijumla, utaonyesha utofauti wa kimaeneo na kikabila wa wananchi wa Kenya.

(5) Mwanachama wa tume anaweza kuhudumu kwa muda.

(6) Mwanachama wa tume au anayehudumu katika ofisi huru—

a) isipokuwa awe na uanachama usio rasmi, atateuliwa kwa muhula mmoja wa miaka sita, na hastahiki kuteuliwa tena; na

b) isipokuwa awe na uanachama usio rasmi au awe anahudumu kwa muda, mtu huyo hatahudumu katika ofisi nyingine au kuajiriwa ili kupokea



SIO YA KUUZWA

mapato, katika ofisi ya umma au ya kibinafsi.

(7) Malipo na marupurupu atakayopata kamishna au anayehudumu katika ofisi huru, yatalipwa kutoka kwenye Hazina Jumuishi.

(8) Malipo na marupurupu atakayopata kamishna au anayehudumu katika ofisi huru hayatabadilishwa na kupelekea hasara kwa mtu huyo.

(9) Mwanachama wa tume au anayehudumu katika ofisi huru hatawajibika kisheria kwa jambo lolote lililofanywa kwa nia njema katika utekelezaji wa jukumu la ofisi hiyo.

(10) Wanachama wa tume watamchagua naibu mwenyekiti kutoka miongoni mwao—

a) katika kikao cha kwanza cha tume; na

b) kila inapohitajika kujaza nafasi katika ofisi ya naibu mwenyekiti.

(11) Mwenyekiti na naibu mwenyekiti wa tume hawatakuwa wa jinsia moja.

(12) Kutakuwa na Katibu wa kila tume, ambaye—

a) atateuliwa na tume; na

b) afisa mkuu mtendaji wa tume hiyo.

**251.**

*Kuondolewa ofisini.*

(1) Mwanachama wa tume (isipokuwa mwanachama asiye rasmi), au anayehudumu katika ofisi huru anaweza kuondolewa ofisini kwa sababu tu ya—

a) ukiukaji mkubwa wa Katiba hii au sheria nyingine yoyote, ikijumuisha ukiukaji wa Sura ya Sita;

b) mwenendo mbaya zaidi, iwe katika utekelezaji wa majukumu ya mwanachama huyo au anayehudumu katika ofisi hiyo au vinginevyo;

c) kutokuwa na uwezo wa kimwili au kiakili wa kutekeleza majukumu ya ofisi hiyo;

d) kutokuwa na uzoefu unaohitajika; au

e) kufilisika.

(2) Mtu anayetaka kuondolewa kwa mwanachama wa tume au anayehudumu katika ofisi huru kwenye msingi wowote uliotajwa katika ibara ya (1) anaweza kuwasilisha maombi au malalamishi yanayoelezea madai yanayohusiana na msingi huo kwa Bunge la Kitaifa.

(3) Bunge la Kitaifa litatathmini maombi au malalamishi hayo na, ikiwa litaridhika kwamba yanafichua msingi chini ya ibara ya (1), litatuma maombi au malalamishi hayo kwa Rais.

(4) Baada ya kupokea maombi au malalamishi chini ya ibara ya (3), Rais—

a) anaweza kumsimamisha kazi mwanachama wa tume au anayehudumu katika ofisi huru huku akisubiri matokeo ya uchunguzi wa malalamishi hayo; na

b) atateua taasisi iliyo na mamlaka ya mahakama kulingana na ibara ya (5).

(5) Taasisi hiyo itajumuisha—

a) mtu anayehudumu au ambaye amewahi kuhudumu kama jaji wa mahakama ya ngazi ya juu, ambaye atakuwa mwenyekiti;

b) watu wasiopungua wawili ambao wanastahiki kuteuliwa kama majaji wa Mahakama Kuu; na

c) mwanachama mwingine mmoja ambaye anastahiki kutathmini madai yanayohusiana na msingi wa kuondolewa.

(6) Taasisi hiyo itachunguza suala hilo kwa haraka, na kutoa ripoti kuhusu ukweli wa madai hayo, na kutoa mapendekezo atakayofuata Rais katika kuchukua hatua ndani ya siku thelathini.



SIO YA KUUZWA

(7) Mtu atakayesimamishwa kazi chini ya Kifungu hiki ana haki ya kupokea nusu ya mshahara na marupurupu ya ofisi aliyokuwa akihudumu.

**252.**

*Kazi na mamlaka ya kijumla.*

(1) Kila tume, na kila anayehudumu katika ofisi huru—

a) anaweza kufanya uchunguzi kwa kuchukua hatua hiyo kivyake au kwa malalamishi yaliyotolewa na mwananchi;

b) ana mamlaka yanayohitajika katika upatanishina mazungumzo kwa madhumuni ya kutatua mzozo;

c) atawaajiri wafanyakazi wake; na anaweza kutekeleza majukumu na mamlaka mengine yoyote yaliyotolewa kwa mujibu wa sheria, zaidi ya majukumu na mamlaka yaliyotolewa na Katiba hii.

(2) Malalamishi kwa tume au kwa anayehudumu katika ofisi huru yanaweza kuwasilishwa na mtu yeyote ambaye ana haki ya kuwasilisha kesi mahakamani chini ya Kifungu cha 22 (1) na (2).

(3) Tume na ofisi huru zifuatazo zina mamlaka ya kumwita shahidi ili kutoa usaidizi kwa madhumuni ya uchunguzi wa tume au ofisi hiyo—

a) Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu na Usawa;

b) Tume ya Huduma za Mahakama;

c) Tume ya Kitaifa ya Ardhi;

d) Mkaguzi Mkuu.

*Tume na ofisi huru kuwa kama kampuni au shirika.*

**253.** Kila tume na ofisi huru—

a) ni shirika lililosajiliwa, lenye urithi unaoendelea na lina muhuri wake; na

b) ina uwezo wa kushtaki na kushtakiwa kwa jina lake la shirika.



SIO YA KUUZWA

**254.**

*Kuripoti kwa tume na ofisi huru.*

(1) Mwishoni mwa kila mwaka wa kifedha, kila tume na kila anayehudumu katika ofisi huru, atawasilisha ripoti kwa Rais na kwa Bunge, haraka iwezekanavyo.

(2) Kwa wakati wowote, Rais, Bunge la Kitaifa au Seneti inaweza kuitaka tume au anayehudumu katika ofisi huru kuwasilisha ripoti kuhusu suala fulani.

(3) Kila ripoti itakayohitajika kutoka kwa tume au anayehudumu katika ofisi huru chini ya Kifungu hiki, itachapishwa na kutangazwa.

## SURA YA KUMI NA SITA — MAREKEBISHO YA KATIBA HII

**255.**

*Marekebisho ya Katiba Hii.*

(1) Pendekezo la marekebisho ya Katiba hii litatekelezwa kulingana na Kifungu cha 256 au 257, na kupitishwa kulingana na ibara ya (2) katika kura ya maamuzi, ikiwa marekebisho hayo yanahusu suala lolote kati ya masuala yafuatayo—

a) ukuu wa Katiba hii;

b) teritori ya Kenya;

c) mamlaka makuu ya wananchi;

d) maadili ya kitaifa, kanuni za kiutawala zilizotajwa katika Kifungu cha 10 (2) (a) hadi (d);

e) Sheria za Haki;

f) muhula wa kuhudumu katika ofisi ya Rais;

g) uhuru wa Kitengo cha Mahakama na tume na ofisi huru zinazorejelewa katika Sura ya Kumi na Tano;

h) majukumu ya Bunge;

i) malengo, kanuni na muundo wa serikali ya ugatuzi; au

j) vifungu katika Sura hii.

(2) Pendekezo la marekebisho litapitishwa kwa kura ya maamuzi chini ya ibara ya (1) ikiwa—

a) angalau asilimia ishirini ya wapiga kura waliosajiliwa katika angalau nusu ya idadi ya kaunti itapiga kura katika kura ya maamuzi; na

b) marekebisho hayo yanaungwa mkono na idadi kubwa ya wananchi wanaopiga kura katika kura ya maamuzi.

(3) Marekebisho katika Katiba hii ambayo hayahusiani na masuala yaliyofafanuliwa katika ibara ya (1) yatapitishwa—

a) na Bunge, kulingana na Kifungu cha 256; au

b) na wananchi pamoja na Bunge, kulingana na Kifungu cha 257.

**256.**

*Marekebisho kwa njia ya mapendekezo ya bunge.*

(1) Mswada wa kurekebisha Katiba hii—

a) unaweza kuwasilishwa katika Kitengo chochote cha Bunge;

b) haupaswi kuangazia suala lolote lingine isipokuwa yale yanayotokana na marekebisho ya sheria katika Mswada huo;

c) hautawasilishwa ili kusomwa kwa mara ya pili katika Kitengo chochote cha Bunge, katika muda wa siku tisini baada ya kusomwa kwa Mswada huo kwa mara ya kwanza katika Kitengo hicho cha Bunge; na

d) utakuwa umepitishwa na Bunge kila Kitengo cha Bunge kitakapopitisha Mswada huo katika usomaji wa Mswada huo kwa mara ya pili na tatu, kwa idadi isiyopungua thuluthi mbili ya wanachama wote katika Kitengo hicho.

(2) Bunge litatangaza kuhusu Mswada wowote wa kurekebisha Katiba hii, na kuwezesha mjadala wa umma kuhusiana na Mswada huo.

(3) Baada ya Bunge kupitisha Mswada wa kurekebisha Katiba hii, Maspika wa Vitengo vyote viwili vya Bunge watawasilishia Rais, kwa pamoja—

a) Mswada huo, ili kuidhinishwa na kuchapishwa; na

b) cheti kinachothibitisha kwamba Mswada huo umepitishwa na Bunge kulingana na Kifungu hiki.

(4) Kwa kuzingatia ibara ya (5), Rais ataidhinisha Mswada huo na kuufanya uchapishwe katika muda wa siku thelathini baada ya Mswada huo kupitishwa na Bunge.

(5) Ikiwa Mswada wa kurekebisha Katiba hii unapendekeza marekebisho yanayohusiana na suala lililotajwa katika Kifungu cha 255 (1)—

a) kabla ya kuuidhinisha Mswada huo, Rais ataiomba Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka kuandaa kura ya maamuzi ya kitaifa katika muda wa siku tisini ili Mswada huo uidhinishwe; na

b) katika muda wa siku thelathini baada ya mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi na Mipaka kumthibitishia Rais kwamba Mswada huo umepitishwa kulingana na Kifungu cha 255 (2), Rais ataidhinisha Mswada huo na kuufanya uchapishwe.

**257.**

*Marekebisho yanayoanzishwa na idadi kubwa ya wananchi.*

(1) Marekebisho ya Katiba hii yanaweza kupendekezwa kupitia kwa juhudi za wengi ikiwa angalau wapiga kura milioni moja waliosajiliwa watatia saini kwenye pendekezo hilo.

(2) Marekebisho ya Katiba hii yanayoanzishwa kupitia juhudi za wananchi wengi yanaweza kuchukua muundo wa pendekezo la kijumla au Mswada ulioandaliwa.

(3) Ikiwa pendekezo la wananchi wengi litachukua muundo wa pendekezo la kijumla, wanaoongoza pendekezo hilo wataliandaa liwe Mswada rasimu.



SIO YA KUUZWA

(4) Wanaoongoza pendekezo hilo la wananchi wengi watawasilisha rasimu ya Mswada pamoja na saini zinazounga mkono rasimu hiyo kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ambayo itathibitisha kwamba pendekezo hilo linaungwa mkono na angalau wapiga kura milioni moja waliosajiliwa.

(5) Ikiwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka itaridhika kwamba pendekezo hilo limetimiza mahitaji ya Kifungu hiki, Tume itawasilisha pendekezo hilo kwa kila bunge la kaunti ili kujadiliwa katika muda wa miezi mitatu baada ya tarehe ya kuwasilishwa na Tume hiyo.

(6) Ikiwa bunge la kaunti litaidhinisha rasimu ya Mswada huo katika kipindi cha miezi mitatu baada ya tarehe ya kuwasilishwa na Tume, spika wa bunge la kaunti atawasilisha nakala ya rasimu ya Mswada kwa Maspika wa Vitengo vyote viwili vya Bunge, pamoja na cheti kinachothibitisha kwamba bunge la kaunti limeidhinisha rasimu ya Mswada huo.

(7) Ikiwa rasimu ya Mswada imeidhinishwa na idadi kubwa ya mabunge ya kaunti, rasimu hiyo itawasilishwa Bungeni bila kuchelewa.

(8) Mswada chini ya Kifungu hiki umepitishwa na Bunge ikiwa umeungwa mkono na idadi kubwa ya wanachama wa kila Kitengo cha Bunge.

(9) Ikiwa Bunge litapitisha Mswada huo, utawasilishwa kwa Rais ili kuidhinishwa kulingana na Vifungu vya 256 (4) na (5).

(10) Ikiwa mojawapo ya Vitengo vya Bunge kitakosa kupitisha Mswada huo, au Mswada huo unahusu suala lililotajwa katika kifungu cha 255 (1), marekebisho yaliyopendekezwa yatawasilishwa kwa wananchi katika kura ya maamuzi.



SIO YA KUUZWA

(11) Kifungu cha 255 (2) kitatumika, kwa kuzingatia mabadiliko yoyote yatakayohitajika, katika kura ya maamuzi chini ya ibara ya (10).

## SURA YA KUMI NA SABA — VIFUNGU VYA KIJUMLA

**258.**

*Utekelezaji wa Katiba Hii.*

(1) Kila mtu ana haki ya kuwasilisha kesi mahakamani, akidai kuwa Katiba hii imekiukwa, au kuna tishio la kuikiuka.

(2) Zaidi ya mtu anayewasilisha kesi kwa maslahi yake mwenyewe, kesi mahakamani chini ya ibara ya (1) inaweza kuwasilishwa na—

a) mtu anayewasilisha kesi kwa niaba ya mtu mwingine ambaye hawezi kuwasilisha kesi kwa jina lake mwenyewe;

b) mtu anayewasilisha kesi kwa niaba ya, au kama mwanachama wa kikundi au tabaka la watu;

c) mtu anayewasilisha kesi kwa manufaa ya umma; au

d) shirika linalowasilisha kesi kwa manufaa ya mwanachama mmoja au zaidi.

**259.**

*Kufasiri Katiba Hii.*

(1) Katiba hii itafasiriwa kwa namna ambayo—

a) inakuza malengo, maadili na kanuni zake;

b) inaendeleza utawala wa sheria, haki za binadamu na uhuru wa kimsingi katika Sheria za Haki;

c) inaruhusu kuendelea kwa sheria; na

d) inachangia katika utawala bora.

(2) Ikiwa kuna mgongano kati ya matoleo ya Katiba hii katika lugha tofauti, toleo la lugha ya Kiingereza ndilo litakalotawala.

(3) Kila kifungu katika Katiba hii litafasiriwa kulingana na kanuni ya ufasiri kwamba sheria inazungumza kila mara, na kwa hivyo, kati ya masuala mengine—

a) jukumu au mamlaka yaliyotolewa na Katiba hii kwa ofisi yanaweza kutekelezwa na mtu anayehudumu katika ofisi hiyo kulingana na hitaji;

b) rejeleo lolote katika Katiba hii kwa Serikali au ofisi nyingine ya umma au afisa, au mtu anayehudumu katika ofisi hiyo ni rejeleo kwa mtu anayehudumu katika ofisi hiyo kwa muda au anayetekeleza majukumu ya ofisi hiyo kwa wakati wowote ule;

c) rejeleo katika Katiba hii kwa ofisi, kitengo cha Serikali au eneo lililotajwa katika Katiba hii litasomwa kwa kuzingatia badiliko lolote rasmi linalohitajika ili liweze kutumika katika hali hizo; na

d) rejeleo katika Katiba hii kwa ofisi au shirika, ikiwa ofisi au shirika hilo halipo tena, ni rejeleo kwa ofisi au shirika lililorithi, au ofisi au shirika sawa na lile ambalo halipo tena.

(4) Katika Katiba hii, isipokuwa pale ambapo muktadha unahitaji vinginevyo—

a) iwapo neno au maelezo yamefafanuliwa katika Katiba hii, tofauti zozote za kisarufi au za kimatumizi ya neno linalohusiana na jingine, soma ukizingatia mabadiliko yanayotokana na muktadha; na

b) neno "ikijumuisha" linamaanisha "ikijumuisha, lakini bila kudhibiti".

(5) Katika kuhesabu muda uliopita kati ya matukio mawili, kwa madhumuni yoyote chini ya Katiba hii, ikiwa muda huo umeelezwa—

a) kama siku, basi siku ambayo tukio la kwanza linatokea haitahesabiwa, na siku ambayo tukio



SIO YA KUUZWA

la mwisho linaweza kutokea itajumuishwa;

b) kama miezi, kipindi cha muda uliowekwa unaisha mwanzoni mwa siku katika mwezi husika—

   i. ambayo ina nambari sawa kama tarehe ambayo kipindi hicho kilianza, ikiwa mwezi huo una tarehe inayolingana; au

   ii. ndiyo siku ya mwisho ya mwezi huo, katika hali yoyote nyingine; au

c) kama miaka, kipindi cha muda huo kinamalizika mwanzoni mwa tarehe ya mwaka husika inayolingana na tarehe ambayo kipindi hicho kilianza.

(6) Ikiwa muda uliowekwa katika Katiba hii kwa madhumuni yoyote ni siku sita au chini yake, Jumapili na siku za mapumziko za kitaifa hazitahesabiwa muda huo unapohesabiwa.

(7) Ikiwa katika hali zozote maalum, kipindi cha muda kilichowekwa na Katiba hii kinakamilika siku ya Jumapili au siku ya mapumziko ya kitaifa, muda huo unaongezwa hadi siku inayofuata ambayo sio Jumapili au siku ya mapumziko ya kitaifa.

(8) Ikiwa muda fulani haujawekwa na Katiba hii katika utekelezaji wa kitendo fulani, kitendo hicho kitafanywa bila kuchelewa kusio na sababu za kuridhisha, na kulingana na itakavyohitajika mara kwa mara.

(9) Ikiwa mtu yeyote au kitengo cha Serikali kina mamlaka chini ya Katiba hii ya kuongeza kipindi cha muda uliowekwa na Katiba hii, mamlaka hayo yanaweza kutekelezwa kabla au baada ya mwisho wa kipindi hicho, isipokuwa pale ambapo nia tofauti imeelezewa wazi katika kifungu kinachotoa mamlaka hayo.

(10) Isipokuwa pale ambapo Katiba hii inaelezea vinginevyo, ikiwa mtu ameondoka katika ofisi

iliyobuniwa chini ya Katiba hii, ikiwa mtu huyo anastahiki, anaweza kuteuliwa tena, kuchaguliwa au vinginevyo kuteuliwa ili kuhudumu katika ofisi hiyo kulingana na Katiba hii.

(11) Ikiwa jukumu au mamlaka yaliyotolewa kwa mtu chini ya Katiba hii yanaweza kutekelezwa na mtu huyo tu kupitia kwa ushauri au pendekezo, kupitia kwa idhini ya mtu mwingine au mashauriano na mtu mwingine, jukumu hilo linaweza kufanywa au mamlaka hayo kutekelezwa kupitia tu kwa ushauri huo, pendekezo, idhini au baada ya mashauriano hayo, isipokuwa kwa kiwango ambacho Katiba hii inatoa mwongozo vinginevyo.

*Ufasiri.*

**260.** Katika Katiba hii, isipokuwa muktadha uhitaji vinginevyo—

"mtu mzima" inamaanisha mtu ambaye amefikisha umri wa miaka kumi na nane;

"hatua sawazishi" inajumuisha hatua yoyote inayolenga kuondoa hali isiyo na usawa au kunyimwa kwa haki au ukiukaji wa kimfumo wa haki na uhuru wa kimsingi; "mtoto" inamaanisha mtu ambaye hajatimiza umri wa miaka kumi na nane;

"kukiuka" inajumuisha kukosa kutimiza mahitaji yaliyowekwa;

"sheria ya kaunti" inamaanisha sheria iliyotungwa na serikali ya kaunti au chini ya mamlaka yaliyotolewa na Bunge la kaunti;

"ulemavu" inajumuisha ulemavu wowote wa kimwili, kihisia, kiakili, kisaikolojia au ulemavu wa aina nyingine, hali au ugonjwa ambao, au unaochukuliwa na sekta mahususi za kijamii kuwa na athari za muda mrefu kwa uwezo wa mtu wa kutekeleza majukumu yake ya kawaida ya kila siku; "hati" inajumuisha––

a) chapisho lolote au suala lolote lililoandikwa,



SIO YA KUUZWA

kuelezewa au kunakiliwa kwenye kitu chochote kwa kutumia herufi, michoro au alama au zaidi ya mojawapo ya njia hizo ambayo inakusudiwa kutumiwa au inaweza kutumiwa kwa madhumuni ya kurekodi suala hilo; na

b) faili za kielektroniki;

"tarehe ya kuanza kutumika" inamaanisha tarehe ambayo Katiba hii ilianza kutumika;

"kosa" inajumuisha kukataa;

"mwaka wa kifedha" inamaanisha kipindi cha miezi kumi na miwili kinachomalizika katika siku ya thelathini ya mwezi wa Juni au siku nyingine iliyotolewa na sheria ya kitaifa, lakini mwaka wa kwanza wa kifedha wa shirika lolote ni kipindi kinachoanza wakati wa kubuniwa kwa shirika hilo hadi siku ya thelathini ya Juni ifuatayo, au siku yoyote ile itakayotolewa na sheria ya kitaifa;

"Gazeti" inamaanisha Gazeti Rasmi la Serikali linalochapishwa kutokana na kibali cha serikali ya kitaifa, au gazeti lingine linalochapishwa pamoja na Gazeti Rasmi la Kenya;

"udhamini" inamaanisha ahadi kamili au ahadi yenye masharti au kujitolea kwa serikali ya kitaifa katika ulipaji kamili au kwa kiasi wa mkopo wowote wa serikali ya kaunti au wa mtu yeyote;

"afisa wa mahakama" inamaanisha msajili, naibu wa msajili, hakimu, Kadhi au afisa msimamizi wa mahakama iliyoundwa chini ya Kifungu cha 169 (1)(d); "ardhi" inajumuisha—

a) eneo la juu la dunia na miamba iliyo chini ya eneo hili;

b) eneo lolote la maji juu au chini ya eneo la juu la dunia;

c) maji ya bahari katika eneo la bahari lililo kwenye

mipaka ya nchi na eneo la bahari ambalo ni la kiuchumi;

d) mali-asili zilizopo ndani au chini ya eneo la juu la dunia; na

e) eneo la anga juu ya eneo la juu la dunia; "sheria" inajumuisha––

a) Sheria ya Bunge, au sheria iliyotungwa chini ya mamlaka yaliyotolewa na Sheria ya Bunge; au

b) sheria iliyotungwa na bunge la serikali ya kaunti, au chini ya mamlaka yaliyotolewa na sheria kama hiyo;

" mkopo" inajumuisha aina yoyote ya kukopa, kukopesha au malipo ya baadaye ambayo yanaweza kulipwa na fedha kutoka kwenye hazina ya umma, au ambayo yanahitajika kulipwa au kulipwa tena, kupitia fedha zilizo kwenye hazina ya umma;

"jamii iliyotengwa" inamaanisha—

a) jamii ambayo kutokana na idadi ndogo ya watu wake, au kwa sababu nyingineyo, imeshindwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijumla za maisha ya kijamii na kiuchumi ya Kenya;

b) jamii ya kitamaduni, ambayo kutokana na hitaji au tamanio la kuhifadhi utamaduni wake wa na kuzuia utambulisho wake kupotea, imebakia nje ya shughuli za kijumla za maisha ya kijamii na kiuchumi ya Kenya;

c) jamii ya kiasili ambayo imekuza na kudumisha maisha na mitindo ya kitamaduni inayojikita kwenye uchumi wa shughuli za usasi na ukusanyaji; au

d) wafugaji au jamii za wafugaji, iwe ni—

i. wa kuhamahama; au

ii. jamii zinazoishi mahala pamoja na ambazo,



SIO YA KUUZWA

kwa sababu ya kutengwa kijiografia, hazijashiriki kikamilifu katika shughuli za kijumla za maisha ya kijamii na kiuchumi ya Kenya;

"kikundi kilichotengwa" inamaanisha kikundi cha watu ambao, kutokana na sheria au hatua za kabla, wakati wa, au baada ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, walikuwa wamebaguliwa katika mojawapo au zaidi ya misingi inayotajwa katika Kifungu cha 27 (4);

"sheria ya kitaifa" inamaanisha Sheria ya Bunge, au sheria inayotungwa chini ya mamlaka yaliyotolewa na Sheria ya Bunge; "mali-asili" inamaanisha vitu au hali za kimaumbile zisizo za kibinadamu, ziwe zinaweza kutumiwa tena au la, ikijumuisha-—

a) mwanga wa jua;
b) maji kwenye ardhi na chini ya ardhi;
c) misitu, uanuwai wa kiasili na kinasaba; au
d) miamba, madini, malighafi ya mafuta na kwingine ambako kawi inapatikana;

"mzee katika jamii" inamaanisha mtu ambaye amefikisha umri wa miaka sitini;

"mtu" inajumuisha kampuni, shirika au kundi la watu, liwe limefanywa kuwa shirika au ambalo sio shirika; "chama cha kisiasa" inamaanisha muungano wa watu uliobainishwa katika Sehemu ya 3 ya Sura ya Saba;

"mali" inajumuisha haki kamili au iliyotolewa ya, au inayotokana na—

a) ardhi au vitu vya kudumu vilivyo kwenye ardhi, au kuboreshwa kwa ardhi;
b) bidhaa au mali ya kibinafsi;
c) uvumbuzi; au
d) Pesa au njia tofauti zinazotumika kama pesa; "afisa wa umma" inamaanisha—



SIO YA KUUZWA

e) afisa yeyote wa Serikali; au

f) mtu yeyote, mbali na afisa wa Serikali, anayehudumu katika ofisi ya umma;

g) "ofisi ya umma" inamaanisha ofisi katika serikali ya kitaifa, serikali ya kaunti au katika huduma za umma, ikiwa malipo na marupurupu ya ofisi hiyo yanalipwa moja kwa moja kutoka kwenye Hazina Jumuishi au moja kwa moja kutoka kwenye fedha zilizotengwa na Bunge.

"huduma za umma" inamaanisha jumla ya watu wote, mbali na maafisa wa Serikali, wanaotekeleza jukumu katika kitengo cha Serikali;

"Jamhuri" inamaanisha Jamhuri ya Kenya;

"Serikali" inapotumiwa kama nomino, inamaanisha mkusanyiko wa afisa, vitengo na asasi zingine zinazounda serikali ya Jamhuri chini ya Katiba hii;

"ofisi ya Serikali" inamaanisha yoyote kati ya ofisi zifuatazo–

a) Rais;

b) Naibu wa Rais;

c) Waziri;

d) Mbunge;

e) Majaji na Mahakimu;

f) mwanachama wa tume chini ya Sura ya Kumi na Tano;

g) anayehudumu katika ofisi huru chini ya Sura ya Kumi na Tano;

h) mwakilishi wadi katika bunge la kaunti, gavana au naibu wa gavana wa kaunti, au mwanachama yeyote katika kamati ya utendaji katika serikali ya kaunti;

i) Mwanasheria Mkuu;

j) Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma;

k) Katibu wa Baraza la Mawaziri;

l) Katibu Mkuu;

m) Mkuu wa Vikosi vya Ulinzi vya Kenya;



SIO YA KUUZWA

n) kamanda katika huduma ya Vikosi vya Ulinzi vya Kenya;

o) Mkurugenzi Mkuu wa Huduma ya Upelelezi ya Kitaifa;

p) Inspekta-Jenerali, na Manaibu wa Inspekta-Jenerali wa Huduma za Polisi za Kitaifa; au

q) ofisi ambayo imebuniwa na kupewa hadhi ya ofisi ya Serikali chini ya sheria ya kitaifa;

"afisa wa Serikali" inamaanisha mtu anayehudumu katika ofisi ya Serikali; "kitengo cha Serikali" inamaanisha tume, ofisi, shirika au asasi nyingine iliyobuniwa chini ya Katiba hii; "maandishi" inajumuisha upigaji chapa, upigaji picha, lithografia, upigaji taipu, breli na njia yoyote nyingine inayowakilisha au kutoa maneno kwa njia inayoonekana; na

"vijana" inamaanisha jumla ya watu wote katika Jamhuri ambao—

a) wamefikia umri wa miaka kumi na nane; lakini

b) hawajafikia umri wa miaka thelathini na mitano.



SIO YA KUUZWA

# SURA YA KUMI NA NANE — VIFUNGU VYA MPITO NA VITAKAVYOTUMIWA KATIBA HII INAPOANZA KUTEKELEZWA

*Sheria zitakazotungwa baada ya kuanza kutumika kwa Katiba hii.*

**261.**

(1) Bunge litatunga sheria yoyote inayohitajiwa na Katiba hii kutungwa ili kushughulikia jambo fulani katika muda ulioelezwa katika Ambatisho la Tano, kuanzia tarehe ya kutekelezwa kwa Katiba hii.

(2) Licha ya ibara ya (1), Bunge la Kitaifa, kupitia kwa uamuzi utakaoungwa mkono na idadi ya kura isiyopungua thuluthi mbili ya wabunge wote katika Bunge la Kitaifa, linaweza kuongeza muda uliowekwa kuhusu suala lolote kama inavyoelezwa katika ibara ya (1), kwa muda usiozidi mwaka mmoja.

(3) Mamlaka ya Bunge la Kitaifa yaliyobainiwa katika ibara ya (2) yanaweza kutumika—

a) mara moja tu kuhusiana na suala lolote; na

b) katika hali maalum tu ambazo zitathibitishwa na Spika wa Bunge la Kitaifa.

(4) Kwa madhumuni ya ibara ya (1), Mwanasheria Mkuu akishauriana na Tume ya Utekelezaji wa Katiba hii, atatayarisha na kuwasilisha Miswada husika Bungeni, kwa haraka inavyowezekana, ili kuwezesha Bunge kupitisha sheria hizo katika muda uliowekwa.

(5) Ikiwa Bunge litashindwa kupitisha sheria yoyote katika muda uliowekwa, mtu yeyote anaweza kuwasilisha ombi katika Mahakama Kuu kuhusiana na jambo hilo.

(6) Katika kuamua ombi lililowasilishwa chini ya ibara ya (6) Mahakama Kuu inaweza—

a) kutoa amri ya tangazo kuhusu suala hilo; na

b) Kutoa amri inayoagiza Bunge na Mwanasheria Mkuu kuchukua hatua zitakazohakikisha kwamba sheria inayohitajika imepitishwa katika muda uliowekwa katika agizo hilo, na kutoa ripoti kuhusu utekelezaji wa hatua hizo kwa Jaji Mkuu.

(7) Ikiwa Bunge litashindwa kupitisha sheria kulingana na agizo chini ya ibara ya (6) (b), Jaji Mkuu atamshauri Rais alivunje Bunge na Rais atalivunja Bunge.

(8) Ikiwa Bunge limevunjwa chini ya ibara ya (7), Bunge jipya litapitisha sheria hiyo inayohitajika katika muda uliotajwa katika Ambatisho la Tano, kuanzia tarehe ya kuanza kwa muhula wa Bunge hilo jipya.

(9) Ikiwa Bunge jipya litakosa kupitisha sheria kulingana na ibara ya (8), masharti ya ibara ya (1) hadi ya (8) yatatekelezwa upya.

*Vifungu vya mpito na vitakavyotumiwa Katiba hii itakapoanza kutekelezwa.*

**262.** Vifungu vya mpito na vitakavyotumiwa Katiba hii itakapoanza kutekelezwa, vilivyoainishwa katika Ambatisho la Sita vitaanza kutekelezwa mnamo tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii.

*Tarehe ya Kutekelezwa.*

**263.** Katiba hii itaanza kutumika Rais atakapotangaza rasmi au baada ya muda wa siku kumi na nne kuanzia tarehe ya kuchapisha matokeo ya mwisho ya kura ya maamuzi inayoidhinisha Katiba hii katika Gazeti Rasmi la Serikali, yoyote kati ya hatua hizo mbili itakayotekelezwa kwanza.

*Kufutiliwa mbali kwa katiba ya hapo awali.*

**264.** Katiba iliyokuwa ikitumika kabla ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii itafutuliwa mbali mnamo tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, lakini kwa kuzingatia Ambatisho la Sita.



SIO YA KUUZWA

# AMBATISHO

## AMBATISHO LA KWANZA (KIFUNGU CHA 6 (1))

### Kaunti

(1) Mombasa
(2) Kwale
(3) Kilifi
(4) Tana River
(5) Lamu
(6) Taita/Taveta
(7) Garissa
(8) Wajir
(9) Mandera
(10) Marsabit
(11) Isiolo
(12) Meru
(13) Tharaka-Nithi
(14) Embu
(15) Kitui
(16) Machakos
(17) Makueni
(18) Nyandarua
(19) Nyeri
(20) Kirinyaga
(21) Murang'a
(22) Kiambu
(23) Turkana
(24) West Pokot
(25) Samburu
(26) Trans Nzoia
(27) Uasin Gishu
(28) Elgeyo/Marakwet
(29) Nandi
(30) Baringo
(31) Laikipia
(32) Nakuru
(33) Narok
(34) Kajiado
(35) Kericho
(36) Bomet
(37) Kakamega
(38) Vihiga
(39) Bungoma
(40) Busia
(41) Siaya
(42) Kisumu
(43) Homa Bay
(44) Migori
(45) Kisii
(46) Nyamira
(47) Nairobi City


## AMBATISHO LA PILI (KIFUNGU CHA 9 (2))

### Nembo za kitaifa

a) Bendera ya Kitaifa

Kumbuka–– Vipimo vyote vilivyotolewa haviwakilishi urefu au upana wowote na ni linganifu tu. Maelezo––

Mistari mitatu mikubwa yenye upana sawa na yenye rangi nyeusi, nyekundu, na kijani kutoka juu hadi chini na ambayo imetenganishwa na mistari nyembamba ambayo ni nyeupe, na ngao linganifu na mishale nyeupe iliyowekwa katikati ya bendera.



b) Wimbo wa Taifa

1
Ee Mungu nguvu yetu
Ilete baraka kwetu
Haki iwe ngaona mlinzi
Natukae na undugu
Amani na uhuru
Raha tupate na ustawi

2
Amkeni ndugu zetu
Tufanye sote bidii
Nasi tujitoe kwa nguvu
Nchi yetu ya Kenya
Tunayoipenda
Tuwe tayari kuilinda.

3
Natujenge taifa letu
Ee, ndio wajibu wetu,
Kenya istahili heshima
Tuungane mikono
Pamoja kazini
Kila siku tuwe na shukrani.


SIO YA KUUZWA

c) Nembo ya Kitaifa Inayoashiria Mamlaka ya Kujitawala




d) Muhuri wa Serikali






SIO YA KUUZWA

## AMBATISHO LA TATU (VIFUNGU VYA 74, 141 (3), 148 (5) NA 152(4))

## VIAPO NA UTHIBITSHO WA KITAIFA

### KIAPO AU UTHIBITISHO RASMI WA UAMINIFU WA RAIS/RAIS ANAYEHUDUMU KWA MUDA MFUPI NA WA NAIBU WA RAIS

Mimi,........................................................................................ ,
nikifahamu kikamilifu kuhusu mwito mkuu ambao ninatumikia kama Rais/Rais wa Muda Mfupi/ Naibu wa Rais wa Jamhuri ya Kenya, ninaapa/ ninatoa uthibitisho rasmi kwamba nitakuwa mwaminifu na kutoa uaminifu wa kweli kwa Jamhuri ya Kenya; kwamba nitaitii, nitaihifadhi, kuilinda na kuitetea Katiba hii ya Kenya, kama ilivyowekwa kwa sheria, na sheria zote zinginezo za Jamhuri; na kwamba nitalinda na kukuza ukuu, uadilifu na hadhi ya wananchi wa Kenya. (Iwapo ni kiapo–– Ee Mungu nisaidie.)

### KIAPO AU UTHIBITISHO RASMI WA UTENDAKAZI KATIKA OFISI YA RAIS/RAIS WA MUDA MFUPI

Mimi,.............................................................., ninaapa/ninatoa
uthibitisho kwamba kwa kweli na bidii nitawahudumia wananchi na Jamhuri ya Kenya katika ofisi ya Rais/ Rais wa Muda Mfupi wa Jamhuri ya Kenya; kwamba nitatekeleza majukumu yangu na utendakazi wangu kwa bidii katika Ofisi ya Rais/ Rais wa Muda Mfupi wa Jamhuri ya Kenya; na nitawatendea haki wote kulingana na Katiba hii, ilivyowekwa kisheria, na kwa sheria za Kenya, bila woga, upendeleo, upendo au nia mbaya. (Iwapo ni kiapo–– Ee Mungu nisaidie.)

### KIAPO AU UTHIBITISHO RASMI WA UTENDAKAZI KWA NAIBU RAIS

Mimi,.............................................................., ninaapa/ ninatoa
Rasmi kuwa nitawatumikia wananchi na Jamhuri ya Kenya kila wakati kwa ukweli na bidii katika ofisi ya Naibu wa Rais wa Jamhuri ya Kenya; kwamba nitatekeleza majukumu yangu na kutenda kazi kwa bidii katika ofisi hiyo, kwa kadri ya uwezo wangu; kwamba kwa wakati wote ninapohitajiwa nitatoa ushauri wangu kwa Rais wa Jamhuri ya Kenya; kwamba nitawatendea haki wote bila woga, upendeleo, upendo au nia mbaya na kwamba sitafichua kwa njia ya moja kwa moja au vinginevyo maswala nitakayoyafahamu katika utekelezaji wa majukumu yangu na ambayo ninapaswa kuyaweka kwa usiri. (Iwapo ni kiapo–– Ee Mungu nisaidie.)

## KIAPO AU UTHIBITISHO RASMI WA UTENDAKAZI KWA WAZIRI

Mimi,............................................................, nikiwa nimeteuliwa kama Waziri nchini Kenya, ninaapa/ninatoa uthibitisho rasmi kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Jamhuri ya Kenya kila wakati; kwamba nitaitii, nitaihifadhi, kuilinda na kuitetea Katiba hii ya Kenya na sheria zote zingine za Jamhuri; kwamba nitawatumikia wananchi wa Jamhuri ya Kenya kwa ukweli katika Ofisi ya Waziri; kwamba ninaahidi kuhudumu kama Waziri kwa njia ya heshima na hadhi; kwamba nitakuwa mshauri mwaminifu na wa kweli wa Rais kwa madhumuni ya usimamizi bora katika maswala ya umma katika Jamhuri ya Kenya; kwamba sitafichua kwa njia ya moja kwa moja au vinginevyo maswala nitakayoyafahamu katika utekelezaji wa majukumu yangu na ambayo ninapaswa kuyaweka kwa usiri isipokuwa itakapohitajika nifichue maswala hayo katika utekelezaji wa majukumu yangu kama Waziri; na kwamba nitatekeleza majukumu ya ofisi yangu kwa ufahamu na kadri ya uwezo wangu. (Iwapo ni kiapo–– Ee Mungu nisaidie.).

## KIAPO AU UTHIBITISHO RASMI WA UTENDAKAZI KWA KATIBU WA BARAZA LA MAWAZIRI/KATIBU MKUU

Mimi,............................................................, nikiwa ninahitajiwa ili kutekeleza majukumu ya Katibu wa Baraza la Mawaziri/Katibu Mkuu, ninaapa/ninatoa uthibitisho rasmi kwamba, isipokuwa kwa idhini ya Rais, sitafichua kwa njia ya moja kwa moja au vinginevyo, hali na yaliyomo katika kikao, shughuli au hati yoyote ya Baraza la Mawaziri ambayo ninapaswa kuweka kwa usiri isipokuwa itakapohitajika nifichue maswala hayo katika utekelezaji wa majukumu yangu kama Katibu wa Baraza la Mawaziri/Katibu Mkuu. (Iwapo ni kiapo–– Ee Mungu nisaidie.

## VIAPO KWA JAJI MKUU /RAIS WA MAHAKAMA YA JUU ZAIDI, MAJAJI WA MAHAKAMA YA JUU ZAIDI, MAJAJI WA MAHAKAMA YA RUFAA NA MAJAJI WA MAHAKAMA KUU.

Mimi,............................................................, ( Jaji Mjuu/ Rais wa Mahakama ya Juu Zaidi, jaji wa Mahakama ya Juu Zaidi, jaji wa Mahakama ya Rufaa, jaji wa Mahakama Kuu) nina (apa kwa jina la Mwenyezi Mungu)/(ninatoa uthibitisho rasmi) kutumikia wananchi na Jamhuri ya Kenya na kutekeleza haki bila mapendeleo kulingana na Katiba hii na ilivyowekwa kisheria, na sheria na desturi za Jamhuri, bila woga wowote, upendeleo, ubaguzi, upendo, chuki, au mvuto wowote wa kisiasa, kidini,

ama ushawishi wowote mwingine. Katika kutekeleza majukumu ya kisheria ambayo nimepewa, kwa uwezo wangu wote, na kwa wakati wote, nitailinda, nitaitekeleza na kuitetea Katiba hii kwa madhumuni ya kulinda hadhi na heshima ya kitengo cha mahakama na mfumo wa mahakama wa Kenya na nitakuza haki, uhuru, ustadi na uadilifu ndani yake. (Ee Mungu nisaidie.)

## KIAPO/UTHIBITISHO KWA MWANACHAMA WA BUNGE (SENETI/ BUNGE LA KITAIFA)

I,..........................................................., nikiwa nimechaguliwa kama mwanachama wa Seneti/Bunge la Kitaifa ninaapa (Kwa jina la Mwenyezi Mungu) (ninatoa uthibitisho rasmi) kwamba nitakuwa mwaminifu na kuwa na imani ya kweli katika Wananchi na Jamhuri ya Kenya; kwamba nitatii, kuheshimu, kutetea, kulinda na kuhifadhi Katiba ya Jamhuri ya Kenya; na kwamba nitatekeleza majukumu ya mwanachama wa Bunge kwa uaminifu na uangalifu. (Ee Mungu nisaidie).

## KIAPO CHA SPIKA/NAIBU WA SPIKA WA SENETI/BUNGE LA KITAIFA

Mimi,..........................................................., nikiwa nimechaguliwa kama Spika/ Naibu wa Spika wa Seneti/Bunge la Kitaifa ninaapa (kwa jina la Mwenyezi Mungu) (ninatoa uthibitisho rasmi) kwamba nitakuwa mwaminifu kikweli kwa wananchi na Jamhuri ya Kenya; kwamba nitatekeleza kwa uaminifu na uangalifu majukumu yangu kama Spika/Naibu wa Spika wa Seneti/Bunge la Kitaifa; kwamba nitatii, nitaheshimu, nitatea, nitahifadhi, nitalinda na kuitetea Katiba hii ya Jamhuri ya Kenya; na kwamba nitatenda haki kwa watu wote kulingana na Katiba hii ya Kenya na sheria na desturi za Bunge bila woga au upendeleo, upendo au chuki (Ee Mungu nisaidie).

## AMBATISHO LA NNE (KIFUNGU CHA 185 (2), 186 (1) NA 187 (2))

## UGAWAJI WA MAJUKUMU KATI YA SERIKALI YA KITAIFA NA SERIKALI ZA KAUNTI

**Sehemu ya 1—Serikali ya Kitaifa**

(1) Maswala ya kigeni, sera ya kigeni na biashara ya kimataifa.

(2) Matumizi ya maji ya kimataifa na rasilimali za maji.

(3) Uhamiaji na uraia.

(4) Uhusiano kati ya dini na serikali.

(5) Sera ya lugha na ukuzaji wa lugha rasmi na lugha za kiasili.

(6) Ulinzi wa kitaifa na matumizi ya huduma za ulinzi za kitaifa.

(7) Huduma za polisi, ikijumuisha—

a) uwekaji viwango vya kuajiri, mafunzo kwa polisi na matumizi ya huduma za polisi;

b) sheria ya jinai; na

c) huduma za marekebisho.

(8) Mahakama.

(9) Sera ya kitaifa ya uchumi na mipango.

(10) Sera ya fedha, sarafu, benki (ikijumuisha benki kuu) kusajiliwa na kudhibitiwa kwa shughuli za benki, bima na mashirika ya kifedha.

(11) Takwimu za kitaifa na data kuhusu idadi ya watu, uchumi na jamii kwa jumla.

(12) Haki za uvumbuzi.

(13) Viwango vya utendakazi.

(14) Ulinzi wa watumiaji wa bidhaa na huduma, ikijumuisha viwango vya usalama wa kijamii na mipango ya kitaalamu kuhusu kustaafu.

(15) Sera ya elimu, viwango, mitaala, mitihani, na utoaji wa hati za kuidhinisha vyuo vikuu.

(16) Vyuo Vikuu, taasisi za mafunzo na taasisi zinginezo za utafiti na masomo ya juu na shule za msingi, elimu maalum, shule za upili na vyuo vya elimu maalum.



SIO YA KUUZWA

(17) Ukuzaji wa michezo na elimu ya michezo.

(18) Uchukuzi na mawasiliano, ikijumuisha hasa—

a) usafiri wa barabarani;

b) ujenzi na matumizi ya barabara kuu za kimataifa;

c) viwango vya ujenzi na uhifadhi wa barabara zingine zitakazojengwa na kaunti;

d) reli;

e) mabomba ya mafuta;

f) usafiri wa baharini;

g) usafiri wa ndege;

h) usafiri wa angani;

i) huduma za posta;

j) mawasiliano ya simu; na

k) utangazaji wa redio na runinga.

(19) Kazi za umma za kitaifa.

(20) Sera ya makazi.

(21) Kanuni za kijumla za mipango ya ardhi na uratibu wa mipango katika kaunti.

(22) Ulinzi wa mazingira na mali-asili kwa madhumuni ya kubuni mfumo wa maendeleo endelevu, ikijumuisha hasa—

a) uvuvi, uwindaji na ukusanyaji;

b) ulinzi wa wanyama na wanyama pori;

c) ulinzi wa maji, kuhifadhi maji yanayobaki, uhandisi unaohusu maji na usalama wa mabwawa; na

d) sera ya kawi.

(23) Vituo vya afya vya rufaa vya kitaifa.

(24) Usimamizi katika majanga

(25) Minara ya zamani ya kihistoria yenye umuhimu wa kitaifa.

(26) Uchaguzi wa kitaifa.

(27) Sera ya afya.

(28) Sera ya Kilimo.

(29) Sera ya utabibu wa mifugo.



SIO YA KUUZWA

(30) Sera ya kawi pamoja na nguvu za umeme, gesi, na udhibiti wa kawi.

(31) Ukuzaji wa uwezo wa utendakazi na usaidizi wa kiufundi katika kaunti.

(32) Uwekezaji wa umma.

(33) Uchezaji kamari wa kitaifa, makasino na aina mbalimbali za uchezaji kamari.

(34) Sera ya utalii na maendeleo.

**Sehemu ya 2—Serikali za Kaunti**

Majukumu na mamlaka ya kaunti ni—

(35) Kilimo, ikijumuisha—
- a) kilimo cha mimea na wanyama;
- b) viwanja vya kuuzia mifugo;
- c) vichinjio vya kaunti;
- d) udhibiti wa magonjwa ya mimea na wanyama; na
- e) uvuvi.

(36) Huduma za afya za kaunti ikijumuisha hasa—
- a) vituo vya afya vya kaunti na famasia;
- b) huduma za ambulensi;
- c) ukuzaji wa afya ya kimsingi;
- d) kutoa leseni na kusimamia shughuli za kuuza vyakula kwa umma;
- e) huduma za matibabu ya wanyama (isipokuwa udhibiti wa taaluma hii);
- f) makaburi, ukumbi wa matanga na tanuu za kuchomea maiti; na
- g) uondoaji taka, maeneo ya kutupa taka na utupaji taka.

(37) Kudhibiti uchafuzi wa hewa, uchafuzi wa mazingira kupitia kwa kelele, usumbufu mwingine kwa umma na utangazaji wa nje.

(38) Shughuli za kitamaduni, burudani za umma na huduma za umma ikijumuisha—
- a) mchezo wa kamari, makasino na aina nyingine ya kucheza kamari;
- b) mashindano ya mbio;
- c) utoaji leseni kwa uuzaji wa pombe;
- d) Majumba ya sinema;
- e) maonyesho ya video na ukodishaji;



SIO YA KUUZWA

f) maktaba;

g) majumba ya makumbusho;

h) michezo na shughuli za kitamaduni na vifaa; na

i) bustani za kaunti, fuo na vifaa vya burudani.

(39) uchukuzi katika kaunti, ikijumuisha—

a) barabara za kaunti;

b) taa za barabarani;

c) usafiri na uegeshaji;

d) usafiri wa barabarani wa umma ; na

e) vivuko na bandari, lakini bila usimamizi wa usafirishaji wa kitaifa na kimataifa na shughuli zinazohusiana na usafirishaji huo.

(40) Udhibiti na hali ya wanyama, ikijumuisha—

a) utoaji leseni kuhusu ufugaji na matumizi ya mbwa; na

b) Nyenzo za kuhifadhi, kutunza na kuzika wanyama.

(41) Maendeleo na udhibiti wa biashara, ikijumuisha—

a) masoko;

b) leseni za biashara (bila kujumuisha udhibiti wa taaluma);

c) usawa katika shughuli za kibiashara;

d) utalii wa humu nchini; na

e) vyama vya ushirika.

(42) Mipango na maendeleo ya kaunti, ikijumuisha—

a) takwimu;

b) upimaji wa ardhi na utengenezaji wa ramani;

c) mipaka na uwekaji nyua;

d) makazi; na

e) uunganishaji wa nguvu za umeme na gesi na udhibiti wa kawi.

(43) Elimu ya chekechea, vyuo vya kiufundi vijijini, vituo vya utengenezaji wa vyombo vya kinyumbani na vituo vya utunzaji wa watoto.

(44) Utekelezaji wa sera maalum za serikali ya kitaifa kuhusu mali-asili na uhifadhi wa mazingira, ikijumuisha—

a) uhifadhi wa udongo na maji; na

b) misitu.

(45) Huduma za kazi kwa umma katika kaunti ikijumuisha—

a) mfumo wa usimamizi wa maji ya tufani katika sehemu za majengo; na

b) huduma za maji na usafi.

(46) Huduma za kuzima moto, na udhibiti wa majanga.

(47) Udhibiti wa dawa za kulevya na ponografia.

(48) Kuhakikisha na kusimamia ushiriki wa jamii na sehemu za mashambani katika utawala wa viwango hivyo vya mashinani na kuzisaidia jamii pamoja na maeneo hayo kukuza uwezo wa kiusimamizi ili kuwezesha utekelezaji mwema wa mamlaka na majukumu na kushiriki katika utawala wa mashinani.



SIO YA KUUZWA

## AMBATISHO LA TANO (KIFUNGU CHA 261 (1))

### SHERIA ZITAKAZOTUNGWA NA BUNGE

| Sura na Kifungu | Muda Uliowekwa |
|---|---|
| Sura ya Pili—Jamhuri | |
| Sheria kuhusu utamaduni (Kifungu cha 11 (3)) | Miaka mitano |
| Sura ya Tatu–– Uraia | |
| Sheria kuhusu uraia (Kifungu cha 18) | Mwaka mmoja |
| | |
| Uhuru wa vyombo vya habari (Kifungu cha 34) | Miaka mitatu |
| Familia (Kifungu cha 45) | Miaka mitano |
| Ulinzi kwa watumiaji wa bidhaa na huduma (Kifungu cha 46) | Miaka minne |
| Haki katika hatua za kiutawala (Kifungu cha 47) | Miaka minne |
| Usikilizaji kesi kwa haki (Kifungu cha 50) | Miaka minne |
| Haki za walio kizuizini, waliokamatwa au waliofungwa gerezani (Kifungu cha 51) | Miaka minne |
| Tume ya Kitaifa Kuhusu Haki za Binadamu na Usawa ya Kenya (Kifungu cha 59) | Mwaka mmoja |
| Sura ya Tano—Ardhi na Mazingira | |
| Ardhi ya jamii (Kifungu cha 63) | Miaka mitano |
| Udhibiti wa matumizi ya ardhi na mali (Kifungu cha 66) | Miaka mitano |
| Sheria kuhusu ardhi (Kifungu cha 68) | Miezi 18 |
| Makubaliano yanayohusiana na mali-asili. (Kifungu cha 71) | Miaka mitano |



SIO YA KUUZWA

| | |
|---|---|
| Sheria kuhusu mazingira (Kifungu cha 72) | Miaka minne |
| **Sura ya Sita—Uongozi na Uadilifu** | |
| Tume ya maadili na kupambana na ufisadi (Kifungu cha 79) | Mwaka mmoja |
| Sheria kuhusu uongozi (Kifungu cha 80) | Miaka miwili |
| **Sura ya Saba—Uwakilishaji wa Watu** | |
| Sheria kuhusu uchaguzi (Kifungu cha 82) | Mwaka mmoja |
| Mizozo kuhusu uchaguzi (Kifungu cha 87) | Mwaka mmoja |
| Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (Kifungu cha 88) | Mwaka mmoja |
| Sheria kuhusu vyama vya kisiasa (Kifungu cha 92) | Mwaka mmoja |
| **Sura ya Nane—Bunge** | |
| Kukuza uwakilishi wa makundi yaliyotengwa. vikundi (Kifungu cha 100) | Miaka mitano |
| Mbunge kuondoka ofisini. (Kifungu cha 103) | Mwaka mmoja |
| Haki ya kumwondoa mbunge mamlakani (Kifungu cha 104) | Miaka miwili |
| Uamuzi katika maswali yanayohusiana na uanachama wa Bunge (Kifungu cha 105) | Miaka miwili |
| Haki ya kuwasilisha ombi Bungeni (Kifungu cha 119) | Miaka miwili |
| **Sura ya Tisa—Mamlaka Kuu ya Serikali Inayosimamia Utendaji** | |
| Mamlaka ya Msamaha wa Rais (Kifungu cha 133) | Mwaka mmoja |
| Kuchukua hatamu za uongozi katika ofisi ya rais (Kifungu cha 141) | Miaka miwili |
| **Sura ya Kumi—Kitengo cha Serikali Kinachosimamia Mahakama** | |
| Mfumo wa mahakama (Kifungu cha 162) | Mwaka mmoja |
| Kuondolewa ofisini (Kifungu cha 168) | Mwaka mmoja |



SIO YA KUUZWA

| | |
|---|---|
| Hazina ya Mahakama (Kifungu cha 173) | Miaka miwili |
| Ukaguzi wa majaji na mahakimu (Ambatisho la Sita, Sehemu ya 23) | Mwaka mmoja |
| **Sura ya Kumi na Moja—Serikali ya Ugatuzi** | |
| Spika wa bunge la kaunti (Kifungu cha 178) | Mwaka mmoja |
| Sehemu za miji na majiji (Kifungu cha 183) | Mwaka mmoja |
| Usaidizi kwa serikali za kaunti (Kifungu cha 190) | Miaka mitatu |
| Kuondolewa kwa gavana wa kaunti (Kifungu cha 181) | Miezi 18 |
| Kuondolewa ofisini kwa mwakilishi wadi katika bunge la kaunti (Kifungu cha 194) | Miezi 18 |
| Kushiriki kwa umma na mamlaka ya bunge la kaunti, haki maalum na kinga dhidi ya mashtaka (Kifungu cha 196) | Miaka mitatu |
| Usawa wa kijinsia na utofauti katika bunge la kaunti (Kifungu cha 197) | Miaka mitatu |
| Sheria kuhusu utekelezaji wa Sura ya kumi na moja (Kifungu cha 200 na Ambatisho la sita, Sehemu ya 15) na | Miezi 18 |
| **Sura ya Kumi na Mbili—Fedha za Umma** | |
| Hazina za Mapato za serikali za kaunti (Kifungu cha 207) | Miezi 18 |
| Hazina ya Dharura (Kifungu cha 208) | Mwaka mmoja |
| Udhamini wa mikopo ya serikali ya kitaifa. (Kifungu cha 213) | Mwaka mmoja |
| Udhibiti wa fedha (Kifungu cha 225) | Miaka miwili |
| Hesabu na ukaguzi wa mashirika ya umma (Kifungu cha 226) | Miaka minne |

| | |
|---|---|
| Ununuaji wa bidhaa na huduma za umma (Kifungu cha 227) | Miaka minne |
| Sura ya Kumi na Tatu—Huduma za Umma | |
| Maadili na kanuni za huduma za umma (Kifungu cha 232) | Miaka minne |
| Sura ya Kumi na Nne—Usalama wa Kitaifa | |
| Idara za usalama wa kitaifa (Kifungu cha 239) | Miaka miwili |
| Uongozi wa Huduma ya Polisi ya Kitaifa (Kifungu cha 245) | Miaka miwili |
| Kijumla | |
| Sheria nyingine yoyote itakayohitajiwa na Katiba hii; | Miaka mitano |



SIO YA KUUZWA

## AMBATISHO LA SITA (KIFUNGU CHA 262)

## VIFUNGU VYA MPITO NA VITAKAVYOTUMIWA KATIBA HII ITAKAPOANZA KUTUMIKA

### Sehemu ya 1—Vifungu vya Kijumla

*Ufasiri.*

**1.** Katika Ambatisho hili, isipokuwa muktadha uhitaji vinginevyo—

a) "Tume ya Mipaka" inamaanisha Tume Huru ya Muda ya Mipaka;

b) "Tume ya Uchaguzi" inamaanisha Tume Huru ya Muda ya Uchaguzi;

c) "katiba ya awali" inamaanisha Katiba iliyotumika kabla ya Katiba hii kuanza kutumika.

**2.**

*Utekelezaji wa vifungu vya Katiba hii Kusitishwa.*

(1) Kutekelezwa kwa vifungu vifuatavyo vya Katiba hii kumesitishwa hadi tangazo la mwisho la matokeo yote ya uchaguzi wa kwanza wa Bunge chini ya Katiba hii––

a) Sura ya Saba, isipokuwa kwamba vifungu vya sura hii vitatumika kwa uchaguzi mkuu wa kwanza chini ya Katiba hii;

b) Sura ya Nane, isipokuwa kwamba vifungu vya Sura hiyo vinavyohusiana na uchaguzi wa Bunge la Kitaifa na la Seneti, vitatumika katika uchaguzi mkuu wa kwanza chini ya Katiba hii; na

c) Vifungu vya 129 hadi 155 vya Sura ya Tisa, isipokuwa vifungu vya Sura hiyo vinavyohusiana na uchaguzi wa Rais, vitatumika katika uchaguzi mkuu wa kwanza chini ya Katiba hii.

(2) Utekelezaji wa vifungu vya Katiba hii vinavyohusiana na serikali ya ugatuzi, ikijumuisha Kifungu cha 187, umesitishwa hadi tarehe ya uchaguzi wa kwanza wa mabunge ya kaunti na magavana utakaofanywa chini ya Katiba hii.

(3) Licha ya ibara ndogo ya (2)—

a) uchaguzi wa mabunge ya kaunti na magavana utafanywa kwa mujibu wa Vifungu vya 177 na 180 vya Katiba hii; na
b) sheria zinazohusu serikali ya ugatuzi, zinazohitajiwa na Ambatisho hili na Sura za Kumi na Moja na Kumi Mbili za Katiba hii, zitatungwa katika muda uliowekwa chini ya Ambatisho la Tano.

(4) Kutekelezwa kwa Kifungu cha 62 (2) na (3) kutasitishwa hadi Tume ya Ardhi ya Kitaifa itakapobuniwa.

**3.**

*Kuongezwa kwa muda wa kutumia vifungu vya Katiba ya awali.*

(1) Hadi Bunge litakapopitisha Sheria inayotarajiwa katika Vifungu vya 15 na 18, sehemu ya 93 ya Katiba ya awali itaendelea kutumika.

(2) Sehemu za 30 hadi 40, 43 hadi 46, na 48 hadi 58 za Katiba ya awali, vifungu vya Katiba ya awali vinavyohusu kitengo cha serikali kinachosimamia utendaji na Sheria Kuhusu Muungano wa Kitaifa na Maridhiano zitaendelea kutumika hadi uchaguzi mkuu wa kwanza utakapofanywa chini ya Katiba hii, lakini vifungu vya Katiba hii kuhusu mfumo wa uchaguzi, ustahiki wa kuchaguliwa na mchakato wa uchaguzi vitatumika katika uchaguzi huo.

(3) Hadi Tume ya Huduma za Polisi za Kitaifa iliyotajwa katika Kifungu cha 246 itakapobuniwa, sehemu ya 108(2) ya Katiba ya awali itatumika katika uteuzi,



SIO YA KUUZWA

hatua za kinidhamu na kuondolewa ofisini katika Huduma za Polisi za Kitaifa.

*Kamati Teule ya Bunge*

**4.** Kutakuwa na kamati teule ya Bunge la Kitaifa itakayojulikana kama Kamati ya Kusimamia Utekelezaji wa Katiba, itakayowajibika katika kusimamia utekelezaji wa Katiba hii, na ambayo, kati ya masuala mengine—

a) itapokea ripoti za mara kwa mara kutoka kwa Tume ya Utekelezaji wa Katiba kuhusu utekelezaji wa Katiba hii, ikijumuisha ripoti kuhusu—

i. maandalizi ya sheria yanayohitajiwa na Katiba hii na changamoto zozote kuhusu maandalizi hayo;

ii. mchakato wa kubuni tume mpya;

iii. mchakato wa kuunda miundombinu inayohitajika ili kutekeleza shughuli za kila kaunti kwa njia mwafaka ikijumuisha hatua zilizopigwa katika kuweka ofisi na mabunge pamoja na kuajiri na kuhamisha wafanyakazi.

iv. ugatuzi wa mamlaka na majukumu kwa kaunti chini ya sheria inayobainishwa katika sehemu ya 15 ya Ambatisho hili; na

v. vizuizi vyovyote katika mchakato wa kutekeleza Katiba hii;

b) itashirikiana na Mwanasheria Mkuu, Tume ya Utekelezaji wa Katiba na kamati husika za Bunge ili kuhakikisha sheria zinazohitajiwa na Katiba hii zimewasilishwa bungeni na kupitishwa kwa wakati ufaao; na

c) itachukua hatua zinazofaa kuhusiana na ripoti hizo ikijumuisha kutatua matatizo yoyote katika utekelezaji wa Katiba hii.

**5.**

*Tume ya Utekelezaji wa Katiba.*

(1) Tume ya Utekelezaji wa Katiba imebuniwa.

(2) Tume hiyo inajumuisha—

a) mwenyekiti; na

b) wanachama wengine nane.

(3) Wanachama wa Tume—

a) watajumuisha watu wenye uzoefu katika masuala ya usimamizi wa umma, haki za binadamu na serikali; na

b) haitajumuisha mtu yeyote aliyehudumu kama mwanachama katika Tume ya Wataalamu iliyoteuliwa chini ya Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya, 2008.

(4) Vifungu vya 248 na 254 vinatumika kwa Tume hiyo.

(5) Baada ya Tume ya Ugavi wa Mapato kubuniwa, Tume ya Utekelezaji wa Katiba itatuma notisi ya mikutano yake kwa Tume hiyo, na mwanachama wa Tume ya Ugavi wa Mapato ataruhusiwa kuhudhuria na kushiriki katika mikutano yoyote kama hiyo, lakini hatapiga kura.

(6) Majukumu ya Tume hiyo yatakuwa ni—

a) kufuatilia, kusimamia na kuwezesha utungaji wa sheria na taratibu za kiutawala zinazohitajika ili kutekeleza Katiba hii;

b) kushirikiana na Mwanasheria Mkuu na Tume ya Marekebisho ya Sheria ya Kenya katika



SIO YA KUUZWA

kutayarisha sheria itakayowasilishwa Bungeni ambayo itahitajika ili kutekeleza Katiba hii; na

c) itatoa ripoti za mara kwa mara kwa Kamati ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Katiba. Kamati ya Usimamizi—

i. hatua zilizopigwa katika utekelezaji wa Katiba hii; na

ii. vizuizi vyovyote katika utekelezaji wake; na

d) itafanya kazi na kila tume ya kikatiba kuhakikisha kuwa madhumuni na vifungu vya Katiba hii vinaheshimiwa.

(7) Tume ya Utekelezaji wa Katiba hii itavunjwa miaka mitano baada ya kubuniwa kwake au baada ya kutekelezwa kikamilifu kwa Katiba hii kama itakavyoamuliwa na Bunge, yoyote kati ya hatua hizi itakayotimia mwanzo ikichukuliwa, lakini Bunge la Kitaifa linaweza kuiongezea muda Tume hiyo kwa uamuzi.

**Sehemu ya 2—Majukumu, Sheria na Haki Zilizopo**

*Haki, majukumu na Wajibu wa Serikali.*

**6.** Isipokuwa Katiba hii inapoeleza vinginevyo, haki na majukumu yote ya Serikali au Jamhuri, bila kujalisha yalivyotokea, na ambayo yalikuwepo kabla ya tarehe ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii yataendelea kama haki na majukumu ya serikali ya kitaifa au Jamhuri chini ya Katiba hii.

**7.**

*Sheria zilizopo.*

(1) Sheria zote zinazotumika kabla ya tarehe ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii zitaendelea kutumika na zitafasiriwa kwa kuzingatia mabadiliko yatakayoweza



SIO YA KUUZWA

kuambatanishwa na Katiba hii. Ikiwa, kwa mujibu wa suala lolote—

a) sheria iliyokuwa ikitumika kabla ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii inatoa majukumu kwa kitengo fulani cha Serikali au afisa wa umma; na

b) kifungu katika Katiba hii kinachotumika kinatoa majukumu kuhusu suala hilo kwa kitengo tofauti cha Serikali au afisa wa umma, vifungu vya Katiba hii vitatawala kwa kiwango cha ukinzani huo.

**8.**

*Ardhi iliyopo na makubaliano kuhusu mali-asili.*

(1) Katika tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii ardhi yoyote inayomilikiwa na mtu ambaye si raia wa Kenya itarejeshwa kwa Jamhuri ya Kenya ili kumilikiwa kwa niaba ya wananchi wa Kenya, na Serikali itampa mtu huyo kipindi cha miaka tisini na tisa cha kukodisha ardhi hiyo na kumtoza kiasi kidogo cha kodi.

(2) Katika tarehe ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii, umiliki au haki zozote katika ardhi ambazo zinazidi muda wa kukodisha ardhi kwa miaka tisini na tisa, ardhi hiyo ikimilikiwa na mtu ambaye sio raia, itabadilishwa na kuwa ardhi inayokodishwa kwa muda wa miaka tisini na tisa.

(3) Mwongozo unaotolewa na Kifungu cha 71 hautatekelezwa hadi sheria inayorejelewa katika Kifungu hicho itungwe.



SIO YA KUUZWA

**Sehemu ya 3—Serikali ya Kitaifa**

**9.**

*Uchaguzi na uchaguzi mdogo.*

(1) Uchaguzi wa kwanza wa Rais, Bunge la Kitaifa, Seneti, mabunge ya kaunti na magavana wa kaunti chini ya Katiba hii utafanywa kwa wakati mmoja, katika muda wa siku sitini baada ya kuvunjwa kwa Bunge la Kitaifa mwishoni mwa muhula wake.

(2) Licha ya ibara ndogo ya (1), ikiwa muungano uliobuniwa chini ya Maridhiano ya Kitaifa umevunjwa na uchaguzi mkuu kufanywa kabla ya mwaka wa 2012, uchaguzi wa kwanza wa mabunge ya kaunti na magavana utafanywa katika mwaka huo wa 2012.

*Bunge la Kitaifa.*

**10.** Bunge la Kitaifa lililokuwa kabla ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii litaendelea kama Bunge la Kitaifa kwa madhumuni ya Katiba hii kwa muhula wake uliosalia.

**11.**

*Seneti.*

(1) Hadi Seneti ya kwanza itakapochaguliwa chini ya Katiba hii—

a) majukumu ya Seneti yatatekelezwa na Bunge la Kitaifa; na

b) jukumu lolote au mamlaka yoyote yanayohitajika kutekelezwa kwa pamoja na vitengo vyote viwili vya Bunge au kitengo kimoja baada ya kingine, yatatekelezwa na Bunge la Kitaifa.

(2) Jukumu lolote au mamlaka ya Seneti, ikiwa yatatekelezwa na Bunge la Kitaifa kabla ya tarehe inayobainishwa katika ibara ndogo ya (1), yatachukuliwa kuwa yalitekelezwa kikamilifu na Seneti.



SIO YA KUUZWA

**12.**

*Kitengo cha Serikali Kinachosimamia Utendaji.*

(1) Watu wanaohudumu katika ofisi za Rais na Waziri Mkuu kabla ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, wataendelea kuhudumu kama Rais na Waziri Mkuu mtawalia, kwa mujibu wa Katiba ya awali na Sheria Kuhusu Muungano na Maridhiano ya Kitaifa ya mwaka wa 2008 hadi uchaguzi mkuu ufanyike chini ya Katiba hii, isipokuwa waondoke ofisini kwa mujibu wa Katiba ya awali na Sheria hiyo ya Maridhiano.

(2) Watu wanaohudumu katika ofisi za Makamu wa Rais na Naibu Waziri Mkuu au wanahudumu katika Baraza la Mawaziri au

kama Waziri Msaidizi kabla ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, wataendelea kuhudumu kulingana na Katiba ya awali hadi uchaguzi mkuu wa kwanza utakapofanywa chini ya Katiba hii, isipokuwa waondoke au kuondolewa ofisini kulingana na Katiba ya awali na Sheria Kuhusu Muungano na Maridhiano ya mwaka wa 2008.

(3) Mtu aliyechaguliwa kuwa Rais kabla ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii hastahiki kugombea uchaguzi wa urais chini ya Katiba hii.

*Kiapo cha uaminifu kwa Katiba hii.*

**13.** Katika tarehe ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii, Rais na afisa yeyote wa Serikali, au mtu yeyote ambaye kabla ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii alikuwa amekula kiapo au kutoa uthibitisho wa kuhudumu katika ofisi hiyo chini ya Katiba ya awali, au anayetakiwa kula kiapo au kutoa uthibitisho chini ya Katiba hii, ataapa au kutoa uthibitisho ufaao chini ya Katiba hii.



SIO YA KUUZWA

**Sehemu ya 4—Serikali ya Ugatuzi**

**14.**

*Kutumika kwa vifungu vinavyohusiana na Serikali ya ugatuzi.*

(1) Sheria zinazotajwa katika sehemu ya 2 (3) (b) na ya 15 zinaweza kupitishwa tu baada ya Tume ya Utekelezaji wa Katiba na, ikiwa Tume ya Ugavi wa Mapato imebuniwa, Tume hiyo pia imetoa mashauri na mapendekezo yoyote ya Tume hizo yamezingatiwa na Bunge.

(2) Tume hizo zitapewa angalau siku thelathini ili kutathmini sheria chini ya ibara ndogo ya (1).

(3) Ibara ndogo za (1) na (2) hazitatumika tena Tume ya Utekelezaji wa Katiba itakapovunjwa.

**15.**

*Mwongozo kuhusu ugatuzi wa majukumu kutolewa na Sheria ya Bunge.*

(1) Bunge, kupitia kwa sheria, litatoa mwongozo wa kuhamishwa kwa awamu, wa majukumu kutoka kwa serikali ya kitaifa hadi serikali za kaunti kama yalivyotolewa chini ya Kifungu cha 185, kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu kuanzia tarehe ya uchaguzi wa kwanza wa mabunge ya kaunti.

(2) Sheria inayotajwa katika ibara ndogo ya (1)—

a) itatoa mwongozo wa jinsi serikali ya kitaifa—

i. itakavyowezesha ugatuzi wa mamlaka;

ii. itakavyosaidia serikali za kaunti kujenga uwezo wao wa kujitawala na wa kutoa huduma zinazostahili kutolewa na serikali hizo; na Kiapo cha uaminifu kwa Katiba hii.

iii. itatoa msaada kwa serikali za kaunti;

b) itaweka vigezo ambavyo lazima vitimizwe kabla ya majukumu fulani kugatuliwa kwa



SIO YA KUUZWA

serikali za kaunti, ili kuhakikisha kwamba serikali hizo hazipewi majukumu ambayo haziwezi kuyatekeleza; na

c) itaruhusu ugatuzi wa mamlaka ili kuhakikisha kwamba majukumu yanagatuliwa kwa haraka kwa kaunti ambazo zina uwezo wa kuyatekeleza, lakini kwamba hakuna kaunti iliyopewa majukumu isiyoweza kutekeleza; na

d) itatoa mikakati ambayo itahakikisha kwamba Tume ya Utekelezaji wa Katiba inaweza kutekeleza jukumu lake la kufuatilia utekelezaji wa mfumo wa serikali ya ugatuzi kwa ufanisi.

*Ugavi wa mapato*

**16.** Licha ya Kifungu cha 217 (1), maamuzi ya kwanza na ya pili kuhusu misingi ya ugavi wa mapato kati ya kaunti yatafanywa kila baada ya miaka mitatu, badala ya kila baada ya miaka mitano kama inavyoelezewa katika Kifungu hicho.

*Utawala wa Mikoa.*

**17.** Katika kipindi cha miaka mitano baada ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, serikali ya kitaifa itafanya marekebisho katika mfumo wa utawala unaojulikana kama utawala wa mikoa, ili uafikiane na kuheshimu mfumo wa serikali ya ugatuzi uliobuniwa chini ya Katiba hii.

*Ofisi za Utawala wa Mitaa*

**18.** Ofisi zote za utawala wa ndani zilizobuniwa chini ya Sheria Kuhusu Serikali za Mitaa (Sura ya 265 ya Sheria za Kenya) zilizokuwa kabla ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii zitaendelea kuwepo lakini kwa kuzingatia sheria yoyote inayoweza kupitishwa.



SIO YA KUUZWA

**Sehemu ya 5 – Utekelezaji wa Haki**

*Kanuni za utekelezaji wa Sheria za Haki.*

**19.** Hadi Jaji Mkuu atakapotengeneza kanuni zinazorejelewa katika Kifungu cha 22, Kanuni za utekelezaji wa haki na uhuru wa kimsingi chini ya sehemu ya 84 (6) ya Katiba ya awali zitaendelea kutumika lakini kwa kuzingatia mabadiliko muhimu yatakayoziambatanisha na Kifungu cha 22.

**20.**

*Tume ya Huduma za Mahakama;*

(1) Tume ya Huduma za Mahakama itateuliwa katika muda wa siku sitini baada ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, na Tume hiyo itachukuliwa kuwa imebuniwa ipasavyo chini ya Katiba hii licha ya kwamba huenda kukawa na nafasi wazi katika uanachama wake kwa kuwa idara zozote zinazowateua au kuwachagua wanachama hazijafanya hivyo.

(2) Licha ya ibara ndogo ya (1), Tume ya Huduma za Mahakama haitatekeleza majukumu yake isipokuwa wanachama watano wameteuliwa.

(3) Ili kuhakikisha kuwa kuna mwendelezo katika shughuli za Tume ya Huduma za Mahakama, licha ya Kifungu cha 171 (4), Tume itakapobuniwa kwa mara ya kwanza, wanachama wafuatao watateuliwa ili kuhudumu kwa miaka mitatu pekee—

a) (A) Jaji wa Mahakama ya Rufaa aliyeteuliwa chini ya Kifungu cha 171 (c);

b) jaji wa Mahakama Kuu aliyeteuliwa chini ya Kifungu cha 171 (4) (d);

c) mmoja kati ya wakili walioteuliwa chini ya Kifungu cha 171 (4) (f), watakaotambuliwa na shirika la kisheria linalowajibika katika udhibiti



SIO YA KUUZWA

wa kitaalam wa mawakili; na

d) mmoja wa wanachama walioteuliwa na Rais chini ya Kifungu cha 171 (4) (h); atakayetambuliwa na Rais.

(4) Hadi Tume ya Huduma za Umma inayorejelewa katika Kifungu cha 233 itakapobuniwa, mtu aliyeteuliwa na Tume ya Huduma za Umma chini ya sehemu ya 106 ya Katiba ya awali atahudumu katika Tume ya Huduma za Mahakama lakini, Tume mpya ya Huduma za Umma itakapobuniwa, mtu huyo atawacha kuwa mwanachama wa Tume ya Huduma za Mahakama na Tume hiyo mpya ya Huduma za Umma itamteua mtu atakayehudumu katika Tume ya Huduma za Mahakama.

**21.**

*Kuundwa kwa Mahakama ya Juu Zaidi.*

(1) Kubuniwa kwa Mahakama ya Juu Zaidi na kuteuliwa kwa majaji wa Mahakama hiyo kutakamilishwa katika muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii.

(2) Hadi Mahakama ya Juu Zaidi itakapobuniwa, Mahakama ya Rufaa itakuwa na mamlaka katika kesi zinazopaswa kusikizwa na kuamuliwa na Mahakama ya Juu Zaidi.

*Usikilizaji wa kesi na kesi ambazo hazijakamilika.*

**22.** Kesi zote ambazo hazijakamilika katika mahakama yoyote zitaendelea kusikilizwa na uamuzi kutolewa na mahakama iliyokuwa ikisikiza kesi hiyo au mahakama ya kiwango sawa iliyobuniwa chini ya Katiba hii au itakavyoelekezwa na Jaji Mkuu au Msajili wa Mahakama Kuu.



SIO YA KUUZWA

**23.**

*Majaji.*

(1) Katika muda wa mwaka mmoja baada ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, Bunge litatunga sheria itakayotekelezwa licha ya Kifungu cha 160, 167 na 168, ambayo itaweka mikakati na utaratibu wa kukagua ustahiki wa majaji na mahakimu wote waliokuwa ofisini mnamo tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, wa kuendelea kuhudumu kwa mujibu wa maadili na kanuni zilizotolewa katika Vifungu vya 10 na 159, muda huo wa kukaguliwa ukiamuliwa katika sheria hiyo.

(2) Kuondolewa au utaratibu utakaopelekea kuondolewa kwa jaji kutoka ofisini kwenye msingi wa utekelezaji wa sheria inayorejelewa katika ibara ndogo ya (1) hakutapingwa au kukaguliwa na mahakama yoyote.

**24.**

*Jaji Mkuu.*

(1) Jaji Mkuu aliye ofisini kabla ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, ataondoka ofisini katika muda wa miezi sita baada ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii na anaweza kuchagua—

a) kustaafu kutoka katika kitengo cha mahakama; au

b) kwa kuzingatia mchakato wa ukaguzi huo chini ya sehemu ya 23, kuendelea kuhudumu katika Mahakama ya Rufaa.

(2) Jaji Mkuu mpya atateuliwa na Rais, kwa kuzingatia Sheria Kuhusu Muungano wa Kitaifa na Maridhiano, na baada ya kushauriana na Waziri Mkuu na kwa idhini ya Bunge la Kitaifa.

(3) Ibara ndogo ya (2) pia itatumika ikiwa kuna nafasi

za ziada katika ofisi ya Jaji Mkuu kabla ya uchaguzi mkuu wa kwanza chini ya Katiba hii.

**Sehemu ya 6 – Tume na Ofisi**

**25.**

*Tume za Kikatiba.*

(1) Tume ya Utekelezaji wa Katiba na Tume ya Ugavi wa Mapato zitabuniwa katika muda wa siku tisini baada ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii.

(2) Tume ya Mishahara na Malipo itabuniwa katika muda wa miezi tisa baada ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii.

(3) Hadi sheria inayorejelewa katika Kifungu cha 256 itakapoanza kutumika, watu watakaoteuliwa kama wanachama au mwenyekiti wa Tume ya Mishahara na Malipo watateuliwa na Rais, kwa kuzingatia Sheria Kuhusu Muungano wa Kitaifa na Maridhiano, na baada ya kushauriana na Waziri Mkuu na kwa idhini ya Bunge la Kitaifa.

**26.**

*Tume ya Kitaifa Kuhusu Haki za Binadamu na Usawa ya Kenya.*

(1) Makamishna wa Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu na Usawa ya Kenya walioteuliwa chini ya Sheria ya Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu ya Kenya ya mwaka wa 2002 (Na. 9 ya 2002) na makamishna wa Tume ya Kitaifa ya Jinsia na Maendeleo walioteuliwa chini ya Sheria ya Tume ya Kitaifa ya Jinsia na Maendeleo ya mwaka wa 2003 (Na. 13 ya 2003), mbali na Makatibu Wakuu na Mwanasheria Mkuu au mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu, watakuwa wanachama wa Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu na Usawa kwa muhula wao uliosalia,

lakini kila mmoja wao atadumisha masharti yake ya utendakazi yalivyokuwa mnamo tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii.

(2) Mwenyekiti wa Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu ndiye atakayekuwa mwenyekiti wa Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu na Usawa kwa muhula uliosalia wa mwenyekiti huyo, na mwenyekiti wa Tume ya Kitaifa ya Jinsia na Maendeleo atakuwa Naibu Mwenyekiti wa Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu na Usawa ya Kenya kwa muda wa muhula wa mwenyekiti huyo uliosalia.

**27.**

*Tume Huru ya Muda ya Uchaguzi.*

(1) Tume ya Mipaka iliyobuniwa chini ya Katiba ya awali itaendelea kuhudumu kama ilivyobuniwa katika Katiba hiyo na kwa masharti ya sehemu za 41 B na 41 C lakini—

a) haitaweka mipaka ya kaunti zilizobuniwa chini ya Katiba hii;
b) itaweka mipaka ya maeneo bunge na wadi ikitumia vigezo vilivyotajwa katika Katiba hii; na
c) wanachama wa Tume hiyo watakuwa chini ya Sura ya Saba ya Katiba hii.

(2) Hitaji katika Kifungu cha 89 (2) kwamba ukaguzi wa mipaka ya maeneo bunge na wadi utakamilishwa angalau miezi kumi na miwili kabla ya uchaguzi mkuu halitumiki katika ukaguzi wa mipaka kabla ya uchaguzi wa kwanza chini ya Katiba hii.

(3) Tume ya Mipaka itahakikisha kuwa ukaguzi wa kwanza wa mipaka ya maeneo bunge utakaofanywa chini ya Katiba hii hautasababisha kupotea kwa eneo

bunge lililokuwepo katika tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii.

**28.**

*Tume Huru ya Muda ya Uchaguzi na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka.*

(1) Tume Huru ya Muda ya Uchaguzi iliyobuniwa chini ya sehemu ya 41 ya Katiba ya awali itaendelea kuhudumu ofisini kwa mujibu wa Katiba hiyo kwa muda wa muhula uliosalia au hadi Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka itakayobuniwa chini ya Katiba hii ibuniwe, hali itakayotokea mwisho ikitumiwa.

(2) Wanachama wa Tume ya Uchaguzi na Mipaka watakapoteuliwa, hitaji la kuendeleza na kudumisha ustadi na uzoefu utazingatiwa.

**29.**

*Uteuzi mpya.*

(1) Mchakato wa uteuzi wa watu ili kujaza nafasi zitakazotokea kutokana na kutekelezwa kwa Katiba hii, utaanza mnamo tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii na kukamilika katika kipindi cha mwaka mmoja.

(2) Isipokuwa Ambatisho hili litoe mwongozo vinginevyo, Katiba hii inapohitaji uteuzi ufanywe na Rais na kuidhinishwa na Bunge la Kitaifa, hadi baada ya uchaguzi wa kwanza chini ya Katiba hii, kwa kuzingatia Sheria Kuhusu Muungano wa Kitaifa na Maridhiano, Rais atamteua mtu baada ya kushauriana na Waziri Mkuu na kwa idhini ya Bunge la Kitaifa.



SIO YA KUUZWA

### Sehemu ya 6—Masuala ya Ziada

*Uraia kwa kuzaliwa.*

**30.** Raia wa Kenya ni raia kwa kuzaliwa ikiwa raia huyo—

(1) alipata uraia chini ya Kifungu cha 87 au 88 (1) cha Katiba ya awali; au

(2) angepata uraia ikiwa Kifungu cha 87 (2) kingesema ifuatavyo:

" Kila mtu ambaye alizaliwa nje ya Kenya, na mnamo tarehe 11 Desemba, 1963 ni raia wa Uingereza na Koloni zake au mtu aliyepata ulinzi wa Uingereza, mtu huyo atakuwa, iwapo mama au baba yake atakuwa, au isipokuwa kufariki kwake angekuwa raia wa Kenya kwa mujibu wa ibara ndogo ya (1), atakuwa raia wa Kenya mnamo tarehe 12 Desemba, 1963."

**31.**

*Ofisi zilizopo.*

(1) Isipokuwa Ambatisho hili litoe mwongozo vinginevyo, mtu ambaye kabla ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii alikuwa anahudumu au kutoa huduma kwa muda katika ofisi iliyobuniwa na Katiba ya awali, kufikia tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii ataendelea kuhudumu au kutoa huduma kwa muda katika ofisi hiyo chini ya Katiba hii kwa muda uliosalia wa muhula wa mtu huyo, iwapo kuna muda wowote uliosalia.

(2) Kwa kuzingatia ibara ndogo ya (7) na sehemu ya 24, mtu ambaye kabla ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii alikuwa anahudumu au kutoa huduma kwa muda katika ofisi ya umma iliyobuniwa kisheria, ataendelea kuhudumu au kutoa huduma kwa muda katika ofisi hiyo kwa kiwango kinachoambatana na

Katiba hii, kana kwamba aliteuliwa kwa nafasi hiyo chini ya Katiba hii.

(3) Vifungu vya sehemu hii havitaathiri mamlaka yaliyotolewa kwa mtu yeyote au shirika chini ya Katiba hii au sheria ya kuvunja ofisi au kuwaondoa watu kutoka ofisi inayorejelewa katika ibara ndogo ya (2).

(4) Ikiwa mtu ameondoka katika ofisi ambayo alikuwa akihudumu kabla ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, na ofisi hiyo ipo au imeundwa chini ya Katiba hii, ikiwa atastahiki, anaweza kuteuliwa, kuchaguliwa tena, au vinginevyo kuteuliwa ili kuhudumu katika ofisi hiyo kulingana na vifungu vya Katiba hii, isipokuwa kwa kiwango ambacho Katiba hii inatoa mwongozo vinginevyo.

(5) Majukumu ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma yatatekelezwa na Mwanasheria Mkuu hadi Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma atakapoteuliwa chini ya Katiba hii.

(6) Majukumu ya Msimamizi wa Bajeti yatatekelezwa na Mkaguzi Mkuu hadi Msimamizi wa Bajeti atakapoteuliwa chini ya Katiba hii.

(7) Licha ya ibara ndogo ya (1), Mwanasheria Mkuu na Mkaguzi Mkuu wataendelea kuhudumu ofisini kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na miwili baada ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, na uteuzi utakaofuata katika ofisi hizi utakuwa chini ya Katiba hii.

*Malipo ya uzeeni, bahashishi na manufaa mengine.*

**32.** Sheria inayotumika katika malipo ya uzeeni kwa maafisa wa ofisi za kikatiba chini ya Katiba ya awali itakuwa sheria iliyotumika wakati manufaa hayo

yalipotolewa au sheria yoyote itakayokuwa ikitumika hapo baadaye na ambayo haitamwathiri vibaya mtu huyo.

*Taasisi, ofisi, mali na madeni kurithiwa.*

**33.** Ofisi au taasisi ambayo ilibuniwa chini ya Katiba hii ndio inayorithi kisheria, ofisi au taasisi iliyokuwepo, ambayo ilibuniwa chini ya Katiba ya awali au Sheria ya Bunge iliyokuwa ikitumika kabla ya tarehe ya kutumika kwa Katiba hii, ofisi au taasisi hiyo iwe inajulikana kwa jina lile lile au jina jipya.

*Sarafu.*

**34.** Hakuna chochote katika Kifungu cha 231 (4) kinachoathiri uhalali wa sarafu na noti zilizotolewa kabla ya tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba hii.



SIO YA KUUZWA